

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Ishirini – Tarehe 10 Julai, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Orodha ya Shughuli za leo za Mkutano wa Nane, Kikao cha Ishirini. Katibu tuendelee.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Tumbaku Tanzania, kwa Mwaka wa Fedha Ullioishia Tarehe 30 Juni, 2010. [The Annual Report and Audited Accounts of Tanzania Tobacco Board for the Financial Year ended 30th June, 2010].

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 163

Upandishwaji Vyeo Watumishi wa Manispaa Nchini

MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MHE. RACHEL M. ROBERT) aliuliza:-

Kumekuwa na utaratibu wa Manispaa zetu nchini kuwapandisha vyeo waajiriwa wake wakiwemo Wauguzi wakiwapa barua na maelekezo yote yapasayo ya upandishwaji vyeo hivyo. Lakini utekelezaji wa yale yaliyoelezwa kwenye barua zao hayafanyiki na pengine huchukua muda mrefu sana, hata zaidi ya miaka miwili bila kutekelezwa:-

Je, kwa nini Serikali haitekelezi maelekezo yaliyomo kwenye barua za watumishi wanaopandishwa vyeo wakati wanatekeleza majukumu yao kwenye cheo alichopandishwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watumishi kuchelewa kurekebishiwa mishahara yao baada ya kupandishwa vyeo lilichangiwa na utaratibu uliokuwepo ambao mtumishi alipopewa barua ya kupandishwa cheo alitakiwa kukubali kwanza ndipo mwajiri wake aziwasilishe ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imechukua hatua madhubuti katika kushughulikia suala hili kwa kusimika mfumo wa kieletroniki wa taarifa za utumishi (*Human Capital Information Management System LAWSON Version 9*) katika kila Halmashauri.

Maafisa rasilimali watu wamepatiwa mafunzo ya kutumia mfumo huu ambapo barua za kupandishwa cheo hutumwa kwa kutumia mfumo huo. Hivyo, malipo ya mishahara sasa yanafanyika ndani ya muda mfupi baada ya mtumishi kupandishwa cheo. Kwa mfano taarifa za mtumishi zikitumwa kabla ya tarehe tano (5) mtumishi atapokea mshahara mpya ndani ya mwezi huo.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Halmashauri kuzingatia na kutumia huu mfumo kikamilifu ili kuepuka malimbikizo ya madeni ya watumishi. Mara mtumishi

anapopandishwa cheo taarifa zake ziingizwe katika mfumo na kutumwa mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

MHE. LETICIA NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwa kuwa kupandishwa cheo kwa mtumishi huambatana na marupurupu mengine.

Je, ni jinsi gani sasa Serikali imekuwa ikiwapatia watumishi hawa marupurupu mengine ikiwemo kuhakikisha kwamba wanapata sehemu za kuishi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi anapopata ajira au anapopandishwa cheo, ile barua yake ya kupandishwa cheo au kupata ajira ndani yake inatamka pia marupurupu pamoja na haki zote za mtumishi ndani ya ile barua. Kwa mfumo huu niliouzungumza hapa maana yake ni kwamba wataipeg moja kwa moja katika huu mfumo na ita-*appear* katika mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba hizi sehemu zote zinazozungumziwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere, zilishakuwa *consolidated zikaingizwa* katika mshahara wa mtumishi. Kama ni suala la nyumba, kama hakupata nyumba *physical then* atapata *allowance* ambayo itaingizwa katika mshahara wake kwa maana ya kufidia. Ataangalia

illigibility au kama huyu ni *viable* na vitu vingine vya namna ile.

Na. 164

Namba za Usajili wa Vijiji Nchini

MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. ABDUL J. MAROMBWA) aliuliza:-

Mwaka 2010 Serikali ilianzisha vijiji vipyta karibu nchi nzima.

Je, ni sababu zipi zinachelewesha vijiji hivyo kupatiwa namba za usajili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mwaka 2010 Serikali ilianzisha vijiji vipyta 4,583 Tanzania Bara na kuvitangaza kwenye Gazeti la Serikali Na. 180 la tarehe 14 Mei, 2010 na Gazeti la Serikali Na. 392 la tarehe 15 Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 26(1) cha sheria za Serikali za Mitaa Serikali ya Kijiji

kufanyika, Msajili wa Vijiji anapaswa kutoa pamoja na mambo mengine namba ya usajili wa kijiji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya kuchelewa kutolewa kwa namba za usajili wa vijiji vipyta vilivyotangazwa mwaka 2010 ni kutokana na zoezi la uanzishwaji wa maeneo mapaya ya utawala kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa wananchi, zoezi ambalo limesababisha baadhi ya vijiji kugawanywa kutoka Kata moja kwenda Kata nyingine na baadhi ya Wilaya kutoka katika Mkoa Mmoja kwenda Mkoa mwingine, kwani namba za usajili hutolewa kwa kuzingatia Mkoa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile zoezi la kuanzisha maeneo mapya linaelekea kukamilika, kwa sasa zoezi la uhakiki wa vijiji vinavyotakiwa kupata namba za usajili linaendelea, zoezi ambalo linafanyika kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri husika. Aidha, jumla ya vijiji 2000 kati ya vijiji 4,583 vilivyotangazwa havina mapungufu na vitapatiwa namba za usajili ifikapo tarehe 30 Agosti, 2012. Vijiji 2,583 vyenye mapungufu vinaendelea kuhakikiwa kabla ya kupewa namba za usajili.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru Naibu Waziri kwa maelekezo mazuri lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, ni dhahiri kwamba Watanzania wanaongezeka na hivyo wananchi watahitaji vijiji vipyta, Kata mpya, Serikali ina mpango gani wa kuweka kitengo maalum kuhakikisha hatupati matatizo tena

mara vijiji vinapotangazwa, mapungufu yote yameisha na vijiji vinapatiwa usajili wao ili waweze kufanya shughuli nyingine za kijamii?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa vizuri, hakuna haja ya kuweka kitengo maalum. Kama unataka kuanzisha Mkoa na Wilaya, kipo kitengo TAMISEMI na Idara ambayo inazungumza mambo ya *Regional Administration*. Kama unataka kuanzisha Kata au Vijiji ambavyo vinakwenda katika *Local Authorities*, kipo kitengo ambacho kipo chini ya *Director of Local Authorities*. Kwa hiyo, kuanzisha kitengo kingine sijui labda sikumwelewa vizuri Mheshimiwa Njwayo. Labda kama anataka tuwe makini zaidi na tuweze kuwa *focus* zaidi, atanielewesha baadaye tutakapokutana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nikuthibitishie kwamba vitengo tumeanzisha, sasa hivi tumeanzisha *Secondary Schools* na *Primary Schools* zote zipo TAMISEMI na kweli tumeanzisha vitengo na Idara zinazohusika na haya maeneo. Kwa hiyo, nataka nimthibitishie kwamba sasa hivi tuko *systematic*. Mtu akileta Vijiji hapa anataka tuvisajili, tutaondoka tutakwenda mpaka pale Tandahimba tuende tukaangalie hicho kilichoandikwa katika huu muhtasari kinalingana na kilichopo pale kwenye ardhi na baada ya hapo ndipo tuna-*issue certificates*. Kwa hiyo, nakuomba uwe na hakika kabisa kwamba kila kitu kipo *under control*.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, wananchi wa kijiji cha Managa Wilaya ya Babati, Kata ya Ari, wamekuwa wakifuatilia Kijiji chao kwa muda mrefu sana pamoja na kwamba *GN* ya Serikali ilitangaza Kijiji Mama kitakuwa Managa, lakini kijiji hicho kimechakachuliwa kwa ajili ya maslahi ya kisiasa ya baadhi ya viongozi na kutangaza kitongoji kimojawapo cha kijiji hicho kuwa Kijiji pamoja na kwamba Serikali imetoa *GN*. ya kijiji hicho cha Managa.

Je, Waziri sasa yupo tayari kuingilia tatizo hilo la wananchi hao kwa sababu wameshafuata ngazi za Wilaya, Mkoa tatizo lao halitatuliwi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika sana kama hiki anachokisema ni kile Kijiji ambacho kila wakati huwa tunazungumza na kuna simu napigiwa nyingi sana kuhusu hiki kijiji kinachosemwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa, tunavyo Vijiji 4500, hivi vijiji 2000 tumeshavi-*clear* tumekubaliana kwamba *this is okay*. Nakubaliana na Mhehsimiwa Gekul kwamba inawezekana pia kwamba hiki kijiji tunachokisema hapa kinaweza kikawepo. Haya mapungufu unayosema wakati mwingine unakwenda kucheki kwenye orodha unakuta Kata hii

ndiyo inasema kijiji hicho kumbe kijiji kimehama kutoka kwenye Kata hiyo kimekwenda kwenye Kijiji nyingine, Waziri Mkuu hatasajili Kijiji cha namna hiyo. Akikuta Kijiji Namba hiyo na Namba hiyo inatokea kwa mtu mwingine pale hatasajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa labda niweke vizuri, kwamba mmefanya uchaguzi pale, mmemchagua mtu pale unaweka tu utaratibu wa kisheria ambao nimeusoma hapa ili sasa uweze kusema naam. Kwa maana ya kwamba unakuwa na Serikali ya Kijiji yenye watu 25, yenye Mwenyekiti. Serikali ya Kijiji ya watu 25 ndilo Bunge la Kijiji. Ndipo unaposema *this is board cooperate* inaweza ikakopeshwa, inaweza ikawasued, inaweza ikafukuza, inaweza ika-acquire ardhi na kadhalika. Nitakwenda kucheki hiki anachokisema. Nitaiangalia hii *unnormarly* anayoizungumzia Mheshimiwa Gekul. Tukikuta tutarekebisha katika vile Vijiji kama ilivyosemwa. (*Makof*)

Na. 165

Manufaa ya Sheria ya Mikopo ya Nyumba

MHE. SALIM HEMED KHAMIS aliuliza:-

Sheria ya mikopo ya nyumba ilipitishwa na Bunge mwaka 2010:-

Je, Watanzania wangapi wamenufaika na mikopo ya nyumba na wangapi wanatarajiwa kunufaika katika mwaka huu wa fedha 2011/2012?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya nyumba ni mikopo ya muda mrefu inayotolewa na mabenki kwa ajili ya kununua au kukarabati nyumba. Mabenki yaliyo wanachama wa *Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC)* hutumia amana za muda mfupi kutoa mikopo ya nyumba ya muda mrefu kwa matarajio kuwa, mabenki haya yatakopeshwa kwa muda na *TMRC* kupitia mkopo wa Serikali kwa *TMRC* ambao ni wa miaka 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Juni, 2012, *TMRC* ilikuwa imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi za Kitanzania bilioni 4.2 tangu ianze shughuli zake rasmi mwezi Novemba, 2011. Mikopo hii imenufaisha jumla ya wateja 95. Hadi itakapofikia Desemba, 2012. Wanachama wa *TMRC* kwa pamoja wanatarajia kutoa mikopo yenye thamani ya shillingi za Kitanzania bilioni 44 kwa wateja wapatao 230.

MHE. HEMED SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri ninapenda nimwuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, changamoto kubwa zinazowakabili wakopaji na wakopeshaji ni viwango vidogo vyamishahara jambo ambalo linawafanya Watanzania wengi kutokukopesheka.

Je, Serikali imejipanga vipi kuona kuwa hawa nao wanafaidika na mikopo ya nyumba?

Swali la Pili. Kwa kuwa Watanzania wengi hawana Hati za Kumiliki viwanja kwa sababu Serikali imeshindwa kuwapimia na kuwapa Hati.

Je, Serikali haioni kwamba mikopo ya nyumba itawanufaisha zaidi wale wanaoishi mijini na wale wenye uwezo mkubwa wa kifedha? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna changamoto mbalimbali katika masuala ya mikopo ya nyumba, mojawapo ikiwa ni vipato vidogo kwa Watanzania wengi.

Lakini vile vile nataka nimfahamishe Mbunge na Wabunge wote mliopo kuwa *TMRC* ina dirisha lingine ambalo linahudumia wakopaji wadogo kwa maana ya kukusanya vyanzo vyamapato mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wakopaji wadogo kupata mikopo hii.

Lakini vilevile kuna taasisi zisizokuwa za Kiserikali ambazo zimeanzisha mifumo kama hii ya *SACCOS* kwa ajili ya kukopesha watu wenye vipato vidogo.

Kwa hiyo, hizi zote ni fursa ambazo zinaweza zikisimamiwa vizuri na kwa Uongozi wa Serikali kuhakikisha kuwa wakopaji wenyewe vipato vidogo wanaweza vile vile kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili kwamba Watanzania wengi hawana Hati za viwanja, ni kweli kuna mikakati inaendelea ya kurasimisha Hati za Vijijini na Mijini ambako hakujapimwa na kwa hali hiyo sasa hivi kuna uwezo mkubwa kwa watu wengi kukopa kwa kutumia huu mfumo ninaouzungumza wa hili dirisha la pili la watu wenyewe vipato vidogo kuweza kukopa kwa ajili ya mikopo ya nyumba.

Hata hivyo, haiondoi umuhimu wa Serikali kuendelea kufanya juhudi zaidi ya kuhakikisha kuwa watu wengi zaidi wanapata mikopo hii katika hali ambayo inawawezesha na wao kuishi katika mazingira mazuri.

MHE. AMINA BDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu lilikuwa linafanana na swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, naona limeshajibiwa na mimi nimeridhika na jawabu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana kwa busara zako. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Utafiti wa Maeneo ya Madini

MHE. MARGARETH AGNES MKANGA aliuliza:-

Thamani ya eneo la uchimbaji madini hutokana na utafiti wa madini uliokwishafanyika:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya tafiti za kina kwa kutumia Shirika la *NDC* kwenye maeneo yenye madini na kuiwezesha Nchi kuingia mikataba yenye maslahi zaidi na wawekezaji?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna thamani ya eneo linalofanyiwa utafutaji wa madini huongezeka kadri mashapo ya madini yanavyogunduliwa. Kulingana na Sera ya Madini ya mwaka 2009 uwekezaji katika sekta ya madini hufanywa kupitia wawekezaji binafsi au Serikali kupitia mashirika yake ya *STAMICO* na *NDC*. Iwapo eneo la utafutaji wa madini litakuwa chini ya mwekezaji binafsi ni wajibu wa mwekezaji huyo kuingia gharama za uwekezaji katika shughuli za utafutaji au uchimbaji madini. Aidha, Serikali ina wajibu wa kuendeleza maeneo ya utafutaji madini katika maeneo yanayomilikiwa na *STAMICO* na *NDC* kwa

kutumia mitaji yake au kuingia ubia na wavezekaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi uwekezaji katika shughuli za utafutaji madini unahitaji mtaji mkubwa na iwapo madini hayajapatikana kwa kiwango cha kuweza kuchimbwa kwa faida mtaji uliotumika katika shughuli hiyo hupotea. Serikali kupitia *STAMICO* na *NDC* inaendelea kuwekeza kwenye miradi ya madini kwa kupata hisa kupitia (*free carried shares*) na kuendeleza shughuli za utafutaji wa madini katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa maana hiyo, Serikali itaendelea kuimarisha *STAMICO* na *NDC* ili ziweze kushiriki ipasavyo katika miradi mbalimbali ya madini kwa manufaa ya nchi. Hata hivyo shughuli za utafutaji madini huhitaji mitaji mikubwa na Serikali kupitia *NDC* au *STAMICO* haiwezi kufanya utafiti wa madini nchi nzima kwa mara moja. Maeneo mengine lazima yafanyiwe utafiti na wavezekaji binafsi na Serikali inaweza kuingia ubia kwa kupata hisa. (*Makofii*)

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwanza nataka kufahamu hii *free carried shares* ndio nini ili hata wananchi tuweze kuelewa kwa sababu ni sheria sijui, mimi personally nawaulizia hata na wenzangu?

(b) Serikali imesema kwamba itaendelea kuiwezesha *STAMICO* na *NDC* kuweza kufanya utafiti kwa kutumia mtaji. Napenda kufahamu kwa mwaka huu na Bajeti hii maeneo haya mawili yamewezeshwaje ili waendeleze miradi ile ambayo imekwishaanza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *free carried interest* ni hisa au maslahi ambayo kampuni zetu za *NDC* au *STAMICO* zinapata kwa sababu ndizo zinazomiliki hizo leseni. Kwa hiyo, mwekezaji anapokuja pamoja na mtaji anaokuja nao haifanyi yeye akamilike asilimia zote kwa sababu amefanya utafiti na anaendesha uchimbaji. Makampuni yetu haya ya Umma ya *NDC* na *STAMICO* ndio yatakayomiliki kwa niaba ya Watanzania hisa na maslahi yoyote yale yatakayotokana na uzalishaji na mapato yanayotokana migodi hiyo kwa maslahi ya umiliki wa leseni zile.

Lakini la pili ameuliza juu ya *STAMICO* na *NDC* na kama je, kuna maeneo gani katika Bajeti ya mwaka huu 2012/2013ambayo tunaweza tukawa tumeamua kufanya utafiti. Ni kweli Serikali inafanya jitihada pamoja na kwamba mitaji ya kufanya utafiti ni mikubwa na wakati mwengine unaweza ukafanya

utafiti wenyewe gharama kubwa na ukaambulia patupu. (*Makofi*)

Lakini kwa kiasi fulani tutajitahidi na mwaka huu wa fedha Serikali itaitumia *GST* yaani wakala wa Jiolojia Tanzania na kufanya utafiti wa kutumia ndege *Air Born Survey* katika maeneo ya Mikoa ya Singida, Manyara, Dodoma, Tanga, Pwani, Morogoro na Ukanda wa Lupa Tingatinga Wilaya ya Chunya.

MHE. SULEMANI SAID JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika kipindi cha karibuni tumeona makampuni mengi yakipita maeneo mbalimbali kwa ajili ya utafutaji wa madini pamoja na mafuta. Lakini watu wale walikuwa wanakuja moja kwa moja bila kuzi-*consult* Halmashauri za Wilaya na wanapokuja katika vitendo hivyo maana yake ni njema. Lakini utakuja kuona kuna uharibifu wa mazao ya wananchi.

Je, utaratibu ukoje wa ulipaji wa fidia kwa wananchi hawa ambao magreda na matrekta yamepita katika mashamba haya katika utafutaji wa madini na mafuta?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba shughuli nyingi za utafutaji na uchimbaji zinaendelea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikishirikisha wawekezaji. Lakini kwa mujibu wa sheria yetu tulioipitisha ya madini ya mwaka 2010 tulikubaliana na tulipitisha sheria inasema ni lazima kuwe kuna mawasiliano mazuri kati ya Halmashauri zetu na vijiji katika kuhakikisha kwamba shughuli zote zinazofanyika zinafanyika katika mawasiliano ambayo hayaleti matatizo.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa watu wote wanaofanya shughuli zozote ziwe za utafutaji, wawe wachimbaji wadogo wa ndani au wachimbaji wa nje ni lazima wahakikishe wanawasiliana na Halmashauri zetu kabla ya kufanya jambo lolote lile.

Na. 167

Hitaji la Umeme Vijiji vya Jimbo la Rungwe Magharibi

MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA) aliuliza:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha umeme toka Isangati hadi Maitika ili kunufaisha na kuchochea maendeleo katika vijiji vya Kipande, Ighembe, Libigi, Kinyala na Lukata?

(b) Je, ni lini Serikali itasambaza umeme katika Kata ya Saya Vijiji vya Swaya, Ishinga, Malangali na Isebelo kutokea Kijiji cha Ntakela B ambako mradi wa sasa umeishia?

(c) Je, Serikali inasema nini kuhusu kupeleka umeme Vijiji vya Bigela, Kyambambahembe, Ijinga na Masukulu kutokea Kiwanda cha Chai Musekera ambako tayari kuna umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, lenye vipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini iliyofanyiwa na Shirika la Umeme *TANESCO* inaonesha kuwa gharama za upelekaji wa umeme katika Vijiji vya Isangati, Kipande, Ighembe, Libigi, Kinyala na Lukata ni shilingi milioni 670.1. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *KV 33* wenyе urefu kilomita 8, njia ya umeme ya msongo wa *KV 0.4* wenyе urefu wa kilomita 12 na ufungaji wa *transfoma 5* zenye uwezo wa *KVA 100*.

Mradi unatarajia kuwaunganishia umeme wateja takribani 275 wa njia moja na wateja 25 wa njia tatu. Maombi ya kupata fedha za kutekeleza mradi huu yamepelekwa kwa wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) ili mradi huu utekelezwe katika mwaka wa fedha 2012/2013. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Ntokera B, Swaya, Ishinga, Malangali

na Isobelو kunahitajika ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *kV 33* yenye urefu wa kilomita 8. Njia ya urefu wa msongo wa *kV 0.4* yenye urefu wa kilomita 6 na ufungaji wa *transfoma 3* zenye uwezo wa *KVA 100*. Gharama za mradi huu ni shilingi milioni 469.3.

Mradi unatarajiwا kuwaunganishia umeme wateja 75 kwa njia moja na wateja 10 wa njia tatu. Maombi ya kupata fedha za kutekeleza mradi huu yamepelekwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini ili mradi huu utekelezwe katika mwaka wa fedha 2012/2013.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Bujela, Kyambambene, Masukulu na Ijigha, kunahitajika ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *kV 33* yenye urefu wa kilomita 15.3 njia ya umeme ya msongo wa *kV 0.4* yenye urefu wa kilomita 15.5 na ufungaji wa *transfoma 5* zenye uwezo wa *KVA 100*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini iliyofanywa na *TANESCO* kwa ajili ya kutekeleza mradi huo ni shilingi bilioni 1.03. Mradi unatarajia kuwaunganishia umeme wateja 335 wa njia moja na wateja 14 wa njia tatu. Maombi ya kupata fedha za kutekeleza mradi huu yamepelekwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini ili mradi huu utekelezwe katika mwaka wa fedha 2012/2013.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri yenye ahadi za matumaini. Kwa matumaini hayo aliyoyatoa.

(a) Je, Wizara yake iko tayari kufuatilia huko REA mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa kama ilivyopangwa?

(b) Kwa kuwa Wilaya ya Rungwe inayo maporomoko mengi ya maji. Je, Serikali iko tayari kuwahamasisha wawekezaji wengi iwezekanavyo ili waweze kusaidia usambazaji wa umeme katika vijiji vyote vya Wilaya ya Rungwe?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, kama ifuatavyo:-

Ametaka kujua kama Serikali iko tayari kufuatilia *REA* kuhusiana na fedha hizi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Jibu langu ni kwamba Serikali iko tayari. (*Makof*)

Lakini pili, ametaka kujua kama Rungwe kuna maporomoko ambayo yanaweza kuzalisha umeme na kama Serikali iko tayari kutafuta wawekezaji au kuwavutia wawekezaji au kuwaelekeza wawekezaji. Jibu langu ni kwamba Serikali itafanya kazi hiyo.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme Mjini Namanyere inasua sua sana kinyume na ahadi ya Mheshimiwa Rais ambaye aliwaahidi wananchi wa Wilaya ya Nkasi kwamba umeme utafika mwezi Desemba mwaka 2011. Sasa ni mwezi wa 7 mwaka 2012. Ahadi hii inaonekana kama

ni udhalilishaji wa makusudi kwa Rais wetu kwa wananchi wa Nkasi ambao wanamheshimu sana. Je, Serikali aliyoiunda inayotekeleza ahadi hii inatuambia nini ili wananchi wa Nkasi waweze kuwa na imani na Rais wao ambaye wanamheshimu sana?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mipata, kama ifuatavyo:-

Naiona *concern* ya Mheshimiwa Mbunge na natambua namna ambavyo anafanya jitihada kubwa ili wananchi wa Namanyere waweze kupata umeme. Ahadi ya Rais nikuhakikishie Mheshimiwa Mipata na wananchi wa Namanyere kwamba ni lazima itatekelezwa kabla ya mwaka 2015 kwa sababu ndio ilani yetu itatekelezwa kwa kiwango hicho ndio muda wake.

Ahadi ya Rais ni lazima itatekelezwa, yako matatizo madogo madogo ambayo yamesababisha kuchelewa haya tutayashughulikia na nikukaribishe ofisi kwangu ili tuweze kujadiliana tuone namna ya kushirikiana.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, timu iliyopiga kambi kule Namanyere imelala kwenye giza. Basi ahadi itatekelezwa.

Kuanzisha Anuani za Mitaa, Mikoa na Miji

MHE. MHONGA SAIDI RUHWANYA aliuliza:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Anuani za Mitaa, Miji na Mikoa kwa ajili ya utambuzi ikiwa ni pamoja na kurahisisha ukusanyaji wa kodi?
- (b) Je, ni lini kazi hiyo muhimu itakamilika?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Saidi Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeanzisha mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta kwa ajili ya kuwezesha uwepo kwa mfumo mpya wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta nchini. Mfumo huu utatumia majina ya mitaa, barabara na namba za nyumba kwa ajili ya kutoa anuani kwa kila mwananchi nchini.

Mfumo huu utarahisisha utambuzi wa eneo analoishi kila mwananchi, eneo ilipo kila biashara na shughuli mbalimbali za kiuchumi hivyo kusaidia shughuli mbalimbali za Kiserikali ikiwemo ukusanyaji wa kodi.

(b) Sehemu (b) ya swali la Mheshimiwa Ruhwana inauliza ni lini kazi hii muhimu itakamilika? Mradi huu

umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016 kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Jitihada mbalimbali zinaendelea za kuhamasisha wananchi, wafanyabiashara na wahisani mbalimbali kuchangia utekelezaji wa mradi huu.

Mbali na utekelezaji ulioanza katika baadhi ya Kata za Mikoa ya Arusha na Dodoma iliyotumika kama majaribio, utekelezaji katika maeneo mengine nchini umeanza ikiwa ni hatua za mwanzo katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo shughuli zilizinduliwa na mwana wa Mfalme wa Uingereza *Prince Charles* mwezi Novemba, 2011 wakati wa kuelekea maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Aidha, kama sehemu ya kutoa elimu na umuhimu wa mradi huu, semina kwa viongozi na watendaji mbalimbali zimetolewa ikiwemo Semina kwa Waheshimiwa Wabunge kwenye Bunge lililopita Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Makatibu Wakuu Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Madiwani kwa baadhi ya Mikoa ikiwemo Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha, Dodoma pamoja na Zanzibar.

Vile vile mafunzo yametolewa kwa watendaji wa Serikali za Mitaa na baadhi ya Madiwani kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa mradi huu. (*Makofi*)

MHE. MHONGA SAIDI RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unaonekana ni muhimu sana lakini vile vile unaonekana utahitaji fedha nyingi na utatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Lakini nauliza kulingana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali haioni kwamba inaweza ikapunguza gharama kwa kuwashirikisha Wenyeviti wa Serikali za Mitaa waweze kupendekeza majina ya mitaa yao halafu wale watalaan waweze kuweka zile namba au waweze kufanya *codification*.

Lakini vile vile wawashirikishe makampuni binafsi ambao watashiriki katika kuweka vibao na kuweka matangazo yao katika vibao hivyo vyta mitaa kwa mfano makampuni ya simu?

(b) Nilikuwa napenda kufahamu utekelezaji wa mpango huu utakuwaje katika maeneo ambayo yamejengwa kiholela katika miji na vijiji vyetu kwa sababu amesema hii itatekelezwa katika nchi nzima? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Zoezi la kutambua kila eneo katika nchi yetu katika kila Kata limeshakamilika. *Codification* imeshafanyika na nchi nzima tayari mfumo huu umekamilika na kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni mfumo muhimu sana na hatua inayofuatia sasa ni kweli ni gharama kubwa kwa sababu lazima kila mtaa uwekwe kibao cha jina na kila nyumba iwekwe namba. Tumeanza katika maeneo baadhi, kwa mfano Dodoma hapa nyumba 5000 tayari zimeshabandikwa namba na mitaa, Arusha nyumba karibu 7500 na tumepata uzoefu hata kwenye maeneo ambayo hayajajengwa rasmi na tumeshirikiana na uongozi wa Serikali za Mitaa. Ni kweli kwamba ili zoezi hili lifanikiwe ni lazima ushirikishe viongozi wa vijiji na mitaa na vitongoji na hilo linafanyika. Lakini tunachukua wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba ni lazima tushirikishe sekta binafsi. Lakini vile vile ni muhimu kwamba hivi vibao vyta mitaa visigeuke kuwa vibao vyta matangazo ya biashara ikawa vurugu, lazima vibao hivi vibakie rasmi na lazima tuweke utaratibu ambapo wananchi watashiriki kwenye kuvilinda na kuhakikisha kwamba having'olewi. Kwa hiyo, ushiriki wa wananchi ni muhimu sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nifafanue kama alivyoeleza Naibu Waziri suala la kuweka anwani kwenye Makazi yaani mradi wa *addressing the world* ni mradi ambao na sisi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tunashiriki kwa karibu tukishirikiana na Wizara ya Sayansi na Teknolojia na nichukue nafasi hii kusema kwamba

katika kongamano la dunia litakalofanyika *Qatar* Septemba tutashiriki tutakuwepo na mimi nitakuwepo pia pale katika wadhifa wangu kama ni Balozi wa mradi huu kidunia kwa sababu ya kazi yangu niliyokuwa nafanya Umoja wa Mataifa.

Kwa upande wa Tanzania nielezee kwamba hapa tatizo la Mipango Miji kidogo linakwamisha mradi huu na hapo niwapongeze wenzetu kwa juhudini wanayofanya kuweka *post code* lakini sisi kwa upande wetu na katika Bajeti yetu tunakazania Halmashauri zote ziwe *master plan*. Nichukue nafasi hii kuzitangazia Halmashauri zote kwamba mtu yejote atakayetuletea *master plan* kama majina ya mitaa hayakuwekwa kusudi yaiingie kwenye ramani zetu za kudumu hatutakubali kupitisha mipango hiyo. (*Makofi*)

Niwahimize tu katika kutoa majina pia tunapata tatizo la kuwa na jina moja katika kila Mji, kitu ambacho kitakuja kuleta *confusion*, lakini kuna vigezo ambavyo mimi naomba nishauri kabisa. Kwa mfano, katika Miji midogo hususani Mji wa Muleba ambapo mimi natoka, lakini Miji ya Kasulu, Sengerema, nikienda labda na Namtumbo na sehemu nyingine ndogo, jamani, hakuna waanzilishi wa TANU mkawatambua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali tuwe na vigezo vya kuweka majina, hakuna Mito mkaitambua? Hakuna Machifu ambao walipigana na Mkoloni tukawatambua? Kwa hiyo, mimi nafikiria kwamba hizi siasa za sasa hivi za wakati huu zisitukwaze. Kuna waasisi wa kila sehemu ambao naomba watambulike

na mimi napendekeza Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ridhaa yako, napendekeza waasisi wa *TANU* bila kujali vyama vyovyote vile maana yake wote tumetoka huko huko, kwamba watambulike katika kila Halmashauri na ramani itakayokuja bila waasisi wale, nasikitika sintaitisha. (*Makofii*)

Na. 169

Kurudisha Somo la Ufundu Katika Shule za Msingi na Sekondari

MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC aliuliza:-

Kukosekana kwa ajira Serikalini kumesababisha ongezeko kubwa la vijana wengi kukaa bila shughuli yeyote ya kufanya na kusababisha vijana wengi kujitumbukiza kwenye vitendo haramu kama utumiaji wa dawa za kulevyia, ujambazi, ubakaji na vitendo vya ngono haramu.

Je, Serikali ipo tayari kurudisha elimu ya ufundu (Stadi za Kazi) kwenye shule za Msingi na Sekondari ili kuwapa vijana maarifa ya kuweza kujajiri wenyewe mara wanapomaliza masomo yao?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Marystella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Ufundi inaendelea kufundishwa katika Shule za Msingi na Sekondari. Elimu ya Ufundi ni dhana pana ambayo inajumuisha stadi mbalimbali za kumwezesha binadamu kukabiliana na maisha. Stadi hizo ni pamoja na elimu ya mazingira, afya, ujasiriamali na elimu ya jamii. Aidha, kwa mujibu wa Sera ya elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Stadi za Maisha zinajumuisha Useremala, Kilimo na Ufugaji, Ufinyanzi, Uashi, Uhunzi, Maarifa ya Nyumbani na Uchoraji, ambapo Stadi hizi zipo katika Mtaala wa Elimu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Elimu ya Msingi, Elimu ya Ufundi (Stadi za Kazi) hufundishwa kama somo la Stadi za Kazi na katika Elimu ya Sekondari hufundishwa kutegemea mchepuo wa shule husika kama Biashara ambapo kuna masomo ya *Bookkeeping* na *Commerce* ama Kilimo, Ufundi na Sayansi Kimu. Aidha, kwa sasa Wizara inahuisha Mtaala wa Elimu ili kuingiza pamoja na mambo mengine, Elimu ya Ujasiriamali kwa Elimu ya Sekondari.

MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la kumwuliza:-

Kwa kuwa vijana wengi wanaomaliza Elimu ya Sekondari, wanakuwa hawana ujuzi wowote wa kuweza kujiajiri kutoptana na kusoma shule hasa za Kata ambazo hazina vifaa vya kufundishia Elimu ya Ufundi kwa vitendo.

Je, Serikali sasa ipo tayari kuboresha elimu hiyo ya ufundu mashulen i kwa kupeleka vifaa vya Elimu ya Ufundu ili watoto wetu waweze kujifunza Elimu ya Ufundu kwa vitendo na waweze kujiajiri?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Anna Marystella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika kipindi cha miaka sita hii, tumekuwa na shule nyingi sana za Kata yapata shule elfu mbili na kitu lakini ukijumlisha na shule zote za *private* nchi nzima, tuna shule 4367. Lakini shule za ufundu zilishatengwa toka siku nyingi, tunazo shule za ufundu kama nane (8) kwa nchi nzima. Shule hizo ningependa kuzitaja hapa ni *Tanga School*, Moshi, Bwiru, Ihungo *Technical* na shule za Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu shule zimekuwa nyingi sana na hizi shule zilitengwa miaka ya nyuma sana, Serikali inaangalia uwezekano wa kuongeza shule nyingine za ufundu.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo hili limekuwa ni tatizo sugu katika nchi yetu. Je, Serikali sasa iko tayari kuongeza Elimu ya Msingi angalau ifike mpaka Kidato cha nne ili watoto wanaojifunza hizi Stadi za Kazi wawe na sifa ya kuajiriwa, kuo, ama kuolewa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge na Kaimu Kiolngodzi wa Kambi ya Upinzani kwa siku ya leo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Elimu ya Ufundi, upande wa Shule za Msingi zipo Stadi za Kazi na hasa inategemea na mazingira na maeneo.

Kwa mfano mazingira ya wafugaji wanasoma Stadi za Ufugaji, mazingira ya wafinyanzi wanasoma Stadi za Ufinyanzi, mazingira ya wapishi na maarifa ya nyumbani hata Uchoraji na hata Kilimo kwa baadhi ya Shule za Msingi na kwa sababu Kilimo ni Utii wa Mgongo nadhani kila Shule ya Msingi ina Stadi za Kilimo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Shule za msingi vile vile wanasoma Stadi za Kazi. Sasa hivi Wizara iko katika mpango wa kuhuisha elimu ya mafunzo ili tuweze kuingiza vitu vyote hivi katika Mtaala mpya. (*Makofii*)

Na. 170

Chuo cha Ualimu Mtwara Kuwa Chuo Kikuu

MHE. JUMA A. NJWAYO aliuliza:-

Ilani ya CCM ya 2005-2010 iliahidi Chuo cha Ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu Kiambata.

Je, mpango huo umefikia wapi na kwanini kisiwe Chuo Kikuu kamili?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliazimia kuvipandisha hadhi kwa awamu baadhi ya Vyuo vya Ualimu vinavyotoa Stashahada (*Diploma*) ya Ualimu kuwa Vyuo Vikuu.

Lengo lilikuwa ni kuongeza idadi ya wahitimu wa Shahada ya kwanza ya Ualimu kwa ajili ya kufundisha Katika Shule za Sekondari ambazo zimeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na mafanikio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vilivyo lengwa katika zoezi hilo vilikuwa ni Chuo cha Ualimu Dar es Salaam (Chang'ombe), Chuo cha Ualimu Mtwara, Chuo cha Ualimu Mkwawa na Chuo cha Ualimu Marangu. Aidha, vyuo viliv yokamilisha lengo hili na kuwa sehemu ya chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam (*DUCE*) na Mkwawa (*MUCE*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kupandisha hadhi vyuo vya Kada ya Kati kuwa Vyuo Vikuu lilitishwa na Serikali kwa nia ya kubakiza na kuendeleza kuimarisha Kada hii ya Kati (*Diploma*) kutokana na umuhimu wake katika maendeleo ya Taifa.

Katika zoezi hili, Vyuo vya Ualimu Marangu na Mtwara havikupandishwa hadhi kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki/Viambata ili viendelee kutoa walimu wa Stashahada ambao walimu hao pia wanahitajika sana katika utoaji wa elimu ngazi ya Msingi na Sekondari.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mkoa wa Mtwara uko nyuma kimaendeleo ndiyo maana unaitwa Mkoa ulioko pembezoni na kwamba elimu huchangia maendeleo sana na kwamba kama chuo hiki kingepandishwa hadhi, ingehamasisha Wanamtwara kusoma sana:-

(a) Sasa nataka kupata maelezo kutoka Serikalini, kwa nini haikufikiria kupandisha Chuo cha Mtwara na wakakipandisha Chuo cha Chang'ombe Dar es Salaam ambako kuna kila aina za huduma za jamii?

(b) Siku za karibuni, Mkoa wa Mtwara na Lindi na sehemu ya Mkoa wa Pwani kule Mkuranga, kuna mambo yangendelea ambayo ni uchimbaji wa gesi na utafiti wa mafuta. Baadhi ya watu wanaofanya kazi hiyo yaani wataalam, hasa wale wenye Kada ta Kati kama *ma-welders* hulipwa hela nyingi kweli kweli na kuwaacha Watanzania wakiwa hawana ajira,

maana hawana *knowledge* ya kutosha kwenye sekta hii.

Je, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Wizara ya Nishati na Madini, haioni wakati sasa umefika wa kushirikiana kwa pamoja wakaanzisha taasisi au Chuo Kikuu kitakachokuwa kinashughulikia uhandisi wa nishati?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifauatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Chuo cha *TTC*, Mtwara kwamba kilibaki hakikupandishwa kuwa Chuo Kikuu na badala yake vikapandishwa Vyuo viwili vya Mkawa na Chang'ombe. Wataalam waliangalia vile vile na mazingira hasa ukubwa wa eneo.

Chuo cha Mtwara *capacity* yake ya kuchukua wanafunzi, ni wanafunzi 646 tu mpaka sasa na eneo la pale Mheshimiwa Mbunge nadhani analifahamu. Lakini hata hivyo, Mkoa wa Mtwara hata kama upo pembezoni kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, bado kuna Vyuo Vikuu vitatu; Chuo cha *Open University* wanafunzi wa Mtwara wanapata fadia kule na Chuo cha Stellamarys, Mtwara *University College* wanafunzi wanapata huduma ya *Degree* ya kwanza kule. Lakini vile vile watu wa *St. Augustine* tayari mwaka jana wamefungua Tawi la Chuo Kikuu kule

ambapo tayari wanafunzi wa Mtwara wanapata elimu ya Chuo Kikuu kule.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na amani kwamba kwa Mkoa ule kwa Vyuo vitatu hivyo vinatosha na hata hivyo, Vyuo Vikuu vyote nchini suala hili huwa nalisema kila siku kwamba ni vyuo ni vya Kitaifa. Hakuna mwanafunzi yeyote atakaebaki ambaye ye ye yuko Mtwara atakosa nafasi ya kwenda Chuo Kikuu kwa sababu eti Chuo cha Mtwara hakuna nafasi, atapata kwenye nafasi katika Vyuo vingine.

(b) Swali la pili, kwamba Serikali imefanya jitihada mpaka wameweza kugundua gesi kule na sisi ni faida kwa nchi yetu na ni historia tayari. Wizara ya Elimu na Wizara ya nishati na Madini tutakaa pamoja tushirikiane tuone kwamba tunaweza tukafanya kitu fulani kule juu ya uvumbuzi wa hiki kitu, tunaweza tukaanzisha chuo kwa ajili ya vijana wa kule. Haya ni masuala tu ya Serikali itakaa pamoja iweze kuona namna ya kulitatua. (*Makofî*)

Na. 171

Upungufu wa Walimu Manyovu

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Upungufu wa walimu katika Jimbo la Manyovu ni mkubwa sana.

(a) Je, Serikali italeta lini walimu wa kutosha katika Vijiji vya Wilaya Mpya ya Buhigwe?

(b) Je, Serikali inaweza kukubali zitengwe nafasi katika Vyuo vya Ualimu vya Kabanga na Kasulu ili kupunguza tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuna upungufu wa walimu katika baadhi ya shule hapa nchini zikiwemo shule za Wilaya mpya ya Buhigwe. Serikali kuitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inaendelea kulitatua tatizo hilo kwa kuajiri walimu wote wanaohitimu na kufaulu mafunzo ya Ualimu kutoka Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu vilivyopo. Aidha, Walimu hupangwa katika Halmashauri kulingana na mahitaji kila mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wilaya ya Kasulu ilipangiwa walimu wa Cheti 222, walimu wa Stashahada 73 na walimu wa Shahada 94. Kwa kuwa wakati huo Buhigwe ilikuwa sehemu ya Wilaya ya Kasulu, ilipata mgao wake kuitia Wilaya hiyo. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 Wilaya mpya ya Buhigwe pamoja na Wilaya

nyingine mpya, zitapewa mgao wa walimu waliohitimu kupitia Halmashauri husika. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya ualimu ni vyuo vya Kitaifa hivyo huchukua wanafunzi kutoka Halmashauri zote nchini. Aidha, wahitimu wa vyuo hivi hupangwa popote nchini kulingana na mahitaji.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kwanza nimpongeze Naibu Waziri, mwenyewe ulitembelea Mkoa wa Kigoma, ukajionea hali halisi ya elimu na ukachukua baadhi ya hatua, lakini upungufu wa walimu wewe mwenyewe uliuona, uliuthibitisha na kwenye majibu yako hapa unasema kabisa walimu upangwa katika Halmashauri, kulingana na mahitaji ya kila mwaka wa fedha.

(a) Je, ulipanga kwa mahitaji?

(b) Hali halisi ya Mkoa wetu wa Kigoma, uliona vijana wetu wengine wanafaulu kwa pointi 28 na wengi walikuwa wanategemea kwenda ualimu, sasa kwa mwaka huu nasikia mmesikia mmesema pointi 27.

Je, unatoa tamko gani kwa wale ambao wamefikisha pointi 28 na huku ualimu ilikuwa ni tatizo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na mafunzo ya Ufundi naomba kujibu maswali mawili

ya Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza kabisa napenda nipokee ahsante hiyo kwa kunipongeza, nilifika Dodoma, nilipita Kibondo na Kasulu mpaka Kigoma Mjini na nikayafanya yale ambayo niliyoyaona.

Lakini vile vile nilipata ripoti kwa Afisa Elimu wa Mkoa, juu ya upungufu wa walimu Mkoa wa Kigoma na hasa walimu wengi hawakuwa wameripoti karibuni asilimia 54.

Niliagiza walimu ambao hawajari poti Mkoa wa Kigoma waripoti mara moja, *otherwise* huko waliko tutawafutia na baada ya wiki mbili walimu walianza kumiminika kuripoti katika Mkoa wa Kigoma.

Lakini bado hilo si suluhisho Mheshimiwa Obama, wakati nikijibu swali wiki moja imepita hapa, nilitamka kwamba kwa Halmashauri zote na hasa Mikoa ya pembezoni huko Kigoma ambako walimu hawari poti, nimesema mwaka huu wakati tutakapokuwa tunapanga walimu, tupate orodha ya majina ya Halmashauri hizo walimu wanaotaka kufanya kazi katika Halmashauri za Kasulu, Kibondo, Kigoma na sehemu zingine ili tuweze kuwapanga kule ili wasipate tena tatizo la kuripoti.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu mwaka huu tumebadilisha ufaulu wa kujunga na vyuo vya walimu ni kweli kabisa, Serikali iliona kwamba pointi 28, ufaulu wake ni mdogo tupandishe angalau pointi

27. Lakini vile vile kwa mfano kama mwaka jana, tulikuwa na vijana waliokuwa wameomba vyuo vyua ualimu wa pointi 28, vijana 71,000 na mahitaji ya Serikali ilikuwa ni vijana 7500.

Kwa hiyo, hatukuona sababu ya kuendelea na pointi 28 kwa sababu tulikuwa tunaendelea kuwaacha vijana wengi wa pointi 25, 26 mpaka 27. Kwa hiyo, mwaka huu vile vile, wiki iliyopita nilitembelea Chuo cha Mpwapwa ambako tumewaweka watu pale wana-select majina haya, bado hata hivyo pointi 27 bado vijana ni wengi, karibuni vijana 42,000, lakini tunataka sisi vijana 6800 tu mwaka huu.

Kwa hiyo, bado Mheshimiwa usishangae hata kwamba hata mwaka kesho tukaweka ikawa pointi 26. Lakini kutokana na Waheshimiwa Wabunge mnapochangia michago hapa mnasema Kada ya Walimu tupeleke vijana waliofaulu ili wawe walimu wazuri, tuweze kupata elimu bora. (*Makof*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Najua Serikali imejizatiti kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu na kwa kiasi fulani imefanikiwa.

Lakini kuna changamoto ambayo inajitokeza; walimu wamekuwepo, wanashindwa kuripoti kwenye maeneo ya pembezoni kutokana na miundombinu mibovu, mazingira magumu ya kufundishia.

Je, katika mwaka huu wa fedha Serikali imejipangaje kuhakikisha inaanza kukabiliana na tatizo hilo ili walimu wasihame kwenye mazingira hayo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa hitimisho la Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, wiki iliyopita. Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge, Naibu Waziri *TAMISEMI*, anayeshughulikia masuala ya elimu, alijibu kwa ufasaha mzuri sana mipangilio ya Serikali, namna tulivyojipanga kuboresha miundombinu kwenye shule zetu za msingi na sekondari. Kwa sababu, swali hilo linahitaji kidogo takwimu, sikuwa na takwimu kamili hapa juu ya namna gani tutafanya, tutaweka miundombinu, ujenzi wa nyumba, usambazaji wa madawati na ununuvi wa vitabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana tunaposema mazingira magumu ya ufundishaji, ni pamoja na hizo fedha za rada, ambazo zilikuwa zinapigiza kelele. Mheshimiwa Waziri Mkuu, amehitimisha hoja hiyo kwamba, tutapeleka fedha hizo kununulia vitabu na madawati.

Lakini *hardship allowance* ambayo labda ilikuwa inatatiza hata mwaka jana tulikuwa tunajibu hapa kwamba, tunazo bilioni 22 ambazo wafadhili wetu walitupatia tuweze kufanya kama *Piloting System* kwa

ajili ya walimu, kuwagawia kitita cha bahasa ya 500,000/= kwa ajili ya mazingira magumu. Fedha hizo bado zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado Serikali, inaangalia kwamba, kule kwenye Halmashauri, hawapo walimu tu wanaoishi katika mazingira magumu, wapo wagani, watu wa kilimo, lakini vilevile wapo wauguzi, watu wa afya, na kadhalika.

Bado tunaendelea kuhangaika kwamba, tufanyeje zile fedha, namna ya kuboresha mazingira ya walimu na watumishi wengine kwenye Halmashauri. (*Makofi*)

Na. 172

Mahusiano ya Kibalozi Tanzania na Israel

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA aliuliza:-

Je, Serikali, ina mpango gani wa kuwa na Ubalozi wake nchini Israel na Israel kuwa na Ubalozi Tanzania, ikizingatia kwamba, Watanzania wengi huenda nchini humo kwa shughuli za kiroho?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba

kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na heshima kubwa ambayo imejengwa na Viongozi Wastaafu na walio madarakani, Tanzania ina uhusiano mzuri na nchi zote duniani. Kwa misingi hiyo, Tanzania ingependa kufungua Balozi katika nchi nyingi duniani, ili kuendelea kulinda maslahi yake. Hata hivyo, katika kuendeleza azma hii Serikali, imekumbana na changamoto kadhaa zikiwemo upungufu wa wafanyakazi pamoja na ufinyu wa Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, katika nchi ambazo Tanzania haina uwakilishi wa Balozi Mkazi, Serikali, imekuwa na uwakilishi wa Ubalozi Mdogo (*Consulate General*) au Balozi wa Heshima (*Honorare Consulate*). Utaratibu ambao pia hutumika kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina Mwakilishi wa Heshima, Bwana Caspian Nuriel Shirish, ambaye yupo MJini Telaviv. Moja ya kazi zinazofanywa na Mwakilishi huyu ni pamoja na kumsaidia Mtanzania yejote na wageni wengine watakaohitaji msaada wa Kibalozi kuhusu Tanzania, wakiwa nchini Israel. Tanzania, inawakilishwa nchini Israel na Balozi Mkazi wa Tanzania, aliyeko Cairo Misri, Balozi Mohamed Haji Hamza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini, Israel inawakilishwa na Balozi wake anayeishi Nairobi, Kenya.

Suala la wao Waisrael kufungua Ubalozi Tanzania, ni uamuzi wao ambao hatuwezi kuuingilia. (*Makofii*)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake ya kawaida. Lakini ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni vigezo gani vinatumika ili kuweza kupata Balozi Kamili au kupata Ubalozi wa Heshima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na lingine la pili. Ningependa kueleza kwamba, Israel ni nchi mashuhuri na nchi ya historia na ni ya kiroho. Nikinukuu katika Zakaria 14:17, inasema, "*Tena itakuwa ya kwamba, mtu awaye ye yeyote asiyekwea kwenda Jerusalem, ili kumuabudu Mfalme Bwana wa Majeshi, mvua haitanyesha kwao.*" Kwa hiyo, mimi ningependa kujua kwa nini kigezo hiki na kiko ki-Biblia, kisichukuliwe kupata Ubalozi kamili, ili sisi tujisikie vizuri?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli hiki kigezo cha kiroho hatukitumii katika kupeleka Mabalozi. Bahati mbaya au nzuri kwa sababu, tumeamua kwamba, nchi yetu haifuati dini yeyote, ni wananchi ndio wanafuata dini wanazotaka.

Lakini vigezo vya kupeleka Mabalozi, ni pamoja na mahusiano yetu na nchi husika na uwezo wetu kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama nilivyoeleza katika swalii la msingi kwamba, tuna uhusiano mzuri na nchi nyingi. Tusingeweza kupeleka Balozi katika nchi zote ambazo tuna mahusiano mazuri. Ndio maana tunachukua Balozi mmoja, ana-cover nchi nyingi ambazo zipo katika eneo hilo, ndio utaratibu ambaao unatumika. Kwa hiyo, ni kigezo hichohicho ambacho kimetufanya tusiwe na Balozi Mkazi Israel. Hata wao juu kwamba, tuna mahusiano mazuri, pia hawana Balozi Mkazi, Dar-es-Salaam au Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwa na Balozi, *Honorare Consul*. Ni pale ambapo hakuna Balozi Mkazi, ndio huwa tunakuwa na Balozi Mdogo au Balozi wa Heshima.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, niulize swalii dogo la nyongeza. Pamoja na majibu ya kawaida sana ya Naibu Waziri, lakini naomba pia niungane na Mheshimiwa Mbunge, aliyeuliza swalii la Msingi kwamba, Israel ni Taifa Teule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Taifa la Israel pamoja na kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba, nchi yetu sio ya Kidini na bado tunasikia masuala ya Mahakama za Kadhi, lakini vilevile tukumbuke kwamba, Israel ndilo Taifa

lililotuanzishia *JKT* na kutufundishia *JKT* na wana teknolojia ya juu sana. Sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri, labda angetuambia ni lini Ofisi za Kibalozi, zinaweza zikaanzishwa pale Telaviv, Israel? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa hatuna tarehe maalum ambayo tumepanga kufungua Ubalozi Israel.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza kwamba, Tanzania ina uhusiano mzuri na nchi zote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Unadhani Tanzania, ni moja ya nchi ambazo hazijatambua uwepo wa nchi ya Kosovo; unadhani Tanzania ina uhusiano mzuri na Kosovo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, hapo umeshahamisha kabisa swali. Mheshimiwa Naibu Waziri, kama unapenda kwa taaluma yako ndani ya Wizara, jibu, lakini vinginevyo ameshahamisha swali.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile umenipa *option* ya kujibu au kutokujibu; naomba nisijibu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, utalileta swali hilo kwa utaratibu ulio rasmi.

Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kimekwisha. Sasa naomba niwape matangazo. Tangazo la kwanza, naomba nitambue wageni waliopo hapa ndani ya Ukumbi wa Bunge, kwa siku hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa mwanzo kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema, huyu ni Mbunge wa Vunjo na Naibu Waziri Mkuu Mstaafu. Wageni hao, wa kwanza ni Jeremiah Shellukindo, ambaye ni Katibu Mkuu wa *TLP*, naomba asimame. Hawa wageni, wa pili ni Mkumbwa, Mweka Hazina wa *TLP*. Aah, wale, wako hapa, karibuni sana Viongozi wetu, nafikiri wamekaa hapo juu, wote tumewaona.

Tunashukuru sana pia, kwa jinsi mnavyompa ushirikiano Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema. Huyu, Mzee kwa kweli, alikuwa Kiongozi Mkubwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine walioko Bungeni, kwanza ni wanafunzi 150 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Makole, Dodoma. Ningeomba wasimame. Nashukuru Walimu wetu kwa kuwafundisha vijana wetu vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wapanda Baiskeli watatu (3), kutoka *Gerba Circling Club and Youth Training Centre*, wakiongozwa na Ndugu Said Kengele, kutoka Lindi. Huyu Bwana Kengele, sijui yuko wapi na hawa Wapanda Baiskeli? Karibuni sana. Naona haya ndio mambo ya Kusini, huko Lindi huko, yanajidhihirisha hapa. (*Makofi*)

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri wa *TAMISEMI*, ambaye ni Ndugu Mussa Shaban Ali, Afisa Elimu – Taaluma, Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro. Karibu sana Afisa Elimu – Taaluma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo sasa ya kazi. Tangazo la kwanza linatoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala, huyu ni Mheshimiwa Paul Lwanji. Anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala kwamba watakuwa na Kikao cha kamati hiyo leo tarehe 10 Julai, 2012, saa 7.00 Mchana, katika Ukumbi Namba 227. Katiba Sheria na Utawala.

Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo, wakutane leo tarehe 10, katika Kikao Maalum Kabisa cha Kamati, kuanzia saa 7.00 Mchana, Ukumbi wa Msekwa B. Kwa hiyo, Kamati hiyo ya Mambo ya Nje, wao watakutana Msekwa B.

Halafu, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, huyu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Mazingira. Yeye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Mazingira, kuwa tarehe 10 Julai, 2012 leo, watakuwa na Kikao cha Kamati, kitakachofanyika kuanzia saa 7.00 Mchana, katika Jengo la Utawala, Ukumbi Namba 231. Kwa hiyo, Mazingira wao watakuwa 231.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo jingine hapa. Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), linawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, watumishi wa Shirika hilo wako hapa Bungeni, nyuma ya Jengo la Utawala kwenye Banda lao, kwa ajili ya kutoa maelezo mbalimbali kuhusu nyumba na huduma zao. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa kupata huduma mbalimbali za Shirika hilo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tutembelee pale nyuma ya Jengo la Utawala, tukutane na wenzetu hawa wa *NHC*.

Sasa nimepewa hapa tangazo jingine, kutoka kwa Mheshimiwa Faida Bakari, ambaye ni Katibu wa Mchezo wa Ngoma ya Kibati. Kwamba, niwatangazie Wajumbe wa Kamati Tendaji, kutakuwa na Mkutano leo saa 7.00 ili kupanga mazoezi ya ngoma hiyo. Sasa, huu ni mchezo mpya sana Bungeni, lakini naona nao umeanzishwa.

Sasa Wajumbe wa Kamati hiyo, wanaotakiwa kukutana hiyo saa 7.00 ni Mheshimiwa Tauhida Galus, ambaye ndio Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti ni

Mheshimiwa Rukia Kassim, Katibu ni Mheshimiwa Faida Bakari.

Halafu Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Asha Omar, Mheshimiwa Harubu Shamsi, Mheshimiwa Mariamu Msabaha, Mheshimiwa Muhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Ester Matiko, halafu Mheshimiwa Warida Bakari, Mheshimiwa Rita Kabati, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Sadifa. Kwa hiyo, sasa huo mchezo mpya. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, hilo ni tangazo nililoletewa kwa hiyo, timu hiyo nayo inatakiwa kukutana, kwa ajili ya kuanza mazoezi. Maonesho itakuwa lini? Nadhani, watapangiwa na ratiba za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo. Katibu tuendelee na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Wizara ya Maji

(*Majadiliano yanaendelea*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja ilioanza kujadiliwa kutoka jana. Ni mjadala kuhusu Bunge, kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya

Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Hivyo basi, majadiliano ya makadirio hayo, yanaendelea kwa kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge, woto michango yao.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Vicent Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Danstan Kitandula. Mheshimiwa Vicent Nyerere?

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi napata tabu kidogo, labda Wazee watanisaidia, nashindwa kujua hivi *CCM* hii ndio ilikuwa *TANU* au hii ni nyingine? Ninasema hivyo kwa sababu, wakati wa vuguvugu la uhuru, Wazee wa *TANU* walisema wamemtoa Mkoloni, sio kwa sababu ya rangi ni kwa sababu, Wakoloni walishindwa kutoa huduma za msingi, ikiwemo maji. Sasa *CCM* hii imeshindwa kuleta maji nadhani wangekaa wakatafakari, wana umuhimu gani wa kuendelea kuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua Waziri wa Maji ni mgeni katika Wizara na Naibu wake, lakini hakuna simba mgeni porini. Nimesikitika kidogo Ukurasa wa saba (7), aya ya 17, kwa ridhaa yako naomba kunukuu: "Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada kila mwaka Wizara yangu hufanya ukaguzi wa hesabu za mwaka (*Audited Annual Financial Statement*) kulingana na viwango vyatya ukaguzi vyatya kimataifa. Kwa mwaka 2010/2011 Wizara imefanikiwa kupata Hati Safi (*Qualified Opinion*), kufuatia ukaguzi wa hesabu uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali."

"Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu, kwamba Wizara yangu imepata Hati Safi kwa miaka 4 mfululizo kuanzia mwaka 2007/2008. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Watumishi wa Wizara yangu kwa kazi hii nzuri na kuwataka waendelee kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Matumizi ya Fedha za Umma." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawataki Hati Safi, wanataka Maji Safi. Sijui hawa waliomwandikia Waziri, wameongea na wananchi kwamba, wanataka mfululizo wa Hati Safi? Maji sio safi, Wabunge wote, hakuna hata Mmbunge mmoja anayeweza akasimama akasema kwake kuna maji safi na salama, yanayopatikana muda wote na kwa gherama nafuu, hakuna. Wote wanalilia maji. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisingizio sio fedha. Tarehe 13 Februari, 2007, walianza mchakato na wakakopa fedha Benki ya Dunia, 591 milioni, kwa ajili ya Mradi wa maji. Leo wananchi bado wanalia maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina uhakika hata kwako, watu hawana maji. Nilikuwa ninaomba Wabunge wote bila kujali itikadi zao, sijui kuna sababu gani ya kuendelea kuunga mkono Bajeti hii ya Wizara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa ninayoiona hapa ni usimamizi. Fedha zinakopwa, fedha zipo wala sio Bajeti kidogo. Kuna watu baada ya kugundua

fedha zimekopwa Benki ya Dunia, wakaanzisha Kampuni za Uchimbaji wa Maji, kwa sababu, sio kazi yao visima vilivyokuwa vinahitajika kuchimbwa zaidi ya mita 120, wamechimba mita 30 wameacha, wanasema hakuna maji. Shida kubwa ilikuwa ni kupata tu fedha hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tumekopa. Deni la Taifa linaongezeka, fedha za maskini. Leo tunawaachia wazungu mliowafukuza, dhamana ya kutuletea maji. Ukiangalia miradi yote ni ya ufadhili.

Fedha zetu za ndani zinakwenda kwenye matumizi ya ofisi, ununuzi wa magari; maji mnasubiri wananchi wetu waletewe na Wafadhili, ni aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mzuri sana wa maji kutoka Ziwa Viktoria, Ihelele. Huwa nashindwa kufikiria *target* ya mradi ule ilikuwa ni nini? Kuna vijiji vingi katikati, ambapo mabomba yanapita havina maji. Ni vijiji vichache tu vina maji baada ya shinikizo la Wanavijiji kuanza kutobia mabomba. Maji yanakwenda moja kwa moja Mgodini, wanachajiwu watu wa Mgodi, mita moja ya ujazo wa maji kwa 700/=.

Lakini wale Wanakijiji ambao ni wazalishaji, walipa kodi, wanachajiwu ndoo moja ni 100/= mpaka afikie mita moja ya ujazo wa maji, analipa 2,500=/. Nashindwa kuelewa, mradi huu ulikuwa ni kwa ajili, ya

wawekezaji wa migodi au ni kwa ajili ya Watanzania?
(Makofi)

Uwezo wa mtambo ule, kuzalisha maji ni mkubwa sana lakini unatumika asilimia 38 bado tunahitaji maji yafike Dodoma, yafike Singida na maeneo mengine. Hayafiki sijui ni kwa sababu gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka za maji mijini bado pia ni shida mimi nadhani Waziri sasa hivi aangalie, kuna mamlaka ambazo zimepewa daraja A. Kwa mfano Shinyanga, Tabora na Musoma hawastahili kuwa daraja A. Mimi nadhani wangewateremsha wawasaidie kwa sababu gharama ambazo wanawawekea wananchi kwenye kulipa bili za mwezi ni kubwa sana, hawawezi tena kujiendesha kibashara ukizingatia baadhi ya majeshi kama polisi magereza, aidha hawalipi au wanachelewa sana kulipa maji. Gharama zinakwenda kwa raia wa kawaida. Kwa hiyo nilikuwa nadhani, Waziri akae na Waziri wa fedha waangalie namna gani ya kuhakikisha mamlaka hizi za majeshi yanalipa, gharama za maji kwa sababu hawawezi kukatiwa wanakwenda kupewa raia wa kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa tu na ahadi hewa mimi nikiingia hapa swali langu la kwanza lilikuwa maji katika mji wa Bukoba na Musoma, nikaambiwa tarehe 15 Mei, 2011, mradi wa maji unaofadhiliwa na wafaransa wa *AFD* utaanza mpaka leo hakuna kilichofanyika isipokuwa juzi Naibu Waziri aliniambia kwamba mradi wako uko tayari, lakini tayari kwa maneno siyo kwa vitendo kwamba utaanza.

Ahadi ya Serikali ilikuwa ni kukabidhiwa mradi ule Desemba 2013, lakini mpaka sasa haujafanyika sijui watatumia nini kuhakikisha Desemba, 2013 tunapata maji.

Ndugu zangu wa *EWURA* pia wangekaa waangalie mamlaka hizi, maji wanatoa kwa kukadiria, bili zinakuja bila mita mtu anapewa *flat rate* analipa maji anayepata maji na asiyepata maji. Kwa mfano mimi pale kwangu watu wa Wizara wanapita kuangalia kama una ujenzi bili inapanda kwa hiyo wanatoa bili za maji kwa kukadiria tu. Nilikuwa namuomba Waziri katika majumisho yake aende akaulize watangulizi wake, dola 591, milioni zilizokopwa katika Benki ya dunia kwa ajili ya kusaidia maji zimefanya kazi gani. Kwa sababu Wabunge wote wanalilia maji hapa. Nimekwenda katika vijiji ambavyo bomba la maji ya lhele yanapita huku wanalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifikia muda watu wanatoboa bomba la maji ili wapate maji, maji yanatoka Mwanza yanakwenda Kahama Mgodini wakati kuna wanavijiji wanakosa maji. Kama kweli Serikali ina nia ya kupunguza gharama za matumizi katika Wizara nyingine waangalie kwenye maji. Tulikwenda kukagua hesabu za mkoa wa Shinyanga tukakuta wameteketeza madawa ya shilingi milioni 20 tukawa na wasiwasi kidogo kwanini madawa haya yameteketezwa jibu likaja kwamba tumeteketeza madawa kwa sababu hazitumiki magonjwa ya milipuko hayapo tena.

Kwa hiyo, kama tutawapa wananchi wetu maji tutapunguza sana gharama za matibabu kwa watu wetu, Wizara ya Fedha inaweza kuwa na fedha kidogo kwa sababu umuhimu wa kununua madawa mengi haupo. Ufaulu wa shule za vijiji vile vijiji vinavyopata maji japo kwa bei ghali, ulipanda kutoka asilimia 38 mpaka asilimia 41 ndani ya mwaka mmoja.

Kwa sababu muda ambao wanafunzi walikuwa wanautumia kwenda kutafuta maji sasa wanautumia kukaa darasani. Muda ambao walikuwa wanakwenda hospitali kutibiwa magonjwa ya tumbo haupo tena muda mwingi wanakuwa darasani.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani kama Serikali inataka kweli kupunguza gharama za matumizi mengine waangalie sana namna gani ya kuongeza uzalishaji wa maji safi na salama na namna ya kuwafikishia wananchi hawa maji. Kwa mfano maji mmekwenda kuwapa wawekezaji kwa shilingi 700 kwa *cubic meter* moja halafu mwananchi wa kijiji anayaafuata maji mbali kwa punda analipa kwa *cubic meter* moja shilingi 2500.

Mimi nadhani ni vizuri sasa mkaa chini mkaangalia namna gani nani wa kuangalia kwanza aidha mgodi au wananchi. Nchi hii ni ya Watanzania siyo ya wawekezaji, tuwafikirie Watanzania kwanza wapate maji safi na maji salama hapo tutakuwa tumefikisha lengo la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.
(*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Vincent Nyerere kama nilivyosema sasa atafuatia Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Moza Abedi Saidy.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kuwapa pole vijana wangu wa Kata ya Daluni, ambapo juzi walipata ajali walipokuwa wakienda kwenye michezo kule Kata ya Mwakijembe. Wapo kwenye sala zangu namwomba Mwenyezi Mungu aweze kuwapa uponyaji wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2012 dunia ilishangilia kufikiwa kwa malengo ya millenia ya upatikanaji wa maji kwa wanadamu. Taarifa ya umoja wa mataifa mashirika yake mawili *WHO*, na *UNICEF* inaonyesha tumefikia asilimia 89 ya upatikanaji wa maji duniani. Lakini wakati dunia ikishangilia mambo haya hali iko tofauti sana kwetu Watanzania. (*Makof*)

Tumeachwa nyuma, sisi si mionganini mwa wale wanaoshangilia mafanikio haya. Maana Tanzania imekuwa nchi ya 168 kwa upatikanaji wa maji kati ya nchi 179. Upatikanaji wetu wa maji ni asilimia 53 kwa mujibu wa ripoti ile ya umoja wa Mataifa. Lakini wakati dunia ikifikia asilimia 89 sisi ni asilimia 53 jambo hili halikubaliki hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha Watanzania kuhusu kupatikana kwa maji kinasikika kila kona ya nchi

yetu, kwa miaka hamsini sasa Watanzania wamesubiri kupata maji wanasubiri kwa sababu wanaamini tunasikia kilio chao. Wameendelea kuwa wavumilivu hata pale walipougu magonjwa ya tumbo, kuhara damu, kipindu pindu; wamesubiri. (*Makofi*)

Wamesubiri kwa sababu tumewaambia tuna mkakati kabambe wa kuwapatia maji kuitia mradi wa Maji wa vijiji kumi, wanaendelea kutusubiri.

Wimbo huu wa maji kwa vijiji kumi tangu mwaka 2007 unasikika, tumeshuhudia washauri waelekezi wakichaguliwa tathimini zikifanyika utafutaji wa maji ukifanyika. Tumeshuhudia wananchi wakishawishiwa kuchangia miradi hii na kwa mwamko mkubwa wakachangia kati ya asilimia 2.5 mpaka asilimia tano lakini kwa bahati mbaya sana utekelezaji wa miradi hii unakwenda kwa *speed* ya kinyonga (ndogo sana). Sisi wa Mkinga tumechoshwa na wimbo huu. (*Makofi*)

Wananchi wangu wa Mwakijembe, Mbuta, Kilulu Dunga, Bwaga Macho, Bamba Mwarongo, Parungu Kasera na Mapatano wamechoshwa na wimbo huu wanataka maji. Kwanini tumechoshwa kwa sababu katika zile Halmashauri 62 ambazo tumeambiwa zimetimiza vigezo vyote, Mkinga ni mojawapo lakini pamoja na kutimiza vigezo hivyo leo hii ninapozungumza ni kijiji kimoja tu cha Daluni ndiyo kimeanza utekelezaji huo *this can not be right at all*. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake nitaomba anipe maelezo ya kina kwa mwaka huu ni vijiji vingapi vya Mkinga vitapata maji. (*Makofi*)

Nasema haya kwa sababu tumepata nyaraka kutoka Wizarani kwake zikionesha kwamba mpaka mwaka 2014 mwezi Juni, *sealing* yetu ni milioni 322, lakini wakati huo huo nimeangalia hotuba yake inaonyesha pale tuna milioni 105 na vijiji nane havina maji. Tunaomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitangaza wilaya ya Mkinga kuwa na hadhi ya wilaya mwaka 2005, mwaka 2007 Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ikaanzishwa tuliposikia haya tukashangalia tukajua tutapiga hatua ya haraka ya maendeleo. Tukateua muda wa Kasera uwe Makao yetu Makuu ya Wilaya. Mji mpya unahitaji kujengwa tukapata changamoto kwamba hatuna maji, tukabuni mradi pale wa kutoa maji kutoka Kinyatu kwenda kwenye mji wa Kasela Makao Mkuu ya Wilaya, tukaambiwa mradi ule utatekelezwa kwa programu ya maji safi na maji taka mijini.

Mchakato wa kupata zabuni ukaanza mwaka 2010 mwezi Desemba ukakamiliwa mwaka 2011 mwezi Januari. Sisi tukafanya kazi ya kuwapata hawa watu, tukakamilisha makabrasha yale mwezi Mei mwaka 2011 mpaka leo zaidi ya mwaka sasa hakuna *feedback* yoyote kutoka Wizarani. (Makofi)

Makao Makuu ya Wilaya hayana maji hayajengeki, nataka Prof. Maghembe apige picha ya pale Mwanga aone mji ule hauna maji aone mji ule ungejengeka kwa namna gani. Mheshimiwa Waziri

atakapohitimisha hotuba yake tunaomba jibu katika hili. (*Makofi*)

Mwaka jana 2011 nilisema hapa kwamba watu wa Kata ya Bwiti, kwenye vijiji vya Magati Loko Mavovo Mwanyumba na Kiumbo wamefikia sasa wanashikiana mapanga kwa kugombea maji. Mradi ule ulianzishwa mwaka 1979 sasa unahudumia watu wengi kuliko ulivyokuwa umebuniwa tuhahitaji milioni 150 ili kupanua chanzo cha maji ili kukidhi mahitaji. Niliyasema haya mwaka jana 2011 Wizara ikasema imesikia mpaka leo hakuna lilitotekelezwa. Mheshimiwa Waziri utakaposimama kuhitimisha naomba majibu ya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti yetu ya maji kwa mwaka huu ni bilioni 485 ongezeko la bilioni 39.8 kwa Bajeti ya mwaka jana. Lakini katika hizo bilioni 39.8 ni bilioni 19.6 zinazokwenda kwenye maendeleo. Hivi kweli tuna nia ya dhati ya kutatua tatizo hilo la maji kwa Watanzania. Tuna nia ya dhati ya kuondoa vifo vinavyotokana na kipindupindu bila sababu ya msingi kwa Watanzania. Wananchi wa Kuze, Churwa, Mhinduro, Bamba Mavengero wanataka majibu lini Serikali yao itawapatla maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nasubiri majibu.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Kitandula nilisema nitamwita Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, naona hayupo. Kwa hali hiyo nitamwita

Mheshimiwa Felister Bura, atafuatiwa na Rose Kamili.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na nimshukuru Mungu wangu kwa kunipa uhai kusema katika Bunge lako hili Tukufu. Maji ni uhai kwa viumbe vyote, kwa binadamu kwa wanyama, kwa mimea, na katika Tanzania yetu kuna mikoa wana bahari, wana maziwa, ziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika na maziwa mengine makubwa tu.

Lakini sisi katika mkoa wa Dodoma hatuna bahari, wala hatuna maziwa wala hatuna mito mikubwa na Mungu sisemi kwamba ametuonea lakini mvua zinanyesha katika mkoa wa Dodoma kwa miezi miwili tu. Kwa hiyo, ukosefu wa maji ni mkubwa sana. Wanyama wanahangaika wanadamu wanahangaika, mimea inahangaika kwa kukosa maji.

Lakini pia Serikali hatutendei haki sana kwa sababu mabwawa tuliyonayo ni madogo ni machache hayatoshelezi. Pia wanawake wanapoteza muda mwingi sana na wengine akina mama wajawazito wengine wana nyonyesha kwa kutafuta maji mwendo mrefu sana. Tuliambiwa kuna mradi wa Maji vijiji kumi katika maeneo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisikitike kusema kwamba mradi wa Maji vijiji kumi katika Mkoa wa Dodoma haujafanikiwa, haujafanikiwa kabisa na nikueleze kwamba makampuni yale yanayofanya survey katika maeneo yetu sijui kama wanalinganisha

Mkoa wa Dodoma na maeneo kama ya lleje, kama kwako kule Peramiho, kama Mbanga, kama Iringa, kama maeneo yenyeye mvua nyingi, kwa sababu kila wanakopita wanapata lakini maji wale wachimbaji. Pia hawachimbi inavyostahili, wale ma-survey kwanza wanalipwa pesa na Serikali hata kabla hawajamaliza kazi. Kazi hawajakamilisha lakini wameshalipwa pesa.

Je, wasipofanikiwa wanafanyaje? Ninakuomba Ndugu yangu Prof. Mheshimiwa Maghembe makampuni yale yanayo survey wanapokosa maji katika maeneo ya vijiji unawafanyaje, Serikali inawafanyaje, wanatakiwa kurudia au wanatakiwa kuondoa na pesa zetu sisi walipa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkoa wa Dodoma maji yako chini sana kuanzia mita 150 na kuendelea lakini hao wachimbaji wanaoletwa wanachimba mita 70 na 80 wakishakosa maji hawarudi na wala hawatafuti maeneo mengine. Tunaonewa na sidhani kama kampuni hizi zinazopewa kazi katika mkoa wetu ni watu wanaolewa hali halisi ya mkoa wetu, ukame uliopo na maji yanapatikana kutoka mita ngapi. Wengi wanachimba mita 80 na wakishachimba wanaondoka hatuwaoni tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wanafunzi wetu hawasomi vizuri, wanasomaje vizuri wakati hajafua nguo? Anasomaje vizuri wakati hana maji na hakula chakula nyumbani. Mama kaondoka saa 12 kwenda kutafuta maji! Zahanati zetu hazina maji na hata shule hazina maji. (*Makofi*)

Naiomba Serikali yetu Tukufu ijikite sana katika suala la kutafuta maji na upatikanaji wa maji katika vijiji vyetu na yapatikane kabla ya uchaguzi ujao wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano halisi kwamba katika Wilaya ya Kongwa kuna kijiji cha Mlali, wananchi walichanga shilingi milioni 12 tangu mwaka 2008 lakini mpaka leo hawajapata maji na namwonea huruma sana Mheshimiwa Ndugai kwa sababu wananchi wale wanataka warudishiwe shilingi zao milioni 12 wagawane kwa sababu hawajaona maji na kila siku kaka yangu Ndugai anahangaika kufuatilia mradi wa maji Mlali na maeneo mengine, wananchi wanamsumbuwanataka fedha zao. Lakini siyo Mlali tu, bali ni maeneo mengi wanataka pesa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *World Bank* au Benki ya Dunia haujatusaidia sisi wananchi wa Dodoma. Wilaya ya Mpwapwa, mradi wa maji wa vijiji 10 walichimba kisima kijiji cha Kisima barabara ya kwenda Iringa na wakapata maji yaani maji yapo, lakini baada ya kupata maji wakapotea. Sasa sijui mradi kama huo Serikali inasema kwamba umefanikiwa? Sijui kama wanahesabu kwamba wamefanikiwa au hawajafanikiwa. Lakini walipochimba maji katika kijiji cha Kisima, maji yalikuwepo mpaka leo hawajaonekana. Kijiji cha Chinyanghuku pia walichimba wakapata maji, kijiji cha Makose pia walichimba wakapata maji lakini baada ya kupata maji hawajaonekana, wananchi wawaeleweje? Je, vijiji hivi vinahesabika kwamba vimepata maji au havijapata maji? Tunaomba majibu

na wananchi wa Mpwapwa wanaomba majibu. Kuna mradi wa maji wa Chunyu, wamechimba, wakapata maji, wakaondoka, hakuna cha miundombinu wala kinachofoata wala nini, tunaomba majibu Mheshimiwa Waziri. Kijiji cha Iwondo, kabisa hawajaonekana lakini ni kati ya vijiji 10 vya Wilaya ya Mpwapwa lakini hawajaonekana mpaka leo. Kijiji cha Kimagai wamechimba, wamepata maji lakini baada ya hapo wakaondoka zao na walisema wakitoka Kimagai wanakwenda Berege, lakini Berege hawajafika na ni kilomita kama 30, lakini hawajafika kijiji cha Begere. Kijiji cha Berege bado wanasubiri maji ya *World Bank*, wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Bahi wanatumia maji ya Mission, Mjini Bahi, Makao Makuu ya Wilaya wanatumia maji ya *Mission* na siku yule Padri atakapokasirika Wilaya ya Bahi Mjini hawatapata maji. Mwaka wa fedha uliopita tuliomba shilingi bilioni sita na milioni mia tano, zikaletwa na shilingi 1,600,000,000/= yaani 26% tu na mpaka leo Bahi maji hayajapatikana. Mwaka huu tumeomba shilingi 1,500,000,000/= sijui kama tutazipata kwa ajili ya usambazaji. Vijiji kama Zanka, Mindola, Ilindi na Nondwa ni kati ya vijiji 10, hakuna mradi wowote unaoendelea. Katika Wilaya ya Dodoma Mjini, Manispaa ni vijiji vinne kati ya vijiji kumi. Nimeangalia kitabu kutoka Wizara ya Maji taarifa zile sijui wamepata wapi, sisi tunaokaa na wananchi na tunaozunguka vijijini taarifa hii siyo ya kweli kwamba vijiji saba ndani ya Manispaa wamepata maji si kweli na ni vijiji vinne tu vilivyopo kwenye mradi wa maji yaani kijiji cha Ng'ong'ona, Ntyuka, Mkonde na Chididimo lakini hakuna kinachoendelea katika

maeneo hayo. Tuliambiwa kwamba Mhandisi Mshauri angekuja lakini hatujamuona huyo Mhandisi Mshauri na mwaka wa fedha umekwisha, tunasubiri mwaka huu sijui mtatuambia nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kondoa kuna maporomoko ya Ntomoko na miundombinu ya maporomoko haya kila mwaka tumeyazungumza tangu Bunge liliopita, Mheshimiwa Nkamia amelizungumza sana, Mheshimiwa Zabein Mhita amelizungumza sana na maporomoko haya hu-serve vijiji 17 katika Wilaya ya Kondoa. Tuliiomba Serikali Kuu kwamba Halmashauri hawana fedha za kuhudumia miundombinu katika maporomoko haya. Tulisema kwamba Serikali itusaidie basi ili watutengenezee miundombinu ya maporomoko ya Ntomoko ili vijiji 17 viweze kupata maji lakini hatujapata majibu. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri utakapomalizia hotuba yako, utuambie maana tuliomba Serikali Kuu ihudumie miundombinu lakini hatujapata majibu, tunangoja majibu kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji kuvuja katika maeneo ya mijini, mimi Kamati ninayoitumikia tunashughulika na Mamlaka za Maji. Maji yanavuja sana kwa 35% au 40% na maeneo mengine mpaka 50%. Naiomba Serikali yetu itengeneza miundombinu ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili!

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Felister Bura ahsante na sasa nitamwita Mheshimiwa Rose Kamili Sukum na Mheshimiwa Innocent Kalogeris na Mheshimiwa Selemani Nchambi.

MHE. ROSE KAMILI SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji pamoja na kwamba sisi ni Kamati ya Maji pia lakini kuna maeneo ambayo hatuna budi na sisi pia kuyachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri naomba mimi nielekee kwenye suala la visima kumi zaidi kwa sababu inawagusa sanasana wananchi vijijini. Serikali imeelekeza sana nguvu labda kwenye miji na hasa Dar es Salaam ili waweze kupata maji, lakini kwa upande wa vijijini wamejaribu kujisahau na mimi nawaomba sana kwa kweli sasa tumuone Waziri wa Maji unakwenda kukagua vijiji kumi kwenye kila Halmashauri wewe mwenyewe, tukuone kwenye picha na utupe taarifa halisi kwa sababu hii ya kuelezwa kwenye makaratasi mimi nadhani inakudanganya kwa kiwango kikubwa na unaona wazi kabisa kwamba kila Mbunge akisimama anazungumzia suala la maji vijijini. Sasa kila wakati unatupiwa hilo donge, sasa nyanyuka mwenyewe nenda kahakikishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina uhakika Mkaguzi wetu alitoa taarifa ya hivyo vijiji kumikumi kwenye Halmashauri zetu kwamba kuna tatizo, lakini majibu

yenye kamilii hatuyapati kwa sababu kwenye hotuba yako pia imeonyesha wazi kabisa kwamba umechukua taarifa ya mwaka jana ukai-*paste* na kuileta bila marekebisho kwa sababu mwaka jana tulizungumzia suala la vijiji kumi kwamba haukutekelezwa vizuri. Hata mimi nilizungumzia suala la Hanang kwamba visima vilivyo chimbwa Hanang ni kumi na vitano havina maji na vitano vina maji lakini kwenye kitabu chako umerudia kosa lilelile la mwaka jana kwamba vimechimbwa visima 15 na visima nane vina maji. Kwa hiyo, una tatizo Waziri wewe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufanuzi, katika mifuko ya maji ya vijiji 10 inatuchanganya katika Halmashauri zetu kwa sababu sisi tunahudhuria hivyo vikao kama Wajumbe wa Halmashauri. Huu Mfuko wa Program ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini fedha zake sisi Wabunge tungejua ni kiasi gani cha pesa zilizokwenda kwenye Halmashauri hizo. Pia kuna kitu kingine kinaitwa ukarabati wa miradi midogomidogo yenyе kuleta matokeo ya haraka yaani *Quick Win*, huo ni mfuko gani tena mwingine? Tunapenda kuufahamu na ilikwenda fedha kiasi gani kwenye mfuko wa *Quick Win*? Mfuko mwingine ni ule wa pamoja yaani *Water Sector Basket Fund*, huu mfuko pia ni upi? Huu wa Benki ya Dunia ndiyo huo mfuko wa pamoja? Ndiyo fedha zilizokwenda kwenye hiyo miradi ya maji ya vijiji 10? Maana tunashindwa kuelewa, hiyo yote utakuta inaingilianaingiliana katika taarifa. Naomba sana hilo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Waziri kutupatia hiyo taarifa wakati ana-*windup*, pia tungependa kufahamu kwamba mwaka 2011/2012 zilikwenda shilingi 47,025,481,007/= na mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni 51.9 kwenye hiyo miradi ya vijijini. Cha kushangaza, fedha hizo kwenye Wilaya ya Hanang mwaka 2011 haikuingia hata shilingi, kwa taarifa! Lakini kwa huku upande mwingine inasema kwamba fedha zilizopelekwa mwaka huu 2012 kwenye Wilaya zote au Halmashauri zote ni shilingi 1,149,645,466/= lakini ukienda kwenye mchanganuo wake Halmashauri ya Hanang imepata shilingi milioni tano. Mimi nadhani kuna tatizo, kama kweli tumetenga hizo fedha ziende, inakuwaje kweli ifike shilingi milioni tano kwenye Halmashauri? Je, tutaweza kutekeleza ile miradi na wakati imesema kwamba kazi yake ni kwenda kutekeleza miradi hiyo, miradi haitekelezeki, haiishi na wananchi wamebaki kutazama visima vilivyochimbwa na kufunikwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda kujua pia kama fedha mmepeleka na zimekaa hapa katikati tuambiwe na tupewe taarifa katika ile bajeti mlipyopeleka mmesema hiyo fedha shilingi bilioni 1,152 zimekwenda mwaka 2012? Sasa zimekwenda kwenye Wilaya zipi? Si ajabu hata Wabunge wengine hawajui kama kuna fedha zimechezwa hapa katikati kwa sababu katika utekelezaji inaeleza wazi kabisa kwamba zikafanye kazi ya kukamilisha, ya kumalizia, ya kusimamia na ya kutoa elimu. Mimi naomba sana tuelewe hilo suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vijiji 10 mimi nilililamikia sana wakati uliopita na hata swalii niliuliza nikajibowi hovyohovyo. Inaelekea basi huu mradi ni wa watu fulani kwenye Wizara, kama TAMISEMI haihusiki hapa katikati basi Wizara ya Maji mnahusika kwa asilimia mia kwa sababu hamkufuatilia hilo. Kwa nini washauri kama ni wabovu wasichukuliwe hatua mpaka leo? Kwa nini vijiji hivyo ambavyo vimekosa maji, ni kwa nini kama washauri walikuwa wamelipwa wasikatwe fedha ambazo wamelipwa na wakati mlisema wachaguliwe washauri wazuri, wakafanya kazi na washauri haohao tena mwaka huu mnasema watoe matangazo, wafanye usanifu na kadhalika, ni usanifu upi wa pili kwenye vijiji 10 ambavyo maji yameshachimbwa kama siyo kutumia fedha hovyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la kulalamikia kwenye Wizara ni kwamba tulisema vijiji 10 vichimbwe na vikachimbwa lakini leo tena Wizara hii inasema kila Halmashauri ichague visima vitatu katika vijiji vyao, kwa nini iwe vitatu na kwa nini isiwe kumi vyote? Kwa nini hizo fedha ambazo zimepatikana mwaka huu zisigawanywe kwenye vijiji vyote 10 ili mradi kila mtu aonje. Je, vile saba vilivyobaki vitatengenezwa lini? Huo ni uonevu. Kwa hiyo, Wizara iangalie kwamba sasa mmefika mahali labda hizo fedha ni mradi wa mtu fulani katika Wizara hiyo au kama ni zawadi isemekane ni zawadi na kama siyo zawadi basi tuelezwe wazi, kwa nini mpunguze na mfanye visima vitatuvitatu kwenye kila Halmashauri, kwa nini vyote visitekelezwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuzungumzia kwenye Wizara ya Maji ni suala la usafi wa

maji au upimaji wa maji. Watanzania wengi wanakunywa maji machafu, wale wote ambao tunatumia mabwawa au tunatumia maji ya Ziwa au malambo basi yale maji si safi na salama, lakini tukiwatuma wataalam kwenda kupima hayo maji, majibu yao wanasema ni maji safi na salama kwa kutumia wanadamu, ni kweli? Kwa nini wafanye hivyo? Natoa mfano wa Ziwa Basutu, Basutu tulisema maji yale yanatoka kwenye makorongo au mito mbalimbali wakati wa mvua, maji yale yanaletwa mpaka kwenye Ziwa Basutu kwa matumizi ya wanadamu, lakini wakulima wa kule wanalima ngano ambayo inapigwa dawa, ndege wanaopatikana kwenye maeneo yale kama Kweleakwelea, wanakuja kupiga dawa ya sumu kuwaua Kweleakwelea wale na wale Kweleakwelea wanapatikana kwenye miti ambayo maeneo mengine kunakuwa na madimbwi. Leo yale maji yamekwenda kupimwa na wenzetu wa Bonde la Kati wanasema ni safi na salama. Tunapenda kujua hivi kweli upimaji ule ni halali? Watu wa Basutu watapataje unafuu wa kwenda kupimiwa maji yale wajue kwamba ni safi na salama ili waendelee kuyatumia isije ikawaathiri kwenye afya zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuiambia Wizara na Serikali kwa ujumla, kwamba fedha za maji sasa zifikiriwe kwa sababu imefika mahali hatustahili sisi wanadamu tunahangaika kuchota maji kilomita 100 au 20 au kilomita 30 na wengine hawajui maji kabisa. Kweli kama Serikali hii ina upendo na mnapenda wanadamu waweze kufanya kazi basi ifikiriwe kwanza maji, iwe kipaumbele kuliko shughuli nyingine zote kwa sababu

hata viwanda vinatumia maji. Leo akina mama wanakwenda kilomita 20 kuchota maji, kule kwetu ni kukame, hakuna maji ya kutosha, kwa hiyo inabidi watu waende kwenye vyanzo vya maji ambavyo vipo mbali na wao. Serikali ifikirie kuongeza fedha na itafute mahali popote ili tuweze kupata maji vijiji na siyo kuelekeza mijini zaidi, mijini ni sawa tunahitaji kwa ajili ya *population* na watu wanahitaji maji mengi kwa ajili ya viwanda na kadhalika, lakini vijiji pia tunateseka na tunapigika, kwa hiyo tunahitaji maji safi na salama katika viji vyote katika Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inapanga mipango ya muda mrefu na mpango wa kati, lakini kwa nini mnashindwa kutekeleza hiyo mipango wakati mmetengeneza wenyewe? Leo tunatoa ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili hiyo!

MHE. ROSE KAMILI SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru sana kwa kunipa fursa hii lakini siungi mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rose Sukum kwa ushauri na mchango wako na sasa nitamwita Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamesimama hapa wamezungumza kwa uchungu na wote tunatambua kwamba maji ni uhai na maji ni kila kitu. Mimi tu kitu ambacho nimekigundua ni kwamba hapa tatizo ni mfumo. Kaka yangu Prof. Maghembe ni mgeni katika Wizara hii na ndugu yangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Mahenge naye ni mgeni katika Wizara hii, kwa hiyo mna kila sababu ya kujipanga upya na kuangalia tunafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Ndugu yangu Keissy alisema kwamba ikiwezekana wote tupinge hoja ambayo ipo mbele yetu lakini katika staili tunayokwenda nayo hatu tukipinga tutafika mahali tutashindwa. Mimi ombi langu ambalo ni suluhisho la yote, Mheshimiwa Waziri, sasa ni wakati muafaka wewe na Naibu wako na watendaji tutoke katika mfumo ambao tunao hivi sasa katika kuendesha au kuwatumikia wananchi katika Wizara ya Maji. Zamani tulikuwa na mfumo wa *Ma-Regional Water Engineer* ambao ukiangalia mfumo huo ulikuwa unaweza kufanya wananchi wakapata haki zao za kupata huduma ya maji ipasavyo. Tuangalie mfumo ambao sasa hivi upo katika Wizara ya Ujenzi, kuna *Ma-Regional Manager* wa *TANROAD* Tanzania nzima. Uwepo wa *Ma-Regional Manager* wa *TANROAD* Tanzania nzima unasababisha Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kuweza kutoa kero zao kwa karibu na Serikali kushughulikia. Mimi nadhani sasa wakati umefika,

Mheshimiwa Waziri tafadhali turudishie Ma-*Regional Water Engineer*, Wahandisi wa Maji wa Mikoa watakaoshughulikia maeneo yote katika Mikoa yetu tofauti. Sasa hivi haya masuala ya Mamlaka za Maji zinashughulikia mjini tu, hazishughulikii vijijini na ndiyo maana hapa unaona Waheshimiwa Wabunge wananyanya kwa wanapiga kelele sana. Mamlaka za Maji ya Morogoro Mjini kuna kazi inafanyika, DAWASA tunaona kuna kazi inafanyika, Dodoma mjini pia kuna kazi inafanyika, Mbeya na Mwanza na ndiyo maana unaona kuna miradi mikubwa katika maeneo hayo. Mimi nakuomba sasa wakati umefika, tafadhali, turudishie ile *system* ya zamani ya kuwa na Ma-*Regional Water Engineer* ambao tutakabana koo kulekule kwenye Mikoa yetu, wao ndiyo watakaokuwa wanakuletea nini tatizo la Mkoa wa Morogoro, nini tatizo la Wilaya ya Morogoro Vijijini, tofauti na ilivyo hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni vijiji Kumi (10). Tatizo hili liko palepale, hakuna *communication* kati ya Halmashauri na Wizara na ndiyo maana mradi huu umesuasua. Wahandisi wa maji wa Halmashauri zetu wapo kama majina, hawana chochote cha kuweza kudai kwenye Wizara ambacho kitasaidia katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba, tafadhali aturejeshee Ma-*Regional Water Engineers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu, mimi wananchi wangu wa Wilaya ya Morogoro Vijijini wamenituma, Mama Nkya jana amesema, leo na mimi nasema kwamba, Halmashauri yetu ni mionganini mwa

Halmashauri ambazo bado hazijafanikiwa kupata mradi huu na tatizo kubwa ni hilihili kwamba, hakuna *communication*, Wahandisi wakija wakikutana na Watendaji wa Wizara kuna kubabaishanababaishana *end of the day* tunashindwa kupata huduma. Sasa walichonitura ni kitu kimoja kwamba, tunataka maji. Hili siyo ombi, ni agizo na Serikali inatakiwa ilitekeleze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapataje maji kwa sasa? Tunajua huyo Mhandisi Mshauri sijui atapatikana, hakupatikana au kapatikana mwaka kesho kutwa, mpangieni fedha za kumlipa kwa mwakani. Sasa hivi katika Halmashauri yetu tunazo shilingi milioni 498 ambazo ziko tayari kwa ajili ya kumlipa Mhandisi Mshauri. Fedha hiyo ina zaidi ya miaka mitatu (3) ipo tu. Kwa hiyo, tunaomba katika bajeti ya mwaka huu mturuhusu, tuliomba kama Halmashauri shilingi milioni 450 kwa ajili ya kuchimba visima vya maji ili wananchi wapate maji safi na salama kama llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inavyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wakati Mheshimiwa Waziri ana-*windup* atupe ruhusa ya kutumia fedha hizi. Waziri akitupa ruhusa ya kutumia fedha hizi, mimi nitapitisha bajeti, lakini akininyima tafadhali nitakamata shilingi yake, kwa sababu hili ni suala la kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji Kidunda. Mkoa wa Morogoro una miradi mingi lakini Wilaya ya Morogoro Vijijini hakuna mradi wowote ambao tayari Wizara imeishauanza lakini hapo inasikitisha, tuna mradi

wa maji wa bwawa la Kidunda ambao unatamkwa kuwasaidia au kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam na Pwani wanapata maji safi na salama ya uhakika. Mradi huu unatoka katika Mkoa wa Morogoro. Nilitarajia kwamba, wakati Mheshimiwa Waziri ana- *present* hotuba yake akatamka sasa kwamba, Wilaya ya Morogoro Vijijini ni sehemu ya mradi huu. Bwawa linatoka Wilaya ya Morogoro Vijiji; Kata za Serembala, Kidunda, eneo ambalo tunatarajia kujenga Makao Makuu ya Wilaya, Mvuha hakuna mahali walipooneshwa, tunahitaji maji na sisi kule. Kwa hiyo, kwangu nataka niseme kwamba nitapitisha bajeti hii kama Mheshimiwa Waziri atatamka kwamba mradi wa Kidunda ni sehemu ya mradi ambao Wizara imeipa Wilaya ya Morogoro Vijijini kwa kushirikiana na Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nzungumze suala ambalo katika mradi wa Kidunda Halmashauri yetu imeshapeleka kwenye dawati la DAWASA, suala la kupata fedha kwa ajili ya kutengeneza miundombinu, lakini pia kujenga majengo ya huduma za kijamii kama shule, zahanati, nyumba za ibada ili wananchi wote watakapokuwa wamepata fidia stahiki waelekee huko. Nadhani ni vizuri sasa katika bajeti hii nihakikishiwe kwamba, tunapata lini fedha hizo ili Halmashauri iandae makazi na wananchi hawa wakilipwa haki stahili waende huko na kukuta huduma zote za msingi zipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile Mheshimiwa Waziri aeleze nini hatma katika ujenzi huu wa Bwawa la Kidunda. Kuna wananchi

wameshafanyiwa tathmini, lakini kuna wengine ambao hawajafanyiwa tathmini, lini tathmini hiyo itafanyika ili wakati wenzao wanalipwa haki stahiki na wao walipwe ili waondoke kwa pamoja na waache mradi ujengwe? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika ujenzi huu wa bwawa la Kidunda mradi utagharimu shilingi bilioni 156, fedha ambayo naamini iko katika fedha za ndani na nje na hizo za nje naamini tutakuwa tumekopa, niiombe Wizara wakati Mheshimiwa ana-*windup* anieleze Wizara tumejipangaje katika kukabiliana na wingi wa mifugo ambayo ipo katika eneo la mradi? Wizara pia imejipangaje kukabiliana na uharibifu wa mazingira ambao unatokana na uvamizi wa wafugaji holela? Kwa sababu ninaamini kwamba tunaweza tukapeleka fedha ya mradi huu kama Wizara haikujipanga ipasavyo, yaliyotokea Mtera yatatokea katika ujenzi wa bwawa hili, ambapo tunacheza na mifugo ambayo inasababisha uharibifu wa mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vyta mto vitakavyofanya bwawa hili liweze kuwa na maji ya kutosha ni mto Ruvu ambao unatokea katika kata ya Tawa lakini vilevile mto Mgeta Kafa au Mape ambao unatokea katika Kata ya Kisaki. Wafugaji wameshavamia na vyanzo vyote hivyo vitakwama ndani ya kipindi kifupi. Je, Serikali imejipangaje kwa sababu kama haijajipanga ni vizuri fedha hii ikafanya shughuli nyingine za maendeleo badala ya kwenda kujenga bwawa ambalo ndani ya miaka mitatu au mitano litajaa tope na tutakuwa tumeleteza fedha ya

walala hoi huku tukiendelea kulipa madeni ambayo hayana sababu katika taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nikuombe tu, Mheshimiwa mwenzangu jana alizungumza zaidi, naomba leo nisije nikagongewa kengele, nasubiri haya katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri na kwa kweli nataka nimhakikishie kwamba, akinipitishia haya na mimi nitaunga mkono hoja, akikataa siungi mkono hoja, nitang'ang'ania shilingi yake na nitakwenda nayo nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniskiliza. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mungu wa Mbingu na Nchi kwa kuniwezesha leo kuongelea suala zito na nyeti kwa wananchi wa Jimbo la Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri na Wabunge wenzangu umuhimu wa maji. Sisi binadamu tunapozaliwa mama anakabidhiwa mtoto wake baada ya kuwa amesafishwa vizuri, anapewa na kuanza kumnyonyesha. Lakini hapohapo tunapokufa kabla ya kuingia kaburini kuna utaratibu wa kuoshwa kwa kutumia maji. Nilitaka niliweke sawa hili ili tuone umuhimu wa maji ni kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, suala la maji ni tatizo kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Kishapu. Tunao mradi wa maji ya Ziwa

Victoria, nimesema sana na sasa namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, ili tuwe salama na mimi nisiinuke na nikacharuka na hoja binafsi kuhusu maji wakati ana-*windup* michango ya Wabunge anipe tarehe ni lini maji ya Ziwa Victoria yatakwenda Kata ya Songwa, Mwadui Luhumbo, Uchunga mpaka Makao Makuu ya Jimbo la Kishapu, Mji Mdogo wa Muhuze. Hilo ni muhimu sana, naomba hiyo *note* aipokee na hiyo *Hansard* nitakapomaliza kuongea apelekewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili tuna mabwawa makubwa matatu katika Kata ya Songwa. Tuna mabwawa ya Songwa, Mumbu na Mwadui. Nashangaa leo wanasema uhai wa mabwawa ni miaka 10 mpaka 20. Williamson Diamond alichimba haya mabwawa wakati wa uhuru, leo tunaongelea takribani miaka 48 mabwawa yale hayajaja tope, yana maji na hatujaona tatizo lolote lilitotokea. Sasa haya mabwawa yanayochimbwa leo tatizo ni *ten percent* ama nini? Naomba nipate majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo imekuwa ni tafsiri tu kwamba, miaka 20 tu mabwawa yamejaa, miaka 10 mabwawa yamejaa, mbona Williamson toka amechimba leo ni miaka 48 alitumia utaalamu gani, ama aliletu malaika kutoka Mbinguni wakachimba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kwamba, umetokea utaratibu wa taasisi fulani ya kudhibiti mabwawa na maji. Wananchi wanayazunguka yale mabwawa, ni akina mama kama wewe Mwenyekiti, wanayaafuata maji kwa ndoo kutoka nyumbani kwao umbali wa takribani mita 100. Nimesema sana

wanawake na akina dada zetu wa Kishapu wengi sasa wameota vipara kwa sababu ya kubeba ndoo za maji vichwani. Migongo yao sasa, uti wa mgongo ni kuuma tu, viuno vinauma kwa sababu kwa utaratibu na utamaduni wetu sisi Wasukuma mwanaume haendi kuteka maji, anayeenda ni mwanamke. Kwa hiyo, naomba sana yale mabwawa yako matatu, hata watu wa mgodi walioyachimba leo wamedhibitiwa, wanatumia kwa *limit*, wananchi wanaozunguka mabwawa yale hawatumii maji, mradi hauhitaji zaidi ya shilingi bilioni mbili, tutayapeleka Songwa, Mwadui Luhumbo, Kata ya Mondo, Kata ya Seke, Kata ya Bubiki mpaka Bunambiu lakini kumetokea utaratibu, tunasubiri wafadhili, *World Bank*, je, sisi hatuna akili? Mwalimu alituletea uhuru sasa tunajitawala, kwa nini tunashindwa kuhudumia wananchi wetu? Mimi nasema Mheshimiwa Waziri lile la Victoria, Kata ya Songwa aliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya visima. Nimezunguka vijiji 114 vya Jimbo la Kishapu, nimetembelea visima lakini sijaona kisima hata kimoja kirefu. Nimeona visima vilivyochimbwa virefu katika kijiji cha Iboja, nimeona kisima Mwigumbi, lakini leo ni mwaka mzima, vile visima vimewekewa mabomba kisha vimefunkwa na kopo, wananchi hawapati maji. Fedha zililetwa, miradi ile imechimbwa lakini visima vimefunkwa makopo. Nakuomba kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge utembelee visima vyote, mabwawa yote ili uone dhiki wanayoipata wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna fedha zilizotengwa za Mwamashimba shilingi milioni 703. Nataka niwatahadharishe wenzangu wa Halmashauri ya Kishapu, fedha zile zifanye kazi kwa ajili ya bwawa lililokusudiwa. Mradi wa kusambaza maji Mwigumbi fedha zipo takribani ni miezi minane leo, lakini hakuna kazi inayofanyika. Waziri huna faili ofisini, nenda *field*, nenda *site* ukaangalie mambo yanavyoendelea. Nawaomba sana, Mheshimiwa Rais amewachagua kwa nia njema, na ukiangalie umetoka Kilimo, umeletwa hapa, tunaimani na Rais kwamba, ameamini pale una-*fit* lakini kama mambo hayatakwenda sawa, mimi nitakuwa mstari wa mbele kuhakikisha tunapambana ili wananchi wa Jimbo la Kishapu wapate maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bwawa la Sekeididi, shilingi milioni 370, mkandarasi ameweuka magari mawili, amepewa fedha leo ni miaka minne (4) hayupo. Nilikuwa na Mbunge mmoja wa ajabuajabu sana Mpendazoe, hakusimamia kabisa. Miradi imechakachuliwa, leo amekimbia ameenda kambi nyiningine, wacha akajifiche huko, sisi CCM tuko makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema ni kwamba, Mheshimiwa Waziri aende Sekeididi, fedha zimeliwa, mkandarasi ameacha magari mawili pale, leo ni miaka minne. Ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu aniambie ni lini anakwenda Kishapu ili twende naye shati kaptura tunatembelea miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la maji Shinyanga MJINI. Maji ya Ziwa Victoria, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetumia shilingi bilioni 260 kuyapeleka Kahama na Shinyanga, lakini sasa kilichotokea ile siyo huduma ni biashara. KASHUWASA gharama zake za kuyaleta maji yale Old Shinyanga ni shilingi 263, yeze anamuuzia tena SHUWASA shilingi 450, SHUWASA anamuuzia mwananchi shilingi 750, huu utaratibu wa Serikali kufanya biashara umeanza lini? Kwa nini maji yale, taasisi moja isivunjwe ili wananchi wayanunue maji yale kwa shilingi 300 ama 350? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaratibu wa ajira KASHUWASA kundi la watu 20 linaweka bei ya shilingi 463, juu yake shilingi 200/= gharama ile inaenda kumwangukia mwananchi wa Shinyanga MJINI, mimi sikubaliani na hilo! Ndugu zangu nawaomba msisubiri Nguvu ya Umma itumike, angalieni, Rais ni muungwana, mpenda watu na Serikali yake, Chama cha Mapinduzi kwenye llani tulisema tutaleta maji ya Ziwa Victoria lakini nyie sasa mnashindwa kusimamia, kilio cha wananchi maji shilingi 750, migodi mnawauzia shilingi 700/=, sijui mnasema bei ya jumla, wakati bei ya jumla tunaipata 2010 - 2015 kwa kupigiwa kura sisi. Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba vunja kitengo kimoja SHUWASA au KASHUWASA ili wananchi wahudumiwe na kupata maji yale kwa bei nafuu, isiwe ni biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea sana na Mheshimiwa Masele, yuko ziara na ameniomba nilisemee hili. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa

Waziri atembelee Jimbo la Shinyanga Mjini kwa tatizo hilo la kuvunja hako kataasisi kamoja, kundi la watu wachache linalowakandamiza wananchi wa Mji wa Shinyanga. Lakini pia Mheshimiwa Waziri aweke mkakati, gharama za uendeshaji maji yale ni shilingi milioni 70, Wizara inapeleka shilingi milioni 300 wakati wale wanatakiwa wajienteshe na wakati huohuo waendelee kusambaza maji, sasa gharama wanayoipata kila mwezi inajitosheleza kulipa gharama za uendeshaji. Serikali haioni umuhimu wa kulipia gharama za uendeshaji ili bili wanayoipata waendelee kusambaza maji kwenye kaya nyingi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri sasa kama utaona huwezi kufika, unda Tume ya Wabunge wachache twende tukatembelee miradi hii, tukaone *site*, tuna matatizo makubwa sana. Kata ya Kiloreli watu waliahidiwa bwawa, wananchi wakahamasika, wakachanga shilingi milioni 16 mpaka leo hakuna kinachoendelea. Kata za Taraga na Itirima zina vyanzo vikubwa vya maji. Mwaka 1978 CARE walitathmini bwawa kubwa sana lakini baadaye tukaambiwa litakuwa mazalia ya mbu. Kwa hiyo, mbu wakaonekana ni wa maana, mradi ukaondoka, sisi Wasukuma tukabaki hivyohivyo. Mimi nawaomba sana katika mambo ambayo ni muhimu kwa maisha ya wanadamu, lakini tatizo hili la maji linaonekana kuchukua sura kila sehemu, kila Jimbo kuna tatizo la maji, afya, elimu, nawaomba sana mfike Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja endapo Mheshimiwa Waziri atajibu hoja zangu. (*Makofii*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wenzangu wote wameelezea umuhimu wa maji na hakuna yeyote miongoni mwetu anayeweza kubisha kwamba tuna tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafikiri kuna tatizo la msingi na ni lazima tulikubali kwamba, kuna haja ya kufanya operesheni maalum ya kukabiliana na tatizo la maji. Katika kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa wa 104 ameemelezea Mikoa ya Mwanza na Mara, idadi ya visima viliwyochimbwa ni 177, waliopata maji ni 45, 750. Sasa ukichukua Mikoa ya Mwanza na Mara, *population* yao si chini ya watu milioni nane au tisa, lakini vijiji viliwyopo pale, vijiji vyote vya Tanzania sasa hivi vinafikia 12,000 sasa kwa utaratibu huu wa vijiji 177 kwenye *population* ya watu milioni nane au tisa, ni dhahiri kwamba, hakuna wakati wowote ambapo Watanzania watakuwa na uhakika wa kupata maji salama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, la kwanza la kufanya badala ya kuzungumzia jumlajumla, tungeweza kuainisha ni miradi gani mikubwa ambayo itahakikisha idadi kubwa ya Watanzania wanapata maji. Tuainishe hilo kwanza, halafu tuainishe ni vijiji vingapi kwa ujumla kabisa katika vijiji vyote vya Tanzania tunaweza tukawekeza na tukaweza kupata maji, tukafanya operesheni hiyo. Hii tunayoandika ya vijiji 177 kwa *population* ya watu 45,000 wakati tunazaliana kwa asilimia 2.3, ni dhahiri kwamba, tutafikia hatua hata Dunia itamalizika lakini wananchi

hawataweza kupata maji. Inahitaji tufanye operesheni maalum ili kuhakikisha Watanzania wanapata maji. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kawaida hizi fedha nyingi tunazokopa na misada tunayopata si chini ya asilimia thelathini mpaka arobaini (30% - 40%) zinakwenda kwenye *consultancies*, ni asilimia sitini (60%) tu au pengine chini ya hapo ndiyo inakuja kwenye utekelezaji wenyewe. Hivi ni kweli kwa Tanzania tulipofikia hivi sasa tunahitaji kutafuta wataalam wa kutuwezesha kujua kwamba hapa tuna maji au hatuna maji? Hatuwezi kuiokoa hii asilimia 30 au 40 na tukaitumia katika uwekezaji wa maji? Mimi nafikiri hili nalo lazima lifanyike, kama halikufanyika, watu watatumia fedha hizo watakuja likizo na wakirudi hakuna chochote kinachofanyika. Kwa taarifa yenu, sisi tuna *information* zaidi kuliko wataalam tunaoletewa. Tuna tabia tu ya kudharau wataalam wetu wa hapa ndani, lakini wataalam wanaokuja kutoka nje wengine wamemaliza *degree* mwaka mmoja au miwili, wanaletwa hapa, *information* zote wanategemea kuzipata kutoka kwa Watanzania wenyewe. Tufike wakati tuthamini wataalamu wetu, tutumie taaluma zetu, tutumie hii rasilimali ya asilimia 30, 40 wanayoichukua kwenye *consultancies*, tuitumie sisi wenyewe. Hilo lilikuwa ni jambo langu la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri ameelezea vyanzo vya maji, rasilimali za maji lakini amesahau kuzungumzia rasilimali ya maji iliyoko kwenye *air*. Kwenye *air* kuna

maji mengi sana na wenzetu Waisrael wamevumbua hizi *water web making machines*, Wachina sasa wanazalisha kwa wingi, ukienda Latin America ziko nyingi sana na ni dola 12000 zinakupa lita 32 kwa saa moja, una-*plucking*, unapata maji lita 32 kwa saa moja, ni maji masafi kuliko haya tunayokunywa ya chupa. Kwa bahati nzuri hapa Tanzania kuna baadhi ya watu wamezileta. Nilifikiria hizi zingeweza kutatua matatizo na zina uwezo wa kuzalisha mpaka lita 5000 kwa saa 24. Mwaka jana na mwaka juzi nimelizungumza ndani ya Bunge. Waziri akaahidi atalifanyia utafiti ili tuweze kuona ni vipi tunaweza kutumia mashine hizi tukatatua matatizo ya msingi kwenye shule, zahanati, taasisi mbalimbali, vyuo vikuu na kadhalika, lakini limeachwa hivihivi na hii ni teknolojia rahisi, haina gharama yoyote, inawezekana ikafanyika, tukapunguza matatizo haya ya maji ambayo tunayazungumza hivi sasa. Sasa Serikali inapoahidi ni vizuri ikafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ambalo Serikali haijalifanya ni suala la uvunaji wa maji ya mvua. Tunazungumzia uvunaji wa maji kwa kujenga mabwawa. Tumejenga nyumba nyingi hapa Dodoma lakini nenda kaangalie ni nyumba ngapi zimejengwa ili tuweze kuvuna maji ya mvua. Nilitembelea Wizara ya Kilimo hapa Dodoma wameweza kuweka tanki la maji kwa kuvuna maji ya mvua, wana lita 50,000 pale chini ya ardhi. Hebu fungeni safari tu tukatembelee hapo mkaone kiasi gani maji ya mvua yamewekwa pale, ni maji ya kutosha, maji mazuri kabisa. Nyumba ngapi tumejenga leo zina utaratibu huu wa kuvuna maji? Ukienda pale Maldive asilimia 70 ya maji yao wanategemea maji ya mvua ya kuvuna kwenye

majumba. Sisi tunajenga nyumba bado hatujaunganisha namna gani tunaweza kutumia nyumba ileile tukaweza angalau kupata maji ndani yake. Hili nalo lazima tulifanyie kazi, tuondokane na matatizo haya ya maji. Maji yale ni safi kuliko maji wanayokunywa watu ya kwenye mabwawa na yakiweza kupatiwa dawa kidogo ndio yanakuwa safi zaidi na wala hayana matatizo yoyote. Nafikiri nalo hili Serikali limezungumzwa kinadharia, kuna haja ya kulifanyia kazi na ndiyo maana bado tunajenga majumba lakini hakuna nyumba ambayo imeweeka utaratibu wa kuweza kuvuna maji ya mvua na mvua tunazipata, haidhuru wakati mwengine zinakuwa chache lakini bado zinapatikana. Nafikiri nalo hilo tungeweza kulifanya likasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tano ni suala zima la *Private Sector Involvement* katika *Water Production*, nafikiri nalo katika sera zetu bado halijakuwa *clear*, tumeliweka katika umeme lakini katika sekta ya maji bado *Private Sector Involvement* haipo. Tuna wasiwasi labda huduma hii inaweza kuwa ghali, lakini hivi ughali ni upi, kukosa au kupata huduma? Maana leo tumeweka *EWURA* wanasema lita moja shilingi moja, lakini ukienda pale mtu anauza shilingi 20 au 30 naye ananunuliwa, kwa sababu ya shida ya maji. Kwa hivyo, nafikiri *Private Sector Involvement* katika suala zima la uzalishaji wa maji bado halijatiliwa mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la sita, tunayo programu ya uzalishaji wa umeme vijiini. Sasa hivi kuna teknolojia wakitumia mipira ya matairi ya magari, ukipata tani moja na nusu mpaka mbili unapata kilowati 500 za

umeme. Ukitaka hiyo teknolojia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini nitakupatia wakati wowote na Waziri wa Maji pia nitakupatia. Sasa ukiunganisha hii sekta ya maji na uzalishaji wa umeme vijijini, ukachukua na hizi mashine ninazokwambia sasa hivi, *water maker machines*, tatizo la maji na umeme vijijini umelimaliza. Kazi yako ni kuunganisha tu kutoka huu umeme unaozalishwa kidogokidogo ukaunganishwa kwenye gridi. Kazi ya kuweka *transmission line* ni *very expensive* na ndiyo maana *TANESCO* wamefika mahali wamekwama katika kusambaza umeme. Kwa hiyo, tukiweza kutumia sayansi hii, nina hakika matatizo haya ya umeme tunaweza tukayakabili vizuri, matatizo ya maji tunaweza kuyakabili vizuri maana haya mambo ni mtambuka, nyumba, umeme, maji ni mtambuka, ukiyaunganisha kwa pamoja utakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la saba ambalo naona ni muhimu, hatujalizungumzia sana ni suala zima la (*catchments areas*) za maji, vyanzo vyetu vyaa maji tumeviharibu sana. Kwa mara ya kwanza nimesikitika sana hata kule Pemba kuna vile vilimavilima vyote, mikarafuu imekatwa tunajenga nyumba. Nilikwenda North Korea nikakuta wao kwenye milima wanajitahidi sana kupanda miti, sisii sasa hivi unakuta watu wengi wanajenga kwenye milima kumbe kuwa na mti mdogo kwenye mlima ni rahisi sana kuweza kupata mvua kwa uharaka zaidi kuliko mti kuwa chini. Mbali na zile *catchments areas* lakini kwenye vilima sasa hivi tuhakikishe kwa kweli tunapanda miti kwa wingi sana. Ndiyo *area* ambayo inaweza kutusaidia kupata maji kwa wingi na mvua za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi nenda Dar es Salaam utakuta vilima vyote vimejengwa. Watu wana-*enjoy* kwenda kule wanakimbia mbu, lakini kwa kweli tunakosa mvua, tunakosa hali ya hewa nzuri, tunakosa mambo mengi sana. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itilie mkazo suala hili na iliweke katika mpango kwamba kwa kweli mbali na kuzungumzia *catchments areas* lakini kwenye vilima ndiko *source* kubwa ya maji inakotoka. Mlima wa Kilimanjaro unatoa maji, leo mlima wa Kilimanjaro ikiwa nao hauna miti, maji yatakuwa hayapo vilevile. Kwa hiyo, nafikiri kazi kubwa ya kufanya ni ku-*concentrate* namna gani tunavilinda hivi vilima vyetu, watu wasilime kwenye vilima, wapande miti kwa wingi kwenye vilima, tutakuta hali ya mazingira ya maji yatakuwa yamebadilika kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namalizia kwa kuzungumzia suala la usimamizi. Lipo tatizo kubwa sana la usimamizi, nawaonea huruma sana Mawaziri hapa tunapowabana sana, pengine hizi *appointing authorities* hasa tuziangalie vizuri zaidi. Inawezekana kabisa Mawaziri wanajitahidi lakini huko chini *bureaucracy* nayo ina mambo yake inafanya. Naomba sana tuwape *chance* Mawaziri hawa wakaangalie namna gani tunaweza kuboresha miundombinu ya utendaji ili *accountability* iwe kwa Halmashauri, *Municipalities* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa uzoefu wako na ushauri ambao umeutoa katika sekta hiyo ya maji.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitamwita sasa Dkt. Festus Limbu atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, niwapongeze sana Mawaziri kwa kuteuliwa; Mheshimiwa Prof. Maghembe pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mahenge, nawapongeza lakini pia nawapa pole. Nawapa pole kwa sababu kilio cha maji ni tatizo kubwa nchi nzima kama ambavyo Wabunge na wananchi wanashuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mambo ya ujumla. Matatizo tunayo mengi na makubwa katika sekta mbalimbali lakini tumekuwa tukisema kasungura kadogo. Mimi sikubaliani kwamba kasungura kadogo kwa nchi kama ya kwetu, kasungura ni kakubwa na wala sio kasungura tena mimi naweza nikasema ni tembo. Rasillimali tunazo nyingi, fedha tunazo, hatujajipanga vizuri. Kwa hali ya sasa ilivyo, napendekteza mwisho wa bajeti ambapo tutakuja kwenye *Finance Bill*, Waziri wa Fedha tutakuja kupendekteza ili tukate kwenye *OC* tupeleke fedha kwenye maeneo ya maji. Sisemi Magu peke yake, lakini pia kwenye maeneo mengine ambapo kuna tatizo kubwa, tupunguze *OC* asilimia fulani ambayo

tutapendekeza tukubaliane iende kwenye kutatua kero ya maji, hayo ni mambo ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye matatizo ya Jimbo, kuna tatizo sugu la maji katika mji wa Magu. Mji wa Magu miundombinu na mitandao ile ilitengenezwa miaka 30 iliyopita kwa ajili ya wakazi 6,000 wa vijiji vya Kipeja, Sagani, Ilungu na Magu yenye. Sasa hivi kuna wakazi 35,000 zaidi ya mara saba ya uwezo wa mtandao wa maji uliopo. Hadi sasa hakuna uwekezaji ambao umefanyika, uwekezaji kwa maana ya kukidhi mahitaji ya wakazi waliopo hivi sasa. Miaka miwili iliyopita ilifanyika tathmini yaani (*feasibility study*) katika mji wa Magu na ikaja na gharama ya shilingi bilioni 25 kwamba mradi ule ungetekelezwa kwa shilingi bilioni 25, lakini huyu mtaalamu aliyefanya hii *feasibility study* alitumia shilingi milioni 900. Wakati Naibu Waziri wa Maji anajibu swali la Mheshimiwa Ndassa Ijumaa iliyopita, kuhusu tatizo la maji Magu na Ngudu alijibiwa kwamba sasa kuna *feasibility study* nyingine inafanyika itakayounganisha Magu, Ngudu na vijiji vingine pamoja na Sumve na kadhalika, sina tatizo la hilo lakini maadam *feasibility study* ya Magu imeshafanyika na gharama zinajulikana, kwa nini isianzwe kutekelezwa hii ya Magu wakati *feasibility study* ya kwenda Ngudu, Sumve, Nyambiti na kwingine inaendelea kufanyika? Mimi sioni na haliingii akilini kwangu sasa unaahirisha mradi mzima. Kero ya muda mrefu ya Magu na Mheshimiwa Rais alikuja pale akasema kwamba matatizo ya maji Magu msimwuliza Mbunge niulizeni mimi. Hiyo ni ahadi ya Rais. Mimi naomba mradi huu uenze kutekelezwa na mapendekezo yangu ya kuhamisha *OC* inawezekana

kwa kuwa Waziri wa Fedha ana uwezo huo ili fedha hizi ziweze kupelekwa kwenye miradi ikiwemo ile ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi. Ahadi ziko nyingi alizotoa na hazijatekelezwa ikiwemo hii ya Magu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mji wa Magu haiwaingii akilini Serikali inapanga kupeleka maji ya Ziwa Victoria Nzega, Tabora na Singida wakati Magu pale hakuna maji. Watu wanasema eti watu wa Magu wataenda kuchota maji Ziwani kwa sababu ni karibu. Ziwani utakwenda kuchota maji, kwanza yana kichocco halafu ni mbali, kuna mamba wengi wanazaliana mle. Watu wengi wameliwa na mamba halafu unasema sisi watu wa Magu kwa sababu tuko karibu tutakwenda kuchota Ziwani. Watu wa Magu haiwaingii akilini mwao na mimi hainiingii akilini mwangu na napata taabu sana kuunga mkono hoja hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Magu wamenituma kwamba kama mwaka 2015 hakuna maji mimi sipati kura. Sasa na mimi kwa sababu bado nataka niendelee kuwa Mbunge, kwa kweli itaniwia vigumu sana Mheshimiwa Mwenyekiti kuunga mkono hoja kwa sababu Ubunge bado nautaka na mwaka 2015 dalili za kupata maji hazionekani. Kwa hiyo, wananchi wamesema mpaka kieleweke Mheshimiwa Mbunge wetu ukomae na Profesa Maghembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la pili kubwa katika Jimbo la Magu. Kuna Hifadhi ya Msitu wa Sayaka. Msitu huu unajumuisha vijiji nane (8) kutoka Wilaya ya Magu na vijiji viwili (2) kutoka Wilaya ya

Busega. Vijiji hivyo ni Kitongo, Mwabulenga, Bugatu, Salama, Sayaka, Lubugu, Bubinza na Itumbili kwa Magu na Mwagindi na Mwamkala kwa Busega. Sasa kuna Hifadhi hii ya Sayaka ilipitishwa kwa *Forest Declaration Order Cap.389* ya mwaka 1996, miaka 16 iliyopita. Juzi ilitangazwa kwamba mwisho wa kukaa au kufanya shughuli ambazo zimezuiliwa ilikuwa jana tarehe 9 Julai, 2012, wasifanye shughuli zozote pale na kwenye msitu ule, sio msitu tu peke yake, kuna mto ambao unapita katikati ya msitu ule na ndio uhai kwa wananchi wa vijiji hivi nilivyovitaja, wanachota maji mle ya kunywa hasa wakati wa kiangazi. Hivi sasa karibu vijiji vyote hivi havina maji na hawa wananchi wana mifugo ambayo hunywesha kwenye mto ule. Ungekuwa msitu peke yake, tungekuwa hatuna matatizo lakini kuna mto ambao ndio uhai wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa *Engineer Ndikilo* na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mheshimiwa Mabiti, walipokuwa hapa Bungeni, mimi na Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Dkt. Kamani tulikaa nao, tukazungumza hii hali ikoje na wananchi wanasema kwamba mkitufukuza tu hivi, mkatuzuia, tutakufa na sisi hatukubali kufa kwa kukosa maji. Tutakubali tufe kwa kupigwa au kwa kuondolewa na Polisi. Sasa naomba nitahadharishe kwamba kuna tatizo kubwa lisipokuwa *handled properly* na sina tatizo kabisa na nia nzuri ya Serikali kuhifadhi msitu, ni suala zuri kama alivyosema Mheshimiwa Mohamed. Msitu ule, pamoja na mto unazuia uchafuzi wa Ziwa Victoria, kwamba lile pori linakuwa kama *filter*, kama sponji ya

kuchuja uchafu usiingie kwenye Ziwa Victoria kwa faida ya Wakenya, Waganda na wanaokula sangara za kutoka Ziwa Victoria, lakini pia ni mazalia ya samaki ule mto. Sawa sikatai, hilo ni jambo jema, lakini hawa wananchi sasa unawafukuza? Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa hii miwili tulishauriana waka-*extend deadline* iwe mwisho wa mwezi huu tarehe 30 Julai, 2012, nauliza baada ya tarehe 30 itakuwaje? Hawa watu maji watachota wapi? Wanazuiliwa kwenda kuchota maji kwenye mto huo na hakuna maji, hivi vijiji vyote havina maji, maji watakunywa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa sababu sheria iliyotengeneza msitu huu, iliyoweka msitu huu ina *provision*, inasema "*Activities prohibited within forest reserve without permission, there is no...*" yaani hakuna kitu kitakachofanyika bila ruhusa. Kwa hiyo, naomba mambo mawili au matatu yafanyike. Kwanza, wananchi hawa kwa sababu hawajaandaliwa mazingira ya kutokutumia msitu huu na maji kwa miaka 16 toka sheria ipitishwe, waruhusiwe kuendelea kutumia maji yale kwa ajili ya mifugo na wananchi wenyewe angalau kwa miaka miwili kuanzia leo wakati Serikali ikija na majibu ya namna ya kuwapatia wananchi hawa maji kwa ajili ya wao wenyewe na mifugo yao. Sikuona kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri mahali ambapo kuna *provision* hii na suala hili linajulikana. Kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 85, kuna mradi wa *LVEMP*, Ngitili Sayaka, kuna mradi wa kukarabati bwawa dogo la maji Lubugu, halafu kuna kupanda miti Salama, Mwagindi na kuna kurudisha msitu wa Sayaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana unajaliwa msitu zaidi kuliko wananchi. Gharama yote ya miradi hii ya *LVEMP*, ni dola 120,000 ambayo ni kama shilingi milioni 200 lakini kwa nini hazikutengwa fedha kwa ajili ya kutengeneza malambo na kuchimba visima? Ukienda Kitongo, juzi nilikuwa pale, watu wanalamika, wanasema sasa Mheshimiwa Mbunge tunakutuma uende Bungeni na wanansikiliza sasa, nimesema kwamba wananchi wale wanansikitika na wanaionba Serikali na wananiambia kwamba Mheshimiwa usiunge mkono hoja mpaka ituambie, vinginevyo watakuja kusikia watu tumekufa aidha kwa sababu hatuna maji, mifugo yetu imekufa na hatuna mahali pa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mwabulenga wanasema wana matatizo, wamenituma. Kwa hiyo, naomba sana Waziri pamoja na Serikali itafute fedha, hata kama hizi za *LVEMP* ziahirishe kupanda miti wakachimbie mabwawa angalau watakapohamishwa wapate mahali pa kujihifadhi vinginevyo vijiji vyote hivi 10 vihamishwe vipelekwe sijui wapi, utawapeleka kwa gharama gani kubwa hiyo badala ya kuchimba visima virefu kwa ajili ya maji ya kunywa, kwa ajili ya kuchimbwa mabwawa kwa ajili ya mifugo yao tena mabwawa makubwa yasiyokauka sio kama hili bwawa dogo la Bubinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana kwa mara ya kwanza toka niwe Mbunge, nashindwa kuunga mkono hoja hii ambayo mimi nilikuwa Naibu Waziri wa Maji na toka nikiwa Naibu Waziri wa Wizara hii niliwaahidi wananchi wa Magu

kwamba sasa nimefika penyewe, lakini bahati mbaya nilikaa tu mwaka mmoja sikuweza kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nitaunga mkono hoja hapo Mheshimiwa Waziri atakapowahakikishia wananchi wa Magu MJINI na wananchi wa vijiji hivi 10 matatizo yao yanatatuliwa, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji. Namheshimu sana kaka yangu Profesa Maghembe pamoja na kaka yangu Dkt. Mahenge, lakini nawaheshimu zaidi wapiga kura wangu walionileta hapa Bungeni, nataka niseme kwamba sitaiunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mufindi Kaskazini, kuna wananchi takriban wanafika laki mbili, lakini watu wanaopata huduma ya maji kwa uhakika ni watu 25,000 ambao hawazidi hata asilimia 15. Maji ni uhai, maji ni chakula na maji ni dawa. Sasa kama maji ni muhimu kwa mwanadamu na ambao wanapata maji kwa uhakika ni asilimia ambazo hazizidi 15, kwa kweli siko tayari kuunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mufindi Kaskazini, tuna Tarafa tatu. Tarafa ya Ifwagi, Kibengo na Sadani yenye Kata 15. Kata ya Ihanu yenye vijiji sita, Kata ya Mdabulo yenye vijiji vitano, Kata ya Ikweha yenye vijiji vinne, Kata ya Mapanda yenye vijiji vitano, Kata ya Ihalimba yenye vijiji vitano na Kata ya Kibengo yenye vijiji sita na Kata zilizopo pale mjini lakini

katika Kata hizi nilizozitaja hakuna hata kijiji kimoja ambacho kina kisima cha maji. Kwa hiyo, wananchi katika maeneo husika wamekuwa wanatumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya kazi za uzalishaji mali, nataka niseme Serikali imetutenga kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika kitabu hiki, sioni eneo ambalo Jimbo la Mufindi Kaskazini limezungumziwa na nimegundua Waheshimiwa Mawaziri wanadanganywa na wakidanganywa wanatuletea ripoti kama zilivyo. Humu wameandika kwamba miradi ya vijiji kumi, minane imekamilika. Nikimwambia Mheshimiwa Waziri asimame aniambie mradi gani umekamilika, hawezi kusema. Kwa hiyo, wanamdaganya na nataka niseme nimekusudia kushika mshahara wako na nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilipata bahati ya kuongea na Mheshimiwa Profesa Mwandosya kuhusu tatizo la maji lililopo katika Wilaya ya Mufindi na hasa katika Jimbo la Mufindi Kaskazini. Mheshimiwa Profesa Mwandosya alinielewa na aliamua kwa dhati kwamba anataka kunisaidia lakini alipotoka, matatizo yakajirudia. Kuna eneo katika Tarafa ya Sadani, kuna Mto Kihata ambao nilipoongea na Profesa ulikuwa na uwezo wa kuhudumia vijiji vitano na alikubali na alimwita Injinia wangu kumpa shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuanzisha ule mradi lakini alipopata matatizo ya kuugua tu wale jamaa walikataa kutupa zile hela. Kwa hiyo, nimeshagundua kwamba hapa ndani kuna Majimbo mengine na

maeneo mengine yanaonekana bora kuliko maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka kuchangia, ni suala la maji katika Mji Mdogo wa Mafinga. Mji Mdogo wa Mafinga wenyewe wakazi takribani 35,000, miundombinu yake imepitwa na wakati. Sijui *survey*, *design* imefanyika, kila siku wanasema kwamba imefanyika na kwamba mradi huu utaanza si muda mrefu lakini karibu kipindi cha tatu hili jambo halipo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nisipende kuchukua muda mrefu kuchangia kwenye jambo hili kwa sababu hakuna jambo lolote la msingi ambalo nimeliona kwenye kitabu hiki. Kwa sababu wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini shida yao ni maji, nimesema siungi mkono na naomba kuwaambia Wabunge wenzangu nataka kutoa shilingi, ahsante sana. (*Makafi*)

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nichangie kwenye suala muhimu kama hili la maji. Kwanza, ninayo shukrani mbele ya Mungu na mbele za Bunge lako Tukufu kupata wakati mzuri wa kuchangia. Pili, napenda nitoe shukrani kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Nkenge kwa ushirikano mkubwa wanaonipa kwa kuendesha Jimbo letu la Nkenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani kwa UWT kwa kuniachia kuwa mgombea pekee wa Wilaya ya Misenyi ili niweze kuendelea

kuwatumikia na niko tayari kuwatumikia Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema Wanamisenyi wamenionya jambo moja kwamba tunaomba uunge mkono hoja lakini utoe tahadhari kwamba kwa mwaka huu tunakubali lakini kwa mwaka ujao kama suala litakuwa ni hivihivi hutaunga mkono. Kwa hiyo, niseme ninaunga mkono hoja ili hata hicho kidogo kilichopo tuweze kukipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja. Maji ni kitu gani? Maji ni uhai, maji ndiyo uzima, maji ndiyo mtu na maji hayana kitu mbadala katika ulimwengu wote tangu umeanza na utakapokuwa umeisha. Maji na mwanadamu. Mwanadamu unavyomuona asilimia 75 ni maji. Kwa maana hiyo, mwanadamu ni maji na maji ni muhimu kuliko ugali, wali, kuliko hata ndizi. Kwa hiyo, kitu cha msingi kuliko vyote duniani vinavyoonekana ni maji. Kwa hiyo, mimi naomba tu kusitiza maji tunayoyapata sio maji. Sio maji salama; hasa naongelea katika Jimbo la Nkenge. Tangu tume pata uhuru hatujawahi kupata maji safi na salama. Hivyo, naomba kusitiza kama kweli keki hii ndogo tunagawana wote basi na sisi katika bajeti ijayo tukumbukwe kupewa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji salama. Katika llani ya Chama cha Mapinduzi wakati tunagombea tulieleza kabisa ni moja ya sera ya Chama kwamba tutakuwa na jambo kubwa la kufanya juu ya maji lakini ukiangalia katika kitabu hiki cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2011, utaona kabisa suala la maji

limeshuka kwa takribani 2.3 percent. Uwezo wa kuendesha au kufanikisha ukilinganisha na mwaka 2010 umeshuka kwa 2.3 percent lakini katika maelezo ya Serikali ikaeleza jambo ambalo limenichekesha sana, ni kwa sababu ya ukame na umeme. Hivi je, kutokana na ukame na umeme si ndiyo wangechimba visima zaidi ili watu wapate maji? Sasa unapochukua kila neno, umeme na ukame mnachukua kama *copy and paste*. Kila mahali wamebandua na kuweka kwamba hapa tatizo ni umeme, ni maji lakini kama tatizo ilikuwa ni ukame, ilikuwa ndiyo nguvu ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme kwamba tatizo kubwa ambalo nataka niliseme katika Wizara au Serikali hii, ni tatizo la vipaumbele. Ukiangalia katika bajeti hii, huwezi kujua kipaumbele ni kitu gani. Ukiangalia kila Wizara imenyang'anyana na mwenzake kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata na matokeo yake katika utaratibu huo hatuwezi kupima *impact* ya kitu. Kwa nini Serikali yetu isiseme *okay*, vitu vyote ni muhimu lakini hebu twende na vitu sita kwa kila bajeti na tukaviwekea nguvu ya kutosha, tukatoa pesa za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna Wizara 30 tukasema Wizara sita tutazipa bajeti kubwa ili tuondokane na kutokuona matokeo. Hivi sio aibu kila tukisimama tunaponda? Tufike mahali tuseme labda barabara na yenyewe ni watu kuamua *psychologically*, kila mtu anasema barabara safi lakini kama tunataka kusema ukweli, hatuna vipaumbele matokeo yake kupima *impact* kwamba hapa

tumefanikiwa au hapa hatujafanikiwa ni ngumu sana. Kwa nini tusiseme hizi Wizara sita tutaanza nazo, ukaangalia vitu muhimu kutokana na llani yetu tuliyotangaza au tulioieleza kwamba maji yanamgusa maskini, kabwela, bepari kila mtu anahitaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naishauri Serikali yangu kwamba hebu tuje na vipaumbele. Njoo na Wizara sita zenyepesa ya kutosha halafu zingine unaziwekea hela kidogo ili zisife lakini zamu yake ya kuwekewe hela ya kutosha ikifika watafanya vitu vionekane. Hilo ndilo tatizo kubwa la nchi hii. Watu wazuri tunao lakini mimi naomba wakae chini wajiuilize hivi tunavyoenda na Wizara 30 zote kuziwekea mamilioni na mamilioni hivi wataweza kufika mwisho? Tutaona matunda ya hizi pesa? Hatuwezi kuona kwa utaratibu tulionao. Mimi ninaomba Serikali iliangularie hili la vipaumbele. Mwaka huu vipaumbele ni vipi? Mwaka ujao nini kipaumbele? Miaka mitano tutakuwa tumeona na tumepima kwamba tumefanikiwa hapa au hatukufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niongelee visima vya *World Bank*. Hivi visima vya *World Bank* katika wimbo unaosema ni kumi lakini katika Wilaya yangu ni sita na hivyo sita vimechimbwa, kimoja hakina maji. Nauliza hiyo pesa yetu ya kisima ambacho hakikupata maji, tatarudishiwa na mtu aliyechimba au itakuwa ndiyo patapotea, tumepoteza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini tusifikirie kama Serikali kwamba jamani hawa wananchi unaotaka wachangie *20 percent they can not afford*,

hawana uwezo, kwa nini Serikali isiwakopeshe, tukaweka miundombinu halafu wananchi wakaja wakanunua maji kwa pesa ndogo kwa kuwa Serikali imekopeshwa kwa miaka 15, sisi tukasema wananchi wakopeshwe kwa miaka kumi na miaka kumi nina uhakika zile pesa zitakuwa zimelipwa. Kwa hiyo, kuliko kuwalazimisha, maji wananchi wanayaona pale, maji hayatoki wakati nyumbani hawana maji, kisima wanakipita na kimefungwa kinasubiri mwananchi atoe pesa. Kwa hiyo, nashauri Serikali yangu na naiomba sanasana walione hili ili tuondokane na wimbo wa maji. Wananchi wakopeshwe na wao miaka kumi walipie kidogo kidogo na mwisho tutakuwa tumemaliza. Ukiliacha hivyo, miaka kumi na tano ya mkopo wa Serikali itafika wananchi hawajatumia maji na maji tunayalipia na unaendelea kulipa deni. Kwa hiyo, kipi bora, miaka miwili au mitatu tangu tumeingia katika huo mkopo bora sasa tugeuze utaratibu tuwakopeshe wananchi na baadaye waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Misenyi na maji. Nataka niseme kwamba katika Wilaya yetu ya Misenyi tuna Ziwa Victoria, tuna Mto Kagera, tuna Mto Ngoni, tuna na Mito mingine mitano midogomidogo ambayo ni vyanzo vizuri vya maji. Kwa nini na sisi tulie maji? Dodoma walie maji, Singida walie maji na Wahaya walie maji? Sio sahihi, kwa sababu sisi Mungu ameshawapunguzia mzigo. Ameshatuwekea maji pale, ni kazi ya Serikali kutengeneza miundimbinu, ikatuvutia maji na tukatumia maji kama Mungu alivyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa mfano sisi katika Jiografia yetu ya Misenyi, maji yanapatikana mabondeni. Huko juu, milimani watoto wanapoenda shule ndiyo *toilet* huko, watu wanapokuwa wanachunga ndiyo *toilet* huko. Mvua zikinyesha kinyesi chote kinakuja kwenye mto na matokeo yake tunapochota maji, yale maji sio salama hata kidogo na ndiyo maana watoto wengi wanadumaa kwa sababu majii sio salama. Nikwambie katika kijiji cha Kilimilile wanakunywa matope. Siku moja nilipewa maji kunawa nilidhani *juice* kumbe ni maji. Hayo maji kweli huyu mtu anaweza akaifurahia Serikali yake kwa namna hiyo? Mimi nilikuwa naishauri Serikali iangalie ni namna gani watu ambao tayari Mungu amewawekea vyanzo tuweze kuweka maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanamke na maji. Nataka niongee vitu vichache sana kwamba mwanamke anapoondoka asubuhi kwenda kuchota maji, kwetu kwa kweli sio *distance* kubwa namna hiyo lakini mimi ninaweza kuangalia mtu badala ya kuamka asubuhi aende kulima, aende kuzalisha, anaenda kutafuta maji. Mtoto akienda kuchota maji akirudi nyumbani amechoka anasema mama shule siendi. Katika sehemu zingine unakuta tangu asubuhi kuna foleni. Nilikuwa kule Arusha, nilishangaa tangu asubuhi watu zaidi ya 300 wapo kwenye kisima kimoja wanasubiri maji. Kwa kweli hawa watu ukiwaliza moyoni wanaweza kusema kwamba Serikali hii haitutendei haki. Kwa hiyo, mimi naomba tuwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba nikubali lakini *next time* mkija sitaunga mkono hoja ila leo naunga mkono, ahsante. (*Makofi*)

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu nami kuwa mionganoni mwa watu ambao tunachangia *agenda* hii ya maji lakini lazima ni-declare *interest* kwamba mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Maji, ina maana maoni yaliyotolewa na Kamati ya Maji na yangu yamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza ningependa kuwapongeza Mawaziri hawa wawili kwa sababu tunajua wote ni wapya, wameingia katika Wizara mpya yenye changamoto kubwa na Tanzania hii hakuna tatizo kubwa kama tatizo la maji. Kwa kweli ni wazi wala haipingiki hata kidogo maana mionganoni mwa matatizo makubwa ya Watanzania sasa ni tatizo la maji na tukizungumza ukweli halisi hata hii bajeti iliyotengwa ni bajeti ndogo kwa sababu kutokana na tatizo la maji katika Tanzania nzima na hili liko wazi, maana sasa hivi ukienda vijiji vyote kila mwananchi anajua kilio cha maji. Bahati mbaya wenzangu wamesema tatizo ni vipaumbele. Juzi tumezungumzia reli, kila kitu kinahitaji fedha, barabara fedha lakini maji ni tatizo kubwa kweli kwa Tanzania yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu Kisarawe ndiyo maana siku zote nikisimama hapa nazungumza shida ya maji Kisarawe kwa sababu tatizo la msingi katika Wilaya yangu ya Kisarawe ni tatizo la maji. Nilizungumza siku ya nyuma, mimi toka nizaliwe, kule

kwetu tulikuwa tuna utaratibu tunauita "Kilala". Niliseme hili kwamba "Kilala" mtu unasimama, mzee anakwambia vua shati, unavua shati unainama, unapigwa kopo moja tu la maji; umeoga "Kilala" na inawezekana wakati mwingine wiki inakatika ndiyo unapata tena kopo moja la maji. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa sana toka utoto wetu. Niwaambieni maji haya yanaleta athari kubwa sana hata katika suala la uchumi na suala zima la taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Walimu wangu kule Kisarawe maeneo kama ya Chole, Samvula, maji sasa hivi yamekuwa ni tatizo. Walimu hata kufundisha inashindikana kwa sababu hawana maji. Watoto walioko sekondari wanashindwa kusoma kwa sababu hawana maji, wananchi wanashindwa kulima kwa sababu hawana maji. Mama yangu Makilagi siku zote anapokuwa anatembelea kule Kisarawe inafika wakati machozi yanataka kumtoka. Akinamama wanamwambia mama yetu maji, wanaamka saa kumi ya usiku, wanashinda mpaka jioni, kule maji hakuna cha wanaume wala wanawake kama watani zangu Wasukuma, kule kwetu Kisarawe wanaume na wanawake wote wanatafuta maji na wanalala visimani kwa ajili ya shida ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu ninaposimama siku zote hapa, ninapozungumza shida ya maji, kwa kweli Kisarawe tuna tatizo kweli la maji. Lakini ndiyo nasema na mimi nina imani sana na Waziri na Naibu Waziri wangu, naamini kwamba watapambana, wao ni wapya, watasaidia Wizara yetu hii kuona jinsi gani watafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafafanua kiundani katika Jimbo langu la Kisarawe, vilevile napenda kupongeza wadau mbalimbali wanaoisaidia Wilaya yangu ya Kisarawe japo kuna shida kubwa ya maji. Napenda kuwapongeza hasa ndugu zangu wa *Plan International*, ambapo ule Mji wa Kisarawe ulikuwa hata watu kuujenga kwenyewe ni shida kutokana na shida ya maji lakini sasa hivi *Plan International* na Serikali yetu ilitoa fedha pale karibuni shilingi milioni 550 angalau pale Kisarawe Mjini tukapata nafuu ya maji. Pia niwashukuru sana ndugu zangu wa *TANESCO* kwamba tumewalilia sana kwa sababu tulikuwa tunapata umeme mdogo hata mitambo ya maji ilikuwa haifanyi kazi. Sasa hivi Kimani inafanya kazi, ndugu zetu wa *TANESCO*, ndugu yangu Malima alinisaidia sana kipindi kile na ndugu yangu Ngeleja, wamesaidia sana kubadilisha mfumo badala ya kutoka Ubungo sasa tunapata kutoka llala. Sasa hivi tuna umeme wa kutosha na mitambo yetu inafanya kazi na maji pale Kisarawe Mjini angalau tuna nafuu kidogo kwa sasa. Isipokuwa naomba wataalam wangu maana juzi nimepata taarifa kwamba watu wanapanga foleni kwa sababu wanatoa kimgao, naomba tabia hii ikome, iishe, wananchi wa pale Kisarawe wapate maji kwa sababu mitambo yote inafanya kazi. Naomba wataalam wangu mhakikishe wananchi wangu wanapata maji na msilet kero kwa wananchi wangu, wanaweka foleni stendi sielewi sababu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie maji kwa upana. Nimesema naiomba Serikali sana,

katika huu mradi wa Kimbiji, nakushukuru Naibu Waziri siku ile ulivyojibu swali langu la nyongeza, ulisema Kisarawe itapata maji kuitia mradi wa Kimbiji. Niishukuru sana Serikali kwa ahadi hiyo na naiomba katika kuelekeza ile mitambo kuja Kisarawe angalau na maeneo yake ya jirani tuweze kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Tarafa ya Mzenga ni wadau, mradi mkubwa wa maji unaokuja Dar es Salaam unatoka katika Mto Ruvu ambapo mto huu umetoka katika Tarafa ya Mzenga na maeneo ya Morogoro kwa rafiki yangu, naomba Tarafa ya Mzenga iweze kuunganishwa maji kutoka Mlandizi kama nilivyoomba pale awali kwamba bomba litoke Mlandizi lije sasa Tarafa nzima ya Mzenga ambapo watu wanapata kero kubwa ya maji wakati mto unatoka katika maeneo yao. Naomba Serikali katika hili, tutaweza kutatua kwa kiwango kikubwa sana tatizo la maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri pale Mzenga kulikuwa na miundombinu ya maji mpaka kuna matanki kiasi kwamba mkiweka bomba kubwa tu maji yanaingia katika matanki ya pale Mzenga wananchi wa Mzenga kuanzia Zegero, Chakenge na maeneo yake yote mpaka Vihingo kule watapata maji na ili tujue katika Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano Mzenga ndiyo tunakuja kutengeneza bandari kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuitengea maji sasa hivi, baadaye tutazua tatizo lingine la ziada. Naiomba sana Serikali yetu ijue kwamba hiyo tathmini ikifanyika bomba la maji linalotoka Mlandizi kuja Mzenga kutoka

katika mradi wa Ruvu Juu litasaidia sana kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kisarawe angalau sasa hivi tatizo linapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, tulikuwa na vijiji 10 vya Miradi ya Maji na tumeweza kufanikiwa katika baadhi ya maeneo, kama vile Kihare, Boga, Kibuta, Chakenge, maeneo hayo angalau tumeweza kupata maji ya kutosha. Bahati mbaya sehemu nyingine kama Kwala, Chole, Vikumburu pamoja na baadhi ya vijiji vingine hatukupata maji ya kutosha. Naomba vijiji vile ambavyo sasa maji yamepatikana ya kutosha, ipatikane fedha ili mradi wananchi waweze kupata maji katika visima vile. Hivi sasa watu wa Kihale wanapata shida wakati wana kisima kinatoa maji mengi ya lita 14,000 kwa saa. Sasa kwa nini tusilete fedha haraka ili kusambaza yale maji wananchi waweze kupata maji? Maji yale ya Kihale yanaweza kusaidia mpaka Kisangire mpaka Kuresa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iweze kuleta pesa kwa haraka sehemu tuliyopata kwa mfano, Chakenge, Boga, Kihare, Msanga pale maji yaweze kutawanywa wananchi waweze kupata maji katika maeneo yao. Lakini siku zote huwa ninazungumza, ndiyo maana hata mwaka 2011 nilikuwa nimetoa rai yangu ya kutaka kuleta angalau hoja binafsi kuhusu suala zima la matumizi ya mto Rufiji. Mimi sielewi kwa nini mto Rufiji ambao una maji mengi yanatiririka na yanapotea baharini, wakazi wa Kisarawe wanapata shida kubwa ya maji, wakazi wa Mkuranga wanapata shida kubwa ya maji, wakazi wa Rufiji wanapata shida kubwa ya maji; tumeweza kutoa

maji katika ziwa Victoria mpaka hivi sasa tumepeleka Shinyanga na Tabora, kwa nini tushindwe maji kutoka Mto Rufiji kuyaleta Kisarawe na kuingia Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweze kuliona hili, kama tulithubutu kuyatoa maji ziwa Victoria tukapeleka mpaka Tabora, ni lazima tujipange kama Serikali, tupange mkakati kutoa maji kutoka Mto Rufiji yaende Kisarawe, Mkuranga na wakazi wa Rufiji wapate, na hatimaye kuja kuingia katika kijiji la Dar es Salaam maeneo yote tuweze kutatua tatizo la maji. Inakuwa haingii akilini, kwamba tuna rasilimali kubwa ya utajiri wa maji halafu wananchi wanaendelea kukosa maji na tukijua wazi kabisa Kisarawe na Mkuranga ni maeneo ya uwekezaji, viwanda vikubwa vinajengwa hivi sasa, na viwanda vile vinahitaji maji, lazima Serikali tujipange katika mipango endelevu kwamba Mkuranga, Kisarawe na Rufiji tutengeneze miundombinu mikubwa ya maji ili vile viwanda vinavyotengenezwa hivi sasa viweze ku *operate* katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisarawe mwaka huu tumeleta ombi maalumu na lengo letu ni jinsi gani tutapata maji katika vijiji 60? Lakini vile vile tuna bwawa moja linaitwa Bwawa la Zumbi liko kati ya Vikumburu na Mloka pale katikati kuna bwawa kubwa kama ziwa. Naiomba Serikali, kutenga pesa chache mwaka huu kwa ajili ya kufanya *feasibility study and detailed design* muweze kutupa sisi watu wa Kisarawe mwaka huu tuweze kuangalia ni jinsi gani maji yale kutoka bwawa la Zumbi au mto Rufiji pale Mloka yaweze kuingia Kisarawe kwa ajili ya kuweza kutatua tatizo la

maji. Tunajua, tunachimba *bore halls* lakini *bore halls* hizi mara nyingi zinakuwa *dried bore holles*, maji hayapatikani na mara nyingine maji yale yakipatikana kwa muda mfupi yanakuwa hayawezi kukidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusitumie rasilimali tuliyo nayo ambayo ni endelevu kwa muda mrefu? Itaweza kuwasaidia sana wananchi wetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kwa Kisarawe naomba agenda hii muijumuushe kama ni agenda ya Kitaifa, siyo agenda ya Kisarawe. Maji yatakapotoka Rufiji, yakiingia Kisarawe, maana yake ni kwamba yatakuja Dar es Salaam, kuleta ukombozi mzuri sana. Rafiki yangu Mheshimiwa *Innocent* alizungumza sasa hivi mto Ruvu unaojengwa tayari ng'ombe wengi wameshajaa katika mto. Tunaweza kutengeneza mradi, lakini huko baadaye tunakutana na changamoto, tuweze kujipima ni jinsi gani tutajiokoa huko siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotumia mto Rufiji, tutakuwa na jambo kubwa sana la kujivunia kuwa tumetengeneza *project* ambayo itawasaidia wananchi wa Tanzania. Naomba Waziri achukue agenda na ajue sasa hivi kuwa hali hii ni ya hatari, bwawa la Vikumburu limekauka, wananchi wa Chole sasa hivi wanunua dumu Sh. 2000/=, katika Tarafa ya Chole hali ni mbaya sana. Naomba Waziri na Katibu Mkuu watume *team* sasa hivi kwenda kuangalia Chole sasa hivi ni janga. Tatizo la maji ni janga na siku zote naomba, ninalizungumzia hili suala sasa kwasababu Bwawa la Vikumburu lilikuwa karibu kilomita 14 kutoka Chole Mjini na watu walikuwa wanatumia, sasa hivi hilo

bwawa limekauka. Ina maana kila mwananchi sasa hivi anahangaika, hata kwa sasa tunaweza kufunga shule zote kwasababu maji hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja nikitumaini kwamba Wizara imechukua maoni yangu na kwenda kuyafanyia kazi. Ahsanteni sana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, nitaanza kwa kusema kwamba sidhani kama nitaunga mkono hoja, lakini vilevile nahitaji Mheshimiwa Waziri wa Maji anipatie ufanuzi wa masula kadhaa. La kwanza, sote tunajua kuwa kuna barabara ambayo inajengwa Mwenge kwenda Tegeta katika dhamira ya kupunguza foleni katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini kumekuwa kuna uharibifu mkubwa sana wa miundombinu ya maji ambayo inakwenda kwa wananchi. Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri anifafanulie kwasababu wananchi wangu wa Tegeta wanapata taabu sana, mabomba yao yanakatwa, wakienda *DAWASCO* wanaambiwa wanatakiwa wajigharamie upya kuunganisha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijue, katika ujenzi huu ni nani anayewajibika? Inawajibika Wizara ya Ujenzi ama Wizara ya maji kuitia Taasisi zake? Inawajibika pale ambapo miundombinu ya maji inaharibiwa wakati barabara inatengenezwa ama jukumu wanalirudisha kwa mwananchi kuumia mara mbili?

La pili, hivi karibuni kwenye vyombo vy ya habari katika Kata ya Makongo wakati wanafanya ukaguzi *DAWASCO*, Kawe pamoja na Madiwani, Wenye viti wa Mitaa na Wajumbe wa Mitaa wakagundua kwamba kuna baadhi ya watu ambao wamejunganishia moja kwa moja kutoka kwenye tanki ambalo linatokea Chuo cha Ardhi na mmoja kati ya watu hao ni vigogo wakubwa sana. Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha aniambie kama anayo hii taarifa, na kama taarifa ipo wamechukua hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo nataka kuchangia ni kuhusiana na huu mradi wa maji wa Mkoa wa Dar es Salaam ambao unajumuisha miradi mikubwa minne ambayo itagharimu Shilingi milioni 653. Ukiangalia hii miradi katika miradi minne mikubwa, miradi mitatu iko katika hatua za usanifu na tunaambiwa miradi hii inatarajia kukamilika mwaka 2014 Desemba na sasa hivi ni 2012 katikati, maana yake ni kwamba tuna kipindi kifupi sana kuweza kuhakikisha kwamba miradi hii imetekelizwa. Nilitaka Mheshimiwa Waziri vilevile wakati anajibu hoja zake alihakikishie Bunge hili Tukufu kwamba huu mpango wa dharura wa Jiji la Dar es Salaam utakamilika ifikikapo Desemba, 2014, na ni kweli kwamba hizo fedha zote milioni 653.9 zitapatikana kwasababu ukiangalia mafungu ya maendeleo utaona kwamba fedha nyingi sana tunategemea kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiendelea kwenye suala hilohilo la kutumia fedha nyingi kwenye miradi ya maji lakini tuna changamoto kubwa sana linapokuja suala la kutunza miundombinu ya maji. Mwaka huu

mwezi Januari Mkaguzi wa Hesabu za Serikali CAG alitoa taarifa ya ufanisi ya Mamlaka za Maji za Mijini na inasikitisha kuona kwamba katika hotuba Mheshimiwa Waziri hakuna hoja zozote za msingi ambazo zimeonyesha kwamba wanataka kuokoa sekta hii maji kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ni aibu leo tunapitisha mabilioni ya shilingi lakini tunaambiwa na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwamba katika maji yote ambayo yanazalishwa na Mamlaka za Mijini zinapoteza karibia 50% ya maji kwa hiyo, tunazalisha maji 100% lakini 5% ya maji yanayozalishwa yanapotea hoja kama hizi nilitarajia katika mipango ya Wizara watatueleza ni kwa namna gani wana mipango ya dharura ya kuhakikisha kwamba maji ambayo yanapotea barabarani na mengine siyo kwasababu yanasaababishwa na miundombinu mibovu watachukua hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi katika kila maji yanayopotea tathimini inaonyesha kwamba Serikali inapoteza bilioni 2.5 kila mwezi kwa maana yake ni kwamba ukifanya tathmini ya mwaka mzima karibia Shilingi zisizopungua bilioni 40 kwa sababu hii Shilingi bilioni 2.5 ni tathmini ya chini, ni karibia Shilingi zisizopungua bilioni 40 zinapotea kutokana na maji kupotelea barabarani. Mimi nilikuwa ninapenda Mheshimiwa Waziri wakati tunapanga mipango ni lazima tuangalie hoja ambazo zimezungumzwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali zinafanyiwa kazi, tunaambiwa kwamba kwa makadirio ya nchi yetu kwasababu ni nchi ambayo inaendelea ni nchi masikini tunatakiwa maji *at least* yapotee kwa kiwango cha 20% lakini ukija kuangalia utendaji kazi wa Mamlaka

zetu za maji kwa mujibu wa Mkaguzi Mkuu Hesabu wa Serikali hali inatisha, lakini hapa huoni kabisa kama Wizara ina mikakati yoyote ya kuhakikisha kwamba hizi Mamlaka zetu za Maji ambazo pia tumemsikia Mheshimiwa Mbunge wa Shinyanga alikuwa anazungumza, tumemsikia pia Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini alikuwa akizungumza kwamba Wizara inatumia utaratibu gani wa kuweza kuzisimamia hizi Mamlaka na kibaya ama kizuri ni kwamba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amesema humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameonyesha humu kwamba inaonyesha hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kwamba Wizara ama *EWURA* inatumia mbinu za kutosha kuweza kuzisimamia hizi Mamlaka. Jukumu la *EWURA* ambalo ninashangaa hapa imepongezwa wakati Mkaguzi Mkuu Hesabu anasema *EWURA* inakuwa makini wakati wa kupanga zile bei, yaani *tariff*, lakini linapokuja suala la kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria ya Maji ya Mwaka 2009 hawafanyi hivyo, lakini utakuta wakati makadirio ya Wizara ni 20% kuna Mikoa kadhaa ambayo inaongoza kwa kiasi kikubwa cha maji kupotea barabarani au njiani wa kwanza ni Mkoa wa Kigoma na ndiyo maana nikamuuliza Mheshimiwa Muhonga kuwa vipi Kigoma mna maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maji yanayozalishwa 56% yanapotea barabarani sasa yanapoteaje barabarani wakati huohuo kuna Mamlaka ambazo tunaambiwa zinafanya kazi vizuri. Ukija Mkoa wa Dar es Salaam 54% maji yanapotea

barabarani kwa hiyo mimi nilikuwa ninamuomba Mheshimiwa Waziri kwamba haina maana kutumia mabilioni ya shilingi kuwekeza kwenye miradi ya maji lakini tunashindwa kui- *maintain* miradi ya maji tunaambiwa Mamlaka zetu nyingi tena kwa makusudi ikijumuisha Mamlaka yetu ya Dar es Salaam hainunui mita za maji kwa makusudi kabisa mita za maji siyo sehemu ya kipaumbele chao sasa unapokuwa unafanya biashara ya maji bila kuwepo kwa mita huyu mtu anayetumia maji huku chini unamtoza kwa utaratibu upi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninaomba kama kweli tunaenda katika dhana tunayosema Ari, Kasi na Nguvu Mpya tuna haja katika masuala yote ambayo tunayafanya hususani ya maji tuhakikishe mita zipo, tuhakikishe maji ambayo yanapotea barabarani kwa 50% tunamaliza. Na tungeweza kufanya huu utaratibu na nina uhakika suala la matatizo ya maji hata katika Mkoa wa Dar es Salaam lisingekuwa katika kiasi kikubwa kama liliuyo sasa lakini zaidi kuna suala la uuzaji wa maji ninashangaa katika mipango ya haraka ya kupunguza tatizo la maji Mkoa wa Dar es Salaam Waziri hajasema kwa namna gani atazuia watu wanaofanya bishara ya maji, haiwezekani mtu binafsi akatumia mabomba ya DAWASA kwenda kufanya biashara ambayo inamnufaisha ye ye binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake wamekuwa wakijenga matanki makubwa maji ambayo kwa utaratibu wa kawaida unategemea mtu mmoja afunge ili maji yaweze kwenda kwa mtu mwingine yanashindwa kwenda kwa mtu mwingine

kwasababu kuna wajanja wachache wametengeneza matanki makubwa matokeo yake ni kwamba maji yanatoka *fulltime* kuanzia asubuhi mpaka jioni magari yanakuja yanajaza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri kwasababu wanasema mradi wa maji ni wa vigogo ili kututhibitishia kwamba yale magari makubwamakubwa hayawahusu nyie wala hayawahusu watu wakubwa wenye fedha tunaomba mtuambie katika mpango wa dharura wa kupunguza tatizo la maji Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na hii miradi mnajipanga vipi kufanya ukaguzi wa kina kwa watu wote ambao wanauza maji ni bora utaratibu wa kuuza maji ufanywe kwa mchakato wa kutumia *DAWASCO*. Kwasababu Tegeta na Kunduchi tuna kituo cha *DAWASCO* ambacho kinaiza maji na kimeonyesha mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora tutumie Taasisi ya Serikali ambayo itajua ni kwa namna gani *ina-monitor* uuzwaji wa maji, kwa namna gani itafungua, kwa namna gani itafunga na wakati huo huo faida inarudi Serikalini.

Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba *commitment* kutoka kwa Waziri kwasababu hiyo itakuwa ni sehemu ya kupunguza tatizo la maji mimi ni Mbunge wa Kawe lakini kuna tatizo la maji kubwa sana kama vile watu wako vijijini katika Kata 10 ninazoziongoza Kata 5 zina tatizo kubwa la maji lakini sababu moja kubwa ni matajiri wameweka matanki ya maji ambayo yanatakiwa yafike kwa wananchi hayafiki, yanaishia

kwenye matanki yao na hawahawa wanakuja kuwauzia watu, na wanakula na baadhi ya watu wa *DAWASCO* ambao siyo waaminifu, kwa hiyo, mimi nilikuwa ninaomba tufanye upembuzi yakinifu, tufanye *operation* maalum Mkoa wa Dar es Salaam tuweze kuokoa hawa wananchi na wakati huohuo tukisubiri hii miradi iweze kumalizika mwaka 2014.

Mheshimiwa Mweyekiti, siungi mkono hoja mpaka nipate majibu kwa namna gani wamejipanga kuzuia uuzaji wa maji. Kwasababu hiyo ni *crises*. Siungi mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ASAA O. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, ninakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia angalau machache ndani ya Wizara hii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Wizara tulipitisha mambo haya yanayojiri sasa hivi, Waziri wangu ni mpya, Naibu wake ni mpya na mambo pia ni mpya kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji limezungumzwa kwa kina kipana na wanaozungumza wana sababu Watanzania wana tatizo la maji. Watanzania wanateseka na maji sasa ni nini kifanyike Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amemuona *Professor* kamuondoa kwenye kilimo kamkabidhi sekta hii anamuamini, anamuamini hivyo imani hii ya Mheshimiwa Rais ili ibaki na aondoke nayo ana maliza muda wake naomba sana Mheshimiwa Waziri itumie nafasi hii lakini wasikilize sana Waheshimiwa Wabunge ushauri wanaoutoa ni muhimu

vilio wanavyolia mtu mzima akilia kuna jambo siyo bure. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninakuomba sana uwasikilize Waheshimiwa Wabunge. Umuhimu wa maji kwa binadamu, wanyama, misitu, mimea yetu ili uhai ukamilike ni upatikanaji wa maji ndiyo maana ikapatikana tafsri ya pamoja, 'Maji ni Uhai'. Lakini sasa nini Serikali inafanya kulinda uhai huo wa maji hapa ndipo pana shughuli, ili tukabiliane na hilo sasa nguvu zitumike kwa maana ya jitihada zote, raslimali fedha, raslimali watu, huku Mheshimiwa Waziri ukitia maanani sana ushauri huu wa Waheshimiwa Wabunge na masuala mazima ya Mamlaka za Maji huko mijini kwani vijiji hazifiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu sisi ni Wajumbe wa Kamati tunashuhudia namna mama wa Kitanzania, mabinti wa Kitanzania wanavyoteseka na maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafika vijiji tunayaona, na kwa kujua umuhimu wa mama na mtoto na kwa kuthamini hilo, mama huyu ndiye anayekwenda shambani kuzalisha mazao ya killimo. Mama huyu anarudi nyumbani baada ya masaa kupotea kutafuta maji anakuja kuhudumia watoto na baba, mama mwenyewe anaandaa chakula, lakini atarudi tena kutafuta maji, baba anataka kuoga, hahesabiwi mtoto, anahesabiwa baba. Anatumia tena masaa nane kufuatilia maji, anarudi, baba ana huduma ya pekee, mama kachoka mno, anataka

kumlea na baba sasa, lakini anafikiria maji atatoa wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe hapo ni mama, haya ninayoyazungumza unayajua machungu yake, nadhani tutamsaidia Waziri aweze kufanikisha dhana nzima iliyokusudiwa na Mheshimiwa Rais ili haja iweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitazama Serikali kwa hili, bajeti iliyopo kwa mwaka huu 2012/2013 ina matumaini, na ndiyo maana Wabunge wanamwambia mara hii tunakusamehe lakini mwakani hatukusamehe. Lakini unapokuja kuzitazama hizi bilioni 485 najiuliza tunazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe Shilingi bilioni 325 tunatarajia kupata kutoka kwa wachangiaji wa maendeleo! Hili ni tatizo. Kuna usemi huko kwetu wanasema: "Mjima hamalizi ngwe", sijui usukumani ikoje. Lakini Mjima hakumalizii ngwe. Matarajio hapa ni kwamba sisi wenyewe hii Shilingi bilioni 300 ilikuwa ni ya hapa ndani, tukamwomba mhisani hii Shilingi bilioni 140. Lakini sisi wenyewe hatuna uhakika kama itafikia hii, hapa wahlsani watafika mahali wanapoteza imani. Naomba Serikali tuone umuhimu wa maji kwa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija huku kwenye kilimo, Waziri ulikotoka, wala tusijidanganye kama hatuna maji, kilimo na tija leo ni maji. Viwanda na maendeleo yake ni maji, tunajenga viwanda tunahimiza ajira, hatutatoa ajira kama hatuna kilimo chenye tija,

hatutakuwa na viwanda endelevu. Haya yote hayatofikiwa kama hatuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo tunavitunzaje, hiyo ni *challenge* ya Serikali, wenyewe ni kwa gharama yetu. Namwomba sana Waziri, ushauri ule pia wa kurudisha *regional's* mikoani bila kutegemea mamlaka ina umuhimu wake. Lakini hili suala ni mtambuka. Uchafuzi wa mazingira tunaudhibiti vipi, na hapa tunategemeana, siyo suala la Mheshimiwa Maghembe peke yake, hata Wabunge tuna mchango mkubwa juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge na Madiwani, mikutano yetu kwenye Halmashauri tufanye kazi nzuri ya kutazama na kuhakikisha kwamba mazingira hayachafuki, wala hayaharibiwi. Maji tutalaumiana sana, Mikoa iko zero *kilometres*, lakini watu wake wanahangaika na maji. Tatizo ni nini? Majibu yatabaki pale pale! Mwaka 2013 Waziri atakuja kukamatwa koo kwa ahadi ya hii *figure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *figure* hii ya Serikali kumwekea Waziri mwezi wa Nne ndiyo mnammiminia hii fedha, atumile vipi mpaka kukidhi hiyo haja muda uliobaki kufika kwenye bajeti nalo ni tatizo. Maeneo haya nilikusudia niyaguse kwa haraka kama ushauri tuliozungumza kwenye Kamati na hapa ni nyongeza, Waziri naomba sana ushauri wa Wabunge, ushauri niliobahatika kuutoa hapa, suala la fedha Waziri wa Fedha yupo pale Dokta Mgimwa mkamate. Tafadhalii usimtazame mtu machoni. Usikae ofisini, watendaji watakuja kukuweka pabaya. Wabunge ni wakali mno

na hawatakubali, wanataka kura za mwaka unaokuja na wewe unataka urudi ukamilishe ile dhana ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Asaa, ni kweli kabisa Waziri tusaidie kutembela hiyo miradi hali huko ni mbaya utatusaidia ushauri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge nilisema nitamwita Mheshimiwa Paul Lwanji atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo na kama muda utatosha atakuja Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na wale wanaosema kwamba Waheshimiwa hawa wawili ni wageni, hakuna ugeni kwenye shughuli za Serikali. Kwa sababu wana watalaam wa kutosha. Wizara ya Maji imesheheni watalaam wa kutosha mlaka nenda rudi. Kwa hiyo hapa la msingi ni hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Wazungumzaji waliopita hasa Mbunge wa Nkasi na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa *concern* yao waliyoionesha kuhusu tatizo la maji. Mimi Jumamosi na Jumapili nilikuwa ziara Jimboni kwangu, bahati nzuri nilikuwa nimeambatana na Mwenyekiti wa Bunge

Mheshimiwa Mabumba, alijionea mwenyewe. Unapokuta akina Mama wanamnyoshea au wanakunyoshea kidole wewe mtu mwenye umri wa miaka sitini, basi ujue hapo kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tulikuwa katika hali mbaya, kuanzia Mghanga, Jirimwiri, Ipande, Makajenga mpaka Damweru. Hii Kata imekuwa na miradi ya *World Bank* muda mrefu lakini maji hakuna. Ningependa kupata jibu la mradi huu wa *World Bank* katika Kata ya Ipande, zaidi ya shilingi milioni 150 zimetitia pale, lakini maji yanatoka kwa kusuasua na hakuna hata tanki lillojengwa. Wakachomekea tenki la zamani ambalo lilijengwa wakati wa miaka ya 1970, lakini tenki ambalo lilipaswa kujengwa pale hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kupata maelezo juu ya suala hilo, ningependa pia kupata maelezo juu ya mradi wa *World Bank* wa Rungwa, wananchi wamesikia, tukasaidia sana. Walikuwa wanasuasua katika kutoa ile asilimia 20 lakini *Game Reserves Authorities* ya Rungwa wakatoa ile asilimia 20 kuwasaidia, ni muda mrefu lakini mpaka sasa hakuna maji na mradi huo hauja-*take off*. Kisima kimechimbwa kimewekwa *sea/* lakini bado watu wanahangaika na maji, na wakati wa mvua sasa hivi umepita, watu wanashindwa kuelewa wataishi vipi hii miezi inayokuja ya ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii nilimwambia Mheshimiwa Maghembe kwamba umeingia kwenye anga zangu, pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii ajue kabisa Mheshimiwa Kagasheki kama yupo hapa

ameingia kwenye anga zangu. Vijiji vyangu vyote karibu hamsini viro kandokando ya *Game Reserves* za Muheesi na Kizigo lakini watu hawana maji. Hakuna ushirikiano wa dhati kati ya Wizara hizi mbili na Wizara ya Kilimo. Kila mmoja nafanya kivyake, sasa tufanye nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yanayotokana na hifadhi ya mbuga hizi kwa mwezi ni takribani bilioni mbili. Hizi zinakwenda kwenye Idara ya Wanyamapori, nitalizungumza vizuri nitakapopata nafasi kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Shilingi bilioni mbili lakini kinachokuwa *paid back* kwenye Wilaya hiyo ni shilingi milioni mia mbili kwa mwezi. Angalia zinakwenda wapi hizi, hatuwezi kufanana na mzee ambaye hana busara, anawapikia watoto wake chakula halafu anakula nyama zote watoto wanakula mchuzi hatuwezi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilicho haki yetu naomba tupate, watu hawana maji. Ningeomba pia kujua ahadi ya Waziri Mkuu ya kusambaza maji katika Mji wa Itigi iliishia wapi? Mwaka 2010 Waziri Mkuu, mtu mzito alikuja pale akatoa ahadi ya kutoa fedha kwa ajili ya kusambaza maji Mji wa Itigi lakini mpaka leo hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiuliza ofisi ya Waziri Mkuu, hakuna majibu. Ningependa nipate maelezo. Mji wa Itigi hakuna tofauti na Mji wa Manyoni ni Mji mkubwa, lakini tunahangaika. Watu wanategemea visima walivyochimba wao wenywewe. Ningependa kupata maelezo ni kwa nini inavyoonekana wanyama wanathaminiwa kuliko binadamu kwenye masuala

haya ya maji. Kwa sababu kando kando ya Vijiji hivi hata *buffer zone* hakuna ya wanyama na binadamu. Lakini kuna mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, lile bwawa na Itagwa na bwawa la Kengelege kwenye maeneo yale mkajenga, maji yanajaa mwaka mzima, lakini mifugo hairuhusiwi kukanyaga pale. Binadamu hawaruhusiwi. Maombi haya tulituma siku nyingi waweze kuona utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namkumbuka sana Mheshimiwa Zabein Mhita na pia Waziri aliyeondoka juzi Mheshimiwa Maige kwa kutusaidia pale Doroto. Waliamua kwa maksudi baada ya kuona tatizo jinsi wanyama waharibifu walivyokuwa wanawaletea wananchi matatizo wakasogeza mipaka, watu wanaishi kwa amani na watu wanafanya kazi zao vizuri. Lakini suala la maji limeendelea kuwa mgogoro. Watu wanayaona maji lakini hawawezi kuyatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nipate maelezo ya kina juu ya suala hilo, ni nini wanacho-*supplement* sasa kwenye juhudzi za watu katika huu utaratibu wa *water dousing* process. Hii sijui kama Wizara inaelewa *water dousing system* ambapo watu wanachukua pacha la mti anakwenda anapima mahali kutokana na ile *gravity* anagundua pale kuna maji, akichimba anakuta kuna maji. Lakini watu wengi wamechimba visima vyao lakini hata Serikali kufikiria *ku-complement* hizo *efforts* hakuna! Hakuna *pump*, hakuna nini, na kazi ya kuwapatia watu maji ni kazi ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua wanasema nini juu ya juhudhi hizo za wananchi, maana tunachoona ni fedha nyingi kudidimia kwenye huu utaratibu wa kutumwa watalaam wa Idara ya Maji wanakwenda kupima, wakishapima wanagundua kuna maji, wanaweka *sign*, halafu unaanza mchakato wa tenda kutafuta mkandarasi wa kuja kuchimba maji. Mkandarasi anapokuja anachimba pale maji hakuna, Shilingi milioni 50, milioni 100 zinateketea pale. Lakini wananchi wanapochimba visima vyao hawaangaliwi hata kupatiwa dawa ya kuyafanya maji yale yawe salama. Mara nyingine huwa ni maji ya chumvi, walau wananchi wale wapatiwe dawa ya ku-process hayo maji, hata kupatiwa pampu za kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara hii ina mambo mengi ya kufanya, na ninamhurumia sana Mheshimiwa Maghembe kuwepo hapo, yeye ni mzoefu na ametembea Wizara nyingi ni Vasco Da Gama kwenye masuala haya, maana anapita huku na huku, kwa hiyo ni juu yake sasa atueleze atafanya nini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba bajeti ijayo mwakani baada ya kusomwa Wizara ya Fedha afadhali ingekuja Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono pale tu nitakapopata maelezo ya kuridhisha, Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Paul Lwanji, anafuatia Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ajiandae.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi mchana huu ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji tuliyonayo mbele yetu.

Awali ya yote naomba kumpongeza Waziri Rafiki yangu Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Naibu wake Dkt. Mahenge, mmepewa Wizara yenye changamoto lakini mimi ninawaahidi ushirikiano. Kwa sababu hiyo naanza kusema naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa sababu ya kutambua uchapakazi wenu, lakini jambo la pili natambua Jimboni kwangu na Jimbo la Newala na Mtwara Vijiji kuna Mkandarasi Mshauri anafanya kazi ya *land water assessment* kwa ajili ya kuweka sawasawa ule upembuzi yakinifu ambao ulikuwa umefanywa na nadhani hii ikimalizika mambo yanaweza kuwa yameanza vizuri. Kwa hili naomba niunge mkono hoja kwanza kwa matumaini kwamba mambo yatakuwa sawasawa katika muda si mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwakani nisipoona utekelezaji wa yale yanayofanyika kule hatutaelewana hapa, na kwa kweli tutaelewana vibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti naiona kwa kiasi fulani si mbaya, lakini nina wasiwasi na kuchelea na utendaji wetu wa kila siku uliopo Serikalini. Kwa namna

hiyo naomba Waziri na Naibu Waziri msimamie watendaji wenu. Watendaji hawa ndiyo wanaotuangusha kila siku, mambo hayaendi vizuri kwa sababu ya watendaji hawa. Ninaweza kutoa mfano tu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo tatizo la maji ni kubwa wala hakuna usimamizi wa vyanzo vyetu vya maji. Vyanzo vya maji vinaachwa vinaingiliwa ovyo, vyanzo vinachezewa ovyo wakati watendaji wapo, *why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine wakati tuna tatizo la maji yanapungua kwa kiasi kikubwa, upotevu wa maji ni mkubw ana hakuna jitihada za dhati zinazofanywa na watendaji hao kuhakikisha mambo yanaenda vizuri *why?* Ndiyo maana nawaomba mkazane na mjibidiishe.

WABUNGE FULANI: Kelele.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Waheshimiwa Wabunge ni lugha tu.

MWENYEKITI: Hapana, iweke vizuri sentensi yako.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo naomba pia kuishauri Serikali yafuatayo, kwanza maeneo yangu ni maeneo yenye matatizo ya maji sana, nimesema naona kuna dalili nzuri lakini ningeomba kushauri kwamba tunao mto Ruvuma unapita karibu na Wilaya zile ambapo ungetumika vizuri ungeweza kusaidia sana kuongeza

kiasi cha maji kwenye maeneo ya wananchi. Si tu kiasi cha maji lakini pia kiasi cha uzalishaji wa mazao ya kilimo, maana tungeweza kufanya hata *irrigation scheme* pale ikaboresha maisha ya wananchi walioko kule. Naomba jambo hili mliangalie kwa dhati, ili kilimo kupitia umwagiliaji uweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuishauri Serikali kuangalia sasa namna ya kufanya maboresho kwenye laini ya Nanda kwenda Tandahimba, Nanda ni kile chanzo chetu cha maji kilichopo Mitema Kitangari ambacho kinatoa maji kufika Wilayani Tandahimba. Chanzo kile kilipoasiwa kulikuwa na idadi ndogo ya watu, leo kuna ongezeko kubwa la watu katika eneo hilo. Kwa hiyo, kuendelea kuacha kama ilivyo kutofanya marekebisho yanayoenda na idadi kubwa ya watu bado tunaendelea kupata maji kidogo na kwa hiyo hayatakidhi haja kwa wananchi wetu wale. Natoa rai jitihada zifanyike haraka ili wananchi wale waweze kupata maji yanayofanana na idadi ya watu walioko sasa katika eneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuishauri Serikali na kwa kweli hili niliuliza Bungeni hapa kukawa na majibu kwamba yamefanyika. Rai yenewe ni kwamba matumizi ya maji maeneo ya Makonde kwa siku ni *cubic meter* milioni 12. Lakini chujio la maji lilitoko hapa ninaposema Mitema pale kwa siku ni *cubic meter* milioni tatu. Lakini chujio lile linaweza lifanyiwa marekebisho ambayo yanawezekana kabisa tukapata maji ya *cubic meter* milioni tisa. Kwa nini sasa Serikali isiamue kufanya marekebisho hayo ili unapopata maji ya *cubic meter* milioni tisa kukawa na tofauti tu ya

milioni tatu tayari umepunguza tatizo sana. Vyanzo vile vingine vidogo vikaongezewa hapo tutakuwa tumepunguza sana. Mimi naomba jitihada za dhati kabisa zifanyike.

Pia ningependa kujua miradi ile saba ya kitaifa ukiwemo na mradi wa Makonde imetengewa Shilingi ngapi maana hakuna ninapoona *direct* hapa palipo *specific* kwa ajili ya kutaja amount ya miradi hiyo saba ya kitaifa ikionyesha *amount* inayokwenda kwa kutumia maji kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri kwa kuniletea mradi wa maji wa Mihamwe kule Tandahimba zimetengwa hapa karibu milioni 100 fedha za Kimarekani 170 ambayo ni karibu milioni 263 hivi. Lakini natoa rai, yale niliyosema tusiposimamia vizuri bado Wananchi wa Mihamwe hawataelewa, hawatafanikiwa hata kama tunawapa matumaini hapa. Mpango huu uendane na ukamilishaji wa mradi huo na maeneo yale kuna Vijiji vya Michenjele kule, Kata ya Michenjele, Kata ya Mihamwe, Kata ya Mkorea, Kata ya Naputa, zina matatizo kweli ya maji. Kwa kuwapelekea hivi tutaanza kidogo kuwapunguzia adha. Naomba sana mradi huo ukamilike tupunguze adha kwa wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo ningeomba hapa kwetu sisi watu wa Newala, Tandahimba, Mtwara Vijijini tumekuwa tukitumia sana visima, tunavuna maji ya mvua. Lakini maji yale yakikaa muda mfupi yanatulazimisha kununua dawa maana yanakuwa yameharibika, inatulazimika kununua dawa *ku-treat*

hayo maji ili yaweze kutumika vizuri na yasitulete magonjwa na aina nyingine za adha. Kutokana na uzoefu nilioupata ninaomba Serikali sasa iamua kwa dhati kuleta mfumo wa ruzuku kwa madawa na vifaa vyatya maji ili angalau tupunguze uwezekano wa magonjwa na mambo mengine. Pia gharama zilizoko kwenye tatizo la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, likifanyika hili itatusaidia sana. Lakini natoa rai pia bajeti ijayo tubadilike tuone uwezekano wa kutumia fedha zetu za ndani zaidi kuliko fedha za nje. Unamwomba mhisani, unapomuumba mjomba, unamwomba rafiki yako ni lazima ajitosheleze yeze kwanza ndio atakuangalia wewe. Haya Bajeti inaonekana asilimia kubwa iko kwenye ufadhili zaidi ambao wakipata tatizo dogo kule hawawezi wakatuangalia sisi wakati hawajatatua matatizo yao ya ndani. Kwa kufanya hivyo ndugu zangu, itatupa ufanisi sana yaani nikiwa na maana kwamba kwa kuweka bajeti yetu kwenye eneo hili itatusaidia. Mimi nataka kuipongeza Serikali kwamba katika vipaumbele vyatya mwaka huu, vipaumbele namba moja ilikuwa ni miundombinu ambamo wamejumuisha madaraja, kuna daraja 'A' wamesema umeme, daraja 'B' wameweka usafirishaji na uchukuzi kwa maana ya reli na mambo mengine.

Pia maji ndiyo daraja la kwanza 'C'. Zimetengwa karibu bilioni 568.8 hivi. Lakini kwa kuwa hizi bilioni 568 ni za nje, mimi nachelea kwamba mambo yakiharibika kidogo tunaweza tusifanikiwe. Kwa hiyo, rai yangu na msisitizo wangu kwenye bajeti ijayo kiasi kikubwa kitokane na fedha zetu za ndani na tunaweza. Mzee

Mkapa alipoanzisha mradi wa kule lhelele kuja Shinyanga...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili.

MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mungu akubariki. (*Kicheko*)

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwatendea haki wana Iramba kwa sababu kwenye Bajeti ya Maji ni moja ya siku nyeti Wilayani Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Iramba ukiuliza kipaumbele cha kwanza katika vijiji vyote watakuambia ni maji. Ukiuliza kipaumbele cha pili watakuambia ni maji na ukiuliza kipaumbele cha tatu watakuambia ni maji. Sasa kwa leo hii kupata fursa hii nitamuomba Mheshimiwa Waziri asikilize kwa makini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, nimeipitia ukurasa kwa ukurasa, mstari kwa mstari najua kitu gani kimeandikwa kuhusu maji na hususan kwa vijiji vya Jimbo la Iramba Magharibi. Lakini pia najua mpango wa Wizara wa kupeleka maji katika kila Makao Makuu ya Tarafa. Sasa lililopo tunalishangaa kwamba Tarafa ya Kinampanda moja ya tarafa za siku nyingi sana yenye taasisi nyeti haina maji mpaka leo. Kuna Chuo cha Ualimu pale,

kuna *Tumaini Secondary School*, lakini kuna vijiji vingine vinavyozunguka Tarafa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unajumuisha utoe majibu kwamba Tarafa ya Kinampanda sasa itapata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuchangia pia nikushukuru angalau katika kipindi changu kifupi cha kuwa Bungeni moja ya jambo nitakalojivunia ni zile fedha ambazo tayari zimeshaingia kwa ajili ya mradi wa maji, Tarafa ya Ndago katika kijiji cha Nguvumali. Sasa nitakalo kuomba utakapotoka katika kipindi cha leo waagize watendaji wako ile kazi kwa kuwa mikataba tayari ilishasainiwa kibali kilishatoka fedha zimeshaiingia tayari ziko Iramba kazi ianze mara moja. Wale wananchi wa Nguvumali wanapata shida mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri mpaka Bunge litakapoisha kama kazi itakuwa haijaanza mimi nitakuita uje Nguvumali nitaomba usije na suti tutembee kutoka Ndago mpaka Nkingi kule wananchi wanakofuata maji uone jinsi umbali wanavyofuata maji wananchi wa eneo lile na wamehanganya wakitoka saa 2.00 usiku wanarudi saa 10.00 kwa ajili ya kukwepa joto wakati wanafuatilia maji naomba sana utoe agizo, mkataba ni miezi sita lakini naomba kazi isiende miezi sita kwa sababu tayari shida ya maji imeshaanza. Lakini pia kati ya fedha ambazo zimeshaingia ni kijiji cha Mingela naomba pia agizo la aina hiyo hiyo uweze kulitoa.

Jambo lingine ambalo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji moja ya Wilaya ambayo huwa inamshangaza hata Mwenyezi Mungu nadhani

ni Iramba. Mvua ikinyesha ndani ya wiki moja hakuna sehemu hata ya kuweka mguu. Maji yametapakaa na ni mabonde, kuna bonde pale katikati ya vijiji vya Mkulu, Zinziligi, Ndago, Makunda mimea yote inazama kwenye maji. Lakini kungehitajika bwawa moja tu wangetumia kwa ajili ya mifugo, lakini vile vile wangeweza kutumia kwa ajili ya kilimo ambacho vijana wengi wangeweza kupata ajira.

Hivyo hivyo kwenye Bonde la Mtoa, Kikungu, Mgunga, Ujungu ni bonde ambalo maji mengi sana yanaathiri mimea, yanaathiri mazao, yanaathiri akina mama wajawazito wakitaka kupelekwa Hospitalini wanabebwa kwenye vitanda kwa ajili tu kwamba maji yakishaenda kule hakuna barabara inayopitika. Lakini kungejengwa bwawa moja tu pale tungeweza kupata kilimo cha umwagiliaji lakini maji kwa ajili ya mifugo. Nitaomba sana mabwawa hayo mawili Mheshimiwa Waziri uzingatie sana na najua una marafiki wengi, pamoja na bajeti yetu lakini fedha itengwe iende kwa ajili ya kutengeneza mabwawa hayo. Mimi nimeanza mfano huo, kwa kuzingatia hali ilivyo kule Iramba nimeuza V8 kwenda kufufua motor kijiji cha Mkulu, Makunda, Kitusha, Mampanda, Kizaga, Kisharita, Kibaya, Kikonge, Mgundu pamoja na Ruruma. (*Makofî*)

Sasa Wizara zilikuwepo mashine zile za upemo zote zimepukutika zilikuwepo mashine za ku-*pump* kwa mkono zote zimeharibika. Yalikuwepo mabwawa yamejaa tu mchanga hivi kweli vile vitu tulivyoachiwa hata hivi vya kukwangua udongo tu maji yajae hivi ni kweli hilo nalo tunashindwa?

Mheshimiwa Waziri mimi nitaomba wakati unatoa majibu yako uniambie kati ya mabwawa yaliyoharibika katika bajeti yako ni mangapi yataondolewa tope ili mwakani maji yaweze kuingia wananchi watumie kwa ajili ya mifugo pamoja na ujenzi. (*Makofi*)

Haya ni maeneo ambayo tu nimeyaja kuna maeneo mengine kijiji kinapata maji, chanzo kinatokea kwenye kijiji jirani kabisa na kijiji kingine. Inahitajika bomba tu, lakini mchakato unakuwa mrefu kweli kweli. Maji yapo ya kutosha, kwa nini tunagombanisha wananchi mpaka wanachukuani wakati maji yako tu pale na inahitajika tu bomba tu tunasubiri utaratibu mwingine.

Jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri ambalo nitakuomba sana kuna vijiji yanapotokea mafuriko Mheshimiwa Lukuvi huwa ana fedha za dharura lakini kule kwangu kuna vijiji ambavyo ukosefu wa maji ni dharura kuliko hata yale mafuriko. Ukienda Luono kuna visima vimechimbwa kama hapa nilipo na kule uliko wewe yaani kwenda chini kuna kijana mmoja alidondokea mle mpaka leo hii miguu yote ikavunjika. Ni moja ya eneo ambalo nitakupeleka Mheshimiwa Waziri siku ukija. Ukienda Misuna kisima kimechimbwa kwenda chini kama hapa na uliko Mwenyekiti. Mheshimiwa Waziri mnapokuwepo na lile fungu ambalo mnalisema ni dharura kwa nini Iramba msiichukulie vile vijiji kwamba ni dharura? Ukienda Mseko, Malendi, Kizonzo pana shida moja kubwa sana ya maji. Wananchi wanafuata maji kilomita 12 ni dharura gani nyingine ambayo mtawapa watu wa Iramba? (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nitaomba wakati mnatoa majibu kwa kweli kwenye hili msije mkasahau kwa sababu ni moja ya eneo ambalo lina shida kubwa sana. Lakini ukienda hata Kata ya Kidaru mvua iliponyesha walipanda mazao baada ya kunyesha mvua mazao yote yalikwenda na mafuriko na ni eneo ambalo ni zuri kweli kweli kwa kilimo. Kwa nini tusibuni mabwawa haya ili wananchi wanapolima waweze kumwagilia lakini wakati ule ule waweze kutumia maji kwa ajili ya mifugo pamoja na shughuli za ujenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa Iramba vipaumbele vyote vitatu hata ukienda mpaka vitano watakuambia ni maji, kwa sababu tunakosa walimu kwa sababu hakuna maji. Mwalimu akipangiwa muda kama huu anachukua baiskeli kufuata maji kilomita 12. akishatoka akisema nafuata mizigo harudi tena. Tunakosa watalaaam wa huduma za afya kwa sababu hakuna maji. Akipangiwa baada ya hapo na wengine unakuta yuko peke yake kwenye kituo cha kazi nani amletee maji? Ni moja ya eneo ambalo kwa kweli Mheshimiwa Waziri inabidi uliangalie kwa macho yote mawili.

Kuanzia mwezi huu kuna shule nyingi tu za Wilaya ya Iramba hata mimi wakati nasoma ilikuwa hivyo, wanafunzi wataanza kusoma mpaka saa 6.00 baada ya hapo waondoke wakatafute maji. Tutaboresha elimu katika Wilaya yetu. Kwa hiyo, naomba kwenye hili kwa kweli lipewe kipaumbele na mimi Mheshimiwa Waziri nakuamini na Naibu Waziri namuamini naombeni wakati mnatoa majibu muainishe kabisa ni kwa namna

gani katika mwaka huu wa fedha muweze kutenga fedha ambazo zitakwenda kusaidia angalau Makao Makuu ya Tarafa ni miji ambayo inaendelea kama Ulemo iweze kupata maji ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika jambo hilo hilo namshukuru sana Waziri wa Nishati na Madini. Nimepata baadhi ya vijiji ambavyo tayari vinapitiwa na nguzo nimepata umeme. Sasa jambo litakalosalia kama umeme umeshapita kwenye hivyo vijiji kama Kitukutu, Simbalungwala, litakalosalia ni *motor* tu za maji. Maji pale yapo chini. Kwa hiyo, nitaomba sana Mheshimiwa Waziri nikupe ile list ambayo vijiji vimepata umeme mtuwekee bajeti ambayo tutapata maji ili wananchi wa maeneo yale waache kuhangaika kutafuta maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye haya maeneo niliyosema ya mabwawa tungeweza kupata mabwawa mimi nina uhakika hata hii habari ya kuomba chakula cha msaada kwa Iramba itakuwa imeondoka kwa sababu maeneo haya ninayoyasema kama Urugu mabwawa yao ya umwagiliaji yakiweza kuwekwa kwa kiwango cha kutosha ardhi ile ina rutuba na inaweza kulisha Wilaya yote ya Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo ningependa niongelee mimi nisema kule kwa watendaji wenzangu mtu ambaye atacheza na maji tutairudisha sungusungu. Mheshimiwa Waziri nimekuomba na nimeongea kwa utaratibu kwa siku ya leo kwa ajili ya unyeti wa suala hili. Lakini nasema kama hutatoa majibu wakati unahitimisha mjadala huu,

"*tunumao*", naapa kikwetu, haki ya Mungu ukija Iramba hutaoga. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, mimi nitakuomba sana utakapokuwa unajumisha nisikie habari ya Kinampanda, nisikie habari ya Uremo, nisikie Mseko, Mgongo, Malendi, nisikie Kipuma, nisikie Mbelekesi, Kikonge hapo tutaelewana na mimi kwa sababu najua ili uweze kuleta fedha kule kwanza tunatakiwa tupitisha bajeti hapo. Bajeti yako itapita lakini utakapokuwa unajumuisha ni lazima wana Iramba watakuwa makini kusikiliza unasema nini kuhusu tatizo hili la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kupandisha jazba leo kwa sababu nimeongelea mambo ya msingi sana yanayohusu jimbo langu mambo ya maji. Nitaomba niishie hapa lakini nikukumbushe tu leo ndio siku ya saba imefika kwenye suala ulilolitolea muongozo hapa nitaomba baadaye ultolee maelezo ili unielekeze.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, jikite kwenye Bajeti ya Maji.

MHE. MWIGULU L. M. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, niishie hapa kwa hili la leo kwa sababu wana Iramba walikuwa wanatamani sana kusikia habari ya maji. Nakushukuru sana. Naunga mkono hoja hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Spika, alitoa taarifa ya kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu kukaimu nafasi ya Ukuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Lakini kwa

maelekezo niliyopewa ukaimu huo ulikuwa unaishia siku chache. Sasa kwa heshima na taadhima ninaomba niwatangazie sasa nimepokea rasmi barua kutoka kwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pindi akiliarifu Bunge kwamba Mheshimiwa Samuel Sitta atakaimu nafasi ya Ukuu wa Shughuli za Serikali Bungeni kuanzia tarehe 10 Julai, 2012 hadi tarehe 15 Julai, 2012.

Hii inatokana na shughuli inayomkabili Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza anakwenda kushiriki Mazishi ya dada yake huko Mjini Mpanda. Lakini vile vile atakuwa na shughuli nyingine za kikazi na hivyo basi kwa takribani siku hizo alizozisema hapa Mheshimiwa Samuel Sitta ataendelea kukaimu nafasi hiyo ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Nimepokea barua hiyo rasmi, basi tumtakie kila la kheri Mheshimiwa Samuel Sitta katika kusimamia shughuli za Serikali hapa Bungeni na sisi wote tutampa ushirikiano wa kutosha. (*Makof*)

Pia nimepokea tangazo muhimu sana kutoka Ofisi ya Bunge ninaombwa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Tume ya Kukusanya Maoni ya Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea na kazi yake na kwa sasa Tume hiyo iko hapa Mjini Dodoma kuanzia leo tarehe 10 mpaka tarehe 13.

Sasa Ofisi ya Bunge imetuletea ratiba ifuatayo: Waheshimiwa Wabunge mtu atakayekuwa na nafasi kwa saa zile ambazo shughuli zetu za Bunge haziendelei anaweza kwenda kushiriki na kutoa maoni na kuona shughuli zinavyoendelea. Nimeambiwa kwamba tarehe 10 saa 3.00 mpaka saa 6.00 Tume

itakuwa Dodoma Mjini, saa 8.00 mpaka saa 11.00 Tume itakuwa Dodoma Makulu, tarehe 11 mwezi huu wa saba saa 3.00 mpaka saa 6.00, Tume itakuwa Veyula, Saa 8.00 mpaka saa 11.00 Tume itakuwa Ipala. Tarehe 12 saa 3.00 mpaka saa 6.00 Tume itakuwa Hombolo, saa 8.00 mpaka saa 11.00 Tume itakuwa Chihanga, tarehe 13 saa 3.00 mpaka saa 6.00 Tume itakuwa Kizota na saa 8.00 mpaka saa 11.00 Tume itakuwa Kilima. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, watakaopata muda wanaweza kwenda kutoa maoni yao au wataandika na kuwasilisha kwenye kamati hiyo ili kurahisisha kumbukumbu. Lakini ratiba hii tumeambiwa kwamba itagawanywa hili ni tangazo nimeletewa kutoka kwa Kaimu Katibu wa Bunge kwenye Ofisi za Bunge.

Tangazo la mwisho, Mheshimiwa Sylvester Mabumba Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (*Open University of Tanzania*) anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge waliosoma Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wanaosoma na wanatarajia kujunga na Chuo Kikuu hicho kujiorodhesha majina yao kwa ajili ya maandalizi ya Mkutano utakaofanyika Jumamosi tarehe 14 Julai, 2012 katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kujiorodhesha kunafanyika leo jirani na jengo la habari nyuma ya jengo la utawala sehemu zinapofanyikia sherehe. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwa wale wote wanaohitaji waende mahali hapo.

Tangazo langu la mwisho kabisa mchana tutakarudi labda sana sana naweza kuruhusu mchangiaji mmoja ama wawili kulingana na muda

nitakaokuwa nao. Nataka kumpa muda wa kutosha Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi wa mambo hapa. Lakini katika vifungu, ninaomba niendelee kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, tutakapoingia kwenye mshahara wa Waziri eneo hilo sasa siyo tena kila mtu aanze kukumbusha mradi wake ni eneo la kuzungumzia masuala ya kisera.

Mheshimiwa Spika alishatoa mwongozo alipokuwa anahitimisha shughuli za Bunge wiki iliyopita siku ya Ijumaa. Kwa hiyo, naomba sana tupeane ushirikiano isije ikaonekana kitu nacho sasa mara zote kina-intervene na kutoa miongozo ya utaratibu wakati ule wa mafungu si jambo jema sana na halipendezi. Kwa hiyo, naomba sana tujikite kwenye sera ili tuweze kuboresha sera ya maji katika nchi yetu ya Tanzania na kutoa umuhimu wa maji kama kipaumbele kwa wananchi wote wa Tanzania.

Baada ya kusema hayo naomba sasa nisitishe shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00
jioni)
(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia
Kiti*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika kipindi cha jioni na tunaendelea na ratiba ya jioni. Kabla sijaendelea, naomba nimwite Katibu atupe

mwongozo. Kama tulivyoanza, hoja iliyoko mbele yetu ni kwamba Bunge liendelee kukubali kupidisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na majadiliano yanaendelea. Kwa hiyo, nadhani nimwite Mheshimiwa Eugen Mwaiposa na nitaendelea kuangalia muda wangu ili tuone kama tunaweza kuongeza mchangiaji mwingine, halafu niwape nafasi Waheshimiwa Mawaziri. Mheshimiwa Eugen.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, lakini pia nikushukuru kwa kunipatia nafasi. Baada ya shukrani zangu, naomba sasa nichangie na kuleta malalamiko ya wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa Waziri husika kwa kupitia kwako Mheshimiwa Mwenyekiti.

Katika historia tangu Tanzania ipate uhuru, maji safi na salama hayajawahi kupatikana katika Jimbo la Ukonga. Jimbo la Ukonga ni Jimbo ambalo limesahaulika sana katika bidhaa hii muhimu ya maji na maji yanayotumika mpaka sasa ni maji kutoka katika visima vifupi. Kwa kipindi chote ambacho ninaifahamu Ukonga kama nilivyosema kihistoria, hakuna hata wakati mmoja ambapo tumepata maji ambayo ni ya uhakika.

Nitangulie kusema kwamba hata wanawake walinchagua Ukonga kwa sababu waliona kwamba mimi ni mwanamke mwenzao na ninaijua vizuri sana adha ya maji wanayoipata. Kwa hiyo, walitegemea kwa kuwepo kwangu humu ndani, kwa kuwepo

kwangu katika Jimbo la Ukonga kungesaidia sana kupata maji safi na salama. Kwa hiyo, ninamwomba sana Waziri anisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 wakati tunazungumzia bajeti ya Wizara hii, nilisimama na kumuomba Waziri, lakini Waziri aliniahidi kabisa kwamba maji yatapatikana kutoka katika Mto wa Kimbiji, lakini cha kusikitisha mpaka sasa hivi kama Waziri mwenyewe alivyokiri katika kitabu chake hiki ni kwamba mradi huo haukuweza kukamilika na wanategemea kuukamilisha mwaka, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014, imebakia kidogo tu tuingie kwenye uchaguzi na mimi napenda sana kuendelea kuwepo katika Jumba hili. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie njia nyingine ya kuleta maji katika Jimbo la Ukonga bila kutegemea huu mradi wa Kimbiji. Lakini ukiangalia katika mpango mzima pamoja na utekelezaji wake katika kitabu hiki ambacho ametugawia Waziri, hakuna hata sehemu mmoja ambayo Jimbo la Ukonga limetajwa.

Ukiangalia katika kurasa za 56, 57, 58 na kuendelea, ambapo anasema kwamba kuna mpango mkakati wa dharura wa kuleta maji katika Jimbo la Ukonga, hakuna mahali ambapo Jimbo la Ukonga limetajwa. Mpango huo, kuna visima ambavyo vilichimbwa kwa kusaidiana. Wizara yake ikiwa inasaidiana na Serikali ya Ubelgiji lakini pamoja na nchi nyingine za Ulaya.

Katika visima 18 ambavyo vilichimbwa kwa wakati huo, hakuna hata kisima kimoja ambacho kilipatikana katika Jimbo la Ukonga, lakini sio hivyo tu, ukiangalia katika visima ambavyo alivichimba mwaka 2011/2012, pia mbali na visima hivyo 18, vipo visima vingine 11 ambavyo hakuna hata kimoja ambacho kilipatikana katika Jimbo la Ukonga. Visima vitano anasema kwamba vilikwenda Kinondoni, sita vilikwenda katika Wilaya ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati yote ambayo anaifanya Mheshimiwa Waziri, ameelezea pia kwamba mwaka 2010, Mheshimiwa Rais alitembela Jiji la Dar es Salaam na alijionea mwenyewe maneo kadha wa kadha ambayo yalikuwa na shida ya maji na Mheshimiwa Rais ameagiza kwamba vichimbwe visima 27. Ninataka kujua kutoka kwa Waziri: Je, visima hivyo 27 vya Mheshimiwa Rais, Jimbo la Ukonga litapata angalau kisima kimoja au viwili au litaendelea kuachwa hivyo? Ninamwomba sana Waziri katika hitimisho lake na kwa sababu nilishachangia pia kwa maandishi, namwomba sana aniambie kwamba ni kwa vipi tutapata maji katika Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimwambie Mheshimiwa Waziri, hapo alipowekwa ni pabaya. Ni pabaya kwa sababu nadhani Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea na tunamfahamu Mheshimiwa Waziri ni mchapa kazi, lakini kama hakuwa makini katika kutembelea sehemu mbalimbali ambazo zinahitaji maji, naona kwamba hapo, jumba hilo bovu litambomokea. Ninamuomba sana ajitahidi sana

kuhakikisha kwamba anatoka ofisini kutembelea maeneo na asitegemee kabisa watendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo visima ambavyo vimechimbwa na *DAWASA*. Visima vingi vilivyochimbwa na *DAWASA* pamoja na Manispaa mbalimbali havitoi maji. Mfano mzuri ni visima sita ambavyo vilichimbwa katika Kata ya Pugu, ambavyo vilikuwa vimeahidiwa na Serikali kwa ajili ya kuwafanya wananchi wanaoishi pale Pugu ambapo kumehamishiwa lile dampo, wapate maji safi na salama. Mimi nataka kujua vile visima sita ambavyo havitoi maji hata kimoja ni kwamba fedha imepotea na wananchi wameliwa ama vitarudiwa tena. Lakini nataka kujua jambo lingine, hawa wataalamu waliokwenda kupima sehemu hizo na wakahakikishia Serikali kwamba maji yapo chini na maji hayakutoka, wamechukuliwa hatua gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinapotea nyingi na wataalamu wapo na hawachukuliwi hatua za Kisheria na namuomba sana visima hivi sita virudiwe ili wananchi wa Pugu waweze kupata maji safi na salama badala ya kunywa yale maji machafu ambayo yanatoka kwenye kemikali ambazo ni za takataka. Namwomba sana Waziri ajue kabisa kwamba Jimbo la Ukonga liko katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa hiyo, anapoleta miradi, asiishie kwenye maeneo mengine tu kwa sababu Serikali imekuwa na uzoefu mzuri wa kuwaamishia wananchi wake pale tu ambapo wanahitaji sehemu za wananchi hao kwa ajili ya maendeleo mbalimbali. Lakini wameshindwa kabisa

kufuatilia vizuri miundombinu ya maji katika sehemu hizo ambazo wananchi hao wanahamishiwa. Nilikuwa naomba sana mambo haya yaende sambamba nasikia pia kuna wananchi wanaotakiwa kutoka Kipunguni kuletwa katika Jimbo la Ukonga. Kabla Serikali haijafanya hivyo, ihakikishe kwamba inapowapeleka basi na miundombinu ya maji inapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuongea mengi sana, kitu ambacho ninataka kumwambia Mheshimiwa Waziri, kusikia kwamba maji yatakuja lini Ukonga na yatakuja kwa njia gani. Vinginevyo tutaendelea kubanana na Mheshimiwa Waziri mpaka kieleweke kwa sababu ninahitaji sana kurudia tena nafasi ya Ubunge na kuonekana katika Jumba hili, vinginevyo kama ye ye hataki kuniona tena, basi aninyime kabisa visima katika Jimbo la Ukonga, kitu ambacho siamini kama Waziri atakifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikiongea sana naona kwamba naweza nikakosa visima. Nitaunga mkono hoja kama nilivyoandika kwenye mchango wangu wa maandishi iwapo tu atakapokuja kuhitimisha ataniambia kwamba ni namna gani Jimbo la Ukonga linapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Eugen na hasa kwa kutunza muda sasa umenifanya

niongeze mtu mwingine mmoja wa ziada. Mheshimiwa Mkapa na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mipata.

MHE. DUSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ambayo nilikuwa naingoja kwa hamu sana. awali ya yote naomba niunge mkono hoja hii, lakini naiunga mkono kwa sababu moja maalum. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 21, naomba ninukuu.

Anasema: "Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini kuitia mradi wa maji shirikishi unaoratibiwa na SADC zimetengewa jumla ya dola za Kimarekani laki nane kwa ajili ya kutekeleza jumla ya miradi sita ya kijamii. Miradi hiyo imepangwa kutekelezwa katika Wilaya tano za Mkoa wa Mtwara na Ruvuma ambazo ni Songea, Tunduru, Tandahimba na Mbinga. Ujenzi wa miradi hiyo unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2012 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2012". Kwa mtaji huu, nimelazimika niunge mkono hoja hii. Nashukuru ahsante sana. (*Makofi*)

Mradi huu utakuwepo pale Mangaka ambapo wametengewa Dola za Kimarekani 168,700 nadhani. Kwa hiyo, naomba nifikishe shukurani zangu kwa Mheshimiwa Waziri lakini vile vile nawaomba wananchi wa Mangaka waupokee mradi huo kwamba uende ukatatue tatizo la maji pale Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu, Mangaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna changamoto nyingi sana Wilayani kwangu Nanyumbu. Nanyumbu hatuna vyanzo vyatya maji vyatya uhakika,

hakuna Mito inayotiririsha maji kuanzia January hadi Desemba na huko chini ya ardhi hatujui kama kuna maji au vipi. Kwa hiyo, tatizo la maji ni kubwa na ni kero namba moja sana Wilayani kwangu Nanyumbu maji, kila ninapopita kufanya mikutano ya hadhara, hakuna hata Kijiji au Kitongoji nitakachofanya mkutano bila kuambiwa tatizo la maji. Ninaomba sana Wizara ya Maji isikilize kilio changu Wilaya ya Nanyumbu tuna shida ya maji. Kata zote 14 hakuna hata Kata moja ambayo utasema kuna unafuu wa maji. Ukienda Kata ya Chipuputa tatizo la maji ni ukame mtupu. Namaguluvi, Namasogo, Mkohora, Mhinawe kote hakuna maji. Ukienda Kata ya Nanyumbu vivyo hivyo kule Chitowe, Namalombe, Maneme, Ziwani, Nanderu.

Makanya pale wakati tunafanya mkutano nililetewa maji, nikafikiria ni pombe ya kienyeji kumbe ni maji. Yanatisha sana tena sana. Hata mimi niliwaonea huruma. Lakini nakuomba Waziri wa Maji, naomba usikilize kilio changu cha Wilaya ya Nanyumbu. Ukienda Mikangaula, kuna Kijiji pale Nawaje, masikini watu wale hata alipokuja Rais aliona ile hali na akatoa maagizo pale Wizara ya Maji wasaidie pale. Chitandi, Mkwajuni, Namatumbusi, Mkoromwana, Mkambata, Kilosa na Mpindindi huko kote tatizo la maji. Ukienda Kata ya Maratani, Lipupu, Malema, Mchangani, Mraushi kote ni shida ya maji na maeneo mengi ya Wilaya ya Nanyumbu ni kame.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri ukishindwa kuja wewe mwenyewe basi mtume hata Naibu wako aje Wilayani Nanyumbu aone hali halisi kuanzia mwezi huu wa saba hali inakuwa mbaya sana, ukame kila mahali.

Utakuta akina mama wanaamka alfajiri ya saa tisa, kumi, kwenda kutafuta ndoo moja tu ya maji. Huko wanakumbana na wanyama wakali, kuna nyoka na mambo mengineyo ambayo pengine inatokea, hata ndoa zinaweza kuvunjika kwa sababu mama anatoka alfajiri ya saa 10.00 anarudi saa 5.00, 6.00 na ndoo moja tu ya maji. Jamani, naomba mtusaidie Wilaya ya Nanyumbu ili kuweza kutatua kero ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Rais alikuja mwaka 2011 mwezi wa Saba tarehe 29 pamoja na mambo mengine tulimwelezea tatizo la maji Wilayani Nanyumbu, akatoa maagizo Wizara ya Maji kulikuwa na Mkurugenzi pale wa maji akamwambia naomba Wizara itafute mkakati ni kwa jinsi gani mtatatua kero ya Maji Wilaya ya Nanyumbu. Hilo nategemea leo hii Waziri mwenye dhamana ya maji, mwenye hotuba hii, atatupa maelezo, majibu ya maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoagiza kwamba Wizara itafute mpango mkakati au ipange mpango makakati wa jinsi ya kutatua kero ya maji Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili limekuwa kubwa sana, labda niseme mwaka juzi kuna Mama mmoja alikuwa anakwenda kuchota maji alfajiri, sasa kwa kuwa yale yale maji ndiyo yanatumika pamoja na wanyama wakali, masikini Mama yule akakumbana na tembo njiani, akauwawa. Kwa sababu tu alikuwa anakwenda kutafuta maji. Kwa hiyo, unaweza kuja tatizo hilo la maji Wilayani Nanyumbu liliyvo kubwa. Nchi ni kame, kame, kame kupindukia. Wananchi wangu wanapata tabu sana ya maji na nafikiri wanaponisikia sasa hivi, wanajua kweli Mbunge wao

nawatetea, jamani mimi nawateteeni hapa na natumaini kilio changu hiki kitasikika na kitamfikia Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu mwaka 2007 ni watu 8900 amba ni sawa na asilimia 8.1 wa wakazi wote wa Wilaya ya nanyumbu ndiyo walikuwa wanapata maji safi na salama. Lakini mwaka 2011, ni watu 40,000 amba ni sawa na asilimia 26 walikuwa wanapata angalau lita 25 za maji kwa siku. Sasa unaweza kuona ukubwa wa tatizo hili Wilayani Nanyumbu. Mimi naomba sana Wizara ya Maji msikie kilio changu, wananchi wangu wa Nanyumbu wanapata taabu, kote huku Chivirikiti wanapata tabu, Ulanga, Mtalikachau.

Naomba sana Wizara ya Maji mtusaidie. Lakini cha kushangaza kuna maji ya Mto Ruvuma, maji yale yanamwagika tu tena kwa wingi yanaishia Baharini, hivi Wizara haiwezi kupanga mikakati au kutuwekea pale mradi mkubwa wa maji tukafaidika na sisi watu wa Nanyumbu kama walivyo watu Mwanza, Shinyanga na Mikoa mingineyoambayo tayari kuna mradi mkubwa wa maji ulioweza kutatua kero ya maji katika Mikoa hiyo. Naomba sana Wizara ya Maji muone ni jinsi gani mtaweza kuyatumia hayo maji, muone ni jinsi gani mtaweza kuweka pale mradi mkubwa wa maji ili muweze kutatua tatizo la maji Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja hii, lakini naomba mtuone

kwamba watu wa Nanyumbu ni watu tunapata taabu sana ya maji. Ahsante sana.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia Wizara muhimu sana. Nimeisoma Bajeti vizuri na nimeona mafungu yaliyotengwa, nikianzia na mwaka jana, tulitenga zaidi ya shilingi bilioni 446. Katika fedha hizi, fedha za ndani zilizotengwa ni shilingi bilioni 41 tu peke yake. Mwaka huu kadhalika, zaidi ya shilingi bilioni 485 zimetengwa, fedha za ndani ni shilingi bilioni 140 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, bado tuko tegemezi zaidi katika Miradi ya Maji. Tusipokuja na mkakati wetu wa kujitegemea, tutayumbishwa. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali ije na mkakati wa kuhakikisha Miradi hii muhimu na kwa umuhimu wa maji, tuwe tunagharamia kwa pesa yetu kwa kiwango kikubwa zaidi, tusitegemee watu wa nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ibara ya 81, nimeona Bwawa la Kawa, ambalo katika Bunge lako limewahi kuzua kelele nyingi na pia kule nyumbani lilizua kelele nyingi; chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa, tulikutana tarehe 28 Mei 2012 tukakubaliana kwamba, kimsingi, inaeleweka kwamba, Serikali imelikoroga bwawa hili, kwa wananchi halieleweki vizuri. Kwa hiyo, tukakubaliana tuseme yaishe, lakini yaishe namna gani; yaishe kwa vijiji vinavyozunguka na vinavyotajwa

kwenye Mradi ule kupatiwa maji, itabaki na heshima.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa hili limegharimu zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni tisini na mbili, haitaleta maana kama wanufaika watakuwa watu wachache. Wizara ilikuwa inang'ang'ania katika mazungumzo ya juzi tulipokuwa tunalizungumza kwamba, wataweza kuweka miundombinu katika vijiji viwili. Mimi nasema hapana, vijiji viwili bado ni vichache; wapeleke Kijiji cha Fyengelezya, Kijiji cha Nkundi na Kijiji cha Kalundi, ni hela nyingi. Kama Serikali, inataka heshima kwa watu na kelele ziishe, tufanyehivyo. Tupate maji na mwekezaji apate maji kwa sababu sote tulikubaliana hivyo. Hapo mjue kwamba, jambo hili litaisha kwa heshima kwa sababu limeanza kwa vurugu na vurugu mlizianzisha ninyi wenyewe.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mwaka jana kuna mtandao wa maji uliporomoka Mji Mdogo wa Chala ulioko Jimboni kwangu. Niliuliza maswali hapa nikajibiwa, lakini sikupata kitu chochote. Ulitajwa kwenye bajeti na mwaka huu tena umetajwa; Chala - Laela, lakini Miradi haipo na watu hawa wako hoi bin taabani, hakuna maji. Chala ina watu zaidi ya 10,000 na ni Mji Mdogo, hakuna maji kabisa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa asiitaje Chala kwa miaka miwili mfululizo na Mbunge anaona, halafu hakuna hela zinazotoka; haifai. Nataka kuona mwaka huu Chala inapatiwa pesa au mwelekeo *positive*, unaoonesha kwamba, katika siku za hivi karibuni tunapata maji. Isitajwe tu na kuachwa, bora hata

msiandike kwenye Kitabu cha Bajeti; ni ku-*provoke* watu waanze kusema maneno mengi. Hakuna maji Chala na kuna hali ngumu sana.

Chala pia kuna Mradi wa *World Bank* ambao nao unasuasua, upo katika hatua ya kuutangaza hivi sasa, upo kwenye Hatua ya III. Ninataka muusukume haraka, mjenzi ameshaomba, bado tunasubiri matokeo ya Benki ya Dunia katika uamuzi wa mwisho, lakini ni kwa Kijiji kidogo tu cha Chala B. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hii imekuwa na matatizo; pale Kisula kuna matatizo ni Mradi huu, Mpasa wapo kwenye Mradi huu lakini wananchi wanaambiwa wachange shilingi milioni kumi kugharamia ule Mradi ulivyo mkubwa. Tuiangalie hii Miradi ni tabu. Kwa hiyo, ninataka kusema kwamba, Chala na maeneo mengine haya ambayo yako kwenye Mradi huu wa Benki ya Dunia, ipewe msukumo wa pekee kuhakikisha kwamba, maji yanapatikana katika kipindi kisichokuwa kirefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mjini Namanyere, tuna shida ya maji, mwenzangu alizungumza na mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini pia nilizungumza na nimewahi kuuliza maswali mara mbili. Siyo vizuri Rais wetu amekuja pale, akasomewa taarifa vizuri sana na aka-*comment*. Mimi ni Mwenyekiti wa CCM, nilikaa jirani na Rais, akasema ninyi watumishi hebu njooni hapa, acheni kubabaisha ni lazima ufile wakati tatizo la maji Namanyere liishe, hebu semenihapa. Mhandisi yule ni mkakamavu akasema, Mheshimiwa Rais, hali ilivyo hapa tunatoa asilimia 16 tu ya mahitaji ya maji ya

Mji wa Namanyere. Mheshimiwa Rais akasema hapana, tafuta namna nyingine yoyote tuhakikishe tuna-*double* au tunazidisha kupata maji yanayotakiwa kupatikana hapa kabla hata ya uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uchaguzi akaja akasema maji yatapatikana, tukampigia makofi lakini mpaka sasa hakuna maji Namanyere. Mke wangu akienda kuchota maji ni lazima nibebe mkuki nimsindikize; nitasindikiza mara ngapi na Bungeni nimeingia? Bungeni nimeingia ili nije nipiganie maji, sasa bado naenda Nkasi kumsindikiza mke wangu na mkuki kwenda kwenye vidimbwi! Mimi nasema, bila uamuzi wa uhakika hapa katika suala la maji Namanyere, niko pamoja na Mheshimiwa Keissy na wengineo wote, kutounga mkono hoja tena kwa mara ya kwanza nikiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi; umewahi kuona kitu cha namna hiyo? (*Makofi/Kicheko*)

Tusaidie Mheshimiwa Waziri, ndiyo mwenye dhamana ya kutusaidia, ulione hilo. Tunashangaa zaidi tunapoona mahali pengine maji watu wanapewa, ingekuwa hakuna kwa wote tungeelewa. Hapa nayaona na pale nayaona, lakini kwangu tu ndiyo hakuna, haiwezi kueleweka. Naomba hili liangaliwe kwa makini sana. Hatuwezi kwenda Nkasi bila maji tutakosa heshima. Tunaonekana kama Wabunge ambao hatuzungumzii matatizo ya maji au matatizo yanayohusu watu wetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, viji viyetu vyote havina maji ya kutosha. Naomba Serikali ijaribu

kushirikiana na Mradi huu wa Utunzaji wa Bonde la Ziwa Tanganyika ili kuwezesha Miradi ambayo wanaweza wakagharamia wao kule, watusaidie suala hili la maji mwambao mzima; Namansi, Ninde, Wampembe, Kala na Mpasa, kote kunazuka magonjwa mabaya ya kuhara na kipindupindu. Itatusumbua sana tusipopata suluhu ya kudumu katika suala hili. Ningeomba Serikali ije na mawazo ya kushirikiana na wenzetu wa Utunzaji wa Bonde lile, tunaweza kupata maji kwa kusaidiana. Wapo tayari, wamekuwa wakibainisha Miradi mbalimbali, naomba hili liwe katika ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Ufipa yote ya juu hapa kwenye Jimbo la Nkasi Kusini, ukienda Kisura tatizo, ukienda Milundikwa tatizo, ukienda Kasu tatizo, ukienda Kipande tatizo, ukienda Mpasa, Kana, Sintali, Kate, kote huko ni matatizo matupu. Kate, kuna chanzo kizuri sana cha maji tena ya kutega, unaweza kuyatega yakatawanya vijiji zaidi ya kumi, inaweza ikatusaidia. Kadhalika, Wampembe kuna chanzo kizuri sana cha kutega, ukitega pale unaweza ukasaidia Vijiji vyote vya Wampembe, itatusaidia sana. Badala yake, Halmashauri wamekuwa wakitengeneza kwa miundombinu dhaifu ambayo haimudu tena maji kutirishwa kule chini. Kwa hiyo, nawaomba uwepo uangalifu na usimamizi wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Siungi mkono hoja mpaka hapo nitakaposikia maji Namanyere yapo, maji Chala yanasema chochote na katika Jimbo langu la Nkasi Kusini. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo nilioutoa ni kwamba,

Mheshimiwa Mipata, ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho na yeye amezungumza kwa hisia kuhusu maji.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono bajeti hii. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu nzima ya Wizara hii katika kuleta hotuba hii ya maji iliyojaa matumaini. Pamoja na maelezo niliyotoa hapo juu, kubwa la msingi tunachohitaji ni utekelezaji wenye tija tuone matendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai wa kila kitu kwa maisha ya binadamu. Tanzania tumezungukwa na maji na vyanzo vyake pia kila mahali, pia tuna bahari, maziwa, mito na kadhalika hadi kidunia tupo na tunatambuliwa kama nchi iliyoko katika "Great Lakes" lakini jambo la ajabu ni kwa nini maji yanapungua badala ya kuongezeka? Wananchi bado wanaendelea kutaabika na maji yasiyo na uhakika wala salama. Kwa nini tusiwe na "Water Regulatory Authority" au *Fund?* Hizi *Water Agencies* kama DAWASA, DAWASCO zinafanya kazi gani zote zikiwa Dar es Salaam? Za Mikoa ni nazo *effectiveness* yake iko wapi? Haionekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji itokanayo na ufadhili wa Benki ya Dunia imekuwa ni utata siku zote na ni kwa nini hili linatokea na kwa nini tuendelee kutegemea ufadhali huu ambao hauna matunda yoyote? Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipiatiwe majibu ya masuala niliyochangia hapo juu, nawasilisha.

MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono 100/100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika sehemu zifuatazo; maji katika Tanzania, kuondoa tatizo la maji na kuongeza bajeti ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, maji katika Tanzania. Kwa kuwa nchi yetu ina vianzio vingi vya maji kwa mfano Ziwa Victoria, Mto Nile na sehemu nyingi ambazo tukiamua kuchimba maji yanapatikana. Sasa ingefaa Serikali yetu ikasimama imara kwa kuangalia njia madhubuti ya kuweza kutumia vianzio hivi vya maji ili tuondoe lawama kwa Watanzania maana kila Mbunge akisimama anazungumzia tatizo maji, hebu urike wakati wa kulitatua tatizo hilo ili liwe historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuondoa tatizo la maji. Tatizo la maji limekuwa kubwa kwa nchi yetu, nashauri kuangalia upya miundombinu yote ya maji ili kati ya hayo maji yanayopatikana yasipote. Pia sehemu zilizokuwa na mabomba madogo ambayo yalikuwa yanatumika toka zamani ambapo kwa wakati huo kulikuwa na watu wachache, lakini kwa sasa watu wameongezeka, sasa inabidi mabomba yabadilishwe ili yalingane na mahitaji ya watu waliopo sasa kwa kila sehemu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuongeza bajeti ya maji. Maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013

zimekuwa kidogo kwa ajili ya fedha za maendeleo ambazo Sh. 465,756,338,000 ambazo hizo kwa mwaka huu ni kidogo sana kwa kutatua tatizo la maji katika nchi yetu. Kwa fedha hizi tutashindwa kumaliza tatizo la nchi yetu. Nashauri, kwa vile maji ni kila kitu unazaliwa, unaishi na unakufa unayahitaji maji, bajeti hii ingeongezwa maradufu ili tutatue tatizo hili linalotukabili kila mwaka, kwa vile ongezeko la watu ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza Profesa Jumanne Abdallah Maghembe na Naibu wake Mhandisi Dkt. Binilith Mahenge kwa kuteuliwa kwao kwenye Wizara hii yenye changamoto nyingi, kwani Rais ana imani nanyi hivyo msimuangushe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, ni vema ikafahamika kuwa Wilaya za Tandahimba, Newala na Mtwara Vijijini, siasa ni maji. Kama kuna jambo gumu kwa Serikali ni tatizo hili. Hivyo basi ni vyema jitihada za dhati na za kuonekana zikafanywa ili kumaliza tatizo hili. Ilani ya CCM ya 2005/2010 na ile ya 2010/2015 zote zimeonyesha haja ya kupunguza tatizo hili lakini kuna upeo wa kushughulikia tatizo hili, twende kasi, wananchi waone kuna ufumbuzi unaochukuliwa. Mifano ya kero ni pale Mkandarasi Mshauri

anapokamilisha kazi bila kubaini uwezo wa vyanzo vyatya maji ardhini (*Ground Water Assessment*) kwangu hii inatokana na wataalam wengi wa mradi na Wizara kutokuwa karibu sana na kinachoendelea. Matokeo yake ni kuchelewa kufanya ukarabati na hivyo kuleta manung'uniko kwa wananchi. Ipo haja Wizara kutazama na kusimamia kwa ukaribu mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kujua ni kiasi gani kimetengwa kwa mwaka 2012/13 kwa Mamlaka ya Makonde. Kuwepo kwa fungu la kutosha kutajenga mwelekeo wa kuwepo kwa *seriousness* kwenye mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa nini hadi leo hakuna mpango mahsuswa kurekebisha chujio pale Mitema? Chujio la maji la Mitema kwa saa huchuja maji kwa cm^3 3m kwa siku lakini likifanyiwa marekebisho linaweza kutoa maji cm^3 9m kwa siku, huku mahitaji halisi yakiwa cm^3 12m. Hivi Wizara haioni haja ya ukarabati wa chujio hilo ili tupunguze malalamiko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, naomba Wizara kufanya maboresho ya "*line*" ya maji katika Nanda hadi Tandahimba kutokea chanzo cha Mitema - Kitangari. Maboresho yazingatia hali ya ongezeko la watu kwani "*line*" hiyo ilijengwa miaka ya 1980 kukiwa na idadi ndogo ya watu kuliko ilivyo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Wizara isaidie Mamlaka ya Makonde ili kuwepo na mpango wa

uwajibikaji kwa rasilimali watu kwa kila Wilaya zilizopo kwenye mradi. Nikiwa na maana kila Wilaya kuwepo na mtaalam atakayekuwa akiwajibika na mradi badala ya hali ya sasa ambapo kila kitu hutendwa na wataalamu waliopo Makao Makuu ya Mamlaka hivyo hata jambo dogo huchukua muda na gharama kurekebishwa. Hivi tatizo la Mtwara Vijiji mpaka lifike Makondeko na mtaalam apangwe kwenda kurekebishwa unadhani itachukua muda mfupi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kwa nini Serikali isione haja ya kutumia maji ya Mto Ruvu ambayo hayapo mbali na maeneo ya *Makonde Plateau*?

MHE. DKT. EMMANUEL J. NCHIMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza kwa dhati rafiki yangu Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, (Mb) kwa hotuba yake nzuri ya bajeti, lakini pia kwa kazi nzuri anayoifanya yeye na wasaidizi wake katika kutafuta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maendeleo ya mradi wa maji na usafi wa mazingira uliosainiwa hapo tarehe 13 Machi, 2010. Pamoja na mambo mengine, mradi ulilenga kumalizia kazi zillizosalia katika Awamu ya I na II ya mradi wa maji safi na usafi wa mazingira uliokwisha kukamilika mnamo Agosti, 2008 na kufanyika kazi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupitia makabrasha ya mradi uliopita na kufanya usanifu wa mradi mpya ilikabidhiwa kwa Mhandisi Mshauri *Don Consult in Joint venture with consulting Engineering Centre, Jordan*. Kazi ya kutayarisha makabrasha ya

mradi ilianza hapo tarehe 12 Aprili, 2010 na kukamilika Julai, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi hiyo, gharama zilizobainishwa na Mhandisi Mshauri ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kazi za muda mfupi ambazo zilipangwa kumalizia kazi zilizosalia katika mradi wa awamu ya I na II (*immediate works*). Kazi hizi zilikuwa ni pamoja na kuongeza vyanzo vya maji, kumalizia ujenzi wa mtandao wa maji safi katika maeneo ya mradi uliokamilika (Bombambili, Msamala, *Seedfarm*, Mateka, Matarawe, Lizaboni), gharama zake ni jumla ya Sh. 49.52 bilioni.
- (ii) Kazi kwa ajili ya upanuzi wa maeneo mapya ya mji (*new works*) kama vile Mkuzo, Mshangano, Msamala, Ruhuwiko, Chabruma JWTZ, *Seedfarm*, Mateka, Ruvuma). Gharama zake ni jumla ya Sh. 40.314 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilishwa kwa kazi na Mhandisi Mshauri, Makabrasha ya Mradi (*Project Documents*) yaliwasilishwa Wizara (Wizara ya Maji) ili yapelekwe kwa Washirika wa Maendeleo (*Development Partners*) kutoa kibali cha kuendelea na mradi (*No Objection*), hatimaye pangetengenezwa zabuni ya kumpata Mkandarasi wa Ujenzi wa Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Julai, 2011 hadi leo, kibali cha kutangaza ili kumpata Mkandarasi wa Ujenzi wa mradi hakijatolewa. Hali hii inasababisha

SOUWASA kushindwa kufanya upanuzi katika maeneo mbalimbali na pia kuwepo kwa uhaba wa maji kwa kuwa vyanzo vilivyopo vilikuwa na uwezo wa kukabiliana na ongezeko la wakazi wa Songea Manispaa hadi mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba usaidie kufuatilia ili Wizara itoe kibali hicho ili mchakato wa mradi huo uweze kufanikishwa. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. MATHIAS M. CHIKAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitamke kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Nawapongeza kwa kuandaa bajeti nzuri ukizingatia hali halisi ya uchumi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono, naomba kuikumbusha Wizara wajibu wake wa kutenga fedha za kutosha ili kuumalizia mradi wa Mbwinji utakaoleta maji Masasi na Nachingwea. Mradi huu ulikuwa ukamilike mwezi Mei kwa mwaka huu, lakini mpaka sasa bado hakuna dalili na hatujapewa tarehe nyingine. Pengine Mheshimiwa Waziri atapenda kuwaeleza Wananchingwea ni lini wataanza kupata maji ya Mbwinji. Aidha, nashauri kuwa pamoja na chanzo cha Mbwinji, Wizara iangalie uwezekano wa kutumia chanzo cha maji cha Rupinda ili kuongezea nguvu maji yanayotoka Mbwinji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mradi wa kulima Karanga Nachingwea, kila shamba lilikuwa na bwawa lake. Kinachohitajika ni kuyafufua tu

mabwawa haya ili tumalize tatizo la maji katika Wilaya ya Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga tena mkono hoja hii ya Wiziri wa Maji.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa afya na kuweza kufikisha ujumbe huu kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza yeye binafsi Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na wote waliopo katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa kuendelea kutoa pesa kwa ajili ya kuondoa matatizo ya maji katika vijiji vyetu huko tulipotoka. Lakini pia naomba sana Serikali iweze kuwatambua waliotusaidia kuchimba visima ambavyo vimesaidia sana kupunguza kwa kiwango kikubwa tatizo la maji katika Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua waliotusaidia ni pamoja na:-

1. *Islamic Help (UK)* - visima 30;
2. *MIDEF (Mafia Island Development Foundation)* - visima 15;
3. *African Muslim Agency (T)* - visima 15; na
4. *African Relief of Kuwait* - visima 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wengi ambao misaada yao wametusaidia kupunguza tatizo hilo. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote bado tatizo la maji lipo. Nashukuru sana kwa mwaka huu tumetengewa Sh. 267,465,000 itasaidia kupunguza pia kero hiyo, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Mafia, tatizo kubwa ambalo linatukabili ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ametoa wakati wa kampeni ya kuvusha maji katika visiwa vidogo vidogo vya Mafia vya Chole, Juani na Jibondo. Hakika ahadi hii inatutukanisha sana na hata kumdhalilisha kipenzi chetu Mheshimiwa Rais. Naomba sana Mheshimiwa Waziri au Wizara ijitahidi sana kuja kufanya tathmini na hatimaye kuvusha maji katika visima hivyo. Naamini kwa ushirikiano tulionao, Wizara hii ya maji italionna hili na kuja kutekeleza ahadi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naamini tena Wizara itatekeleza ahadi hiyo na naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa hotuba hii na juhudhi wanazozonesha kutatua kero ya maji nchini, nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Maji ya mwaka 2011/2012 (bajeti), ukurasa wa 67 – 68 ilieleza kwamba Mji wa Sengerema ulikuwa umetengewa US\$ 14.8 kutekeleza Mradi huu. Fedha zinatoka AFDB na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Waziri wa Maji alieleza kwamba kazi ya ujenzi wa mradi huu kukidhi mahitaji ya maji ya muda mfupi katika mji wa Sengerema ultarajiwaka kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri, ukurasa wa 45 inaeleza pamoja na mambo mengine kwamba katika mwaka 2012/2013, Mhandisi Mshauri na Mkandarasi wataajiriwa ili kujenga miundombinu ya maji itakayotoa matokeo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua yafuatayo kwa vile mradi huu umechelewa sana.

- (i) Ni kufikia mwezi gani Mhandisi Mshauri na wakandarasi wataajiriwa? Ni muhimu kuelezea *time-frame* badala ya kusema kwa ujumla tu kwamba mradi utatekelezwa ndani ya mwaka 2012/2013.
- (ii) Je, ni lini hasa hii *short term intervention* itakamilika ili wananchi wapate maji ya uhakika kuliko ilivyo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa bajeti yenye

mkakati wa kusaidia wananchi wengi mijini kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iendelee kuchimba visima zaidi (virefu) ili kuyasambaza maeneo mengi wananchi wapate maji. Serikali imejenga malambo mengi na maeneo mengine mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ijikite kuimarisha mabwawa na malambo yaliyopo badala ya kutumia fedha kujenga mapya ambayo kwa sababu ya jua kali na mabadiliko ya tabianchi, visima vingi, malambo mengi yanakauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwe na mpango kabambe wa kutunza vyanzo vyaa maji vilivyopo, mfano mito na mabwawa. Mfano, Bwawa la Nyumba ya Mungu Mkoani Kilimanjaro linaharibika na maji kukauka kwa sababu ya mifugo na wavuvi kuvamia vyanzo vyaa mito inayopeleka maji katika bwawa hilo. Ziwa Jipe limetelekezwa na kwa sababu ya chanzo chake kutokutunzwa limejaa magugu maji kwa upande wa Tanzania. Upande wa nchi ya jirani ya Kenya ni kweupe na mara kwa mara wenzetu wanalikagua kuona kuwa magugu hayashamiri. Mito mingi Mkoani Kilimanjaro imekauka mfano mto Ugwasi Rombo, mto Himo na kadhalii. Nashauri Serikali itoe waraka kwa Halmashauri za Wilaya kutunza vyanzo vyaa maji. Ikitibidi Serikali itoe cheti cha ushindi kwa Halmashauri zitakazofanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji mjini Dar es Salaam bado ni kubwa. *DAWASCO* wanaweka *meter*

za maji lakini bado maeneo mengi hayana meta za maji. Mabomba mengi yanavujisha maji na maji mengi yanapotea njiani. Nashauri Serikali iweke *meter* katika makazi ya watu wengi zaidi ili kuweza kukusanya fedha za kutosha na baadaye kukarabati mabomba machakavu, yanayosambaza maji mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya Dar es Salaam yanaendelea kuwa machafu. Maji yamejaa tope ambapo ni vigumu kufulia nguo nyeupe. Nashauri Serikali iweke madawa ya kutosha/kuchuja maji vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Benki ya Dunia ya vijiji kumi imekuwa ya ahadi nyingi kuliko utekelezaji. Ahadi hii imeanza muda mrefu tangu 2004. Wabunge wanaulizia suala hilohilo Bungeni. Nashauri Serikali ifuatilie kikamilifu zaidi ili vijiji hivi vipate maji. Azma hiyo itakuwa ni utekelezaji mzuri wa llani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa ahadi wa Benki ya Dunia, usiingilie mipango ya maji ya Halmashauri za Wilaya. Nashauri Serikali iendelee kuboresha na kutekeleza miradi ya maji iliyoko katika mipango ya Wilaya na ifanye pia kazi kwa karibu na wafadhili wengine kama *World Vision*, *Plan International*, *GTZ* na kadhalika. Halmashauri za Wilaya zitoe maelekezo kwa wananchi kutunza/kuotesha miti ya kivuli katika vyanzo vyao maji ili viwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasita kuunga mkono kwa kuwa sina mradi unaojidhihirisha kwa kutengewa fungu la maendeleo katika Wizara hii. Mwaka jana Jimbo langu halikuwa na fedha na bajeti hii sijaona fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi iliyoko Jimboni mwangu hata Wilaya kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Chala hauna huduma ya maji na pamoja na maswali ambayo nimekuwa nikiuliza bado Wizara imekuwa kimya. Naomba mradi huu uanze mara moja. Mwaka jana nilielezwa kuwa kwa mwaka huu ungeweza kuonekana kwa hakika sikubaliani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Wampembe, hali ya huduma ya maji katika mji huu ni mbaya sana licha ya kuwa na idadi kubwa ya wakazi. Kwa kuwa kipo chanzo cha maji ya kutiririka, Serikali iweke mipango kunipelekea mradi wa maji mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji inayofadhiliwa na *World Bank*, nashauri Serikali itafute/ije na mpango mkakati kuhakikisha kero ya maji nchini inashughuliwa kwa fedha ya ndani. Maji ni uhai basi tusidhamini uhai wa Watanzania kwa matajiri. Bajeti yetu iwe inatenga fedha za kutosha katika kupunguza kero za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya utunzaji Bonde la Tanganyika, Wizara iongee na wanaosimamia mradi huu ili waweze kutusaidia katika suala la kuwapatia

wananchi maji katika vijiji vyote vinavyokuwa kandokando ya Ziwa. Hii itasaidia wananchi kuitikia na kutoa ushirikiano kwa yale yanayohamasishwa na mamlaka hiyo ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Vijiji ambavyo vina hali mbaya kabisa ni pamoja na Namansii, Ninde, Msamba, Kisambara, Lyapinda, Wampembe, Kala Mpasa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji mjini Namanyere, kama sisi Wabunge wawili kutoka Namanyere hamjatuelewa, naungana na Mheshimiwa Ally Keissy tuwalete akina mama waje wawaeleze shida ya maji iliyoko Mji wa Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliagiza maji yapatikane mjini Namanyere. Sasa nataka kujua nani anazuia, nisipopata jibu, nitamwandikia Mheshimiwa Rais barua iliyosainiwa na akina mama wanaoenda kuchota usiku maji kwenye madimbwi wakati ahadi ya Rais ilikuwa kabla ya wakati wa uchaguzi, alikuwa tayari katoa maelekezo, nani zaidi ya Mheshimiwa Jakaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Kawa. Licha ya kutajwa tu sijaona mahali fedha ya kuboresha miundombinu au kujenga miundombinu ya kupeleka maji kwenye vijiji vya Nkundi, Fyengelezya na Kalundi. Pelekeni maji kwa wananchi vinginevyo mtapata aibu kubwa. Mradi huu umepigiwa kelele sana na wananchi kwa namna ya utekelezaji wake ulivyokuwa, yote tumekubali yaishe lakini maji yaende kwa wananchi. Bila jibu, naondoa shilingi katika fungu la bajeti hii.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie katika hoja ilioletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite moja kwa moja katika hoja kwa kuzungumzia ujenzi wa Bwawa la Kidunda Mkoani Morogoro katika Wilaya ya Morogoro Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa bwawa hili, dhamira yake ni kuhakikisha Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro yenyewe inapata maji safi na salama na ya uhakika. Pesa ambayo imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili ni kubwa mno, shilingi 156.2 bilioni ambazo ni fedha toka nje na za ndani za walipa kodi. Nataka kujua Serikali imejipanga vipi katika kuona kuwa pesa hii italeta manufaa kwa wananchi wa Miji ya Kibaha, Mlandizi, Vijiji vya Kata za Kidunda yenyewe na Selemba ambako bwawa litajengwa pamoja na Jiji la Dar es Salaam ambako ndiko kunakolengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwendelezo wa wafugaji wavamizi katika Wilaya ya Morogoro na kusababisha uharibifu wa mazingira na hivyo kuchangia uharibifu wa vyanzo vingi vya maji (mito), kunaweza kusababisha uwepo wa mradi huu kutokuwa endelevu; kwani vyanzo vyote vya maji katika Mito ya Ruvu, Mvuha na Mgeta Kafa ambayo ndiyo itakuwa inatengeneza bwawa hili, imevamiwa na wafugaji wengi wavamizi. Ombi langu kwa Waziri wa Maji ni kuona kwamba inashiriki vipi katika vita ambayo Wilaya ya Morogoro na Mkoani wa Morogoro inapambana na ongezeko la wafugaji wavamizi

vinginevyo mradi huu pesa ambayo itatumika itakuwa inapotea bure na pengine ni busara ikafanya kazi nyingine za maendeleo. Kuanza ujenzi wa bwawa hili katika hali ya uharibifu wa mazingira katika eneo la mradi wakati hatujajipanga katika kukabiliana nalo, bwawa litakuwa limejaa au kufa si zaidi ya miaka mitano baada ya kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, mradi huu wakati umekusudia kunufaisha watu wa Dar es Salaam na Pwani, ni vizuri vilevile watu wa Morogoro Vijijini wakatamkwa nao watanufaika na mradi kwa maandishi na hasa Kata ya Kidunda, Setembala na Mvuha ambako ndiko kunajengwa Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Halmashauri kupewa pesa na Wizara kuitia (*DAWASA*) ili kupima viwanja na huduma za msingi kwa waathirika wa ujenzi wa bwawa. Tayari Halmashauri tumeshapeleka mahitaji yanayotakiwa ili kukamilisha zoezi hilo kwa Mkurugenzi Mkuu wa *DAWASA*, tungeomba basi tupewe fedha kwa haraka ili tathmini ikikamilika na fidia ikishalipwa, wananchi waelekezwe na kukabidhiwa maeneo ambayo tayari yameshaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Kidunda, nadhani wakati sasa umefika kwa Serikali kuhakikisha wananchi wote ambao wataathirika na ujenzi wa mradi huu wanapata haki zao zote za msingi ili waendelee na kujiletea maendeleo badala ya

kuwafunga kupata maendeleo yao kwa kusubiri hatma ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa visima 10 katika Halmashauri. Halmashauri yetu ni moja kati ya Halmashauri ambazo mradi huu haujaanza kutokana na sababu mbalimbali kama Mheshimiwa Waziri alivyoainisha katika kitabu chake cha bajeti ukurasa wa 28. Tunashukuru sisi kama Halmashauri kupata ridhaa ya Benki ya Dunia ya kufungua mapendekezo ya kiufundi na ya kifedha na kufanya majadiliano na Mtaalam Mshauri aliyejapata alama ya juu. Napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri, Halmashauri yangu imeshakamilisha taratibu zote na nyaraka zinazohitajika ziko Wizarani kwake kwa utekelezaji ili tuendelee na taratibu nyingine. Tunaomba utekelezaji huu ufanyike kwa haraka ili tuwasaidie wananchi ambao wana shida kubwa na kiu ya maji safi na salama kama llani yetu ya Uchaguzi ya CCM inavyosema katika eneo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la mwisho kwa Serikali hasa Wizara ya Maji tupatiwe walau kiasi cha Sh. 450,000,000 ambazo tuliomba katika *Special Request* ili Halmashauri ichimbe visima virefu na vifupi na ujenzi wa miradi ya maji ya mtiririko katika vijiji hivyo vya mradi na vingine ambavyo vina matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji tufanye safari ya pamoja Jimboni ili akaone adha wanayopata wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la maji ni tatizo ambalo linawakumba Watanzania wengi, vijiji na mijini maisha ya watu yanategemea maji, bila maji maisha hayapo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu, kuna Wilaya ambazo zina mito, maziwa makubwa na vyanzo vingine hasa Wilaya ya Mufindi ina vyanzo vingi sana vya maji lakini watu wana tatizo kubwa la maji. Katika Jimbo la Mufindi Kusini, wananchi wanapata shida kubwa ya maji hasa katika vijiji vya Idumulavanu, Ikangamwani, Mkangwe, Irangi, Nyingo, Maguvani, Ihawaga, Iramba, Kiliminzowo, Mtambuka, Kilolo, Maduma, Lwing'wolo, Udumuka, Kasanga, Ihowanza, Kwatwanga, Kiponda, Rugema, Idete, Magunguli, Sawala, Mtwango, Rufuna, Kibao, Igowole, Mnyololo, Bumuilayinga, Matanana, Ulole, Kisada, Kihanga, Mkalala, Ikwega na Mninga, Nzivi, Ibatu, Kisasa na Kitasengwa. Maeneo ambayo nimeyataja hapa ni vijiji ambavyo vina tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mufindi Kusini lina matanki saba (7) ambayo yapo lakini hajafanyiwa ukarabati tangu yajengwe miaka ya 1970/1980 lakini mpaka leo hii miaka ya 2011/2012 hakuna ukarabati wa miundombinu ambayo inasababisha maji yasifike kwenye matanki hayo. Matanki hayo ni Kijiji cha Sawala, Kijiji cha Kibao, Kijiji cha Nyololo, Kijiji cha Maduma, Kijiji cha Ihomasa, Kijiji cha Nyigo na Kijiji cha Igowole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wakati kipindi cha mkutano nauliza swali hili:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji katika Jimbo la Mufindi Kusini?

(b) Kwa kuwa Jimbo la Mufindi Kusini kuna miti mingi ambayo ni vyanzo vya maji, je, Serikali inatoa uamuzi gani wa kupeleka maji katika matanki ya maji haraka ili kuwanusuru watu wa Jimbo la Mufindi kupata maji ya bomba safi na salama?

MHE. STEPHEN M. WASIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeonelea nitoe maoni yangu kuhusiana na tatizo la maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechelewa sana kutekeleza Sheria ya mwaka 2009 iliyokusudia kuanzisha Mfuko wa Maji (*National Water Fund*). Ni vema Mfuko huu ukaanzishwa na kutafutiwa vyanzo vya fedha vya ndani na nje ili kuendeleza huduma za maji nchini. Pia naunga mkono hoja ya kuanzishwa kwa *TANWATER* ambayo itafanya kazi kama *TANROADS* inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji Bunda unaendelea na mkandarasi yuko *site*. Hata hivyo, ni ombi langu kwamba fedha iwepo ili kazi ilivyoanza isisimame tena, kwa vile mradi huu umekuwepo kwa miaka saba bila kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi wa Bunda wafaidike na shughuli za ukandarasi unaoendelea, ni vizuri tuandae mpango wa *distribution*, vinginevyo maji yatafika katika matanki ya mjini Bunda na bado tatizo la maji litaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/2012 katika hotuba ya Waziri, ilitolewa ahadi ya kuanza ujenzi wa Bwawa la Mugeta. Hotuba hii ni ya tatu kutoa ahadi hii bila utekelezaji. Kwa vile bwawa hili lilitanyiwa usanifu na Wizara na kilichobaki ni kuanza ujenzi, ni ombi langu kuwa bwawa lihesabiwe kama mradi unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono na kuwasilisha.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri na timu yake kwa kuleta hotuba hii nzuri sana ambayo imejaa miradi endelevu kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajitahidi sana kutafuta na kuboresha miradi ya maji ndani ya nchi yetu lakini kuna tatizo kubwa la maji safi na salama. Wale wananchi wanaoishi mijini, wenyewe uwezo mkubwa, ndiyo wengi wanafaidika na maji safi na salama na wale walio pemberi mwa mji, hawana maji haya ya bomba na wanunua maji kwa bei ya juu ukilinganisha na wanaotumia maji ya bomba kwani mwananchi anapochimba kisima anauza maji bei anayotaka, ndiyo maana umaskini unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali kama hii, naomba niishauri Serikali, mabomba yakipasuka yatengenezwe ili maji yawafikie wananchi wengi na yasiendelee kupotea kama ilivyo sasa mabomba hayatengenezwi, maji yanamwagika sana. Aidha, Serikali ikae na wananchi waliochimba visima na wapunguze bei ya maji kwa ndoo ili wananchi wapate unaifuu kidogo. Pia Mamlaka za Maji zipanue huduma za maji pembezoni mwa miji kwani wananchi wa maeneo hayo wanapata tabu sana ya maji lakini pia Serikali inapopima maeneo ya makazi ipeleke huduma hii ya maji kwa kusambaza miundombinu ya maji na kupeleka mabomba kwenye eneo husika ili wananchi wakitaka kujenga, huduma hii ya maji iwe imeshafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifanye tathmini ya Watanzania wanaotumia maji ya bomba wanalipaje kwa mwezi na wanaonunua maji kwa ndoo wanunua maji kiasi gani kwa mwezi ndiyo mtajua kwamba wananchi wenyе kipato cha chini wanaathirika kiasi gani juu ya ununuzi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kusema naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri wa Maji, Naibu na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kuandaa bajeti nzuri ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero kubwa na namba moja Wilayani Nanyumbu, ni kero ya ukosefu wa Maji. Nanyumbu tuna tatizo kubwa la maji. Hakuna maji kwenye mito, hatuna mabwawa, hatuna visima virefu vyaa maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007, kaya 1969 sawa na asilimia 8.01 ya kaya zote 25,827 ndizo zilikuwa zinapata maji safi na salama. Hadi kufikia Julai 2011, ni wakazi wapatao 40,410 sawa na asilimia 26.1 ya wakazi wote ndiyo wenyewe uhakika wa kupata walau kiwango cha msingi cha mita 25 kwa siku kupitia mradi inayofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Julai tarehe 29 mwaka jana Mheshimiwa Rais Kikwete alifanya ziara Wilayani Nanyumbu na katika risala iliyosomwa kwake aliambiwa juu ya kero ya maji Wilayani Nanyumbu. Katika kujibu tatizo hili aliwaagiza watendaji wa Wizara ya Maji kuandaa mpango mkakati ambao utatatua kero ya maji Wilayani Nanyumbu. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji awafahamishe wananchi wa Nanyumbu ni jinsi gani Wizara itatatua kero hii kubwa ya maji. Maeneo kama Makanya, Nanderu, Maneme, Likokona, Nawaje, Chitandi, Chipuputa, Chitowe, Mhinawe, Namalombe, Mkwajuni na Namtumbusi na Maratani, ni maeneo ambayo yanapata adha kubwa ya shida ya maji. Maeneo haya ni kame sana kiasi cha kuwafanya wananchi wakose maji kabisa. Wakati haya yakiwakuta, maji ya mto Ruvuma yanatiririka tu na kuishia baharini bila ya kuwahudumia au kutoa huduma kwa wananchi waweze kupata maji safi na salama. Naomba Serikali

ianzishe mradi mkubwa na maji kwenye mto huu ili iweze kusambaza maji Wilayani Nanyumba na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini kupitia Mradi wa Maji Shirikishi unaoratibiwa na SADC limetengewa *USD* 800,000 kwa ajili ya kutekeleza jumla ya miradi sita ya kijamii. Wilaya ya Nanyumbu ni mojawapo itakayonufaika na mradi huu na kwamba unatarajiwa kuanza Agosti 2012 na kukamilika Desemba 2012 (miezi mitano tu). Nachotaka kujua hapa ni kwamba mradi huu utahusisha mambo gani kwani naona muda unaohusika ni mdogo. Je, ina maana sasa itahusisha na usambazaji wa maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya maji, nashauri kila maamuzi juu ya ongezeko la bei ya maji wadau wapate elimu kwanza kabla ya kufikia maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa maji katika Jiji la Mbeya. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya, natoa pongezi kwa Serikali kwa kufanikisha mradi mkubwa wa maji katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya maji katika Wilaya ya lleje. Wilaya ya lleje ina eneo kama ilivyo kwa Wilaya za Nzega na Igunga au Meatu. Naomba Wizara iwakumbuke wananchi walio pembezoni kama lleje wapewe maji ili kuondokana na kero wanayoipata hasa miji ya Mbebe, Ikumbilo na Isongole. Kwa vile miji ya mpakani ya Tunduma, Isongole inafikiwa na wageni toka nchi za nje, za Malawi na Zambia, wanapita pale na kukumbana na adha kubwa ya maji. Kwa hiyo, tufikirie uwezekano wa kuleta maji katika Wilaya za Mbozi na lleje kutokana na maji ya Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wakiongozwa na Mhandisi Sayi, Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nawashukuru kukuta mji wa Katesh pamoja na mradi wa maji vijijini Hanang umeonyeshwa tayari kwa utekelezaji. Naomba utekelezaji usicheleweshwe kwa Hanang ni Wilaya ambayo ina vianzo vichache vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, naomba Wizara itambue kuwa eneo la Wilaya ya Hanang ina matatizo makubwa ya maji. Maji ya visima katika maeneo tuliyochimba hayapatikani kwa urahisi mpaka mita 300 au zaidi. Hatuna mito na kwa hivyo suluhisho la maji kwa Wilaya ni kuchimba malambo na mabwawa. Fedha zinazohitajika kuchimba malambo na mabwawa ni nyingi, Wilaya au Hamashauri ya Wilaya haina vyanzo vya fedha. Naomba Wizara ifanye utafiti na kusaidia Wilaya ya Hanang iondokane

au kupunguza tatizo kubwa la maji. Wanawake wanaenda kilomita 20 kwa kila siku ambapo watoto wanakosa uangalizi wengine wanavunjika viungo au kuungua moto kwa kuachwa wenyewe. Sisi hatuongelei maji safi kwani hata yale yasiyosalama hayapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushie ahadi ya Rais ya maji Kijiji cha Endasak, sasa ni karibu miaka miwili lakini ahadi hiyo haijaingizwa katika bajeti. Namwomba Mheshimiwa Waziri aone kuwa ili ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itekelezwe, ni muhimu ikaingizwa katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha. Tusipofanya hivyo, tunaweza kushindwa kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais, nitafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kama nitapewa ahadi ya maombi yangu ninayotoa katika mchango wangu huu.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji na mwanamke, mzalishaji mkuu wa nchi hii ni mwanamke lakini huyu mwanamke hapati maji safi na salama na kwa sababu hiyo afya ya wanawake inazorota kwa uchovu mkubwa anaopata. Maeneo mengine mwanamke hutembea mwendo mrefu wa kwenda kutafuta maji, sehemu zingine mama huondoka asubuhi na hurudi jioni, je, huyu mama atazalisha saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika llani ya Chama cha Mapinduzi, kuna ahadi ya kuhakikisha nchi nzima tunapata maji safi na salama. Suala hili lingeteklezwa,

wanawake wangepata muda mrefu wa kuzalisha na hivyo uchumi ungekua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa vijiji kumi kila Halmashauri vilivyo kwenye mpango wa *World Bank*, sehemu nyingi *World Bank* wamemaliza lakini wananchi hawana hela ya kuchangia, michango yao inasuasua. Hivyo basi kwa nini Serikali isiwakopeshe wakawa wanalipia kidogokidogo mtu anapokuja kuchota maji mpaka wakamaliza deni? Kuliko sasa mitambo itachakaa kwa kutotumika na itakuwa hasara kubwa.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Serikali, kwa bajeti waliyotuletea ili na mimi niweze kutoa mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Maji kuwa Jimbo la Ukonga liko Dar es Salaam, lakini ni Jimbo pekee Jijini Dar es Salaam ambalo katika historia halijawahi kupata maji safi na salama kutoka *DAWASCO/DAWASA*. Jimbo hili lina idadi ya wakazi takriban 652,000 na ukubwa wa km 3150 na zaidi pamoja na ukubwa huu na wingi wa wakazi bado watumie maji toka katika visima vifupi ambayo si salama sana na hapatikani kwa vipindi vyote. Pamoja na kuwepo visima virefu, vichache sana visima hivi havitoshelezi kabisa. Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika hitimisho namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni kwa nini Jimbo la Ukonga halipati maji safi na salama kutoka

DAWASCO/DAWASA. Pia namwomba aniambie visima vitatu vya dharura nilivyoviomba na nikaahidiwa na utafiti ukafanyika katika maeneo ya umma, nitavipata lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza tena kuwa wakati wa hitimisho Mheshimiwa Waziri aniambie Ukonga ana mpango gani wa kuleta maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha hoja.

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Dodoma MJINI lina Kata 37. Kata saba zipo mjini na zina unafuu mkubwa wa maji. Kata 30 zipo vijiji na zina tatizo kubwa sana la maji safi na salama ya kunywa, lakini pia kuna tatizo kubwa la maji ya malambo kwa ajili ya matumizi ya mifugo, ng'ombe, mbuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dodoma una mvua kidogo sana. Dodoma haina mito mingi, wala mabwawa mengi ya kudumu. Mito mingi na mabwawa mengi ni ya muda (*seasonal rivers and lakes*), hupata maji kidogo wakati wa mvua na kukauka kabisa wakati wa kiangazi. Kutokana na Dodoma kuwa na mvua kidogo, wakoloni walichimba mabwawa mengi ili kuusaidia Mkoa huu kuwa na maji ya kutosha, wakati wa masika na wakati wa kiangazi kwa matumizi ya watu na mifugo lakini mabwawa yaliyo mengi, sasa yamejaa tope na yanatunza maji kidogo na kukauka mapema. Ili kusaidia Jimbo la

Dodoma (Kata 30 za vijiji) kupata maji ya kutosha, napendekeza:-

- (i) Maji vijiji. Serikali ichukue hatua za makusudi kuondoa tope kwenye mabwawa yote 21 (ishirini na moja), yaliyopo katika Wilaya ya Dodoma Vijiji, yaani Dodoma Mjini – Vijiji, najua kazi ni ngumu na inahitaji fedha nyingi, lakini kupitia mpango mzuri wa kazi (*action plan*), Serikali inaweza kuondoa tope kwa mabwawa yote 21 ya Dodoma Mjini – vijiji na kwa muda mfupi wa miaka mitatu tu. Napendekeza Serikali ianze na mabwawa makubwa ya; Zuzu, Mkalama, Mpunguzi, Nkulabi, Mbabala, Kikombo, Vikonde na Mapinduzi. Kijiji cha Mapinduzi kina hali mbaya sana ya maji. Watu wamechimba maji korongo lote pasipo mafanikio. Kijiji cha Mapinduzi kinahitaji msaada wa haraka na dharura la sivyo CCM haitaambua kura mwaka 2015.
- (ii) Shule za bweni hazina maji. Bihawana Sekondari, Dodoma, haina maji, wanafunzi hawaogi mara kwa mara. Wanakaa siku tatu (3) kila wiki bila kuoga. Serikali ifanye bidii kuchimba visima vya maji kwenye shule zote za bweni katika Jimbo la Dodoma Mjini, la sivyo maeneo haya yatakuwa ngome ya CHADEMA. Serikali isitufikishe hapo!
- (iii) Maji Mjini. Baadhi ya viunga vya mji wa Dodoma mfano, Mtaa wa Mbuyuni, Mtube na Chinangali West (katika Kata za Kizota na

Chang'ombe) hazina maji safi na salama. Serikali (Wizara ya Maji) waelekeze Idara ya Maji (*DUWASA*) kupeleka maji huko mapema iwezekanavyo. *DUWASA* wanasema wanaweza kufanya hivyo mara moja, ila maeneo hayo hayajapimwa lakini kuna watu wengi maeneo hayo. Mbuyuni na Mtube ni jumla ya nyumba 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DUWASA* wapo tayari kupeleka bomba na wapo tayari kung'oa bomba hizo kwa hasara yao ila wanakatazwa eti na Serikali. Mheshimiwa Profesa Maghembe, naomba uinusuru Dodoma kama ngome ya CCM, iendelee wakati wote kuwa ngome ya CCM. Waamuru *DUWASA* wapeleke maji kwenye viunga vyote vya Dodoma vyenye maelfu ya watu. Muda si mrefu, magazeti ya upinzani yanajiandaa kupiga picha watu wanaotumbukia kwenye visima virefu vya Dodoma Mjini kutafuta maji huko. Watu wanahoji kuwa hivi hata kama mtu amehukumiwa kunyongwa ndiyo asinywe maji? Kwa nini Serikali isiruhusu *DUWASA* kupeleka maji kwenye viunga vya Dodoma (*suburbs*), kwani kuna maelfu ya watu wanaoishi huko bila maji. Baada ya maeneo hayo kupimwa, ikiwa bomba zitaonekana zimecaa vibaya, *DUWASA* wapo tayari kung'oa bomba hizo na kuzilaza upya kufuatana na ramani mpya ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siajabu zoezi la upimaji viunga hivyo lisifanyike mpaka baada ya miaka 10 ijayo. Je, wananchi waendelee kuteseka kwa kukosa maji hadi ramani ya mji itakapotengenezwa? Ramani hiyo hajatengenezwa kwa takribani miaka 40 sasa

(1973 – 2012). Kwa nini watu waadhibiwe kwa kunyimwa maji kwa makosa ya ramani kutochorwa mapema? Naomba Serikali yetu nzuri ya Chama cha Mapinduzi isiwe chanzo cha kuimarisha upinzani usio na lazima katika Jimbo la Dodoma Mjini. Tunaomba maji kwa viunga vyote vya Dodoma Mjini. Maji yapo na *DUWASA* wapo tayari kupeleka maji, waruhusiwe kupeleka maji ili watu wetu wapate maji, kwa sifa na ushindi wa CCM 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii muhimu sana. Nawatakia utendaji wenye mafanikio. Aidha, nawapongeza tena kwa bajeti nzuri ambayo ninaamini kwamba wameitengeneza kwa ushirikiano na watendaji wa Wizara, hongereni wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kero zifuatazo kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Morogoro Kusini Mashariki,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ukosefu mkubwa wa maji safi na salama kwa Wananchi wa Morogoro Vijijini. Wilaya ya Morogoro ndiyo chanzo kikubwa cha maji kwa Mkoa ya Dar es Salaam na sehemu ya Pwani. Wananchi wangu ndiyo wanabeba majukumu kutunza vyanzo vya mto Ruvu lakini wao wenyewe hawapati maji safi na salama kutohana na vyanzo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe motisha kwa wananchi hawa kwa kuwapatia maji ya bomba ili akina mama wapumzike kupandisha na kuteremka milima wakifuata maji. Vijiji ambavyo vinachangia sana katika utunzaji wa mazingira ya milima ya Uluguru ni kama ifuatavyo:-

- Kata ya Kinole – vijiji vya Amini, Tandani, Kalundwa, Kisambwa, Ludewa na Lungla.
- Kata ya Makuyuni – vijiji vya Msumbwe, Kibwaya, Lukolole, Kivuma, Mwarazi na Madamu.
- Kata ya Kiloka, Kijiji cha Bamba, Kiziwa, Kikundi na Kiloka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mto Ruvu unapita katika Kata ya Tonunguo na Mkulasi. Wananchi hawa wanalinda sana mazingira ya mto huu kwa kuzuia uvamizi wa mifugo na wanaolima katika kingo za mto Ruvu. Pamoja na juhudzi zote hizi, hawa wananchi hawana maji ya kutosha licha ya maji safi na salama. Naomba Serikali iwapatie maji wananchi hawa ili wanawake wasitembee zaidi ya kilomita kumi kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Bwawa la Kidunda, naishukuru Serikali kwa ujenzi wa bwawa hili lakini zaidi kwa utayari wake wa kuwalipa fidia wananchi wanaohamishwa. Napenda kuomba Serikali ilipe Halmashauri mapema gharama za kuwapimia hawa

wananchi viwanja vya makazi mapya pamoja na kujenga miundombinu ya huduma za jamii kama shule, zahanati na maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atamke leo ni lini ujenzi wa barabara ya kutoka Ngerengere – Kidunda itaanza kwani *DUWASA* waliahidi kwamba watajenga barabara hiyo. Wasipoanza mapema, mvua ikinyesha ujenzi hautaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mradi wa Wami – Chalinze, tunashukuru kwamba Serikali imeona umuhimu wa kusogeza haya maji mpaka Tarafa ya Ngerengere, yaani vijiji vya Ngerengere, Kidungalo, Sinyaulime, Gwata, Ujembe na Lubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji haya yangeweza kufikishwa katika vijiji vya Seregete A, Seregete B, Kisemu, Kinonko, Maseyu na Fulwe. Kutokuwafikishia wananchi hawa maji wamejisikia kubaguliwa kwani majirani zao wa Pwani wamepata maji. Naomba Serikali ikubali kuongeza ukubwa wa mradi huu ili vijiji hivi nao wafurahie matunda ya uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, mradi wa *World Bank*, Halmashauri ya Morogoro Vijijini, imejitahidi sana kumaliza mchakato wa kumtafuta *consultant* na *proposal/ipo* kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji. Naomba aione na achukue hatua zinazostahili haraka iwezekanavyo. Hivi sasa tunazo Sh.450m kwa ajili ya “*consultant*”, naomba kama bado huyo *consultant* hajateuliwa na Wizara angalau tutumie Sh.259,000,000

ili tutatue matatizo ya muda mfupi kama kukarabati visima pamoja na kuchimba visima virefu kwenye maeneo ambayo wananchi wanatembea zaidi ya kilomita kumi (10) kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha kwa kuomba Serikali itambue mchango wa wananchi wangu wa kutunza na kulinda vyanzo vya mto Ruvu kwa kuwapatia maji safi na salama. Wananchi wako tayari kuchangia na kuendelea kutunza mazingira ya milima ya Uluguru. Tuzingatie msemo wa wahenga unaosema "Nikune na mimi Nikukune."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, bei za maji, kumekuwa na tabia ya Mamlaka za Maji Mijini kupandisha bei za maji kwa mita bila kuangalia uwezo wa wananchi husika. Vilevile bei hizo zimekuwa zikipandishwa bila mamlaka husika kuimarisha miundombinu iliyopo na kuongeza mgawo wa maji. Waziri atuambie ni kwa nini bei hizi za maji zinatofautiana Mkoa na Mkoa, mfano Mbeya Sh.360 wakati Bukoba ni Sh. 705 na Iringa Sh. 755. Ukiangalia kijiografia, Bukoba imepakana na Ziwa Viktoria lakini bei ya maji iko juu. Hizi bei zipunguzwe sana, zinawaumiza Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mradi wa Benki ya Dunia. Mradi huu bado ni kiini macho kwani umejenga matumaini makubwa kwa Watanzania lakini kiukweli mradi huu umefeli kwani ni maeneo machache ambayo hadi sasa maji yamepatikana, kuna lugha

kwamba "visima vyenye maji" inatumika sana kwenye mradi huu lakini inaonekana kuwa hivi visima ambavyo vinatajwa vyenye maji sio kwamba maji haya yanatumika na wananchi. Waziri wakati wa majumuisho utuambie ni visima vingapi ambavyo maji yake yameanza kutumiwa na wananchi kote nchini mfano Babati TC visima 7 – 3 vina maji lakini bado hayatumiki. Nashauri pia urasimu upunguzwe na Wizara katika mradi huu. Vijiji 10 – 6, Waziri utuambie kwa nini mradi huu umepunguza idadi ya vijiji toka 10 – 6 kama sio dalili za mradi kushindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, bajeti ya Wizara. Inasikitisha bajeti ya Wizara hii kuwa ndogo kuliko Wizara ya Ujenzi. Barabara si muhimu kuliko maji, Waziri atuambie hii bajeti itaendelea kuwa ndogo mpaka lini wakati wananchi hawana maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, tofauti kati ya Bodi na Mamlaka ya Maji. Waziri kupitia Bunge hili Tukufu awafahamishe wananchi tofauti kati ya Bodi za Maji na Mamlaka za Maji kwani *Engineers* wa Maji wa Halmashauri wamekuwa wakilazimisha wananchi kuwa Mamlaka badala ya Bodi hata pale ambapo wananchi wamechangia miradi yao wenyewe bila mchango wa Serikali, Waziri awaelezee wananchi kati ya tofauti hizo mbili ili waelewe na wasiendelee kuibiwa.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa pongezi kwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji

wao, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba ya Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa rasilimali maji hapa nchini kwa matumizi ya binadamu na kilimo, itategemea sana uamuzi wa Serikali kupitia Wizara hii, TAMISEMI, Maliasili na Mazingira na wadau wengine kuamua kupiga marufuku uchafuzi wa mazingira na hasa vyanzo vya maji. Wajibu huu umetolewa kwa Ofisi za Mabonde jambo ambalo ni sahihi. Kazi hii ni kubwa na muhimu sana. Kuna haja kuanzia sasa Wizara kuelekeza nguvu zake za kifedha na utendaji kwa Ofisi za Mabonde ili kuziwezesha Ofisi hizi kukagua maeneo yote ya vyanzo vya maji na kusimamia sheria zinazohusu rasilimali maji na kadhalika ikiwa ni pamoja na kuwatambua watumiaji wa maji bila kufuata sheria. Jambo lingine ambalo ni muhimu Wizara ifanye kuhusu mabonde ni kuyapanga mabonde hayo kwa makundi ya ukubwa wake na uwezo. Si sahihi kuyaacha mabonde yote yajitegemee kwani si yote yana uwezo. Mfano ni kama Bonde la Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza Wizara kwa kuahidi kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Bonde inayojengwa mjini Tukuyu. Hata hivyo, napenda kuishauri Wizara kuhusu utoaji wa fedha kwa mtiririko mzuri ili utekelezaji uendane na mpango mzuri wa ukamilishaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za rasilimali maji kwanza ni mabadiliko ya tabianchi, Wizara ichukulie suala hili *seriously* kwani kwa vyovyote vile inachangia matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji

hana nchini. Umefika wakati Serikali iwe makini sana kufanya kazi kwa karibu sana na taasisi zote zinazosimamia masuala ya mazingira la sivyo tishio la ukame lililopo linatishia sana uhaba wa maji na kuleta manung'uniko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, utekelezaji wa miradi katika sehemu nyingi hapa nchini hasa miradi mikubwa husuasua kwa sababu kubwa hasa kwa uteuzi mbaya wa makandarasi ambao mara nyingi huteuliwa wasio na uwezo kitaaluma lakini pia kifedha lakini wakati huohuo Wizara nayo imekuwa ikichelewesha fedha ili kutekeleza miradi. Katika hoja hii, napenda kutoa mfano halisi wa miradi wa Mwakaleli *Group* na Masoko *Group* ambayo ilikuwa ikamilike mwishoni mwa mwaka jana, mpaka leo inasuasua. Naomba Waziri azungumzie miradi hii wakati atakapofanya majuisho yake, ni lini miradi hii itakamilika? Kuna haja pia ya Wizara kufuatilia utendaji kazi wa Wahandisi Washauri ambao nao pia wamekuwa kikwazo kutokana na kutofautiana na makandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uvunaji wa maji ya mvua. Mpango huu wa uvunaji wa maji ya mvua haujapata msukumo wa kutosha. Nashauri Wizara ianze kujikita katika taasisi za Elimu, Afya hasa Mashulenzi, *Dispensaries* na Vituo vya Afya. Iwapo Wizara itaamua kutoa mafunzo kwa wataalam wa Halmshauri za Wilaya na Miji ili utaalamu huo usambazwe katika maeneo muhimu itasaidia sana upatikanaji wa maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Maji.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Maji kwa hotuba ya Wizara yao pamoja na watendaji ambao wanashirikiana na Mawaziri wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza Wizara kwa kuupatia fedha Mradi wa Maji wa Manyamba kwa ajili ya kuukarabati mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mtwara Mikindani, ni mji ambao unakuwa kwa kasi kutohana na kugundulika kwa gesi na utafiti unaoendelea wa gesi na uwekezaji unaotarajiwa, unafanya mahitaji ya maji kuwa makubwa kwa wakati huu na wakati ujao. Tunaomba Wizara iweke mpango wa kutoa maji katika mto Ruvuma kwa ajili ya kupatia maji ya uhakika Mkoa wa Mtwara hasa Wilaya ya Mtwara Vijiji na Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara Vijiji wanao Mradi ya Mbuo ambao unapeleka maji katika vijiji vya Kata ya Mayanga, Ndumbwe, Mpapura na baadhi ya vijiji vya Namgogori Kisiwa na Mgau. Mradi huu kwa sasa umechakaa sana na unahitaji ukarabati mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Dihimba, Mchuchu na Mnyawi nayo ipo katika hali mbaya sana.

Naomba miradi yangu yote niliyoitaja ikarabatiwe ili kuboresha huduma za maji Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ina Kata za Njengwa, Mnima, Ntekela, Kiyanga, Kiromba, Mtiniko, Mtimbwilimbwi, Chawi na Natumbuka ina miradi ambayo inafadhiliwa na *AMREF*. Miradi hii imechukua muda mrefu sana na maeneo mengi wananchi wamekata tamaa ya kupata maji katika maeneo yao. Napenda kufahamu mradi huu utakamilika lini na kama *AMREF* wameshindwa kutekeleza mradi huu katika baadhi ya maeneo basi Serikali itafute wafadhili wengine ili kero za wananchi ziishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutayarisha bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kondoa Kaskazini, tatizo la maji ni sugu. Ni asilimia chini ya 30 ambapo wananchi wanapata maji na asilimia hii ni mjini. Tatizo hili linasababisha usumbu mkubwa kwa wananchi hasa wanawake na wasichana ambao hutumia zaidi ya saa sita kutafuta maji ambayo si safi wala salama. Maeneo ambapo wanawake na wasichana huenda kutafuta maji ni kwenye makorongo ambapo wanyamaporu pia huenda kunywa maji, matokeo yake ni kuwa wanawake na wasichana hushambuliwa na wanyamaporu, wengi

wamepoteza maisha ama kupoteza baadhi ya viungo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia Wizara hii katika Mkutano wa bajeti mwaka 2011, Serikali iliahidi kuwa kutokana na tatizo hili, Jimbo la Kondoa Kaskazini litapewa kipaumbele katika ugawaji wa miradi ya maji. Je, Waziri anawaeleza nini wananchi wa Kondoa Kaskazini kuhusu ahadi ya Waziri ambao iliwapa matumaini wananchi? Ikumbukwe kuwa ahadi ni deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MUSTAFA H. MKULO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kilosa, Wilaya ya Kilosa, kuna mradi wa Bwawa la Kidete, ambao unatekelezwa kwa takribani miaka mitatu. Mradi huu unakusudia kufufua Bwawa la Kidete ambalo lilijaa mchanga (*sillitation*) kwa miaka mingi. Tatizo hili ndiyo chanzo cha mafuriko ya mara kwa mara ya mto Mkondoa ambayo yalileta madhara makubwa kwa Mji wa Kilosa, Desemba 2009 na Januari/Machi 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye bajeti ya Wizara hii sikuona *provision* yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu kwa mwaka 2012/2013. Gharama za Mkandarasi wa mradi huu ni zaidi ya Sh. 4.50 bilioni na zaidi ya nusu ya gharama hizo hazijalipwa. Mheshimiwa Waziri wa Maji awahakikishie wapigakura wa Jimbo la Kilosa kama mradi huu uko kwenye ratiba ya utekelezaji, gharama zake zitalipwa vipi wakati hakuna *provision* yoyote katika makadirio ya Wizara hii kwa mwaka 2012/2013? Ikumbukwe kuwa

Serikali tayari imekwishatumia fedha nyingi katika mradi huu. Utekelezaji bila ya kutenga fedha za kumalizia itakuwa ni hasara kubwa kwa Serikali. Namshauri Mheshimiwa Waziri atembelee mradi huu kwa wakati muafaka ili ajionee mwenyewe kazi ambayo imeshafanyika na kwa nini fedha zisitengwe ili kuukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hoja iliyowasilishwa Mezani ni nyeti, inayogusa maisha ya watu moja kwa moja katika maeneo yote na kwa kuwa ni kilio cha muda mrefu kisichokuwa na ufumbuzi, kwa maoni yangu kwanza siungi mkono hoja lakini pia kama Serikali haitaweza kuongezea fedha zaidi katika makadirio ya bajeti ya Wizara hii ningeshauri yafuatayo:-

- (i) Bajeti ya Wizara hii isipitishwe; au
- (ii) Fedha za rada ipelekwe kwenye bajeti ya Wizara hii ili Watanzania wote wawe na uhakika wa kupata maji muda wote bila upendeleo hadi vijijini; au
- (iii) Itafutwe pesa kwenye matumizi yasiyo ya lazima kwa maana ya kupunguza matumizi katika maeneo fulani na fedha hiyo ipelekwe au kuongezwa kwenye bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nichangie Wizara hii kwa niaba ya wananchi wa Tanzania na Mkoa wangu wa Dodoma, Kondoa na Wilaya mpya ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya nydingi hapa nchini zina shida ya maji, lakini nchi ya Tanzania sehemu kubwa ina maji na ukame. Wananchi wanahangaika maji kila kona kwani hili ni suala la muhimu na ni janga la Kitaifa, namtaka Waziri atakapokuja hapa kwenye majumuisho yake atueleze kero hii itatatuliwa lini na kwa miundombinu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makadirio ya matumizi ya fedha ya maji, ukurasa wa 85, Jedwali Na.2 inaonyesha visima vya maji vilivyochedimbwa na wakala *PDCA/2011/2012*, Wilaya ya Kondoa ilipata visima vitatu tu na ndani ya Chidwa 89 inaonyesha vilivyopangwa 27 visima vilivyochedimbwa 24 na visima nyenye maji 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dodoma unatengewa Sh.2,726,299,000 hii ni jumla kuu, Wilaya ya Kondoa imetengewa Sh.633,008.00 kwa ujumla na Wilaya mpya. Hali hii inakatisha tamaa ya kupata maji na kuondoa kero ya maji katika Wilaya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali halisi, fedha hizi kwa huduma ya maji ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu kwani hata hao Madaktari wanaoleta migomo, maji yakiwa hakuna, wao wanataka fedha, maslahi, hii hali si nzuri na tukichezea itatupeleka

pabaya kadri miaka inavyoenda, Serikali sasa iangalie hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya maji ni makubwa sana, hasa sehemu kuu ni kwenye huduma za jamii, mifugo, kilimo, hali ni ngumu kila pembe ya Tanzania. Huko Kondoa, kuna vyanzo vya maji ya chemchem. Bwawa la asili kama bwawa la Kisaki, Haubi, Bicha, Mrijo na kadhalika lakini Serikali imeshindwa kuyatunza mabwawa haya yanayozalisha vichocho kama kule Kisaki. Ni lini Serikali itapeleka dawa na kuangamiza vijidudu hivyo na wananchi wa maeneo hayo wangepatiwa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Mrijo, maji ni tatizo, Waziri na yeye afike huko anywe maji yale ya chumvi, hayafai. Bwawa la Bicha haliendelezwi, likawapatia wananchi maji ya kumwangilia mashamba/bustani na matumizi ya wanyama na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee kusema pale palipo na maji, uchangiaji wake ni mkubwa kuliko matumizi, Waziri atamke bei halisi za maji mijini na vijiji na bado maji hayapatikani na hayakidhi mahitaji ya watu. Sasa atuambie pesa hizo zinafanya nini kwani yatoke maji kwenye bomba au yasitoke bei ni kubwa hasa hapa Mkoani Dodoma na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika programu ya maji na usafi wa mazingira vijiji, Wilaya ya Kondoa imepata visima 15 vyenye maji na viwili vya Sabodo. Hivi kweli Serikali inatambua wingi wa ongezeko la watu na matumizi. Katika Wilaya hii maji hakuna

sehemu nyingi na palipo na maji yana matatizo. Kuna kisima nilishawahi kuongelea, kwenye Kata ya Kinyasi, kisima kimechimbwa, maji hayafai kwa matumizi ya binadamu na wanyama wakinywa wanavimba matumbo na kufa. Kuna visima vimechimbwa maji ya chumvi, nashauri watalaam wa kila Wilaya wafuatilie miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ina chemchem hazifuatiliwi, ziangaliwe ili zisaidie upatikanaji wa maji na kusambaziwa wananchi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka wataalamu wa kuchunguza chemchem zenye maji ili kupunguza kero ya maji? Serikali itenge pesa za kutosha kujenga mabwawa ya maji hasa maeneo ya Wilaya ya Kondoa huko Bumbuta, Sarale, Busi, Atta huko Kisese kwani maeneo ya tambarare kuelekea kwenye mwinuko maji yana uwezo mkubwa wa kusimamishwa na wananchi wakavuna maji hayo kwa ukulima, umwagiliaji, kunywesha mifugo na matumizi ya watu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja kwani Serikali inajua maji ni uhai na inadharau Wizara hii nyeti.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu (S.W), Muumba Mbingu na Ardhi, kwa rehema na neema zake nyingi amazonineemesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, “*Water is Life*” and *Life is Water*” huo ni msemo wa Kiingereza, lakini Waingereza wamekariri tu kauli Tukufu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu (S.W.), Mungu Mtukufu amesema kupitia kitabu chake

Kitukufu na hii ni tafsiri isiyo rasmi "Tumejaalia kutokana na maji, kila kitu kipate uhai". Mwenyezi Mungu katika kulithibitisha hilo ameumba theluthi mbili ya tatu ya ulimwengu wetu huu kuwa ni maji yakiwemo bahari, mito, maziwa na hata mabwawa. Kama hiyo haitoshi hata maumbile ya mwanadamu, tukiwemo sisi Wabunge zaidi ya asilimia sabini (asilimia 70) ya viwiliwili vyetu ni maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni utangulizi wa Kisayansi ulioonyesha umuhimu wa maji katika maisha ya mwanadamu, wanyama na hata miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *researches* nyingi zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya maradhi yanatokana na tatizo la maji safi na salama. Kwa mantiki hiyo, Serikali haina budi kuongeza juhudzi za dhati kwa sekta za maji nchini. Ukosefu wa maji unazorotesha ukuaji wa uchumi kwa takribani asilimia 40 – 50, hii inatokana na kuwa wazalishaji wengi ambao ni wanawake, wanatumia muda mwingi kila siku katika kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua shida ya maji na umuhimu wa maji kwa maisha, wananchi wameamua kuchimba visima virefu katika makazi yao maeneo mengi nchini. Miiongoni mwa maeneo hayo ni Jiji la Dar es Salaam, Zanzibar, Chake Chake na kadhalika. Jambo la kushangaza badala ya Serikali na taasisi zake kama Mamlaka za Miji husika kuwasaidia wananchi hawa, zinawabughudhi na kuwanyanya mara kwa mara kwa kuwapelekea barua za kuwatishia kuwatoza kodi za visima, vinginevyo wazungumze

pembeni. Hili ni tatizo na ni lazima Serikali ichukue hatua haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika maeneo machache nchini sehemu zinazopata maji ya bomba, maji hayo si safi na si salama! Hili ni tatizo na ni aibu kwa Serikali. Inakuwaje Serikali yenyewe wataalam wa fani ya maji, waruhusu maji machafu yatoke kwenye mabomba mijini na vijijini hali ya kuwa fedha zinatengwa? Huku si kuwaangamiza Watanzania, hasa watoto ambao ndiyo Taifa letu la kesho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana, Serikali itimize wajibu wake.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua uwepo wa Naibu Katibu Mkuu hapa Bungeni, nampa pole kwa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naulizia ujenzi wa Bwawa la Kimagai Jimboni Mpwapwa. Bwawa hili ni muhimu sana. Kufufuliwa kwake itakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi wa Kimagai pamoja na wananchi wengi wakiwemo hata wa Jimbo la Kilosa na kuokoa Reli ya Kati.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake, kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara Bungeni kwa ajili ya kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ipo katika ukurasa wa 55 unaoeleza kuhusu Mpango wa Dharura kwa Jiji la Dar es Salaam. Nakubalina na dhana hiyo, lakini tayari wananchi wamekuwa na mipango yao ya dharura ambayo katika kila mtaa unaopita tayari unakuta kuna visima ambavyo vimechimbwa na mtu binafsi wa mtaa ule, pia kila mtu anachimba kisima bila ya utaalam. Visima vinachimbwa jirani na vyoo na hasa mitaa hiyo ipo Uswahilini, mfano Temeke kwa Azizi Ali na kadhalika. Visima viro chini ya kuta za nyumba na jirani yake amechimba choo. Hivyo, maji yanatoka chini na choo kinakusanyika chini, uchafu wa choo ni rahisi kwenda kwenye njia ya maji. Watu wanatumia maji hayo, hakuna elimu inayotolewa na uswahilini hakuna anayechemsha maji. Hivyo naomba Wizara kutoa elimu kwa kunusuru maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuboresha huduma ya maji mijini ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwa baadhi ya miji katika kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwa sikuvi na kutenga fedha za kutatua suala la maji ambalo limekuwa kero sana kwa wakaazi wa Dar es Salaam na kwa kuwa ni mpango maalum ulioidhinishwa kuhakikisha kwamba tatizo la maji Jiji la Dar es Salaam linapungua ifikapo mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado nazidi kuiomba Serikali iangalie pia vijijini, hali ni mbaya kama vile vijiji vya Mkao mpya wa Njombe na Iringa pia llula, Ruaha Mbuyuni na Mahenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuiomba Serikali kuondoa VAT katika matanki ambayo yanatumika katika maji ili kupunguza gharama za upatikanaji wa maji safi na salama. Pia naiomba Serikali iondoe gharama ya VAT katika madawa ambayo yanatumika katika maji ili kupunguza gharama za upatikanaji maji safi na salama katika mamlaka zote za Tanzania na sio baadhi tu ya Manispaa na ukiangalia Manispaa hizo matumizi yake ni madogo ukilinganisha na Jiji la Dar es Salaam. Kuondolewa kwa VAT katika dawa za kusafishia maji kutampa unafuu wa kupata maji kwa bei nafuu mtumiaji, hivyo Serikali ichukue suala hili kwa umuhimu wa kipekee.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matatizo ya maji limekuwa sugu na linaleta siyo adha tu kwa watu lakini pia linasabisha upotevu wa muda mwingi ambao badala ya kutumika kutafuta maji watu wangeutumia katika harakati za uchumi kwa maslahi binafsi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Wabunge Dar es Salaam – *DAWASCO*, mimi na Wabunge wenzangu tumetembelea Miradi ya *DAWASCO* na kuona miradi ya upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na Ruvu Chini. Mradi huu unatia matumaini ya kuondoa tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam ukiunganishwa na ule wa

visima virefu vyatia Kimbiji na Mpera. Pamoja na matumaini hayo, bado kuna tatizo kubwa ambalo napenda kupata jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu mingi sana imechoka kwa sababu iliwekwa siku nyingi sana. Hivi karibuni tuliona Kampuni ya Kichina ikibadilisha mabomba, lakini badala ya kuboresha upatikanaji wa maji imefanya hali iwe mbaya zaidi. Ni vipi sasa Wizara imejipanga kukabiliana na miundombinu ili mradi huu uwe wa manufaa yanayotarajiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yanapotea njiani. *DAWASCO* inapoteza maji mengi sana njiani na ningependa kupata jibu. Upotevu huu ni kiasi gani kupitia miundombinu mibovu na kiasi gani kwa kuibiwa na watu wanaouunganisha kiholela. *DAWASCO* inakiri kuwa maji yanayopotea yamepungua toka asilimia 50 hadi sasa wanapanga lengo la maji yatakayopotea kuwa asilimia 30. Hiki ni kiwango kikubwa sana hasa ukichukua thamani ya mradi wa maji yanayopotea. Ni kitu gani kinachofanya *DAWASCO* ikubali kuwa na upotevu huu mkubwa wa maji na dawa/hatua gani *DAWASCO* itachukua kuondoa huu upotevu mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadhifuru wa wafanyakazi, kumekuwa na ubadhifuru mkubwa sana wa watumishi wa *DAWASCO* ambao wamekuwa wakishirikiana na watu mbalimbali kuiba maji na hatu kuwafungia maji watu mbalimbali bila malipo. Maji hayo mengi yamekuwa yakitumika ama kumwagilia mashamba makubwa yaliyo njiani kutoka mitambo ya Ruvu Juu na Chini. Lakini sambamba na hili kuna wizi

wa maji kwa watu wanaoweka matanki makubwa majumbani na ni wamiliki wa magari ya kusambaza maji. Haieleweki kuona kwamba kama *DAWASCO* inatarajia kiasi fulani cha maji, halafu maji hayo hayafiki, hivi hakuna mtu anayehoji ni kwa nini hayafiki au ni mshiriki katika wizi unaoendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bili za maji bila maji. Wananchi wamekuwa wakipelekewa bili za maji hata kama hawapati maji. Hii ni kero kubwa ambayo *DAWASCO* inashindwa kurekebisha. Napenda kupata tamko la Serikali, je, mwananchi kwa nini asikatae kulipa bili kama hapati maji? Rais Mstaifu Mheshimiwa Ali H. Mwinyi aliwahi kuwaambia wananchi wasiopata maji wasilipe bili, nini tamko la Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu kukata mabomba, mwisho kumekuwa na uharibifu mkubwa wa watu kukata mabomba katika harakati ya kutafuta maji. Hili pia linachangia uharibifu wa mabomba, maji na barabara. Je, suala hili linashughulikiwa vipi?

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe kwa hotuba yake nzuri sana ambayo amesoma hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kuhusu kero ya maji Mkoa wa Simiyu. Mkoa wa Simiyu una Wilaya tano nazo ni Bariadi, Italima, Maswa, Meatu na Busega, hizo zote zina ukosefu wa maji hususan Wilaya ya Bariadi na Meatu akina mama wanahangaika sana na tatizo la maji. Tatizo la maji

limekuwa sugu Mkoa wa Simiyu. Hata mwaka jana tatizo la maji niliongelea lakini mpaka sasa naona halijatekelezwa. Tunaomba pia Serikali sasa ifikirie kuvuta maji toka Ziwa Victoria kuja kwenye Wilaya zetu za Bariadi, Italima, Maswa Meatu na Busega kwani ni Wilaya ambazo tuko karibu na Ziwa Victoria. Huu utakuwa mradi pekee utakaoondoa tatizo la maji Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa la Mwanjoro lililopo kule Meatu liishe ili wananchi wa Wilaya ya Meatu waweze kujikomboa na hili tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Waziri wa Maji kwa uwasilishaji wake mzuri wa bajeti. Pia nawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa kuhakikisha wananchi walio wengi wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa Wizara hii ya Maji inavyogusa wananchi wengi na kuwaongeze fedha za ndani kwenye bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji kwenye vijiji kumi. Kutokana na mchakato mzima tokea kutafuta au kupata wataalam wa kusanifu mradi mpaka kuanza

kazi za ujenzi (kupata kibali cha ujenzi) inachukua karibu miaka tisa. Kwa kweli huu ni muda mrefu ukilinganisha na mahitaji ya maji wanayohitaji wananchi katika vijihi hivyo, muda huu wa urasimu upunguzwe ili kazi za utafutaji maeneo ya maji ifanyike kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naishauri Serikali ipunguze VAT kwenye madawa ya kutibu maji ili wazalishaji wa maji waweze kutoa huduma kwa urahisi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, naishauri Serikali kukiwezesha Chuo cha Maji kilichopo Mlimani Dar es Salaam kwa kuwaongezea fedha za kuendeshea chuo ili kiweze kutoa wanafunzi wenyе taaluma sahihi. Pia naishauri Wizara ya Maji iwe na mikakati madhubuti ya kupeleka wafanyakazi wake katika chuo hiki ili wapate mafunzo au waajiri wafanyakazi waliopata mafunzo na kuwapeleka Wilayani ambako kuna upungufu wa wataalam wa sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kutumia mto Rufiji kutatua matatizo makubwa ya maji kwa Wilaya za Mkao wa Pwani hasa Wilaya ya Kisarawe, Mkuranga na Rufiji kwani chanzo hiki ni kikubwa na cha uhakika lakini hakijawahi kutumika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Serikali kupeleka maji katika miji Mikuu ya Wilaya. Nafahamu kuwa ni sera ya Serikali ya kupeleka maji katika miji ya Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa. Hivi karibuni Serikali imeainisha maeneo mapya ya utawala ambayo yanajumuisha Makao Makuu ya Wilaya mpya zinazoanzishwa. Ni dhahiri kwamba kwa kuanzisha Wilaya mpya baadhi ya Makao Makuu ni mapya kwa hiyo hata mipango ya kupeleka maji katika miji hiyo inabidi iangaliwe upya. Natoa mifano miwili ifuatayo:-

(i) Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Kakonko ni Kakonko. Kwa bahati nzuri, kuna mradi mzuri, mkubwa wa maji ya mtiririko ambao unatekelezwa na Shirika la Caritas kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo. Wizara ya Maji ilikwishatoa fedha shilingi milioni 50 za kufanya *detailed design*. Nashauri mradi huo ufuatiliwe kwa ukaribu sana kwa sababu una faida kubwa tatu. Kwanza, utatoa maji Makao Makuu ya Wilaya. Pili, utahudumia vijiji vya Nyakayenzi, Kasuga, Kikonko, Kakonko, Kanyauza, Kiyobera na Kabingo. Tatu, utekelezaji utachangia eneo la kufikia asilimia 65 ya upatikanaji wa maji. Ni

mradi mzuri, wa mtiririko, ambao ungeipa "mileage" nzuri Wizara ikiusimamia. Hivi sasa tumepata mtekelezaji mzuri (*DWE*) anayejituma, anachokosa ni *technical and financial backstopping*.

(ii) Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Uvinza. Kuna miundombinu ya maji (*intake structures supply mains, storage tanks and distribution system*) iliyokuwa inatumika katika Kambi ya Wakimbizi ya Lugufu. Hivi sasa, hakuna wakimbizi na *water facilities* zote za thamani kubwa zilizopo ziko porini na zinalindwa na walinzi (*family*) wanaoishi mahali hapo. Wizara angefuatilia mradi huo ili utumike kupeleka maji katika Makao Makuu ya Wilaya ya Uvinza au vijiji vingine bada ya kuanza kujenga mradi mpya kabisa, *I strongly suggest Wizara (Wataalam) ikajionee mali iliyopo pale at risk!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuiarifu Wizara ya Maji kwamba nimefanikiwa kupata fedha kutoka *Food Aid Counterpart Fund* na kwa kutumia Ofisi ya Bonde ya Ziwa Tanganyika na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, tumefanikiwa kupeleka maji ya mtiririko katika vijini vya Kabingo na Kiyobera; wananchi sasa wanapata maji. Nitaendelea kufanya juhudzi za namna hii kuisaidia Serikali kupata miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, upatikanaji wa maji vijijini na mijini. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la upatikanaji wa maji mijini na vijijini na fedha zinazotengwa zimekuwa hazitoshelezi mahitaji makubwa ya maji kulingana na idadi ya watu kutokana na bajeti ndogo. Nashauri kuwa kuwepo na gawio sawa la fedha za programu ya maji vijijini na mijini. Mara nyingi utakuta kwamba fedha nyingi zinatengwa katika programu za maji mijini kuliko vijijini. Sote tunatambua kwamba kila mwananchi anahitaji maji, kwani maji ni uhai hivyo fedha zitengwe sawasawa ili kuwanusuru wananchi waishio vijijini mfano katika Jimbo langu la Singida Magharibi, Kijiji cha Mgungira, kuna shida kubwa sana ya maji kiasi kwamba wananchi wanagombania maji na wanyama wa porini kama tembo, ni hatari sana kwa uhai wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, miradi ya maji kutokamilika. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuanzisha vyanzo vingine vya maji ikiwemo visima virefu, miradi hii imekuwa ikisucasua kwa kiasi kikubwa sana. Hii inasababishwa na Serikali kuwa tegemezi, maana miradi hii inaendeshwa na fedha za wafadhili. Ni lazima sasa Serikali ione umuhimu wa kuanza kutumia fedha zake za ndani ili kukamilisha miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni umeme kutokupelekwa kwenye miradi hii ya maji. Katika Mkoa wa Singida kuna mradi mkubwa sana wa kuchimba visima unaofadhiliwa na nchi za Kiarabu. Mradi huu umeshafikia katika hatua nzuri, mabomba yameshatandazwa, matanki makubwa mawili kila moja lenye ujazo wa lita milioni tatu yako tayari. Tatizo kubwa ni kutokuwekwa umeme kwa ajili ya ku-pump maji kwenye vyanzo hivyo vya maji. Ni lini Serikali itapeleka umeme katika vyanzo hivyo ili mradi huu usiwe kazi bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, wadaiwa sugu wa maji. Kwa kuwa ni sera ya Serikali kutoa huduma ya maji kwa taasisi za Idara zilizo chini yake mfano, majeshini JWTZ na JKT, Polisi na Magereza lakini kwa masikitiko makubwa taasisi hizi zimekuwa zikiongoza kuwa ni wadaiwa sugu wa maji katika mamlaka za maji zilizoko kila Mkoa. Swali la kujuliza hapa ni hili, kama kila mwaka tunapitisha bajeti za kila Wizara zikiwemo Wizara ya Ulinzi na Mambo ya Ndani na moja ya fedha ni pamoja na hizi za huduma za maji kwa watumishi wake, ni kwa nini fedha hizi hazitumiki kufanya kazi yake na zinakwenda wapi mpaka kunakuwa na malimbikizo makubwa ya madeni kiasi hiki? Mfano mzuri ni Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Mbeya, peke yake linadaiwa jumla ya Sh.100,228,321.49 hadi Mei, 2012 na hivyo kuitia hasara Mamlaka ya Maji ya Mkoa wa Mbeya. Je, Wizara imejipanga vipi kukomesha tatizo la hawa wadaiwa sugu ili kuzitendea haki Mamlaka za Maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala llingine la Mamlaka za Maji ambazo bado zinapata ruzuku toka Serikalini mfano Mamlaka ya Maji Singida – SUWASA. Mamlaka hii imetishiwa kufungiwa maji katika kisima pekee inachotegemea mjini Singida kutokana na deni la TANESCO linalokaribia kufikia Sh.200 Milioni kutokana na Wizara kushindwa kulipa deni hilo. Ni lini Wizara itapeleka fedha katika Mamlaka hii ili kunusuru SUWASA kufungiwa maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ikakague mradi wa visima kumi kuona hali halisi. Naomba Serikali ifanye ukaguzi maalum kuona hali halisi ya mahitaji na matumizi ya maji yalivyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri utaratibu wa vigezo vyta kugawa fedha za maji urudiwe, kwani mgao wa fedha na hali halisi haviendani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la *concentration* ya miradi mikubwa ya maji kuwekwa mijini tu, sasa tuhamishie nguvu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Benki ya Dunia kwa Halmashauri ya Wilaya yangu Songea, fedha zimefika, sasa ni mwaka unapita bado tunasubiri kibali

cha kusaini mikataba. Kibali hiki kina masharti gani? Hivi kikichelewa na gharama zikipanda nani alaumiwe? Wananchi watapata maji kweli? Naomba sana vibali hivyo vitolewe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Benki ya Dunia Kijiji cha Mkongotema baada ya usanifu na upembuzi unagharamia Shilingi milioni 6.7 lakini wataalamu wa asili wametengeneza mradi kama huo Njombe kwa Shilingi millioni 300 tu. Usanifu wao katika Kijiji hicho ni Shilingi millioni 350 tu. Naomba Wizara inisaidie fedha hizo kiasi cha Shilingi millioni 350 ili wananchi wapate maji na miradi mingine iendelee kusubiri Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2012 dunia ilishuhudia uzinduzi wa ripoti ya pamoja ya mashirika ya umoja wa Mataifa mfano *WHO*, *UNICEF*, ripoti inayohusu kufikiwa kwa Malengo ya Milenia katika upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu. Ripoti inaonesha kuwa asilimia 89 ya watu duniani sasa wanapata maji.

Mheshimwa Mwenyekiti, wakati ulimwengu ukishangilia mafanikio haya ya kufikiwa Malengo ya Milenia kwa Sekta ya Maji, kwa Tanzania hali ipo tofauti kabisa. Tumeachiwa ripoti kwamba nchi yetu inashika nafasi ya 168 kati ya nchi 179 duniani, huku upatikanaji wa maji kwa wananchi ukigota katika asilimia 53 ikilinganishwa na asilimia 89 duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha Watanzania kuhusu kupatiwa maji safi na salama kimekuwa cha muda mrefu. Kilio hiki kinasikika kutoka kila kona ya nchi yetu. Wananchi wamesubiri ahadi ya kupatiwa maji safi na salama, kwa miaka 50 sasa, wanasubiri wakiamini kuwa tunasikia kilio chao, kinasikika kutoka kila kona ya nchi yetu.

Mheshimwa Mwenyekiti, wananchi wamesubiri ahadi ya kupatiwa maji safi na salama kwa miaka 50 sasa wanasubiri wakiamini kuwa tunasikia kilio chao. Wameendelea kusubiri hata pale walipouga magonjwa ya tumbo, kuhara damu na kipindupindu wameendelea kuwa na subira. Maana tumewahakikishia kuwa tunao mkakati wa kuwapatia maji kuitia programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo kuitia ufadhili wa Benki ya Dunia vijiji 10 katika kila Wilaya vitapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 Serikali ilipoitangaza Mkinga kuwa Wilaya kamili na 2007 kupata Halmashauri ya Wilaya tulishangilia sana tukajua sasa tunapiga hatua za haraka za maendeleo. Mji wa Kasera ukaamuliwa uwe Makao Makuu ya Wilaya, tukaweka mikakati ya kujenga Mji wetu uwe wa Kisasa. Lakini changamoto tuliyonayo ni maji. Hatuna maji pale Kasera ambapo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya. Tumebuni mradi wa kutoa maji kutoka Kinyatu kwenda Kasera. Utekelezaji wa mradi huu unategemewa kutumia fedha za programu ya maji safi na maji takatua mijini. Wilaya imekamilisha mchakato wa zabuni na kukabidhi majina ya walioonekana

wanaweza kuwa Wahandisi washauri tangu mwezi Mei, 2011, lakini hadi leo hatujapewa jibu lolote.

Mheshimwa Mwenyekiti, katika hili nalo, nahitaji Waziri anipatie majibu ni lini hatua za utekelezaji wa mradi huu zitaanza? (Upembuzi yakinifu, usanifu wa mradi, kuandaa gharama halisi, kuandaa makabrasha ya zabuni ya mradi na usimamizi wa ujenzi tangu mwaka 2007). Wimbo huu umeendelea, tumeshuhudia washauri wa kusimamia miradi hii wakichaguliwa, wakafanya tathmini, michoro ikatengenezwa na kama vile haitoshi, tukafanya kazi ya kuwahamasisha wananchi kujipanga na kuchangia kati ya asilimia 2.5 hadi asilimia tano kulingana na aina ya mradi.

Mheshimwa Mwenyekiti, wananchi wameitikia wito, wamechangia, lakini kwa bahati mbaya sana utekelezaji wa miradi hii unakwenda kwa *speed* ya kinyonga. Wananchi wa Mkinga wamechoshwa na wimbo huu, Mwakijembe, Mbuta, Kiluku Duga, Bwaga-Macho, Bamba Mwarongo, Parungu Kasera na Mupatano wamechoshwa. Kwa nini tumechoshwa? Kwa sababu Mkunga ni mionganini mwa zile Halmashauri 62 zilizokidhi vigezo na kukamilisha taratibu zote muhimu zinazotakiwa, lakini pamoja na kukamilisha huko, nini kimetokea? Leo hii ni mradi mmoja tu umeanza kutekeleza pale Daluni. *This can not be right at all.*

Mheshimwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkinga wanahitaji maelezo ya kina wakati Waziri anahitimisha hotuba yake, aseme ni vijiji vingapi vitapatiwa maji Mkinga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji lipo vilevile kwenye Kata ya Bwiti kwenye vijiji vya Magati, Loko, Mavovo, Kuimbo na Mwanyumba. Tatizo hili limekuwa kubwa kiasi cha kufikia watu kushikiana mapanga. Mradi ule umejengwa miaka ya 1978 – 1979. Chanzo cha magati kimekuwa kidogo kutokana na ongezeko la idadi ya watu. Kuondoa tatizo hili, inabidi kupanua chanzo kile. Jumla ya Shilingi 154 zinahitajika kwa zoezi hili. Inabidi kupanua chanzo kile. Jumla ya Shilingi millioni 154 zinahitajika kwa zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliyasema haya mwaka 2011, lakini hadi leo hakuna lilihofanyika. Hivi tunasubiri maafa yatokee ndiyo tuchukue hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja hii, naomba majibu kuwa Serikali inakuja na utaratibu gani wa dharura kuwaondolea wananchi tatizo la maji?

Mheshimwa Mwenyekiti, chanzo cha mto wa kule Kibago ambacho ni chanzo cha mtiririko cha Kwekanta kina uwezo wa kuhudumia vijiji vya Kuze, Kibago, Churwa, Mhinduro na Bamba Mavongero na maeneo mengine ya karibu ili kutumika zinahitajika Shilingi millioni 752. Watu wa Mkungwa wanahitaji kufahamu, ni lini wataondokana na kero ya maji kwa kutumia chanzo hiki cha uhakika?

Mheshimwa Spika, nawasilisha.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Kibondo Mjini maji yanatoka mara mbili kwa mwezi, wakati mwingine hayatoki kabisa. Napenda kupata majibu ya Serikali, ni lini itatatua tatizo hili? Pia Mamlaka ya Maji imekuwa inatoza pesa kwa kukadiria, kwani hakuna mita. Hivyo wanakadiria tu. Maji yanatoka siku mbili au tatu kwa wiki, wananchi tunapewa bili ya Sh. 28,000. Hii siyo sahihi. Napenda kuishauri Serikali ifunge mita na kuhakikisha maji yanatoka mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali itoe maagizo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, itoe taarifa ya mapato na matumizi kwa wananchi, kwani kwenye kila kisima wananchi wanatozwa fedha na hajulikani fedha hizo zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali itoe muda kwa Mkandarasi ili akamilishe na akishindwa kukamilisha ndani ya muda huo, ichukue hatua. Pia miradi ya visima kumi katika Jimbo la Muhamwe havijatekelezwa na maji hayatoki. Napenda kuishauri Serikali ifuatilie visima katika Jimbo la Muhamwe, vyote kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kutoa ushauri kwa Serikali, kila mwaka kuwa na mradi mkubwa mmoja, mfano. Mradi mkubwa unaweza kutoa maji ziwa Tanganyika ukasambaza Mkoa mzima,

Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi maeneo ya Kusini, Ruaha maeneo ya Iringa, Njombe na kadhalika. Kamati iliyokuwa kwenye Mradi wa *Ziwa Victoria* hadi Kahama, tufikiri kwa upana na kutekeleza.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji nchini limekuwa kubwa, maji safi na salama ni kitendawili ambacho Serikali imeshindwa kukipatia ufumbuzi, vyanzo vyta maji vinaharibiwa kwa wananchi kuchoma misitu, kukata miti na ufugaji unaofanywa bila kuzingataia Sheria. Ninaishauri Serikali kuandaa na kuviendeleza vipindi kupitia redio na *television* mbalimbali ili kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itueleze, ina mkakati gani wa ziada kutumia mito zaidi ya 100 isiyokauka Mkoa wa Morogoro, kuandaa mazingira ya kuwapatia maji wananchi wa Mkoa huo ili waweze kupata maji safi na salama? Hivi Serikali haioni aibu Mkoa kama Morogoro uliyo na mito mingi isiyokauka kuwa na tatizo la maji?

Mheshimwa Mwenyekiti, uvunaji wa maji ya mvua bado Serikali haijaandaa mazingira mazuri ya kutoa elimu juu ya uvunaji wa maji ya mvua. Ninashauri Serikali ijipange vizuri kutoa elimu ya uvunaji maji ya Mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la malipo yasiyo sahihi katika ankara za maji kwa wateja limekuwa likiwasumbua wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji wanayotumia baadhi ya wananchi siyo safi wala salama na wanalipa fedha kila mwezi. Ninaishauri Serikali kuandaa mazingira ya kuboresha malipo ya ankara za maji kulingana na matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itueleze na iwaeleze Watanzania ni kwa kiasi gani Serikali ilitoa fedha kwa wananchi waliong'atwa na mamba au kuliwa na simba wakati wakitafuta maji? Kama Serikali hajatoa fidia, ina mkakati gani wa kutoa angalau fidia au ubani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mabaya ya fedha za miradi inayofadhiliwa na Wahisani limechukua sura nyingine baada ya kugundulika baadhi ya makandarasi siyo waaminifu kwa kupeleka vifaa visivyostahili, baadhi ya vifaa viko chini ya kiwango na mradi unachukua muda mfupi tofauti na malengo. Naishauri Serikali kuliangalia hili ili fedha hizi za Wahisani na fedha za ndani za miradi ya maji zitumike vizuri ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kuwasilisha.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai na mji ni kwa kila kitu. Bila maji siyo binadamu wala mimea ambayo inaweza kuishi na

ndiyo maana wakati wa kiangazi, miti, majani na hata wanyama hypoteza maisha. Lakini na sisi binadamu, nyakati kama hizo na hata kwenye maeneo kame maisha ya Watanzania hayaendi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watanzania hatujaliani, hatuaminiani kwamba tunaweza na wataalamu tunao, ila hatuamini kuwatumia. Hapa ndiyo mimi napata shida. Sijui ni kwa nini hatutumii raslimali watu tulionao (wataalamu wa ndani)! Shaka inaonekana kwamba:-

- (1) Wizara inaweka mbele maslahi binafsi kwa watendaji na kwamba kutumia wataalamu washauri wa ndani hawataweza kupata asilimia 10 yao; na
- (2) Serikali kupitia Wizara, haina mpango mkakati ambao ni madhubuti wa kuwahakikishia wananchi kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kwa Nchi kama Tanzania yetu hii, kwamba ukiacha Waheshimwa Wabunge wengine, lakini hata wale watokao katika maeneo ambayo ni vyanzo vya maji, bado nao wanalamikia maji hapa Bungeni, mfano wa maeneo hayo ni kama vile: Mwanza, Kigoma, Bukoba, Morogoro na kadhalika, hili ni jambo la ajabu sana kwa maeneo haya kuendelea kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha hizi za kisanii ambazo hazifikii mwisho, haziwasaidii wananchi, maana wananchi hawahitaji ushindani wa methali za

Kiswahili, wanachohitaji ni maji safi na salama kwa mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hawa wahandisi, washauri, wasanifu na wataalamu wanaosema kila siku kwamba wako kazini, wanachosanifu hasa ni nini? Mbona jambo hili hakuna angalau eneo moja ambalo tatizo hili limepata ufumbuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali iache lugha hizi za kisanii na ifikiri namna bora ya ya kutatua tatizo hili sugu kwa nchi yetu, kuliko kupiga siasa. Ni ajabu kwamba hadi leo hii, bado Watanzania wanaombwa kwa ahadi ya maji isiyotekelezeka.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara kwa kuwasilisha Bajeti Bungeni kuhusu Maji, sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi hapa nchini hazina maji na hata kama kuna maji hayatoshelezi msimu/mwaka mzima au visima hivi kutotoa maji kabisa kwa msimu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Halmashauri husika na uchimbaji wa visima visivyotoa kabisa maji wawajibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaupongeza sanamradi wa Maji - Ziwa Victoria. Lakini mradi huu tajwa unatakiwa utumike vizuri na ukitumika vizuri ni ukombozi na utakuwa ukombozi wa maeneo mengi, mfano Tabora, Nzega, Igunga na kadhalika.

Kinachotakiwa kifanyike ni Serikali kujipanga kununua mabomba na kuyatandaza maeneo husika, kwa sababu maji hutiririka kwa *gravity*. Serikali izingatie ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upotevu wa maji hovyo kwa sababu wananchi hawana elimu ya uvunaji wa maji ya mvua, maeneo kama mashulenii, majumbani na maeneo mengine. Ombi langu ni kuvitumia vikundi mbalimbali kuelimisha pia mihadhara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama nchi ni maskini, lakini umaskini wa nchi hii hautakiwi kutangazwa kuwa wa kudumu hata kidogo. Tuna raslimali nyngi ambazo fukizitumia vizuri, zinaweza kutukwamua na kuweza kuwa na kipato kikubwa cha ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa tegemezi kwa asilimia 100, kubwa toka kwa Wahisani ni kurudisha maendeleo nyuma ikiwemo ukosefu wa maji kama inavyoonekana sasa katika Bajeti hii.

Mheshimwa Mwenyekiti, mwisho, naomba ahadi za Mheshimiwa Rais kama alivyoomba au kuahidi katika Majimbo mbalimbali kuhusu maji, zitekelezwe.

Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza

Mheshimiwa Waziri kwa kuchaguliwa tena kuwa sasa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko yangu ni mradi wa visima 10 kila Kijiji kwa ushirikiano na Benki ya Dunia. Nashukuru sana mradi umeanza kwa Vijiji viwili vyta Mkuu na Kijiji cha Rombo visima vimechimbwa. Pamoja na shukrani hizo, suala la umuhimu sana ni kuchelewa kwa umaliziaji wa visima hivyo. Baada ya uchimbaji huo, waanze awamu ya pili haraka iwezekanavyo ili hivi visima visije fukiwa na kuiletea tena hasara Serikali na kuwapa ulaji hao wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri katika vijiji kumi, kuna kijiji kimoja katika Jimbo langu la Mkuu, pesa ya asilimia mbili na nusu tayari wamechanga na zipo kwa muda mrefu na hofu yangu zisije kuliwa.

Kijiji hiki ni maji mtiririko ni kiasi tu cha kulenga na kusambaza kijijini kwa gharama nafuu tu. Maji yawe ni safi na salama kwani baadhi ya Taasisi wanatumia wanapeleka kwa wahusika na wataalam wamethibitisha kuwa ni safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huzuni ambalo Wilaya yetu inatukabili ni suala la wataalam wa Idara ya Maji kwamba ni wachache sana. Naomba Mheshimiwa Waziri atupatie wataalamu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, hakuna taarifa yoyote inayohusu

mji mdogo wa Mikumi, na pesa zilizotengwa kwa ajili ya vijiji vya Jimbo langu la Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naegemea maombi na maelezo yangu yatazingatiwa na kufanyiwa kazi kama nilivyoeleza.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

- *Bill za matumizi ya maji ziwe sawa na matumizi;*
- Wakati wa matengenezeo ya mabomba yanayopita ndani ya majumba, basi wenyen yumba waarifiwe na marekebisho yafanyike ili hali ya awali irudie;
- Madawa yawekwe katika maji, wakati mwingine maji yanatoka yakiwa na tope; na
- Maji bado ni kitendawili nchi nzima, licha ya juhud zote, tuendelee kupeleka juhud ili suala lipate ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchimbaji wa visima vifupi na virefu uangalie maeneo yenye taabu ya maji. Mfano, Vijiji vya Makurunge, Misugusugu na sehemu nyingine.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba bili za maji zisiletwe mara mbili kwa mwezi. Ni vyema zipatikane kila mwisho wa mwezi na siyo katikati ya mwezi, kwani zinachanganya.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba Uharibifu uliofanywa na *DUWASA* kwenye nyumba yangu Dodoma area 'D' NIC House urekebishwe. Ukuta kwa ndani umeanza kubomoka baada ya bomba kubwa la maji kuvuja na matengenezo yake kufanyika. Matengenezo hayakuwa makini, hasa yale yaliyofanywa mara ya pili baada ya bomba kubwa kupasuka tena.

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii, pia nimpongeze Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha mpango na makadirio ya matumizi katika sekta hii muhimu ya maji kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji ni uhai, maji ni maendeleo na maji ni kila kitu. Naipongeza sana Serikali kwa kuongeza bajeti ya maji kutoka Shilingi bilioni 30.7 mwaka 2010/2011 hadi Shilingi bilioni 140 mwaka 2012/2013. Pamoja na ukweli huu, bado nchi yetu inakabiliwa na uhaba wa maji kwa matumizi katika maeneo mbalimbali hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa Maji utachochea usawa wa jinsia na maendeleo ya wanawake. Ni ukweli usiopingika kuwa wanawake na

wasichana ndiyo wana jukumu kubwa zaidi la kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani hasa katika maeneo ya vijijini. Mara nyingi hupoteza muda mwingi kwa kutafuta maji, aidha, kwa kutembea muda mrefu angalau kusubiri maji badala ya kushughulika katika shughuli za uzalishaji mali, masomo na/au malezi ya watoto na familia. Wasichana wengi sana hasa walio vijijini hupoteza muda mwingi zaidi wa masomo yao kwa ajili ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji hasa vijijini utachochea kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025. MKUKUTA na lengo la Milenia Na. 3 yanayohusu kufikiwa kwa idadi sawa ya wasichana na wavulana katika ngazi zote za elimu ikiwemo ya Elimu ya Sekondari na vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kuwa, Wizara ya Maji ihakikishe kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya maji maeneo ya vijijini zinatumika kwa ajili ya kuharakisha upatikanaji wa maji na siyo kwa ajili ya posho, vikao na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ni Mikakati gani imepangwa kutatua tatizo la maji katika Mji na Wilaya ya Muheza? Wilaya ya Muheza hasa Mji wa Muheza unakabiliwa na tatizo kubwa sana la uhaba wa maji. Ukosefu wa huduma za maji Muheza, unaweza kusema bila shaka, kuwa ndiyo tatizo kubwa linalowasumbua wananchi wa Muheza. Mzigo mkubwa wa kutafuta maji unakuwa ni kwa wanawake na wasichana.

Tatizo la maji Muheza pia limemgusa Mheshimiwa Jakaya Kikwete ambapo mwaka 2006 alipokuwa anazindua Shule ya Sekondari ya Mtindiro aliahidi kushughulikia tatizo la Maji Muheza (Mradi wa Maji wa Mbabara).

Mheshimwa Mwenyekiti, ni wakati sasa, Wizara ikatatua tatizo la maji Muheza. Mradi wa Maji kutoka chanzo cha Ziggi (ahadi pia ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2004/2005). Mradi huu ndiyo wa uhakika kwa kukidhi mahitaji Muheza. Hivyo ni muhimu utengewe fedha za kutosha na utekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalamu kwa kazi waliyofanya ya kuandaa hotuba ya bajeti. Ni wazi kazi imefanyika na hotuba imewasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina sera nzuri sana ya maji. Lakini kwa sababu mbalimbali, lengo la kuwapatia wananchi maji safi na salama bado liko mbali sana na kwa kiasi kikubwa zaidi kwa watu wa Vijijini. Kwa sababu hii, hata lengo la afya bora, bado liko mbali, kwani bila maji safi na salama hakuna afya bora pia. Inawezekana wapangaji wa mipango ya maji hawalizingatii hili. Lakini wataalamu wa afya waliofanya utafiti kuhusu uhusiano baina ya maji safi na afya za watu, wamehitimisha kuwa wananchi wakitumia maji safi na salama wataacha kupata maambukizi mengi yatokanayo na maji yasiyofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo moja. Ipo hasara nyingine kubwa ambayo kama Taifa hatuwezi kupuuza, nayo ni kwamba watu wengi sana kila siku hupoteza masaa mengi ya kazi kutafuta maji. Hakuna mtu ambaye amefanya utafiti kuhusu ni masaa mangapi ya kazi ambayo hupotea kila siku, masaa ambayo yangetumika katika shughuli nyingine za tija za kiuchumi, lakini bila shaka ni masaa mengi, ni mamilioni. Tatizo hili hasa liko Vijijini ambako wananchi katika maeneo siy machache, hulazimika kufuata maji umbali mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitajielekeza kwenye matatizo ya maji yaliyo kwenye Jimbo langu la Bukombe. Bukombe ni mionganini mwa maeneo yaliyo pembezoni ambayo bado yanakabiliwa na matatizo makubwa ya maji kutokana na upatikanaji wake; pili, yale yanayopatikana mara nyingi siyo safi wala salama. Ukiiondoa sehemu kadhaa chache (sehemu za Miji midogo ya Ushirombo na Uyovu), maeneo mengi yaliyobaki katika Jimbo la Bukombe yana matatizo ya maji. Vijiji vinavyokabiliwa na matatizo makubwa zaidi ni Nalusunguti, Kabagole, Nakayenze, Busonzo, Namonge, Namsegwa na Vijiji vingine. Kijiji cha Nalusunguti, kina tatizo kubwa zaidi kwa sababu akina mama wengi huhangaika kwa masaa mengi kwenda kuchota maji katika Wilaya ya Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti, Bukombe imetajwa kuhusiana na miradi ya Maji ya Benki ya Dunia. Bukombe imetajwa katika jedwali Na. 12 ukurasa 98. Wilaya ilipokea Sh. 2,902,990,461 kati ya

mwaka 2007 - 2012 kwa ajili ya miundombinu na Sh.144,266,260 kwa ajili ya kujenga uwezo. Swali ninalotaka nijibiwe ni: Je, fedha hizi zote zilitumika katika miradi ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti, Bukombe pia imetajwa kwamba ilichimba visima 16, na vyenye maji ni 15. Je, Waziri anaweza kuniambia visima hivyo 16 au 15 viko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mahitaji ya maji safi na salama Bukombe, wananchi wamenitura niiombe Wizara izingatie mahitaji yafuatayo:-

- (1) Kipaumbele ni mradi wa maji ya Ushirombo. Kinachohitajika ni kusambaza maji katika Mitaa yote ya Mji Mdogo wa Ushirombo. Waziri Mkuu katika Ziara yake Kanda ya Ziwa mnamo Machi, 2012 aliwaahidi wananchi wa Ushirombo kuwa angehakikisha Serikali inatoa Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga mtandao wa mabomba ya maji ili tatizo la maji liishe. Ahadi hii ya Waziri Mkuu mbona haionekani katika hotuba ya bajeti?
- (2) Mradi wa maji wa Kata ya Uyovu unahitaji pia kujengewa mtandao wa mabomba.
- (3) Vijiji vingi vinahitaji miradi ya visima vifupi.
- (4) Maeneo mengi pia panahitajika visima virefu. Upimaji wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya visima virefu haujafanyika vijiji vingi.

- (5) Mabwawa makubwa katika maeneo yenye matatizo makubwa zaidi yanahitajika.
- (6) Serikali ijipange vizuri, itoe elimu kuhusu njia rahisi ya kuvuna maji kwenye nyumba za makazi. Hili likifanyika litapunguza tatizo la maji kwa kiasi fulani.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuandaa bajeti hii na hasa ukizingatia kwamba maji ni uhai. Pamoja na matatizo mengi yanayoikumba Wizara hii yakiwemo ya kutopatikana kwa maji ya uhakika vijiji na mijini kwenye visima na Majimbo, naomba nipate maelezo ya kina katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji vingi na miji mingi hapa nchini viko karibu na maji ya maziwa na mito, lakini wanachimbiwa visima ambapo vingi havitoi maji au vinatoa maji kidogo. Kuna sababu gani za msingi vijiji hivi na miji hii kutopatiwa maji ya bomba toka Ziwani au Mtoni? Kwa mfano, Jimbo la Mwibara Kijiji cha Namhula ambacho ndicho kinaongoza kwa kuwa mbali na maji ya Ziwa Victoria kiko kilimita tisa tu. Ni jambo la kushangaza sana ambapo tayari kuna miundombinu ya maji ya bomba katika vijiji vya Nyamitwebili (*Kasahunga Water Pump House*), Kibara (*Kibara Water Pump House*) na Isanju (*Isanju Water Pump House*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mwibara tukiongezewa uwezo wa *pump*, vijiji vyote vitakuwa na maji ya bomba ya uhakika kutoka Ziwanî badala ya sasa kuendelea na mtindo wa kuchimba visima na kukosa maji au kupata maji kidogo. Hii ni kupoteza fedha, kutafuta maji yasiyoonekana wakati kuna maji yanayoonekana kwa macho. Kama maji ya Ziwa *Victoria* yanachukuliwa na kusafirishwa kwenda Mikoa ya Shinyanga na Tabora zaidi ya kilomita 250, inakuwaje Kijiji kilichoko kilomita tisa tu ndicho kichimbiwe maji ya kisima? Hii haikubaliki, na ninaomba nipate maelezo ya kina juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo letu tulipata miradi minne ya maji chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia katika vijiji vya Bulamba, Kibara na Karukekere, vyote kwa mradi wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria na Mumagunga kwa mradi wa maji ya kisima kirefu. Wananchi wa vijiji hivyo wanaambiwa wachangie shilingi milioni 20 wakati hizi fedha ni zaidi ya asilimia tano zinazotakiwa kuchangwa. Aidha, hadi sasa miradi hii imekwama na hivyo kuwakatisha tamaa wananchi ambao wameamua kuchangia miradi hiyo. Naomba nipate maelezo ya kina juu ya miradi hii ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia hususan, ni kiasi gani kinachotakiwa kuchangwa na wapiga kura wangu wa Jimbo la Mwibara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, naunga mkono hoja.

MHE. DONALD K. MAX: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nimefuatilia sana mradi wa

maji wa Geita wa Shilingi bilioni 15 ambapo mgodi wa dhahabu wa *GGM* unachangia Shilingi bilioni 6.0 na Serikali Shilingi bilioni 9.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mgodi, tayari vifaa vilivyoagizwa toka nje kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hadi kwenye tanki la kuhifadhi maji vimekwishafika Geita, lakini kwa upande wa Serikali kila nilipokuwa nafuatilia, naambiwa fedha imepatikana toka *ADB Bank*, ila sioni kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi wa *GGM* utakabidhi sehemu yao ya mradi mwezi wa Kumi lakini sisi usanifu wa usambazaji wala haujaanza na hii itakuwa haipendezi. Maji yafike kwenye tanki la usambazaji, lakini sisi tupo tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu kuhusu suala hili la maji Geita Mjini ambapo hadi sasa ni miaka saba na Wakazi Mjini Geita wako zaidi ya 600,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maombi ya visima katika vijiji vya Geita, niliomba visima 47 katika Kata 14 kati ya Kata 19, lakini huu ni mwaka wa pili hakuna hata kisima kilichofikiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa suala la usambazaji maji Geita Mjini ambapo yanki litakuwa Mjini pale pale, Serikali ilishughulikie, kwani sasa Wanageita wamevumilia miaka saba na maji ni ya shida sana.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii muhimu na adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri pamoja na uwasilishaji wake, umuhimu wa maji kwa afya na uhai wa kila kiumbe katika dunia ni muhimu na inapaswa kuthaminiwa kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama vijiji ambao ndiyo wazalishaji mashambani hasa katika kilimo, ndiyo wanaolazimika kupoteza muda mwingi katika kushughulikia maji. Akina mama wanasumbuka umbali mrefu kutafuta maji kwa matumizi ya kila siku. Hivyo, muda mwingi wanaopoteza katika kutafuta maji. Wanakosa muda mzuri katika kuzalisha, katika shughuli za kujenga Taifa kwa ajili ya kufanya kazi hii ngumu ya kuchukua maji umbali mrefu. Wanadhoofu na kupata magonjwa ya kazi ngumu. Taifa linapata hasara mara mbili. Kwanza, kukosa watu wenye afya na kuchapa kazi na pili gharama za madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa maji unasababisha wananchi kunywa maji ambayo siyo salama kwa afya ya binadamu na husababisha maradhi mbalimbali yanayo sababishwa na maji machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ipange mipango madhubuti, mipango endelevu tuwaokoe wananchi katika usumbufu na maradhi, tupate watu wenye afya katika kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali, kwa kutumia wataalamu tulionao, ipange mikakati madhubuti kuchimba visima virefu na vifupi vijijini. Serikali ichimbe mabwawa ya maji, sehemu mbalimbali vijijini, vile vile tuanzishe utaratibu wa kutega maji ya mvua katika majengo ya nyumba zetu. Haya tutakapoyatengeneza kwa ufanisi, basi yatasaidia katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni tatizo baya na kubwa ndani ya nchi yetu. Tatizo la maji athari yake siyo afya na uchumi tu, bali baadhi ya watu wamepoteza maisha kwa kuuliwa na simba wakati wakitafuta maji, wengine wameuliwa na mamba na wengine nyoka. Matukio mengi mabaya ambayo yamesababishwa na usumbufu wa maji, hata nyumba nyingine zimeanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi yenye vyanzo vingi vya maji. Ni aibu miaka 50 ya uhuru kukosa maji na mpaka wale wanaoishi kwenye maziwa na mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujenge Taifa la watu wenyе afya kwa kupata maji safi. Ahsante. Maji ni uhai.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kabla ya majibu kuhusu makadirio ya mwaka mpya wa fedha, Wizara itoe majibu ya kina namna ilivyoshughulikia maoni na

mapendekezo ya mwaka wa fedha 2011/2012. Ikiwa Wizara haitatoa majibu ya kutosha ikiwemo kutekeleza ahadi ya kutembelea Jimbo la Ubungo kushughulikia matatizo ya maji na kusimamia utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais Kikwete alizozitoa Jimbo la Ubungo mwanzoni mwa mwaka 2010 eneo la Kimara Bunyokwa na mwishoni mwa mwaka 2010 eneo la Manzese, ikiwa Wizara haitaeleza hatua inazopanga kuchukua kuhusu Jimbo la Ubungo, nitaendelea na hatua ya kuwasilisha hoja binafsi katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya mwaka 2012/2013, naomba Wizara irejee mchango wangu nilioutoa wakati wa kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji na bajeti ya Ofisi ya Rais, na kuongeza fedha za mradi wa Kidunda na pia uwekaji wa miundombinu maeneo ya pembezoni ya Makoka, Goba, Kwembe, Kibwegere, Mbezi Makobe na mengineyo katika Jimbo la Ubungo.

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukerewe inazungukwa na maji ya ziwa Victoria kwa asilimia 90 na Rais wa awamu ya kwanza, Hayati Mwalimu Julius Nyerere alifanikiwa kuweka *pump* za maji katika vijiji vya Nansio, Chabilungo, Ihebo (Nabungona) Gallu, Bugorola, Bukindo, Bwisya na Irugwa. Pampu hizi zilikuwa zikiendeshwa kwa mafuta ya (*Diesel*) wakati Ukerewe hakukuwa na umeme. Leo hii Ukerewe tuna umeme katika vijiji vilivyo na pampu, hivyo, ni suala la kukubali na kuweka *motor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atueleza ni lini pampu hizo nilizozitaja zitawekewa *motor* ili zianze kusukuma maji ili kuwaondolea kero wananchi wa Ukerewe?

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia bajeti hii ya maji katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mtaro wa Ntomoka una uwezo wa kuhudumia zaidi ya vijiji 13 katika Wilaya ya Chembba na viwili katika Wilaya ya Kondoa. Mradi huu kwa sasa upo katika hali mbaya kutokana na miundombinu yake kuchakaa. Naomba Serikali kuu ichukue mradi huu ili urudi katika hali yake ya kawaida, kwani kuuacha chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa itakuwa ngumu kuuendesha kutokana na Halmashauri kutokuwa na uwezo wa kifedha ikitiliwa maanani kuwa mradi huo Miundombinu yake imechakaa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Mheshimiwa Mbunge na wafadhili kadhaa tumefanikiwa kuchimba visima zaidi ya kumi, lakini mfadhili amegoma kutoa pesa za mashine na *pump* za kusukuma maji kwa sababu visima hivyo ni virefu na mfadhili anasema anaweza kutoa "*Hand Pump*" tu ambazo haziwezi kusukuma maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ilichukue jukumu la kutusaidia fedha za kufunga mashine na *pump* ili wananchi hawa waondokane na kero hii. Naiomba Serikali ikamilishe taratibu za kujenga

Bwawa la Farkwa haraka ili maji hayo yasaidie vijiji kadhaa ikiwa ni pamoja na Wilaya mpya ya Chemba ambayo ipo kilomita 45 tu kutoka eneo la Farkwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja na baada ya kuunga mkono, naomba kuchangia maeneo machache kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake, miradi ya maji inayotegemea ufadhilli wa Benki ya Dunia hajasaidia, kwani kwa kiasi kikubwa hamna mafanikio.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana Wilaya mpya na Jimbo la Kalambo hakuna hata mradi mmoja ambao ulishafanikisha upatikanaji wa maji. Katika vijiji vya Jimbo langu, vijiji vitano hakuna hata kijiji kimoja ambacho maji yamepatikana kwa maana ya mradi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyote vilivyo Mwambao mwa Ziwa Tanganyika vina hali mbaya sana, naomba vijiji vya Kusanga, Kipwa, Kilewani, Kapele, Kusumba, Kipanga na Samaza visaidiwe vipate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza, Wilaya ya Kalambo hakuna hata mradi mmoja wa Kitaifa. Naomba Waziri aseme neno angalau moja.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na katibu Mkuu kwa kuwasilisha Bajeti yao vizuri na yenye kuleta matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara, napenda kutoa ombi rasmi la kupatiwa maji Mji mdogo wa Ilala Wilaya ya Kilolo kutokana na ongezeko kubwa la watu kutoka watu 3000 (1968) hadi kufikia zaidi ya 50,000 mwaka huu wa 2012. Uwezo wa Halmashauri katika hili umefikiwa ukomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana msaada wa Serikali kuu katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa maji kwa vijiji kumi katika kila Halmashauri umekuwa hautekelezeki na hasa ukizingatia kwamba wananchi katika miradi hii walichangia għarama. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia fedha za ndani ili kuitimiza azma hii ya muda mrefu?

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi japo pia nimeomba kuchangia kwa kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba katika Tanzania baada ya miaka 50 ya kiuchumi kwa nchi yenye vyanzo vingi vya maji, lakini hadi leo hakuna

Mbunge yeote humu anayeweza kusimama na akasema kuwa Jimboni kwake kuna maji safi, salama yanayotoka muda wote na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika hali hii, lazima sasa Mawaziri hawa wapya wafanye kazi ya ziada ya kuhakikisha malalamiko ya maji yanapungua. Kama kuna maeneo ambayo Serikali ingependa kupunguza gharama katika uendeshaji wake, basi ni kupeleka maji vijiji na mijini. Mfano mdogo ni kwamba tangu maji yafike Shinyanga Mjini magonjwa ya milipuko sasa yamepungua na fedha za madawa zinazopelekwa na Wizara ya Afya zimepungua hasa kwa yale magonjwa ya milipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa pongezi kwa Serikali kuhusiana na mradi mkubwa wa maji wa Ihelele (Mwanza).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni wa fedha nyingi sana, lakini cha ajabu matumizi ya mradi huu bado haijafikia asilimia 50, kwa kuwa watumiaji wa maji haya ni wachache kuliko mradi wenyewe, wakati bado vijiji ambavyo bomba la maji kuelekea Shinyanga, kutowapa maji wanavijiji vya mahali ambapo bomba linapita, kumepelekea wananchi wengi kutoboa mabomba na kusababisha hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa kupeleka na kuwapa maji wanavijiji ambao mabomba ya mradi wa maji ya Ihelele, basi wanapata maji na kuepuka hasara

inayojitokeza. Pia, ikumbukwe kwamba ni haki yao ya msingi kupata maji, na maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda pia kujua na kupata ufanuzi wa Waziri kuhusu miradi ya maji katika Miji ya Musoma na Bukoba. Kwa kweli miradi hii ni muda mrefu sana na kila siku majibu ya Serikali yamekuwa ya kuridhisha tu na ya kuomba tuvute subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ambao unafadhiliwa na Serikali ya Ufaransa *AFD*, umekuwa ukisika tu masikioni mwa Watanzania na haupo machoni mwa Watanzania. Haionekani! Je, katika mwaka huu wa fedha, ni lini mradi utaanza na ni lini mradi utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali langu la Wizara hii, majibu ya aliyekuwa Naibu Waziri wa wakati huo alijibu kuwa mradi ungeanza tarehe 15 Mei, 2011 na kukabidhiwa Desemba, 2013. Lakini cha kushangaza, hadi leo hakuna lolote ambalo limefanyika (*field*). Itakuwa vigumu sana kwangu kuhakikisha na kuiunga mkono bajeti hii kama Serikali haitaonesha dalili za wazi kabisa za kutekeleza mradi huu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kabisa kwa kweli hakuna hata Mbunge mmoja humu ndani ambaye anaweza kukiri kuwa anayo maji ya kutosha na ya uhakika kwa muda wote na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa maji na kuhakikisha basi Watanzania walio wengi wanapata maji safi, salama na kwa gharama nafuu na kwa muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anakumbuka tangu tarehe 13 Februari, 2007 mlkopaa fedha Benki ya Dunia Dola milioni 59 kwa *Project ID P 087154*. Je, unajua zimetumikaje? Mbona watu wanalilia maji wakati fedha hizi ziliwa za *water project*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fuatilia
www.worldbank.org *water sector project*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iwe *serious*. Nashukuru.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri hapa Bungeni. Kipekee kabisa, naomba nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kwa kuupokea ujumbe toka Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ulioongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri. Pia namshukuru kwa kupokea barua yangu ya maombi ya mradi wa maji katika Mji mdogo wa Kayanga hasa Mji wa kibiashara wa Omurushaka na vitongoji jirani vya Kishao, Nyakahanga, Ihanda, Bujuruga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa maji ya eneo hili ni muhimu sana, kwani Mji huu mkubwa kwa

biashara na wa kwanza Wilayani Karangwe hauna hata tone moja la maji. Yaani upatikanaji wa maji katika mji huu wa Omurushaka na vitongoji vyake ni asilimia sifuri. Tatizo siyo chanzo cha maji, kwani eneo hili chanzo cha maji kiko chini ya kilomita tano.

Tatizo ni miundombinu tu ambayo tayari Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe pamoja na bajeti ndogo inayopata imejitahidi kupeleka umeme eneo hilo kwa gharama ya Sh. 80,000,000 na pia eneo la chanzo cha maji lilisafishwa kwa gharama karibia Shilingi milioni 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ili ukamilike, unahitaji gharama ya Shilingi bilioni 1.5 na Shilingi bilioni mbili. Fedha hizi zinaweza kuonekana ni nyingi kwa Wizara, lakini ukizingatia umuhimu wa maji katika mji huu ni lazima zitafutwe zote ili wananchi wa eneo hili waondokane na kunywa maji machafu ya madimbwi tangu miaka ya 1970. Ahadi ya Katibu Mkuu Wizara ya Maji ni kutenga fedha zote katika bajeti hii ya mwaka 2012/2013. Naomba sana ahadi hii itimizwe, pia izingatiwe kuwa hii ni ahadi ya Rais tangu mwaka 2005. Naomba ahadi hii itekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Karagwe lina maeneo mengi ambayo hayana maji, lakini kwa kuanzia, naomba Serikali itatue tatizo hili la Omurushaka. Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe ina mahitaji mengi ya maji, naomba Serikali ilete mpango kabambe wa kutoa maji katika Ziwa Kajunju au Mto Kagera au Ziwa Ngoma au Ziwa Brigi na kadhalika. Tumejaliwa vyanzo vingi vya maji, lakini hatuna maji,

Serikali ikiweza kuleta mradi huu, tatizo la maji Karagwe litakwisha.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji katika Wizara hii, binafsi siungi hoja mkono kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini kuna tatizo la maji katika Vijiji, Wilaya, Mkao, Miji na hata Majiji? Tuna mito ya kila aina; mikubwa, midogo, mirefu, mifupi, minene na myembamba, karibu kila Mkao au kanda. Kuna mto mkubwa, tatizo liko wapi? Tuna mabonde ya mito mikubwa hapa nchini. Je, mabonde haya yanasaidaje kutatua tatizo la maji hapa nchini? Kuna Maziwa makubwa katika nchi yetu, hali kadhalika karibu kila kanda kuna ziwa. Najiuliza tena, tunashindwa kutumia maji haya ya Maziwa ili kuwatatalia wananchi wetu tatizo hili la maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bahari kubwa ya Hindi ambayo imezunguka ukanda mkubwa wa Pwani. Je, Serikali inatumiaje hii bahari ili kutatua tatizo la maji hapa nchini? Kwa nini hatuna sera na mipango mkakati maalum wa kuondoa tatizo la maji katika vijiji vyetu hapa nchini? Kitu kinachonishangaza ni kwamba, tunakazania sana kutatua tatizo la maji katika Miji na Majiji na kusahau wananchi wa vijijini! Naishauri Serikali kuitia Wizara hii ya Maji itenye fedha za kutosha ili kuhakikisha kuwa tatizo la maji linatatuliwa vijijini. Hii ni kwa sababu kuna Wizara kama vile Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Elimu, kuna mkakati maalum ambao ulifanyika kwa kutenga fedha za kutosha katika

Wizara hizi na hadi sasa kuna mafanikio kidogo. Hivyo, naishauri Serikali itambue wazi kuwa ukosefu maji ni janga la Taifa katika karne hii ya 21. Tufikirie zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wananchi wa Tarime wanateseka kwa ukosefu wa maji? Naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kuwa kwa muda mrefu sasa wananchi wangu wa Tarime wanateseka sana kutokana na ukosefu wa maji safi na salama kwa afya zao. Kuna ahadi nyingi zimetolewa na viongozi wa kitaifa tangu enzi za Mwalimu Nyerere, Rais Mwinyi, Rais Mkapa na sasa Mheshimiwa Rais Kikwete, lakini hakuna chochote kilichofanyika! Tatizo ni kubwa sana, wananchi wa Tarime wamechoshwa na ahadi feki zisizotekelzeza. Tatizo liko wapi? Naomba Waziri aje na majibu yakinifu kuhusu ahadi za viongozi wa kitaifa kuhusu kero ya maji katika Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike wazi kuwa Wilaya ya Tarime imebahatika kuwa na Mto Mara ambao ni mto mkubwa Mkoani Mara ambao unaunganisha Wilaya za Tarime. Mto huu unapita katika Kata za Nyarukoba, Nyamongo, Kibasuka, Manga, Komaswa, Nyanungu na Gorong'a. Naishauri Serikali itumie maji ya mto huu ili kusambaza maji vijiji. Ni imani yangu kuwa Wizara ikijenga tenki kubwa la maji katika Mji mdogo wa Nyamwaga, maji hayo yanaweza kutumika karibu robo tatu ya vijiji vyote vya Tarime. Sasa kazi kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Ziwa Victoria ambalo ni kubwa sana katika Bara la Afrika. Ziwa hili liko takribani umbali wa kilometra 15 tu toka Wilaya ya

Tarime. Je, Ziwa hili linawanufaishaje wananchi wa Tarime? Inasikitisha na kushangaza na vilevile haiingii akilini kuwa Serikali inaweza kuanzisha mradi wa maji toka Ziwa Victoria hadi Kahama, Shinyanga na Igunga umbali wa takribani kilometra 500 au 700 na kuwaacha wananchi wa Mara katika Wilaya zote za Tarime, Serengeti, Bunda, Musoma, Butiama na Rarya wanaendelea kutaabika kwa ukosefu wa maji. Wananchi wa Tarime wamenituma nitamke kwamba, wamechoka, sasa wanataka maji. Je, ni lini Serikali itaanzisha mradi mkubwa wa maji toka Ziwa Victoria kuelekea Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mengine yanayotatanisha, tutaendelea kutegemea wafadhili kwenye sekta hii ya maji hadi lini? Je, raslimali zetu tulizonazo haziwezi kutumika kuimarisha miundombinu ya maji hapa nchini? Je, mradi wa visima vya *World Bank* umefikia wapi? Je, visima vinavyochimbwa vijiji vinatoa maji au ni mapambo tu? Msaada wa visima 700 vya *Sabodo* umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime imefanya upembuzi yakinifu katika viji 50 na kubaini kuwa kuna maji ya kutosha ikiwa tutachimba visima katika maeneo hayo. Je, Serikali inatoa msaada upi ili kuhakikisha kuwa visima hivyo vinachimbwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mazingira ya Tarime ni magumu sana hasa suala la kijigrafia, hasa kwa upande wa udongo, ni mwekundu sana. Naiomba Serikali iharakishe suala la miundombinu ya maji safi na salama kwa wananchi wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RAMADHANI HAJI SALEH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa afya na uzima. Pia napenda kukupongeza wewe kwa ujumla kwa mafanikio ya kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania bado ina matatizo ya upatikanaji wa maji, miundombinu ya maji katika Miji, Vijiji hadi Mitaa, bado haikidhi haja ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matatizo makubwa hasa katika vijiji vingi kukosa maji hali ambayo inapelekea hata uzalishaji kupungua na watu kukosa mazao pamoja na maji ya kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imejiandaaje kuweza kupata maji ya kutosheleza katika sehemu hizo. Kama msemo wa watu wa kale unavyosema "maji ni uhai" wa kila kiumbe; je, Mheshimiwa Waziri ni lini utamaliza matatizo hayo ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kupiga hatua katika nchi yetu, bila ya maji safi, siyo rahisi kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wahisani waliochangia mradi wa maji ya kunywa wa Tarafa ya Pawaga hawakutajwa na wahisani wanaoendeleza mradi wa maji hivi sasa Ismani, hajajatajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hii miwili ina thamani ya Shilingi zaidi ya bilioni tano. Bwawa la Iguluba limekamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua mpango wa Wizara wa kujenga mabwawa zaidi katika maeneo ya Ismani yenye ukame mkubwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa wapo wataalam toka Italia wameangalia uwezekano wa kupata maji ardhini, Ismani. Naomba wataalam wake watembelee haraka kabla hawajaondoka tarehe 15 Julai, na kuwashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kusaidia mradi wa Pawaga na kuwajengea ofisi ya mradi na usafiri wa pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara isaidie visima 15 katika eneo la Ismani kama hatua za dharura wakati tunasubiri mradi mkubwa kukamilika mwaka 2015. Nimeweza kupata wahisani kwa kushirikiana na

Halmashauri, tumechimba visima tisa, tupo tayari kuchangia gharama za *pump* kama ni lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa utata uliojitokeza katika maeneo ya vijiji vya Migoli na Makatapora kwa tishio la kubomoa nyumba zao kwa kisingizio kwamba wamejenga kwenye eneo la Bwawa la Mtera. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ikague na kurekebisha mradi wa maji katika Tarafa ya Idodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isaidie kukamilisha mradi wa maji wa Pawaga kwa Kata ya Mlenge ambao wahisani hawajaweza kufikisha. Aidha, Wizara isaidie Halmashauri ya Iringa kufikisha maji toka Pawaga kwenda Kata za Izizi na Migoli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja ya Waziri wa Maji katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Benki ya Dunia vijiji 10 katika Jimbo la Mvomero katika hotuba ya Waziri ameainisha kuwa vijiji sita visima vimeshachimbwa na maji yanapatikana vijiji vya Doma, Salawe na Hoza ni vijiji vitatu tu. Vijiji vya Mlumbilo, Kwadoli, Bumu, Mlali na Kipera, Kigagu havijachimbwa. Naomba Waziri aanishe vijiji sita vilivyochimbwa ni vipi? Vijiji vingine vitachimbiwa visima

lini? Pamoja na vijiji vya Salawe na Hoza na Doma kuchimbwa visima virefu, naomba Wizara sasa ikamilishe kwa kasi utandazaji wa miundombinu ya maji uwafikie wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maji Turiani na Mvomero, kazi ya utekelezaji inasusua na katika kikao cha *KCC* Mkoa wa Morogoro nilihoji kusuasua kwa miradi hii na kujulishwa kuwa tatizo ni fedha, Wakandarasi wamesimamisha ujenzi. Naomba Serikali initibitishie mwaka huu wa fedha 2012/2013 kuwa imetenga fedha na Miradi hii ya Mvomero na Turiani itakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo bado tatizo la maji ni kubwa sana katika maeneo kama Gonja, Masimba (Kata ya Pemba); Pandambili, Kibogoji na Mburama (Kata ya Kibati); Vijiji vya Dihinda, Mfinga, Kenga (Kata ya Kanga), Kijiji cha Lukanga, Kunke, na Kidundwe (Kata ya Mtibwa); Kijiji cha Misengele, Msongozi, Sewe na Maharaka (Kata ya Doma); vijiji vya Lubongo, Vianzi (Kata ya Mzumbe); vijiji vya Yowe, Homboza, Mongwe na Mauza (Kata ya Mlali). Vijiji vya Kibaoni, Lukuyu (Kata ya Mgeta) vijiji vya Bumu, Lagali (Kata ya Lagali) bado tatizo la maji safi na salama ni kubwa katika Tarafa nzima ya Mgeta yenye Kata za Buduki, Luale, Mgeta, Langeli, Nyandire, Tchenzema, Kikeo na Luale. Naomba Serikali iangalie uwezekanao wa kusaidia Tarafa hii kwa kutenga maji ya mserereko ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Makao Makuu ya Wilaya Dakawa Sokoine panahitajika huduma ya maji

kwa ajili ya Mji huo utakaokuwa na mahitaji makubwa ya maji kwa watumishi wa Halmashauri, wakazi wa Kijiji cha Sokoine, Kijiji cha Wami, Lulindo na *Sokoine Memorial High School*. Maeneo yote haya yanahitaji mradi mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ione uharaka wa kupeleka huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. SLYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipe Serikali pongezi kwa kazi nzuri inayofanya. Maji ni huduma muhimu na ya kipekee kabisa kwa binadamu na maendeleo yake. Mji wa Kibaha unaokuwa kwa kasi unakabiliwa na tatizo kubwa la maji. Licha ya maji yatokayo Mto Ruvu kwenda Dar es Salaam kupitia Mji wa Kibaha, wananchi hawa wamebaki tu kutazama na kushuhudia wakati zaidi ya wakazi asilimia 60 hawana huduma ya maji safi ya bomba na wanakunyuwa maji machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ule mradi wa vijiji na Mitaa 10 wa visima, bado sisi hatujafaidika, kwa sababu ardhi na miamba ya Kibaha haina hifadhi ya maji na yakipatikana ni ya chumvi, hayafai kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumaini kubwa ambalo wananchi wa Kibaha wanalo ni mradi wa bomba litokalo Mto Ruvu hadi Kimara. Hii ni ahadi ya Serikali kupitia Waziri wa Maji, na ahadi hii imetamkwa wazi hata kwenye rekodi za Bunge kuwa mradi huu utaanza

mwaka 2012. Mradi huu umeahidi kutoa maji ya kutosheleza kuhudumia Kibaha hadi Kimara na kuwa hata bwawa la Kidunda ni kuimarisha mradi huu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa bado tuko gizani. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kwa Wananchi wa Kibaha, ni lini mradi huu utaanza kutoa huduma kwenye Mji wa Kibaha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa mabomba maarufu kama mabomba ya Wachina umebakia kuwa kiini macho, kwani mabomba haya hayana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mji wa Kibaha ukue kwa kasi uweze kufaidika na mpango huu, ni muda muafaka sasa Mji huu ambao ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani ipewe fursa ya kuanzisha Mamlaka ya Maji ya Kibaha au Pwani. Hii itasaidia sana kuhimiza miradi hii, lakini pia kuisimamia kwa tija zaidi, maana ni wazo. *DAWASCO* wamezidiwa na huduma kwa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu chanzo cha maji tunacho na Mto Ruvu unapita Kibaha Mjini. Naomba kupata maelezo kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini ataleta Muswada wa Sheria Bungeni ili ibadilishwe na kuruhusu Kibaha ianzishe mamlaka yake ya maji? Naomba jambo hili lipewe kipaumbele kabisa ili kuondoa kero kubwa ya maji Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Benki ya Dunia huchelewa sana katika utekelezaji. Maeneo mengi

wananchi wamechangia ile asilimia kumi na kwa miaka takribani miwili hawajaona au kujua ni lini fedha za Serikali zitapatikana na miradi ianze utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naishauri Serikali iweke bayana ramani (*Master Plan*) ya miundombinu ya maji ili wananchi watambue maeneo ya hifadhi maji, chemchemi na njia za kupita mabomba makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, endapo Wizara itaifanyia kazi kero hii ya maji Kibaha.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Jumanne Maghembe - Waziri wa Maji, kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa.

Pili, nampongeza kwa imani na uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika utendaji wake wa kila siku. Pia nampongeza Naibu Waziri Dkt. Mahenge kwa uwezo mkubwa alioonyesha kwa kipindi kifupi tangu uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uwasilishaji wa hotuba, tumeona kuwa wananchi wanasisitizwa kutunza vyanzo vya maji, rasilimali za maji na matumizi bora ya rasilimali za maji, lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Wizara ya Mazingira, kuweka mkakati wa wananchi wakashirikishwa kulinda na kuelimishwa umuhimu wa uhifadhi. Ifike wakati sasa miti na rasilimali zote ziingizwe kuwa ni mali ya Taifa na ziwe

zinakabidhi kwa uongozi wa vijiji kama (*assets*) ambazo zinafanyiwa *inventory* kila mwaka au kila baada ya muda fulani ambao utapangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi inayohusu *Word Bank* hakika ni kero kwa maana kila eneo lina tatizo la aina yake. Ila katika Wilaya ya Kilwa, tatizo kubwa lipo katika kuchangia kwa asilimia kumi. Naiomba Serikali kwa maeneo ambayo yana hali duni kimaisha, basi yenye we ibebe jukumu la kuchangia kwa niaba ya wananchi, licha ya kuchangia pia Serikali iweke jitihada katika usimamizi wa miradi, maana yapo maeneo mengi ambayo miradi imefanyika, lakini hakuna mafaniko kwa maana maji hayakupatikana na Wakandarasi wameshalipwa stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa mgawanyo wa fedha za maji uangaliwe upya, maana maeneo ya Mijini yanapangiwa pesa nyingi bila sababu za msingi na mara zote wao ndiyo wamekuwa chanzo cha matatizo kwa maana walishindwa kulipia *bills* za maji katika mamlaka husika hadi kupelekea mamlaka hizo kufilisika. Pia ukataji wa miti au uharibifu wa mazingira unachangiwa sana na mahitaji ya mijini.

Napendekeza katika mgawanyo wa miradi, licha ya kubuniwa na Halmashauri au Wizara, tuweke mfumo ambao viongozi kama Waheshimiwa Wabunge na Madiwani, washiriki katika usimamizi wa miradi au mingine ipitie katika mifuko ya Jimbo. Hali ya wananchi kutokubaliana na vigezo vinavyotumika sasa kwa maana ya idadi ya watu, wananchi wa vijijini kama Kilwa wana mazingira hatarishi zaidi kuliko mijini. Lakini

pia izingatiwe kuwa ukubwa wa eneo la Kilwa kama Wilaya, ni sawa na Mkoa mzima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitabu cha hotuba (kundi la nne) katika utekelezaji miradi ya maji, Mheshimiwa Waziri ameianisha kuwa Wilaya ya Kilwa ina miradi kadhaa ambayo inasubiri usanifu. Ifike wakati tuone umuhimu wa kuteleza miradi hii kwa haraka ili kuwaondolea wananchi adha kubwa katika maisha yao. Ni kwa kiasi gani tumesahau kauli mbiu ya Maji ni Uhai?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia ibara ya 32 katika kitabu cha hotuba, imezungumziwa wakala wa uchimbaji visima na mabwawa. Sielewi wakala huu unafanya kazi gani huku tukipoteza pesa nyingi mno kwa kuwapa Wakandarasi binafsi kazi ambazo pia huzifanya kwa kiwango cha chini, lakini kwa gharama kubwa mno? Hatua madhubuti zichukuliwe ili kuimarisha ujenzi wa mabwawa ili kuhifadhi maji ambayo mengi yanapotea bila kutumika huku ikifika wakati wa kiangazi kunakuwa na upungufu mkubwa sana wa maji katika maeneo yote nchini, hasa Vijiji. Kama inayoeleweka, Tanzania haina tatizo la maji kwa maana vyanzo ni vingi mno. Tatizo ni *management* ya maji haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo sasa katika maeneo mengi, hasa Mijini ambapo wananchi kwa nguvu zao wameamua kuchimba visima, lakini matokeo yake wanalazimishwa kulipia kila mwezi, hali ya kuwa wametumia vyanzo vyao vya fedha kuanzisha visima hivyo na wanatumia kwa matumizi yao binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia sasa kubuni mbinu mpya za mapato ili kuweza kuimarisha huduma za maji vijiji hasa kwa kutumia mamlaka za maji mijini kama (*DAWASCO*, *DUWASA*, *MUWASA* na kadhalika) ziwe zinatoa gawio kwa mfuko maalum utakaoanzishwa ili kumaliza tatizo la maji Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki na utekelezaji hasa ukizingatia umahiri wa Mawaziri na Watendaji wa Wizara hii. Nakutakia kila la kheri, namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma Mjini, tumezungukwa na Ziwa Tanganyika pande zote, na maji ya ziwa yanafaa kwa kunywa. Cha kushangaza na kusikitisha, Mji wa Kigoma una tatizo kubwa la maji. Tumeahidiwa kutatuliwa tatizo la maji kwa muda mrefu mpaka tumekata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na tatizo kubwa la maji, mamlaka imepandisha sana ankara za maji kwa kiasi kikubwa bila kujali maji yanatoka au la? Hii haikubaliki kabisa, na wananchi kwa hali hii wameamua kwenda Mahakamani kudai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tatizo la maji litatatuliwa lini? Bei za maji kwanini mtu asilipe kama anavyotumia? *And this is the prudence principal, tutumie then tulipe.* Kama maji hayatoki, while tunalipishwa, hii haikubaliki.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya vijiji vya Jimbo la Mchinga yana upungufu mkubwa wa maji. Naomba Mheshimiwa Waziri, baada ya Bunge hili kufanya ziara ya makusudi katika vijiji vya Namkogo, Lihimilo, Maloo, Kilolambwani, Mnang'ole, niongee yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufa kwa pampu/mota ya kusukuma maji katika Kijiji cha Mipingo, kumesababisha wananchi wa Jimbo la Mchinga hasa kijiji cha Mipingo kukosa huduma ya maji. Tatizo ni kuwa *Engineer* kutoka Wizarani ameombwa kwenda kutengeneza *pump* hiyo toka mwaka 2010 hadi leo hajapata muda. Baada ya Bunge hili, naomnba Wizara kumwelekeza Mhandisi huyo kwenda Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo ya kijiji cha Mchinga I na II tumechimba maji, lakini ni ya chumvi na wataalam wameshauri kujengwa kwa matenki ya kuvunia maji ya mvua. Je, Serikali katika bajeti hii itakuwa tayari kuingiza mpango huo katika utekelezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Shule ya Sekondari Mipingo, Rutamba na Milola zijengwe matenki ya maji kwa matumizi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha kwa hatua zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ABUU HAMOUD JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema kwa kuniwezesha kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2012/2013. Umuhimu wa maji katika maisha ya kila siku, kwa binadamu na viumbe wote duniani, pamoja na mimea unafahamika. Hivyo, msemo wa maji ni uhai, ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa bajeti yake ambayo imeandaliwa kwa umakini ikizingatia mahitaji ya maji Mijini na Vijijini, utunzaji na udhibiti wa vyanzo vya maji utakaokwenda sambamba na utunzaji wa mazingira. Bajeti hii imekidhi kabisa na kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasilitiza kuhakikisha wananchi wetu siyo tu wanapata maji safi na salama, bali vyanzo vya maji vinatunzwa na kuhifadhiwa na kutoa rai katika uwajibikaji wa wananchi kutunza mazingira ili nchi yetu iendelee kuwa na neema katika killimo, mimea, viumbe na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyoko mbele ya Wizara hii, bado ni nzito. Kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi waishio Mijini na Vijijini yanayohusu upatikanaji wa maji safi na salama, pia maji kwa ajili ya umwagiliaji katika maeneo ya ukame yenye matatizo ya maji. Malalamiko pia yako katika udhibiti na uhifadhi wa mfumo wa majitaka kuhakikisha

maji haya hayawi kero kwa kutoa harufu mbaya na kuhatarisha afya za watu, bali yanaweza kuhifadhiwa vizuri na pia kwa kutumia teknologia kidogo yanaweza kutiwa dawa na kurudiwa (*recycled*) katika matumizi ya kawaida.

Nitakuwa mtomvu wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zake za kutembelea vyanzo vya maji na hasa katika Jimbo langu la Kibaha Vijijini na kutambua mchango wa wananchi wangu katika kutunza maji ya Mto Ruvu kuhakikisha kwamba yanaendelea kuwepo kwa manufaa ya wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Wizara hii mwaka 2011, nilitoa kilio cha wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini, lakini wananchi wale wanaotunza mazingira ya Mto ule, wana matatizo ya maji. Maji ya Mto Ruvu yanapita Mlandizi kwenda kutumiwa na watu wanaoishi Kibaha Mjini na maeneo ya jirani na kwa wingi yanatumiwa na wananchi wanaoishi Dar es Salaam. Wananchi wa Kibaha Vijijini nao wanaomba wapatiwe maji haya kwani wao ni wadau wa kwanza kama haki ikizingatiwa, kipaumbele kikiwa kwa wananchi wa Kata za Mlandizi, Vijiji vya Vikuruti, Mande na Ruvu kwa Dosa, Kata za Magindu, Ruvu, Kwala, soga, Kikongo, Dutumi, Boko, Janga na kilangalanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kutoa kilio na kuomba Serikali iwave motisha wananchi wanaojitolea kulinda vyanzo vya maji, hasa wananchi wa Kibaha Vijijini ukizingatia kwamba maji ya Mto Ruvu yanatumika kwa matumizi mbalimbali Mkoani Dar es

Salaam kwa maana ya viwandani, maofisini na majumbani. Wateja hawa wote wanalipa fedha nyingi sana kwa matumizi ya maji, wakati wanaotunza vyanzo vya maji yale hawana maji na pia hawapati faida yoyote ama binafsi au inayorudi kwao moja kwa moja kuimarisha huduma za jamii katika maeneo yao, kwamba wahusika wa kutoza huduma ya maji kwa wateja wahakikishe wateja hawa wanapata huduma kabla ya kuwapelekea ankara za kulipia huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji. Wizara ya Maji waelimishe wananchi kuhusu uvunaji wa maji ya mvua ambayo yatahifadhiwa vizuri na kutumika ama kwa shughuli za majumbani au kwa umwagiliaji wa bustani na matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba pamoja na mipango mizuri ilioainishwa kwenye bajeti hii, wananchi wangu wa Jimbo la Kibaha Vijiji watapata maji safi na salama safari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Naomba pia nichukue fursa hii kutoa kilio cha muda mrefu kilichoambatana na ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Mji wa Sikunge na maeneo yanayozunguka. Kutokana na tatizo la maji kuwa kubwa kwenye Mji wa Sikunge, Serikali imechimba bwawa la Ulyanyama lenye maji ya kutosha, kazi ya

usanifu imekwisha kamilika, lakini mpango wa kuleta maji mji wa Sikonge haujatengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kukamilisha mradi huu muhimu kwa wakazi wa Mji wa Sikonge ili waondokane na tatizo kubwa la uhaba wa maji kwa wananchi wa Mji wa Sikonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga mabwawa makubwa yatakayokuwa vyanzo vya maji kwenye Kata za Kipiri, Kiloli na Kitunda ambazo ziko Tarafa ya Kiwere, ambako kuna tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Serikali katika jitihada za kupunguza matatizo ya maji kwa wananchi wa Tanzania, naomba hayo niliyoyaomba yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono hoja.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mchango katika hotuba ya Wizara ya Maji. Sambamba na shukrani hizo, nampongeza Mheshimiwa Prof. Maghembe kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake. Nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Mahenge - Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara. Kimsingi, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hoja hii ya Wizara ya Maji, itakuwa katika hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kila sababu ya kuangalia kwa upya mpango wa kupeleka au kusambaza maji vijijini. Serikali kutegemea tu Benki ya Dunia kutusaidia kwa ajili ya *program* ya kusambaza maji vijijini, itakuwa ni ndoto licha ya kwamba Serikali ina nia nzuri. Lakini juhudini au nia nzuri ya Serikali, inazimishwa na utegemezi wa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu maji ni bidhaa muhimu kwa matumizi ya mwanadamu, ni muhimu Serikali ikaangalia upya njia nyingine au vyanzo vingine vya ndani au vinginevyo, kwa ajili ya kuwapatia maji wananchi waishio vijijini. Miradi hiyo inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, inachukua muda mrefu mno kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuweka Wakala wa kusambaza maji vijijini ni muafaka kama ilivyo kwa Wakala wa kusambaza umeme vijijini (*REA*). Bila Wakala, nia ya Serikali ya kuwapatia wananchi maji katika vijiji itakuwa ni ngumu sana. Kuna vijiji ambavyo vilitakiwa kupatiwa maji miaka minne iliyopita, lakini hadi sasa hakuna mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai. Kuna vijiji ambavyo vimechangishwa fedha kwa ajili ya kuchangia mradi, lakini fedha hizo haziwezi kufanya chochote kwa sababu miradi haitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Wizara ya Maji -Mheshimiwa Prof. Maghembe na Naibu Waziri wa Maji - Mheshimiwa Dkt. Mahenge kwa kushika wadhifa mpya katika Wizara hii. Pia nampongeza Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu. Aidha, kwa namna ya pekee, namshukuru Naibu Katibu Mkuu wa Wizara Eng. Mrindoko kwa jinsi ambavyo tulishirikiana katika kushughulikia mgogoro wa bwawa la Kewa Mkoani Rukwa. Mradi huu ni mkubwa na una manufaa makubwa kwa wananchi wa Rukwa hususan kijiji cha Ntendo, Nkundi, Fyengerezye na kadiri hali ya upatikanaji wa maji itakavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuomba Wizara pamoja na hali ya sintofahamu inayojitokeza kwa baadhi ya wadau, na kwa kweli pengine ni kutokana na migongano yao binafsi zaidi, ni vyema Serikali iumalize mradi huu ambao umeshatumia pesa za Serikali ili wananchi wapate maji kama ambavyo tulikubaliana kufuatia kikao cha pamoja cha wadau kilichofanyika Mkoani Rukwa baina ya Wawakilishi wa Wizara na Ofisi ya Mkoa wa Rukwa. Hata hivyo, nawaamini sana na naamini tatizo hilo litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita, nilichangia juu ya mradi wa maji wa Mango ambao ulifadhiliwa na *DANIDA*. Mradi huu ni muhimu sana,

kwani unahusisha vijiji vitano vya Kata ya Kihegari, yaani Mango, Tumbo, Ngehe, Songambele na Kihegere yenye we pia unahusisha Kata ya Liuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu kwa muda mrefu umejiendesha wenyewe ukiwa chini ya Wizara ya Maji, mpaka hivi karibuni ulipohamishiwa Wilaya ya Mbanga na sasa itakuwa Wilaya ya Nyasa. Nilitathmini na kuona kuwa mradi huu ungeweza kujijendesha kabisa kama kungekuwa na udhibiti wa mapato pamoja na *proper maintenance*. Lakini watu hawalipi, *leakage* ya mabomba ni kubwa na maeneo mengine bado hayapatiwi maji. Tenki liliopo ni karibia lita za ujazo 300,000. Nilifuatilia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wao wanao uwezo wa kutengeneza *billing system* (ndogo) inayoweza kusaidia. Nilikabidhi *quotation* hiyo kwa Naibu Waziri aliye pita Mheshimiwa Eng. Lwenge. Gharama kwa wakati ule ilikuwa kama Shilingi milioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusitiza kutumia Vyuo vyetu vya Tanzania kuweza kutoa *solution* kwa baadhi ya matatizo yetu yasiyo ya lazima. Miradi mingi nchini (ya maji) inakufa kwa sababu *means* za *sustainability* hazipewi nguvu inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kukawa na *machine* katika Mikoa ambayo itasaidia angalau kuchimba visima katika maeneo kwa bei nafuu.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa uongozi wa Wizara, Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na

wafanyakazi wote, naomba Serikali iwasaidie maji wananchi wa Mbinga hasa katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Mbinga, vyanzo vya maji vina maji mengi sana, tatizo ni kuyaleta MJini. Maji yamefikishwa mpaka sehemu fulani na yameachwa kumwagika hapo kwa miaka minne sasa. Nimekwishaiandikia Wizara, jambo hili kupitia Naibu Waziri wa Maji (wakati ule Mheshimiwa Lwenge, na kufanya pia mazungumzo na Katibu Mkuu, lakini Serikali kupitia aliyekuwa Naibu Waziri - Mheshimiwa Chiza,) aliahidi, kuhakikisha maji hayo yanafikia Mji wa Mbinga, kuhakikisha maji yanapatikana Kigonsera, Mkako, Luhagara na Litumbandyosi. *Hansard* zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hali ipo palepale na wananchi wanaendelea kupata shida. Mbaya zaidi, hakuna mawasiliano juu ya nini kinachoendelea. Naomba majibu na maelezo ni lini sasa yale maji yanayomwagika eneo la tisini (Mbinga) yataletwa mjini Mbinga ili rasilimali hiyo ya maji isiendelee kupotea na wananchi wapate maji katika Mji wa Mbinga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mpango gani licha ya ahadi ya Serikali ya kuwapatla maji wananchi wa Luhagara, Litumbandyosi na Kingoli (katii ya Litumbandyosi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawasaidiaje pia wananchi wa vijiji katika Kata ya Ukata hasa kijiji cha Litoko ambacho kulikuwa na mradi wa Benki ya Dunia, lakini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi kupata majibu ya maandishi. Naunga mkono hoja nikiamini kwamba hoja nilizoeleza hapa zitapatiwa si tu majibu, bali wananchi watapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kazi njema.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimwa Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti ya maji inaongezeka kila siku, lakini tatizo la maji lipo pale pale. Bajeti ya maendeleo ya maji vijiji ni imeongezeka na pia ya bajeti ya *program* ya maendeleo Sekta ya Maji (*WSDP*). Pamoja na jitihada zote hizi, lakini bado upatikanaji wa maji Tanzania umezidi kuwa hafifu. Imefika hatua sasa inabidi tujulize tumekosea nini na wapi? Je, bado tuendelee kuwekeza kwenye sekta isiyokuwa na matokeo mazuri? Imefika wakati sasa hivi tufahamu kiini cha matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu, naona kutodumu miradi ya maji kila siku ni kujielekeza katika miradi mipyä ya maji. Juhudi zetu hizi zinakwenda sambamba na kufa kwa miundombinu ya maji. Inaonekana kila mwaka asilimia 17 ya miradi ya maji inakufa. Je, kwa nini miradi hii haidumu? Kwa ushauri wangu, ni vyema kujenga miradi mipyä inayoendana na kufufua miradi iliyokufa, na kuwe na mfumo wa kufanya miradi iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kuzingatia aina ya teknolojia tunayotumia na vipuli vyake. Jamii inalalamika vifaa mbalimbali vyä miradi vinakufa kutokana na kuwa feki na hii inaongeza

gharama za uendeshaji wa maji na kuwafanya wananchi kushindwa kumudu. Kwa hiyo, Serikali inapaswa ichukue hatua ili kudhibiti uingizaji wa vifaa feki. Zipo sababu nyingine zinazosababishwa na miradi kufa. Ni uelewa wa wananchi katika kuendesha miradi ya maji na Halmashauri kukosa pesa za ufatiliaji. Cha msingi, wadau wote tubebe changamoto hizi na kuzifanyia kazi. Tukumbuke wananchi wanataka maji, hawataki sera, magari, au hadithi nyingine zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ni muhimu katika kulinda afya. Lakini hadi leo hasa vijijini, wananchi wengi hutumia maji yasiyo salama. Hili ni tatizo kubwa kwa nchi yetu. Naiomba Serikali ilione hili na lipatiwe ufumbuzi wa haraka kwa kuwajengea visima.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Wazirim amezungumzia, mradi wa hifadhi ya mazingira ya Ziwa Victoria. Katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuwa mradi huu unalenga kuimarisha Taasisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki kukarabati mifumo ya kusafisha majitaka katika Miji mikubwa iliyoko kando kando ya Ziwa, yaani Mwanza, Musoma na Bukoba. Kati ya walengwa, Mheshimiwa Waziri ametaja Halmashauri ya Kwimba kama mlengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe ufanuzi, miradi hiyo iko kwenye vijiji gani Kwimba? Naomba majina ya vijiji hivyo vitajwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba ina takribani vijiji 150. Je, ni jinsi gani visima tisa vinaweza kukidhi mahitaji ya vijiji hivyo? Naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, wakati akitoa majumuisho ya hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Ngudu na vijiji vingine vya Welamasonga, Jiojiro, Ngudulugulu, Mwanh'aranga, Mwamashimba, Hungumalwa, Kiliwi, Mp'alo, Dodoma na kadhalika, pamoja na kuwa na visima, vijiji hivi vimeduwa havipati maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge lako Tukufu, ni lini Serikali itafanya ukarabati ili wananchi wa vijiji nilivyovitaja waanze kupata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. MCH. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi ya bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa yote mliyoweza kutekeleza. Ahsante kwa juhudini hiso, mwendelee mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba suala la maji Kilombero hasa Mji wa Ifakara mlipe kipaumbele. Miundombinu ya maji Ifakara ni ya mwaka 1976 wakati

mji ukiwa na watu 7,000 tu. Sasa hivi Mji wa Ifakara una wakazi zaidi ya 100,000, lakini miundombinu ni ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Vyuo Vikuu mbalimbali, mashule, hospitali, kote wanahitaji maji. Lakini watu wanahangaika, mito yetu inapeleka maji Bahari ya Hindi. Wenyewe hatuna maji, tunachangia kila bajeti, lakini hakuna hatua. Ukombozi ni mradi wa maji wa Kiburubutu ambao unagharimu Shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akumbuke Kilombero na mradi wa maji Kiburubutu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wenye chanzo cha maji katika Kijiji cha Lukululu Kata ya Mlangali Wilayani Mbozi ambao ulishaingizwa katika mipango ya Wizara ya Maji katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, bado hawajapewa msukumo wa kutosha. Mradi huo unaokisiwa kutumia Shilingi bilioni 1.5. Ukikamilika utavipatia maji vijiji zaidi ya 12 katika Kata za Mlangali, Nyavizi na Mlowa. Tayari Serikali ilishafanya vipaumbele yakinifu vya mradi huu ambapo zaidi ya Shilingi milioni 50 zilitumika kwa ajili ya kazi hiyo. Sasa nataka kujua, Wizara ina mpango gani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miji ya Mlowo na Uwawa inakua kwa kasi kubwa sana, mathalan Mji wa Mlowo una wakazi zaidi ya 30,000 na ule wa Uwawa una wakazi zaidi ya 40,000 lakini Miji yote hiyo miwili ina matatizo makubwa sana na maji. Kuna mradi wa maji Mlowo ambao bado haujakamilika. Naomba Serikali kupitia Wizara hii ikamilishe mradi huo ili wananchi hao wapate huduma ya maji safi na salama. Kuhusu Mji wa Uwawa ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi, bado unatumia maji ya kutega ambayo uhakika wake ni mdogo sana. Maji ni ya mgao wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara, ilishaahidi kuupatia mji huo maji. Sasa nataka kujua, ni lini Serikali itanza utekelezaji wa kuupatia Mji wa Uwawa maji?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha. Naunga mkono hoja.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kazi ya kusambaza maji Jimbo la Vunjo inaendelea vizuri. kata zilizo na maji ni Kata ya Kirua Vunjo Magharibi, Kata ya Kirua Vunjo Mashariki, Kata ya Kirua Vunjo Kusini, Kirua Vunjo Kusini, Kahe Mashariki na Kahe Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchaguzi wa mwaka 2010, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho aliwaahidi wananchi wa Mji mdogo wa Himo kwamba watapatiwa Sh. 150,000,000 kwa ajili ya kusambaza maji safi ya kunywa. Mpaka sasa Serikali imekwishatoa

Sh. 50,000,000. Mradi ule haujakamilika na umeleta usumbufu na manunguniko mengi. Naomba sasa kuuliza ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko jitihada zinazofanywa na Serikali katika kusambaza maji njia panda Himo, zinaungwa mkono na Serikali ya Ujerumani. Ningombua kujua mpango huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata za Mwika Kusini na Mwika Kaskazini katika Jimbo la Vunjo, kuna ukosefu mkubwa wa maji. Hii inatokana na ukweli kwamba maji ya Vunjo yanapelekwa katika Wilaya ya Rombo. Je, Wizara ya maji itatusaidiaje? Kwa sababu hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kilema Kaskazini, kuna mpango mzuri wa kusambaza maji kwa wananchi. Sasa hivi wananchi wanachimba mtaro kwa ajili ya kulaza mabomba ya maji. Je, mradi huu utakamilika lini?

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Mwenyezi Mungu akujalie hekima na busara na akupe afya njema.

Pia nachukua fursa hii kuwapongeza sana Mawaziri wote wawili; Waziri wa Maji - Mheshimiwa Prof.

Jumanne Maghembe, pamoja na Naibu wake - Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, naomba kupata maelezo stahiki kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ya Maji ina mpango gani wa kuwapelekea maji ya kutosha, safi na salama wananchi wa Ludewa Mjini, hasa ikizingatiwa kwamba Mji wa Ludewa una wakazi wapatao zaidi ya 10,000 na unakua kwa haraka kutokana na miradi ya Liganga na Mchuchuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Ludewa hauna maji kabisa. Naiomba Wizara ya Maji itoe tamko thabiti juu ya upatikanaji wa Maji katika Mji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ya Maji inawaambia nini wananchi wa vijiji vya Ilininda, Mbwila, Mdilili na Mapogoro kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Maji ya Benki ya Dunia?

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu, tatizo hili limeongezeka na kuwa kubwa sana kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Maeneo mengi yaliyokuwa na maji ya kutosha, maji ya mito, maji ya mabwawa, maji yaliyotokana na mvua nydingi kutokana na uwepo wa misitu, lakini pia idadi ya watu ilikuwa ndogo, maji wakati huo yaliweza kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wananchi wengi hawakuwa na maji ya bomba, lakini walipata maji kirahisi na tatizo halikuonekana kubwa. Lakini pia Miundombinu ya maji mingi ilikuwa mipyä na hajachakaa, wananchi walipata maji kirahisi. Leo miundombinu imechakaa na kukua kwa Miji au Vijiji na idadi ya watu, miundombinu hiyo haitoshelezi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo miaka 30 baadaye nchi imekauka, watu wanahangaika kwa ukosefu wa maji, katika maeneo mengi ya nchi yetu. Kutokana na ukweli huo, niliouelezea hapo juu, sisi kama Taifa tunahitaji kuifanya Sekta ya Maji kuwa sekta ya kipaumbele na kuitayarishia mkakati maalum wa kuiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuipatia fedha ya kutosha ili kuiendeleza, ni lazima tuihudumie sekta hii kama tunavyoihudumia Sekta ya Miundombinu. Tutafute fedha za kutosha, tutatue tatizo la maji nchini, vinginevyo maji yataleta mauaji miaka ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, ni muhimu tuhakikishe Wananchi wetu wanapata maji ili kuendelea kuishi. Tuendeleze Miundombinu ya maji kwa mtazamo mpyä.

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naungana na Wabunge wenzangu kukushukuru wewe na Mwenyezi Mungu

kwa kuweza kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu wa mawazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wale wote walioshiriki kwa hali na mali kuandaa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2011/2012. Baada ya kuunga mkono naomba nitoe ushauri wa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Maji, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ya kuhakikisha wananchi vijijini wanapata maji safi na salama ifikapo mwaka 2015, katika Miji 19 kwa kiwango cha asilimia 84 Mjini na kwa kiasi cha asilimia 36 Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kama ifuatavyo:-

- (1) Kasi ya usambazaji maji vijijini bado si ya kiwango kikubwa, naomba Serikali iongeze bidii katika kuongeza kasi ya kutenga fedha kwa ajili ya kusambaza maji Vijijini.
- (2) Miji mingine iliyobaki inayokarabati mifumo ya maji iboreshwe kwa kukarabati miundombinu na kuongeza kiwango cha usambazaji wa maji

- (3) Kupeleka maji katika moja ya maeneo ya Igunda, Nzega, Tabora kutoka Mkoa wa Shinyanga, Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye kila linalowezekana kuongeza fedha katika Wizara ya Maji ili mradi huo uweze kutekeleza Ibara 86 ya llani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa miundombinu ya maji inayosababisha upotevu wa maji. Serikali ijitahidi kuongeza na kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya maji ili kupunguza upotevu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Maji Mgango, Kiabakari na Butiama. Naomba Serikali ifanye kila linalowezekana kusambaza maji kutoka chanzo cha maji cha Mgango katika vijiji vinavyozunguka chanzo cha maji ili maji yafike katika Kata ya Kiabakari mpaka Butiama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la uchimbaji wa maji ya visima na kutoa maji, Serikali ichukue hatua. Kuhusu maji Vijijini, hapa Serikali haikueleza ni kiasi gani kimefikia katika usambazaji wa maji vijijini, hali si nzuri, jitihada ziendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa maji katika Vijiji kumi na visima, bado unasuasua. Ushauri wangu kwa Serikali ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ijitetahidi kutenga fedha za ndani kwa ajili hiyo; na

(ii) Bajeti ya maji vijiji naomba iongezwe ili kuongeza upatikanaji wa maji na kuwapunguzia adha wanayoipata wanawake kwa kutembea masafa marefu kilomita moja mpaka nane wakitafuta maji (maji ni uhai).

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya Mradi wa Maji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ijitahidi kupeleka fedha hizo kwa wakati ili kazi ya kukarabati miundombinu ya Ruvu Chini na Ruvu Juu na ujenzi wa visima vyta Mpera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba, badala ya Mradi huu wa Dar es Salaam kuhudumia Wananchi wa Dar es Salaam, Bagamoyo na Kibaha, tuongeze wigo ili Mradi huu pia uhudumie Wananchi wa Mkuranga na Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matanki ya kusambaza maji Dar es Salaam yatawekwa kwenye Mlima wa Ruvu ambao ni Kilometra moja kufika Kisarawe, vile vile vyanzo vyta maji vyta Mpiji na Mpera viko karibu na Wilaya ya Kisarawe na chanzo cha maji cha Mpera kipo Wilaya ya Mkuranga.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili husema maji ni uhai, ikimaanisha

kuwa viumbe vyote hutegemea maji ili viishi. Msingi huu unadhihirisha wazi kuwa, kuna umuhimu mkubwa wa kujali na kutunza bidhaa hii adimu. Naomba kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchafuzi wa maji kutokana na kemikali katika maeneo ya uchimbaji wa madini ni jambo ambalo halikubaliki. Inasikitisha sana kuona jinsi ambavyo tunaruhusu kitendo hiki cha kinyama kitokee. Swali la kujiuliza ni je, tunawaogopa hawa wawekezaji na je tumeshindwa kujali hata maisha yetu wenyewe? Serikali itoe majibu ya uhakika katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watu hasa mijini ni changamoto ambayo inatakiwa kuangaliwa kwa umakini sana ili miundombinu ya maji iendane na kasi ya ongezeko la watu. Imekuwa ni desturi iliyozoleka kwa Serikali kuja na hoja za, tuko katika mpango wa mchakato na mengine yafananayo na hilo. Ifike mahali Serikali itende yale inayosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haina shida ya maji kwa asilimia tisini, ila tatizo ni kutengeneza miundombinu ya kuvuna haya maji ambayo yako tele ardhini. Inashangaza sana kusikia nchi zilizo jangwani kama Libya, Misri na nyingine zikiwa hazina shida ya maji ilihali Tanzania iliyozungukwa na maji kila kona ikilia shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maji inategemea wahisani kwa kiasi kikubwa sana, kwa mujibu wa taarifa ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo,

Mifugo na Maji. Hii ni aibu na ni wazi Tanzania haitapata maji kwa ukamilifu. Serikali imeshindwa nini kutengeneza utaratibu wa ndani ili kupata pesa za ndani kugharamia miradi ya maji. Pesa nyingi sana zinapotea katika rushwa na matumizi mengine yasiyo na manufaa. Hivi karibuni tumepata kusikia billioni 300 ziko Uswis na nyingine nyingi. Hizi pesa zingekuwa hapa ndani, zingetumika kugharamia miradi ya maji na mengine.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri wa Maji kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Pamoja na kuunga mkono hoja, nishauri Wizara ya Maji kuchukua hatua za makusudi ya kuanza kufikiria kuipatia Wilaya ya Mbogwe maji kutoka Ziwa Victoria hasa ikizingatiwa kwamba maji toka Ziwa Victoria tayari yamefikishwa Mjini Kahama, Mji ambao ulikuwa na matatizo ya huduma ya maji. Historia inayoonesha kuwa Wilaya ya Kahama kabla ya kugawanywa na Wilaya ya Bukombe na sasa Mbogwe, matatizo katika Wilaya ya Mbogwe kama ilivyokuwa kwa Wilaya mama ya Kahama bado yapo na ndiyo maana tunaomba maji toka Ziwa Victoria ambayo tayari yako jirani hapo Mjini Kahama ili Wanambogwe tuweze kuwa na maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu miradi ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuwezesha Wilaya kupatiwa fedha kwa ajili ya miradi ya maji katika vijiji vya Masumbwe, Shenda, Bulugala, Lulembela. Nafurahi kusema kwamba Miradi hii inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iendelee kutenga fedha zaidi ili kuwezesha miradi ya uchimbaji wa visima vya maji katika maeneo mbalimbali katika Wilaya mpya ya Mbogwe. Aidha, itapendeza pia kuiomba Wizara ya Maji iandae utaratibu wa kuteua Wataalam wa maji kwa Wilaya na Mikoa Mipyä.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilichangia kwa kuzungumza na kwa maandishi pia, lakini naomba nitumie fursa hii kuongeza jambo ambalo pengine lilisahaulika kutokana na ufinyu wa muda. Kuna malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi wanoishi kwenye mamlaka ya Mji Mdogo wa Usa River kuhusu utaratibu wa ankara za maji. Wananchi wamepewa ankara za miaka ya nyuma hata kama hawakutumia maji, lakini pia hakuna meter za maji na wanatakiwa kulipa *flat rate regardless of their consumption differences*. Matokeo yake Mamlaka inawakatia maji na kukata mabomba ya maji ambayo wananchi waliingia gharama kuyafunga au kuunganisha. Tafadhali naomba Wizara itoe ufanuzi kuhusu sintofahamu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa nini Wizara haijafikiria kutupa maji kutoka Chemchem ya Teema-Magadirisho (Kata ya Usa River) ili maji haya yatosheleze kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo wa Usa River, ukizingatia chemchem hii ina maji ya kutosha,

safi na salama na ipo kilomita zisizozidi mbili kutoka yalipo Makao Makuu ya Mamlaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhalii naomba Wizara inipatie *clarification* ili kuondoa sintofahamu hii.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara pamoja na Waziri wake kwa kuwasilisha hotuba nzuri inayohusu sekta ya maji. Pia naomba kuchukua nafasi hii kuiomba Wilaya ya Kisarawe kwa jicho la kipekee kwani wakazi wa Kisarawe wanataabika sana kutokana na shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwezeshe upatikanaji wa maji kwa Mji wa Kisarawe kutoka vyanzo vya maji vya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwezeshe upatikanaji wa maji kwa Tarafa ya Mzenga kutoka chanzo cha Mto Ruvu kutokea eneo la Mlandizi ambapo kutoka Mlandizi hadi Tarafa ya Mzenga ni kilomita chache sana. Kama Wizara ya Maji itawezesha uwekaji wa bomba la maji kutoka Mlandizi kwenda Tarafa ya Mzenga itasaidia sana kupunguza adha kubwa kwa wakazi hao amba wao ni wadau wa Mto Ruvu na wanaendelea kuhifadhi vyanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Tarafa ya Chole ndani ya Wilaya ya Kisarawe ina shida kubwa sana ya maji, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kutoa maji kutoka Bwawa la Zumbi lililo kati ya Chole na Mloka au.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia maji kutoka Mto Rufiji ili kuondoa tatizo la maji kabisa ndani ya Wilaya ya Kisarawe na hata jiji la Dar es Salaam. Ijulikane kuwa maji ya kutoka Bwawa la Zumbi au Mto Rufiji hayajatumika kabisa kutatua tatizo hilo la maji Kisarawe na Mkoa wa Pwani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ihakikishe kuwa visima vilivyochimbwa vya *World Bank* vinawekewa miundombinu iliyokamilika ili kupunguza kero hiyo ya maji. Naomba visima vya Chakange, Kihare, Kibuta, Boga na Msanga vikawekewe pampu na kusambazwa kwa wananchi katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu juu ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uongozi wa Awamu ya Kwanza wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika Wilaya ya Meru, Arusha, kulikuwa na bomba kubwa la maji kutokea Ngarenanyuki kupitia Kingore hadi Sakila na Kikatiti yalijengwa matanki makubwa ya kuhifadhia maji katika maeneo hayo, matanki ambayo yapo hadi leo, lakini kwa hivi sasa hayana maji ingawa kwa wakati ule hayakuwa yanakosa maji. Wanawake na wasichana wa eneo hili, leo wanatembea umbali mkubwa na kupoteza masaa mengi kutafuta maji. Mfano, huko

Sakila punda mmoja bei imepanda toka Shilingi elfu ishirini hadi shilingi laki moja kwani hutumika kwenda umbali mkubwa kuyatafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Wizara au Mheshimiwa Waziri katika hitimisho lake awaambie wananchi wa Meru, maji yaliyokuwa yakipatikana kutokea Ngarenanyuki yalipatwa na nini au yalikwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu maji mengi yanayotumika mahotelini Arumeru Mashariki kwa mfano, Hoteli ya Ngurdoto na maji mengi yanatumika katika Mashamba ya maua Usa River kwa nini maji hayo kiasi yasichukuliwe kwa wenyeji wanaoishi karibu na maeneo hayo ambao kwa kiasi kikubwa wanateseka kwa adha ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Maghembe ni mgeni katika Wizara hii, nashauri atafute njia za kufuatilia maji yanayotoka Ruvu-Ubungo Dar es Salaam hayafiki yote. Maji mengi yanapotea njiani kutokana na miundombinu chakavu. Pia kuanzia Kibamba, bomba limetobolewa sehemu sehemu, njiani maji yanauzwa kwa malori ambayo inawezekana ni ya wakubwa ndiyo wenye uwezo wa kununua malori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je fedha hiso zinaingia Serikalini au mifukoni mwa watu binafsi? Udhhibit unahitajika kwa vishoka wa maji wanaotoba bomba kubwa la maji, wengi ni wafanyakazi wa DAWASCO, Maana ndiyo wenye vifaa vya kutobolea. Uuzwaji wa

maji kwa malori, ningependa kuhoji, je, Ofisi za DAWASCO Kimara zimeshindwa kudhibiti au na wao ni wahusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 56 wa kitabu cha Hotuba ya Mheshimwa Waziri wa Maji kuna maelezo ya kuchimba visima 20 virefu maeneo ya Kimbiji na Mpera kama chanzo cha maji Dar es Salaam ili kupunguza tatizo la maji ambalo limeathiri uchumi na maisha ya wakazi wa Dar es Salaam kwa ujumla. Fedha zilizotengwa kufuatana na *volume IV, Vote 49, subvote 3001, item 3439* kwa mwaka 2012/2013 ni Sh. 1,000,000,000 tu fedha za ndani, wakati fedha za nje ni Sh. 29,992,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya ndani ndiyo tuliyo na uhakika nayo kwa mradi ambao unategemewa usaidie kupunguza tatizo la maji Dar es Salaam ungepaswa utengewe fungu la kutosha, fedha za nje sio za kutegemea sana. Maendeleo yetu yataletwa na sisi wenyewe. Wafadhili wanaweza wakachelewesha fedha na hivyo kazi ya mradi ikachelewa. Ni vema fedha ya ndani ikatafutwa na kuongezwa ili mradi huo ukamilike endapo kweli Wizara inataka kwa dhati kutatua tatizo la maji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika fedha iliyotengwa kulingana na *Volume IV, Vote 49, Sub-Vote 3001, Item 3306 - Rehabilitation and Expansion of Urban Water Supply* kwa mwaka 2012/2013 ni fedha za ndani Sh. 135,817,994,800. Kweli ADB, kwa vyovoyote ikichelewesha au kushindwa kutoa fedha hizo ni

kwamba, mradi utakwama, kiasi cha fedha za ndani ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukweli kwamba kwa miaka 50 ya Uhuru Watanzania bado kwa asilimia kubwa tunategemea wafadhili kwa huduma muhimu kama maji. Je, tuite ni ukoloni mamboleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia vyanzo vingine vya maji, nashauri Wizara au Serikali kujenga mabwawa ya maji ili kuvuna maji ya mvua hasa katika maeneo yenye maji mengi na ya kati kama vile Mbugani, Arumeru Mashariki yako mabonde na mvua zikinyesha maji huwa ni mengi sana. Kwa msaada wa mabwawa maji yanaweza kutumika wakati wa kiangazi kwa mifugo au hata umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, Juu ya juhudini inayochukuliwa na Serikali vijijini hususan na upatikanaji wa maji vijijini lakini bado wanayatumia si safi wala salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kawaida inaweza ikaanzishwa miradi mipya kwa sherehe kwa mategemo ya wananchi kupata maji. Maji hupatikana siku chache baada ya uzinduzi wa mradi husika baada ya hapo huwa ndiyo basi. Je, Serikali inasemaje na hali hiyo? Je, hatuna wataalam au hununuliwa vifaa feki na fedha zikaliwa? Je, Serikali

itahakikisha vipi kuwa miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji mijini bado una matatizo na baya zaidi maeneo ya baadhi ya miji yanapoadimika maji unakuwa huna eneo la karibu unaloweza kuchota maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miji yetu kwa uchakavu wa miundombinu ya maji kuna upotevu mkubwa wa maji na kwa vile baadhi ya mamlaka za maji hazina uwezo wa kifedha au kusema haziwezi kujitegemea basi hali ya uvujaji wa maji huwa gari zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko sheria inayolinda vyanzo vya maji inayotaka kwenye umbali wa mita 60 kutoka vyanzo vya maji pasiwepo na shughuli yoyote ya binadamu kwa maana ya kuwepo majengo, shughuli za kilimo, ufugaji na kadhalika. Sheria hii ipo, lakini utekelezaji wake ni mdogo mno. Bila ya kutekeleza kwa ukamilifu sheria hiyo vyanzo vya maji husika vitatoweka na kuongezeka tatizo la upungufu wa maji. Ipo haja Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira walipe uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba za bajeti ya Wizara hii, kwa miaka iliyopita, ilikuwa inaahidi ifikapo mwaka 2013 Dar es Salaam itakuwa haina tatizo la maji tena. Inavyoonekana uwezekano wa ahadi hiyo kutekelezeka haipo. Kwani hivi sasa licha ya kuwa kuna upungufu wa maji yanayozalishwa Dar es Salaam pia miundombinu ya maji ni mibovu na maji

mengi yanapotea. Hivi sasa kwa maelezo ya Dar es Salaam kwa maji ni lita za ujazo 455,000 kwa siku lakini yanayopatikana ni lita za ujazo 300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda uliobakia kufikia mwaka 2013 licha ya kuongeza wingi wa maji, kuweka mtandao mpya tu wa miundombinu ya maji kwa Dar es Salaam haiwezekani hata kama uwezo wa kifedha ungeruhusu kufanya hivyo. Sasa naiomba Serikali itupe ahadi nyingine ni mwaka gani tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam litakuwa limekwisha.

MHE. DKT. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Suala la tatizo la maji katika Jimbo langu la Segerea kwenye maeneo yote ya Buguruni, Vingunguti, Kiwalani, Kipawa, Tabata, Kimanga, Kisukuru, Bonyokwa, Kinyerezi na Segerea ni kubwa sana. Pamoja na ahadi ya Serikali na mipango iliyoelezwa, inaonekana kwamba mpango wa kuboresha upatikanaji wa maji toka mtambo wa Ruvu Juu uko nyuma kulinganisha na ule wa Ruvu Chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonekana mradi wa Ruvu Chini utakamilika mapema na upande mmoja wa Jiji kupata maji ya uhakika mwaka 2014 wakati upande wetu unaotegemea Ruvu Juu utakuwa haujakamilishiwa Mradi wake. Hii italeta shida kwa wananchi wa maeneo ya Majimbo ya Ubungo, Segerea, Ukonga na kuona kama wametengwa. Nashauri miradi hii miwili (Ruvu Chini na Ruvu Juu)

iende sambamba na yote ikamilike 2014 kama ilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iko hatari kama mradi wa Ruvu Juu usipokamilika mapema, wananchi wanaweza kuanza kuhujumu mabomba ya Wachina (yasiyotoa maji).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga tena mkono hoja hii.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja na napenda kuchangia nyanja ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu teknolojia ya kutumia maji ya Bahari kwa matumizi ya kawaida. Kwa kuwa Tanzania ina upungufu wa maji katika sehemu mbalimbali jambo linalorudisha nyuma maendeleo hasa ya kilimo na matumizi ya binadamu na wanyama na kwa kuwa nchi nyingi duniani ina utaalam na matumizi ya ubadilishaji wa maji ya Bahari kuwa maji ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa utaalam huu ni gharama sana, lakini ni vyema Serikali iweze kuliangalia wazo hili la kupata utaalam wa kubadilisha maji ya Bahari kuweza kutumika kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa tatizo la maji katika nchi yetu. Naishauri Serikali kutumia njia hii ili kuondosha tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu ukamilishaji wa Mradi wa Maji katika Mji wa Bunda, kila mwaka Serikali imekuwa ikizungumzia kuhusu ukamilishaji wa matanki mawili ambayo yamewekwa muda mrefu. Si kweli kwamba tayari mabomba yameanza kulazwa kwani hata mitaro haijakamilika kuchimbwa. Je, Serikali inatoa tamko gani na lini wananchi wa Bunda watapata maji safi na salama? Mradi huo wa maji umeanza tangu mwaka 2006 hadi sasa haujakamilika na Serikali imekuwa ikitoa ahadi kila mwaka. Wananchi wa Bunda wanataka maji, wameanza kukosa imani na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe tamko juu ya ubadhirifu na ujisadi unaofanywa na Mamlaka ya Maji Shinyanga, hawafuati Sheria ya Manunuzi, wafanyakazi wamevunjika moyo kutokana na utendaji usiozingatia maadili ya viongozi. Kuna taarifa kwamba Wizara ina taarifa na ubadhirifu huo. Je, wamechukua hatua gani na kwa nini usifanyike ukaguzi maalum ili kungudua ukweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga shilingi ngapi ili kukamilisha mradi wa Ruvu Chini ambao unatarajia kukamilishwa mwakani, lakini ni asilimia 45 tu ya kazi iliyofanyika. Bado haijulikani hatma ya ujenzi wa mabomba makubwa mawili yatakayotoa maji kutoka Ruvu kwenda Dar es Salaam utaanza lini? Je, ni kweli

huu mradi utakamilika mwakani kwa mradi huo kuendelea kusuasua?

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, maji ni dawa, maji ni chakula. Hakuna maisha kama hakuna maji, hili halipo katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini yenze tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mufindi Kaskazini lina Kata 15 zenze Vijiji zaidi ya 60 na Tarafa tatu zenze wakazi wasiopungua laki moja na elfu themanini, lakini wananchi wanapata maji ya uhakika hawazidi elfu thelathini sawa na asilimia 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka kumekuwa na ahadi hewa ambazo hazitekelezeki. Nasikitika kuona baadhi ya Kata hazina hata klsima kimoja mfano, Kata ya Ihanu yenze Vijiji sita vya Lulanda, Ibwanzi, Ihanu, Kilosa Mfindi, Isipii na Nandala. Kata ya Mdabalo yenze Vijiji vya Ihefu, Ilasa, Ikanga, Kidete Ludilo na Mlevelwa. Kata ya Kibengu yenze Vijiji sita vya Igaleke, Kipanga, Illogombe, Usokami, Kibengu. Kata ya Mapanda yenze Vijiji vya Ihimbo, Ukami, Uhafiwi, Mapanda na Chogo. Kata ya Ikweha yenze Vijiji vya Ikweha, Uyela, Ukelemi na Ugenza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wanatumia miradi muda mwingi sana kutafuta maji badala ya kufanya kazi za uzalishaji mali. Serikali haijadhmiria kwa dhati kutatua tatizo la maji katika Jimbo langu ambalo lina vyanzo vingi vya maji.

Inaonekana kuna upendeleo wa wazi kabisa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Waziri aliyekuwepo alituahidi kushughulikia tatizo la maji Tarafa ya Sadani kwa kutumia Mto Kihata kwa ajili ya vijiji vitano vya Igumbavanu, Tambalangumba, Kibada, Mbugi na Utosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana katika Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mafinga, kuna baadhi ya mashine zimekufa, matanki ya kuhifadhi maji yanavuja na uwezo mdogo wa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mafinga kushughulikia haya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali na hasa Wizara hii ya Maji, haijatupa Mradi hata mmoja mwaka huu, sitakuwa tayari kuunga mkono bajeti hii na naomba Wabunge waniunge mkono nizuie mshahara wa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ni nzuri na mipango ni mizuri, lakini naona fedha zilizo nyingi ni za kufikirika na halisia ni chache sana. Sasa naomba kujua kama Wizara ina mkakati gani pale ambapo

hawatapata fedha walizotarajia? Mfano, fedha za Wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Waziri amewashukuru Wahisani kwenye hotuba yake na tena ni wengi sana, je, wametusaidia nini? Naomba Waziri atupe orodha ya miradi au misaada na thamani yake na ilipo iliyokamilika. Nimetaka orodha hiyo ili kujua nani mwenye matatizo, maana Wafadhili mara zote huahidi na huishia kutotimiza ahadi zao kwa asilimia kubwa kisha Serikali inaathirika na inalaumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana naomba Waziri anipe maelezo ni Wahisani gani ambao wameahidi kutoa ufadhili au fedha au msaada au mkopo na kadhalika. Ili tuwapembue tuone walio wakweli na wasio wakweli tuwaache tutengeneze upya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu hauna maji, ukianzia Singida Mjini, Wilayani, Vijiji ndiyo usiseme. Nashindwa kuandika nina hasira kweli, hivi naungaje mkono hoja jamani? Ukweli hata Waziri na Watendaji mnajua kuwa hamtaweza kufanya kazi kwa fedha mliyonayo au iliyotengwa. Naomba niishie tu hapa, suala la kuunga mkono au kutounga namwachia Mungu.

MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja. Pia nikushukuru kwa Wizara ya Maji kukubali kujenga matanki ya maji ili kupata huduma ya maji kwenye Vijiji vya Chongongwa na Likwachu, Kata ya Chingonewa

Wilaya ya Ruangwa, kutoka mradi mkubwa utokao Mbwinji, Ndanda kwenda Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwa mujibu wa takwimu za mradi wa Mbwinji una chanzo kikubwa na kwamba maji ni mengi zaidi ya uwezo wa matumizi ya Mji wa Nachingwea na kwa kuwa Wilaya ya Ruangwa haina vyanzo vya uhakika vya maji na hauna maji kabisa na umbali wa Nachingwea na Ruangwa ni kilomita 35 tu. Wizara kupitia ombi langu kwako la mradi huo uendelezwe hadi Ruangwa ili wananchi wa Ruangwa waweze kunufaika na Mradi huu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mkubwa wa Maji wa mwaka 1970 uliokuwa unahudumia Vijiji vya Ng'au, Naudagala, Namahene na Chimbila kwa sasa miundombinu yake imechoka na haitoi maji na ni gharama kusaidia kurudisha huduma hii kwa kugharamia mabomba na tanki ambalo kwa sasa ni dogo.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia hoja kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kuhusu bajeti; bajeti ni finyu sana, shilingi 485.7 bilioni ni kwa ajili ya maendeleo. Kwa nchi kubwa na pana yenye wakazi zaidi ya milioni 40, fedha Sh. 465.7 bilioni. Siyo chote kugharamia utafiti wa maji, usanifu na hatimaye utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Miradi ya Benki ya Dunia; Miradi ya Maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia ni ubabaishaji. Tangu 2007 hadi leo ule Mradi wa Maji katika Vijiji 10 haujatekelezwa, bajeti iongezwe kama vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, maji safi na salama; kutokana na mipango ya utafiti watu wengi wanatumia maji machafu yenye kuambukiza maradhi. Nashauri kwamba, Wataalam wa Maji wasimamiwe kutekeleza kazi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu maji shuleni; taratibu za haraka zifanyike ili kila Shule ya Sekondari ipate maji ya kisima kwani wanafunzi wanapata taabu sana kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni kuhusu gharama; maji imekuwa ghali kwa sababu ya kodi ya (*EWURA*) na kodi kwenye bidhaa za kujenga miundombinu ya maji, nashauri kodi kwa maji vijijini zisamehewe.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya *World Bank* kuhusu maji hairidhishi. Mfano, pamoja na Wananchi wa Kijiji cha Rungwa, Kata ya Rungwa, Tarafa ya Itigi kulipia asilimia 20 ya mchango wao, tangu 2010 mpaka leo hii maji hakuna. Naiomba Wizara hii inipe majibu ya kuridhisha kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Itigi na Wilaya nzima ya Manyoni shughuli muhimu ni za ufugaji wa mifugo, ng'ombe, mbuzi na kondoo. Wananchi hawana uhakika wa maji kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maliasili imejipanga vipi kutatua tatizo hili kubwa la maji, kama vile uchimbaji wa mabwawa na malambo. Eneo hili lina utajiri mkubwa wa Maliasili (Rungwa, Kizigo na Mhesi *Game Reserve*) na vitalu vingi vya uwindaji vipo eneo hili. Idara ya Wanyamapori hukusanya takriban shilingi bilioni mbili, kila mwezi kutoka Mbuga za Akiba za Rungwa, Kizigo na Mhezi, lakini hurudisha kiasi cha shilingi milioni 200 tu, Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhuluma kwa wananchi, napenda kujua Wizara ya Maji inasema nini juu ya utaratibu wa wananchi kujikwamua na matatizo ya maji kwa njia ya *Water Dousing System*, inaahidi kuwasaidia nini mfano, pampu za maji wakichimba maji kwa njia hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali haijatambua utaratibu huu na badala yake inafifisha juhudzi za wananchi kwa njia hii? Naiomba Serikali itamke wazi na ifadhili utaratibu huu ili kuokoa fedha za wananchi au Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Waziri Mkuu aliyoitoa Itigi mwaka 2010 kusambaza maji Mji wa Itigi mpaka leo haijafanyiwa kazi na hakuna mpango wowote wa kutimiza ahadi hii. Naomba majibu ya kuridhisha juu ya ahadi hii kabla ya kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika maeneo mawili, tatizo la maji katika Mji wa Dar es Salaam kwa vile tatizo la maji linachangiwa na kuwepo kwa viwanda vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyewe viwanda watumie maji ya Bahari, watumie njia *Evaporation* na kuyakondesi (kuyapoza ili kutoa chumvi) hapo hapo watauzwa chumvi. Nchi za Uarabuni ambako ni jangwa hawana mvua lakini wanaishi na ni wauzaji wakubwa wa maji na chumvi. Vile vile tusingoje mpaka na sisi nchi iwe jangwa, tunatakiwa tukaijenge na kujifunza teknolojia za wenzetu. Ndiyo maana tunatakiwa tupeleke wataalam wakajifunze, mfano, Miji iliyo mwambao mwa Bahari ingetumia Teknolojia ya maji ya bahari tungepunguza tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie upande wa ujenzi wa mabwawa ya kati na makubwa hasa katika Mikoa na Wilaya zenyetukame zipewe kipaumbele. Pia Mikoa na Wilaya zichimbiwe visima virefu ambavyo vitatoa maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha aniambie Wilaya mpya ya Mkalama itapata lini visima virefu hasa Kata ya Mkalama, Kata ya Matongo, Kata ya Nkito, Kata ya Miganga. Iramba Mashariki, maeneo mengi yako kwenye mwamba mgumu yanahitaji visima virefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo yanayoikabili Wizara hii, Wananchi wa Jimbo la Kahama wamenituma na kunitaka niunge mkono hoja, hivyo naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vijiji Kumi vyatya Miradi wa Benki ya Dunia, katika Miradi huu Jimbo la Kahama lina Miradi mitano. Bahati mbaya sana, hakuna hata kisima kimoja ambacho kimekamilika. Sasa nasikia kati ya Miradi hiyo kumi ni miradi mitatu tu itatekelezwa katika Wilaya yote ya Kahama yenye Majimbo mawili; Kahama na Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa sintofahamu, nashauri badala ya kutekeleza miradi mitatu naomba iwe miradi minne kwa maana miwili katika kila Jimbo. Kinyume chake ni kuwachonganisha wananchi wa Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunga kwangu mkono kutategemea sana maelezo ya Waziri kuhusu jambo hili kwamba kila Jimbo litakuwa na miradi miwili itakayotekerezwa katika mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Wizara ya Maji, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, kmisingi bajeti hii ni

finyu mno kulingana na matatizo ya huduma hii muhimu katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuwatendea haki Watanzania walio wengi nashauri bajeti iongezwe, katika Jimbo la Mbarali upo Mradi wa Maji ya kutegwa kutoka Wilaya ya Njombe, sasa Wanging'ombe na Vijiji sita kutoka Kata ya Mawindi ambavyo ni Kangaya, Matemela, Ipwani, Mkandami, Manienga na Itipingi, Vijiji ambavyo ndiyo hasa vilivvolengwa, kwani havijawahi kupata huduma hii muhimu ya maji toka nchi hii ipate uhuru. Mbaya zaidi, majirani zao wa Wilaya ya Njombe wanayo maji ya bomba. Inahuzunisha sana jinsi wananchi hawa wanavyopata tabu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu unafadhiliwa na *World Bank*. Gharama za mradi huu baada ya kufanyiwa upembuzi yakinifu, umeonekana utagharimu Shilingi bilioni nane, fedha ambazo Halmashauri haina uwezo nazo. Naomba Wizara itazame upya namna ya kusaidia ufanisi wa mradi huu ambao ukikamilika una uwezo wa kusambaza maji Kata za Rujewa, Igava pamoja na Kata ya Mawindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tatizo la maji katika Jimbo la Mbarali ni kubwa mno, miundombinu ya maji iliyopo ni chakavu kwani ya zamani sana kwa hiyo, imechoka. Hata hivyo, kwa vile idadi ya watu imeongezeka sana, Miradi ya Maji iliyopo haiendani na hali halisi ya sasa, kinachotakiwa ni kuboresha na kupeleka mtandao mpya katika maeneo ambayo hayana maji kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matumizi mabaya ya fedha za Mradi wa Maji, mfano, bajeti ya mwaka 2011/2012, Wilaya ya Mbarali, upembuzi yakinifu tu shilingi milioni 380, alilipwa mtaalam. Chanzo cha habari hii ni taarifa iliyosomwa na Naibu Waziri ndani ya Bunge. Shilingi milioni 83, vilichimbwa visima ambavyo bado siyo vyote vinyavotoa maji, kama zaidi ya milioni mia nne zinaweza kupotea kabla wananchi hawajapata maji, ni kiasi gani cha fedha kitahitajika ili kuwawezesha wananchi kupata maji? Haikubaliki kabisa, naomba ufuatiliaji ufanyike ili kuona ukweli wa matumizi ya fedha hizi za Watanzania na ikibainika kuna ubadhirifu, hatua kali zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamka kwenye Kamati kuwa ingekuwa vigumu kuunga mkono hoja hali wananchi hawana huduma ya uhakika ya kupata maji. Kutounga mkono hakumaanishi kuchukia Uongozi uliopo, hapana, kwanza Wizara ya Maji ili Watanzania wengi wanufaike, Serikali iangalie upya Wizara hii kwani Shule za Sekondari, Msingi na Zahanati nyingi hazina maji. Naomba fedha za miradi hii ya maji zinapopatikana usimamizi kutoka Wizarani uwe wa karibu, fedha huko Halmashauri hazina usimamizi mzuri, huenda zinaliwa au kupewa matumizi mengine. Ahsante.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama Mheshimiwa Waziri anakumbuka ombi la Shilingi milioni 200 kwa ajili ya maji katika Jimbo la Kasulu Mjini kwa ajili ya vijiji vitatu ambavyo vina

miundombinu iliyochakaa na kuharibika kutokana na kutokarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tanki kubwa kwa mujibu wa Mhandisi wa Maji, Wilaya ya Kasulu, ni kwamba kiasi cha shilingi milioni 200 kinaweza kusaidia kufufua miundombinu hiyo na hivyo kuwezesha vijiji vitatu vya Herujuu, Kalunga na Muhunga kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alinieleza atanisaidia kutupatia fedha, tulipozungumza naye hapa Bungeni, niliandika barua na kumpatia Naibu Waziri, nauliza vipi tutapata fedha hizo kwa mwaka huu wa fedha wa 2012/2013?

MHE. MWIGULU L.N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niipongeze Serikali kwa kuwakumbuka wananchi wa Kyengege kupata mradi wa maji. Aidha, naipongeza Serikali kwa kuwakumbuka wananchi wa Ngurumali na wananchi wa Mingela kwa kupata mradi wa Benki ya Dunia. Tunaiomba Serikali ifuatilie kwa ukaribu utekelezaji wake ili mradi ukamilike kwa wakati uliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba Serikali kuharakisha awamu ya pili yenyewe Vijiji vya Ng'anguli, Mgungia, Mlandala na Ujungu. Aidha, naomba Serikali itoe kipaumbele kwenye Vijiji vya Kicharita, Ulemo, Kinampanda, Mseko, Kizonzo, Malendi, Masimba, Kisimba, Ndurumo, Kipuma, Mbelekesi, Misuna, Kibaya, Zinziligi, Makunda, Tintigula, Msansao, Galangala, Mgongo, Fyulia, Ruvuma, Mgundu, Maluga

na Luzilukulu. Katika Vijiji hivi wananchi wanapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali ishughulikie ufufuaji wa mashine na mabomba ya maji yaliyoharibika ikiwemo Kitusha, Mampanta, Uwanza na Urughu. Wizara pia itusaidie kufufua mabwawa mengi yaliyokuwa na msaada kwa wananchi wengi na mifugo. Katika miaka ya nyuma mabwawa ya Makunda, Mkulu, Kitusha, Ruvuma, Mampanta ni mionganini mwa mabwawa yaliyokuwa ya misaada sana kwa wananchi na mifugo yao. Naiomba Serikali itoe tamko la suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii ya Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inastaajabisha sana kuona katika karne hii ya 21, bado kuna watu wanaendeleza *barter trade* kwa kubadilishana maji kwa debe la nafaka, vitu ambavyo haviendani hata kidogo. Ni vema sasa tuje na mkakati wa makusudi ili kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Same, kwa huduma za maji. Hata hivyo, niiombe Serikali sasa iwakumbuke wananchi wa Milimani hususan Suji, Chome, Tae na

maeneo mengine ya milimani, bila ya kusahau maeneo ya Makanya. Aidha, ningeshukuru endapo Waziri wakati wa majumuisho angetueleza vijiji vilivyofaidika na Miradi ya Maji ni vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baada ya kueleza haya, niunge mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara hii kwa kuwasilisha ripoti nzuri. Pili, naunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo mengi sana ya maji katika Jiji la Dar es salaam. Mengi ya matatizo yanatokana na uzembe wa Taasisi inayohusika pamoja na Wizara kutoisimamia vizuri Taasisi hii. Imebainika kuwa watu wengi wanajiunganishia maji kiholela bila ya kupata kibali. Hii husababisha kuzuia maji na kupungua nguvu na hivyo yasifike katika maeneo yenze muinuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa wa kudhibiti uungaji wa maji holela ili kuongeza ufanisi. Jambo llingine linalosababisha upungufu wa maji Dar es Salaam ni miundombinu iliyochakaa na kuchakaa. Mabomba yamejaa *calcium*, hivyo maji hayawezi kupita katika boma. Vile vile kuna uvujaji mkubwa wa maji, maji yanamwagika ovyo. Inasemekana kuna upotevu wa maji kutokana na miundombinu chakavu pamoja na mambo mengine ni zaidi ya asilimia 30. Nashauri hatua za haraka zichukuliwe kudhibiti upotevu huu wa maji kwa kuweka miundombinu mipyä.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wizi mkubwa wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, wananchi wanashirikiana na viongozi wa *DAWASCO*. Naiomba Wizara ichukue hatua za makusudi ili kudhibiti upotevu mkubwa wa mapato kutokana na wizi wa maji.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe; Naibu Waziri Daktari Binilith Mahenge; Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijawekeza kabisa katika vyanzo vya maji, imekuwa ikitenga pesa kidogo sana kwa ajili ya kutunza vyanzo hivyo. Changamoto kubwa zinazokabili vyanzo hivi ni ongezeko la idadi ya watu na shughuhli za kiuchumi na kijamii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti kutoka *Great Ruaha*, Bwawa la Mtera, linazalisha *megawatt* 80 na bwawa la Kidatu *megawatt* 204 ambazo ni sawa na asilimia 45 ya umeme wa maji yote nchini. Kuna mito mingi inapoteza mikondo ya maji, mito mingine imejaaj michanga na udongo, mito yote inayotoka Usangu inaungana na kupeleka maji *Great Ruaha* asilimia 30, Mito ya Usangu inapeleka maji lhefu na lhefu inapeleka maji hifadhi ya Taifa ya Ruaha mpaka bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, point yangu hapa nilikuwa nataka kusema kuwa bado Serikali haijawekeza katika vyanzo nya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti ninavyoju, Idara ya Rasilimali za Maji kazi yake kubwa ni kutunza, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za maji na kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na ongezeko la watu rasilimali za maji zimekuwa zikipungua siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo hii Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja mbalimbali atuambie ametumia vigezo gani katika kutenga bajeti ya Idara ya Rasilimali Maji. Ukiangalia utaona bajeti ya Idara hii nzima ni ndogo hata ukilinganisha na bajeti ya Halmashauri moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti utakumbuka Chuo cha Rourkee India kilianzishwa kufundisha Mainjinia wa Maji katika miaka ya 1960. Chuo hicho ndiyo chanzo cha maji UDSM wao walifundishwa kufanya miundombinu ya maji inaimarika. Utashangaa leo hii kila siku mabomba yanapasuka ovyo, utaona hakuna uwiano kati ya idadi ya watu na uunganishwaji wa mabomba ya maji hayo. Mfano, bomba la Ruvu lilikuwa linahudumia watu chini ya milioni moja, sasa hivi bomba hilo hilo linahudumia mamillioni ya watu, hivi hawa wataalam wapo kweli au tatizo hili hawalioni?

Mheshimiwa Mwenyekiti lipo tatizo kubwa sana katika Mkoa wa Dar es Salaam hasa majitaka mabomba yanapasuka ovyo, mpaka kusababisha Jiji kuwa na majitaka yaliyosambaa na kuleta harufu

mbaya na kuwa kero kwa wakazi wa Jiji. Pia kuna wizi wa mifuniko ya chuma inayotumika katika mashimo, je, Serikali inakabiliana vipi na wimbi hili la vyuma chakavu katika kunusuru mifuniko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie na Mji mdogo wa Ilula kuna tatizo kubwa sana ambalo Serikali iweke mkakati kuhakikisha kuwa tatizo hili linakwisha kabisa. Mji huu wa Ilula upo katika Jimbo la Kilolo, wananchi wamechangia sana mradi huo wa Benki ya Dunia lakini bado wanapata mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Tumekuwa tukizungumzia sana kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, lakini kauli hii haiwezi kufanikiwa bila kupata maji ya uhakika. Kule Moshi Vijijini, Kata ya Mabogini, Wajapani walianzisha kilimo cha mpunga kwa umwagiliaji, lakini sasa hivi maji yale hayapo ya kutosha? Ni lini wananchi wa Mabogini watapatiwa maji siyo ya umwagiliaji tu hata maji ya matumizi ya kawaida hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi Vijijini, Kata ya Mbokomu wana matatizo ya maji nimekuwa nikilizungumzia tangu Bunge la Tisa, akinamama wanatoka zaidi ya kilomita kumi kutafuta maji, watoto wa shule hawasomi, wanakwenda kuchota maji. Naibu wa Wizara ya Maji Mheshimiwa Chiza alikuja na kutembelea Kata ya Mbokomu na kuangalia vyanzo

vya maji na kuahidi kushughulikia tatizo hili. Mpaka sasa hivi ni zaidi ya miaka sita, hakuna kilichofanyika. Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa Mbokomu kuhusu Mradi huu wa Maji na lini utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Moshi Mjini kwa sasa hivi linakabiliwa na tatizo kubwa la maji sababu ya ukame uliokumba Mkoa wetu wa Kilimanjaro ikizingatiwa Mkoa huu ni kati ya Mkoa unaoingizia pato la Taifa fedha nyingi na hivyo huwa tumepata Watalii wengi sana wanakuja kupanda Mlima Kilimanjaro. Watalii hawa wanapata shida sana wanapofika kwenye mahoteli wanakosa maji ya kuoga inabidi wakingiwe kwenye ndoo. Hii ni aibu kwa nchi yetu yenye vivutio vyenye kuliingizia Taifa hela, halafu huduma muhimu kama maji hakuna? Serikali ina mikakati gani kuhakikisha maji safi yanapatikana Moshi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam ni kioo cha nchi yetu, lakini maji ni tatizo katika Jiji letu, maji yanayotoka kwenye bomba ni machafu na yananuka, mengine yanachanganyika na vinyesi ambayo hupelekea hata magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na kadhalika. Je, tatizo la maji yasiyo salama katika Jiji letu litakwisha lini? Mpaka sasa hivi Kinondoni hakuna maji zaidi ya wiki mbili na wananchi hawajaelezwa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji safi na salama katika Jiji la Dar es Salaam ni muhimu sana kutatuliwa, ikumbukwe Dar es Salaam ina wakazi zaidi

ya milioni nne. Mlipuko wa kipindupindu ukitokea kuna Hospitali za kuwabeba watu hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinga ni bora kuliko tiba.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia bajeti hii ambayo ndiyo kiini cha uhai wa viumbe vyote kuanzia mimea, wanyama na hata sisi binadamu ambao ndiyo watumiaji wakubwa wa maji haya kwa maana ya matumizi kwa ajili ya kunywa, kufulia, kuogea, kupikia na matumizi mengineyo ya kufanya usafi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu huu, Tanzania licha ya kuwa na vyanzo vingi vya maji, kwa maana ya mito, maziwa, bahari na chemchem nyingi zitokazo kwenye milima. Cha kusikitisha, Tanzania inaendelea kuwa ni nchi yenye uhaba wa maji katika sehemu zake nyingi na hasa vijijini ambapo ndiyo Watanzania wengi tunaishi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosekanaji huu wa maji waathirika wakubwa ni akinamama ambao si tu tunapoteza muda mwingi kutafuta maji, bali tunapata athari nyingi sana kama kutembea muda mrefu kutafuta maji, kuamka asubuhi huku tukikatisha usingizi na hata tunaweza kuvamiwa njiani, ongezeko la unyanyasaji wa wananchi au wanawake toka kwa waume zao pale wanapochelewa kurudi toka mtoni au visimani. Talaka imeongezeka kwa kasi kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Mkao wa Mara, Mkao ambao una vyanzo vingi sana vya maji, kwetu tuna Maziwa (Ziwa Victoria), Mto Mara, chemchemi ya mito kama Mto Mori, Mirale na mingine mingi, lakini cha ajabu Mara maji ni bidhaa adimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Shirati wakazi wa vitongoji vyake wanositishwa na mambo yafuatayo:-

Toka mwaka 2004 ambapo *KMT* ilikabidhi mamlaka ya uendeshwaji maji Serikalini na mashine ikaharibika mwaka huo huo. Wakazi wa vitongoji hivyo hawajapata maji hadi leo hii licha ya kuomba maji toka Ziwa Victoria ni chini ya kilometa moja na nusu tu. Cha kushangaza na kusikitisha, watumishi wa mamlaka wanaendelea kupata mishahara bure huku hawana wanadolifanya kwa maana baada ya mashine kufa hamna usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe mwaka jana wakati Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda akifanya ziara yake Mkoani Mara. Alipokuwa Shirati aliahidi urejeshwaji wa huduma hiyo baada ya wiki mbili, cha ajabu mpaka leo wananchi wale hawajapata maji, sasa tueleweje ile kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwa ni hadaa kwa wananchi wa Shirati au dharau kwa Watendaji kutokutii kauli ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza sana ukizingatia enzi za *KMT* wakazi hawa walikuwa wakipata maji ya

kutosha na hivi sasa wanataabika na maji hadi kufikia kununua maji ndoo moja kwa shilingi 500. Hii haikubaliki hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali imekuwa ikizungumzia uchimbaji wa lambo la Kanyisambo katika Kata ya Nyahongo na hii imekuwa ikisomwa katika bajeti ya Wizara ya Maji toka mwaka 2006 na 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye, uchimbaji wa hili bwawa uliondolewa kwenye bajeti ya Wizara tena bila utekelezaji wake. Napenda kupata majibu ya hili, kwa nini Serikali imeliondoa suala la uchimbaji wa bwawa au lambo la Kanyisambo, limeishia wapi? Maana imeyeyuka bila kutekelezwa. Naomba Serikali inipe majibu ya haja kwenye hizi hoja zangu mbili; Mamlaka ya Maji Shirati kufa tangu 2004 na ahadi ya Waziri Mkuu na uchimbaji wa lambo la Kanyisambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, sasa Tanzania hatutaki uhai wa viumbe hai wetu ikiwemo sisi wenyewe. Maji siyo tu hayapatikani bali sio safi na salama, wananchi wanapata madhara mengi kama vichocho, kuhara, *amoeba* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali ichukulie ukosekanaji wa maji ni janga la Taifa. Hivyo kuipa Sekta hii kipaumbele na hivyo kuelekeza fedha za ndani kwenye Wizara hii na si tu kuwaachia wafadhili, ndiyo kuwa wasimamiaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango nilioutoa kwa kuzungumza, napenda kuongeza mapendelekezo na ushauri ufuatao hasa ikizingatiwa malalamiko makubwa nchi nzima juu ya udhaifu wa utekelezaji wa Miradi ya Vijiji kumi chini ya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kupitia upya mfumo wa utekelezaji wa Mradi wa Benki ya Dunia. Marekebisho yafanyike ili kupunguza muda mrefu wa mchakato wa kupata Kibali cha Mradi toka Benki Kuu. Kuna awamu ya kwanza ya kuchimba kisima kisha awamu ya ujenzi wa miundombinu, muda ni mrefu na ucheleweshaji ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu mchakato wa miradi. Ikiwa lazima miradi iwe ya visima kwa vijiji vyote, miradi ya maji ya mtiririko ni miradi ya kutoa maji katika mito, maziwa, mabwawa ina upeo mkubwa wa uwezo wa kusambaa kwenye eneo kubwa zaidi ya miundombinu ya visima. Mifano michache ni kama ifuatavyo:-

- (a) Mradi wa maji wa Mto Wami, Chalinze hivi sasa umehudumia eneo kubwa zaidi ya umbali wa kilomita 60 na Vijiji zaidi ya 50 na sasa una mwelekeo wa kuelekea toka Mkoa wa Pwani hadi Mkoa wa Morogoro;
- (b) Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria; na

(c) Mradi wa Maji toka Mto Ziggi toka Muheza hadi Tanga kilomita 70. Gharama za Miradi ya Benki ya Dunia kwa Wilaya mbili kukamilika hadi ujenzi wa Miundombinu ina uwezo wa kugharamia mradi wa maji mtiririko au toka chanzo cha Mto na kutoa huduma kwa zaidi ya Wilaya Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kujenga mfumo wa tathmini ya Miradi mikubwa ya Maji na kutafuta fedha za utekelezaji. Nchi ya Tanzania ni kubwa, lakini imezungukwa na hazina kubwa ya vyanzo vyta Maji kama vile Mito, Maziwa, Mabwawa, Maji mtiririko toka Milimani, Mabwawa na maji chini ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujenge uwezo na mkakati wa ubunifu wa miradi kutoka maeneo hayo na tuwe na hazina ya tathmini hizo na kutafuta fedha kwa utekelezaji. Nafahamu kazi hizo zinafanywa na mamlaka kama vile Mamlaka ya Maji Bonde la Mto Pangani. Je, ni mradi gani umebuniwa na kutekelezwa na Mamlaka hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Mamlaka hizo zijenge mfumo wa kutambua vyanzo thabiti vyta miradi ya maji, kuifanyia tathmini na kujenga kumbukumbu ya rekodi, ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa. Kutojenga mfumo huo hakuipi nafasi Wizara ya Maji kuwa msimamizi mkuu wa utekelezaji mfumo wa huduma za maji kwa Taifa letu. Kwa mfano, Wizara ya Maji inafahamu kwamba Wilaya ya Muheza ina vyanzo na Miradi ya Maji ifuatayo?

- (i) Mradi wa Maji Mtiririko wa Potwe;
- (ii) Mradi wa Maji mtiririko wa Mlingano unaoanza Magula (Kata ya Magoroto)- Misozwe (Kata ya Misozwe), Kicheba Kata ya Misozwe hadi Mlingano, Kata ya Mlingano;
- (iii) Mradi wa Maji Mtiririko toka Magoroto- Mkurumuzi hadi Muheza Mjini;
- (iv) Mradi wa Maji wa Mbabara (ulioharibika) wa ahadi ya Mheshimiwa Rais kuukarabati);
- (v) Mradi wa Maji wa Mto Ziggi (unaopeleka maji Jiji la Tanga);
- (vi) Mradi wa Maji Mtiririko wa Misalai;
- (vii) Mradi wa Maji mtiririko wa Kambai; na
- (viii) Mradi wa Maji mtiririko wa Ubembe, Kwemhosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi na vyanzo vyote hivyo, Mji wa Muheza hauna maji ya kutosha. Tatizo ni mfumo na uwezo wa Watendaji katika ngazi ya Wilaya na kukosa muunganisho wa mfumo wa ushauri, msaada na uwezo wa utendaji ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji kama mhimili mkuu haina kumbukumbu nilizotaja hapo juu.

Hii inathibitishwa pale ambapo Wizara ya Maji ilipokubali hoja yangu kama Mbunge kuleta wataalam, kuisaidia Wilaya ya Muheza kutatua tatizo la maji katika Mji wa Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa imethibitisha kwamba vyanzo viro vingi ila kwa udhaifu wa utendaji ndani ya Wilaya, tumeshindwa kuzitumia fursa hizo kuondoa tatizo la maji Muheza Mjini. Je, sio jukumu sasa la Wizara kama mhimili mkuu kuisaidia Wilaya ya Muheza kuondoa tatizo hilo hata kwa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais Mkuu wa nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Wizara inapopangiwa upeo wa juu wa Bajeti (*ceiling*) basi inashindwa kuweka utekelezaji wa mipango mingi muhimu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi nzuri anayoifanya. Juhudi zilizofanyika kwa kuwapatia wananchi maji haziwezi kubezwa. Hata hivyo, kwani niwaombee Wananchi wa Wilaya ya Muleba ambao bado hawajapata maji, miaka 50 baada ya Uhuru, sina budi kumuomba Waziri atuangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muleba maji yako mbali sana, wanawake wanahangaika katika vijiji vyote takribani 250, visima vinapatikana katika vijiji chini ya 20

tu, isitoshe vyanzo vya asili vinavyotoa maji ya kunywa ni viwili (2), vingi vimekauka kwa sababu ya kukata miti na shughuli za kilimo katika maeneo oevu. Matokeo ni ukosefu mkubwa wa maji Wilayani kote. Namwomba Mheshimwa Waziri wa Maji atuunge mkono katika zoezi letu sisi wananchi wa Muleba, katika juhudu zetu kuchimba visima vya kina kirefu *deep boreholes*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji vyote, zoezi hilo limeanza kwa juhudu zetu kwa kugharamia *Hydrological* na *Geological Survey* kwa kuwalipia wataalam wa Wizara ya Maji kukamilisha zoezi hilo. Mimi kama Mbunge wa Jimbo nimetafuta mkopo kuziwezesha Kata kukamilisha zoezi hili. Hii inaonesha dhamira yetu ya kupata maji, zoezi zima limegharimu Shilingi milioni 30. Sasa kinachofuata ni kuchimba visima hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunamwomba Mheshimiwa Waziri aagize Wizara yake kutoa fedha za kuchimba visima hivyo ili zoezi likamilike. Itakuwa jambo la kusikitisha kama wataalam wa Wizara ya Maji waliokaa mwezi mmoja Muleba wakitafuta maji watashindwa sasa kuchimba visima. Wananchi wa Muleba wako tayari kutunza visima na vyanzo vya maji ili mradi viboreshw. Lengo letu ni kutekeleza malengo ya Millenia ya maji safi kwa kila kijiji ifikapo 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati niko Umoja wa Mataifa nikiwa Katibu Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa na Mkurugenzi Mtendaji wa nne, Shirika la Makazi Duniani nilianzisha Mradi wa Maji na Usafi katika Eneo la Bonde la Ziwa Victoria. Mradi huo wa UN-

Habitat, Water and Sanitation Initiative for Secondary Towns in Lake Victoria, uliboresha maji katika Mji wa Bunda, Sengerema, Muleba, Bukoba na Mtukula. Nimefurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu, lakini pia Taifa kwa ujumla kwamba mradi huo ambao upo chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki unajumuisha nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi sasa kwa juhudi nilizozianzisha nikishirikiana na Daktari Koberuka, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo Africa (*ADB*) sasa umepanuka na kuingiza pia eneo la Ziwa Tanganyika. Najivunia hatua hiyo, aidha na Benki ya Maendeleo Ulaya *European Development Bank* pia imeanza kutoa fedha nyingi zaidi ya *Euro* milioni 100 kwa mradi huu katika Miji Mikubwa kama Kampala na sasa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa jambo la kusikitisha kama Wizara ya Maji itasahau historia hii na kutelekeza utunzaji wa Miradi ya Maji katika ile miji ambapo maji yaliletwa na mradi huo wa *Un-habitat* kwa makubaliano kuwa Serikali itachangia usambazaji. Nasikitika kusema kuwa katika Mji wa Muleba Maji ya *UN-habitat* yako kwenye tanki lakini hivi sasa limepasuka kwa kukosa *Distibution*. Ni kama yametuama humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aje Muleba ajionee tatizo hili. Wananchi wa Mtaa wa Kagombiro hapo Muleba ambao walitoa ardhi kwa mradi huo hawafaidiki na maji hayo. Naomba Mheshimiwa Waziri aniondolee kero hii, atoe

bajeti ya dharura kusambaza maji hayo Mjini Muleba. Sasa hivi Umoja wa Mataifa wanani sumbuwa sana wakidhani sifuatilii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UN-Habitat* pia iiltoa *master plan* ya Mji wa Muleba, wakati Wizara yangu ya Ardhi na Makazi itapima Mji huo, Wizara ya Maji nayo iwepo kupitishwa mabomba ya maji safi na maji taka ili tuwe na Mji uliopangwa vyema. Kusambaza maji ni shughuli inayohitaji mipango miji, wakati nikitoka Muleba iwe mfano, utaratibu huu unatakiwa kufuatwa nchini kote. Bila mipango iliyonyooka mabomba ya Spongeti hayatoi maji. Nawashukuru *DAWASA* kushirikiana na Wizara ya Ardhi katika Mradi wa Kuboresha Makongo Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natoa wito kwa Mamlaka za Mji Mijini kushirikiana na Mipango Miji katika kazi zao tuachane na Spongeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji ina jukumu pia la miundombinu ya usafi (*sanitation*). Naomba Wizara pia iangalie suala hili katika Miji midogo, hivi sasa mabwawa ya maji huko yapo tu katika Miji mikubwa. Nitoe tu angalizo kuwa katika Miji mingine *on site sanitation* kwa kutumia vyoo vya latrines na septic tanks zilizo karibu sana na maji ya chini ya ardhi (*pollution of underground water*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mwenyekiti wa *UN-Water Supply and Sanitation Collaborative Council (WSSCC)*, wadhifa ambao Mheshimiwa Rais alinipa ridhaa niendelee nao. Nafurahi kulijulisha

Bunge lako Tukufu kwamba nimefanikiwa kupata msaada wa Dola za Kimarekani milioni tano kwa ajili ya kutatua tatizo la uchafu katika Mkoa wa Dodoma. Msaada huo umetokana na Mfuko wa Dunia wa Usafi (*UN-Sanitation Fund*) ambao unafadhili mifano ya kuigwa kwa kujikita katika eneo fulani na kumaliza tatizo. Naomba Wizara ya Maji iangalie utekelezaji wa Mradi huu ili uzae matunda bora na kufanikisha malengo. Itakuwa sifa kubwa kuona tutafanikiwa hapa Makao Makuu, Dodoma ili niwe na nguvu ya kuomba msaada kwa Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze pia, kuwa nikiwa *UN-HABITAT* tulifadhili *DAWASA* kuboresha *capacity building*. Nashauri Mamlaka zote nchini ziimarishwe na hasa katika eneo la fedha, *billing and revenue collection*, ni kero kuleta *bill* wakati maji hayatoki. Lakini haina tija kuboreshwa maji na tukajisahau kuweka tozo ndogo kwa ajili ya ukarabati mdogo. Mamlaka za Maji zitakiwe kuonesha mipango waliyonayo katika eneo hili. Aidha, Wilaya ya Muleba katika visima vitakavyochimbwa wananchi tujiwekee utaratibu wa tozo ndogo kuhakikisha ukarabati una pesa za kutosha. Sasa kama Mamlaka za Maji Mijini hazina *Rehabilitation Reserves* na zinaitegemea Wizara au Halmashauri, Wizara inatakiwa kutuelimisha na kutuongoza katika hili nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake na watoto ndiyo wahanga wakubwa wa ukosefu wa maji. Kwa niaba ya wanawake na watoto wa Tanzania, namtakia Mheshimiwa Waziri afya tele, nguvu, nia na ari ya kuendeleza sekta ya maji na usafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie hoja hii kwa kusema naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maji kwa hotuba nzuri na ya kina ambayo inatoa matumaini kwa Watanzania waishio vijiji na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, ndiyo maana kila Mbunge anayesimama anaelezea hali halisi ya maji katika maeneo yao. Itapendeza iwapo kwa miaka ijayo bajeti ya Serikali kwa Wizara hii itaongezwa ili kukabiliana na changamoto zilizopo. Aidha, ni vema bajeti ya maendeleo ya Wizara hii ikawa na sura ya kujitegemea kuliko ilivyo hivi sasa ambapo ni asilimia 30 tu ya bajeti ya maendeleo inatokana na fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Bariadi Magharibi yapo malambo yaliyojengwa miaka ya sitini na sabini ambayo sasa sehemu kubwa ya malambo hayo imefunikwa na magugu maji na hivyo kuyafanya yakauke. Ningependa Mheshimiwa Waziri afahamu, je, haiwezekani kuanzisha programu maalum ya kupambana na hayo magugu maji kama ilivyofanyika kwa magugu maji katika Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi katika Jimbo langu wameitikia vizuri Sera ya Serikali ya kuanzisha vikundi vya watumiaji maji. Wametekeleza wajibu wao ikiwa ni pamoja na kufungua akaunti, kuchimba visima na kadhalika. Tatizo lililopo ni uhaba wa pampu kwa ajili ya visima vya vikundi hivyo. Tatizo hili limekuwa ni kikwazo kikubwa na sasa limeanza kuwavunja moyo na hivyo kutufanya sisi Wanasiasa tuonekane kuwa tunahamasisha mipango ambayo haitekelezeki. Hivi tatizo la uhaba mkubwa wa pampu za visima kiini chake hasa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda Mheshimiwa Waziri anieleze kuhusu mradi wa visima kumi pale ambapo Wilaya imegawanywa na kupata Wilaya mpya, je idadi ya visima itaongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Bariadi tunaishukuru Serikali kwa kuchukua hatua mahsus ya kufanya maandalizi ya kiufundi ambayo hatimaye yatawezesha kuwa na mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Bariadi, tunashukuru. Hata hivyo, katika kipindi cha muda mfupi na wa kati, naendelea kuishauri Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuchimba visima virefu pale Bariadi mjini ili kukabiliana na tatizo kubwa la uhaba wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kama nilivyoanza kwa kusema kuwa, naunga mkono hoja.

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wilaya ya Chunya, ni Kijiji

kimoja tu ndiyo mpaka sasa kimepata fedha za mradi wa visima kumi vya maji, wakati kwenye kitabu cha hotuba yako ulisema kila Halmashauri ni vijiji vitatu kati ya 10 kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wilaya ya Chunya ni kavu sana sana, wananchi wanatumia maji ya mbugani ambako wachimbaji wadogo wadogo wanaochimba dhahabu ndimo wanaosafishia mchanga ili kupata dhahabu kiurahisi. Maji haya ya mbugani huisha miezi ya kiangazi kati ya Agosti, Septemba, Oktoba na Novemba baada ya hapo kutumika maji ya mvua mabwawani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mradi wa Maji Chunya haujafanana na Wilaya zingine, kwa nini iwe Kijiji kimoja badala ya Vijiji vitatu kama ilivyo kwenye Halmashauri zingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Maji Kitunda, umeme umefika lakini hakuna pampu za kuvuta maji kuingiza katika matanki. Katil ya visima saba, vinne vimeshindwa kutoa maji kutokana na kinachosemekana tope liliroziba visima hivyo. Aidha, taarifa inaonesha kuwa kiwango cha maji katika chanzo hicho ni kidogo na hivyo baada ya muda mfupi matarajio ya kupata maji kutoka chanzo hicho yatatoweka. Serikali ituambie maeneo iliyotenga kama vyanzo mbadala na tufahamishwe ni lini program za kuanzisha vyanzo hivyo itaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ombi maalum kwa Manispaa lilitolewa wakati wa ziara ya Mheshimwa Rais mwezi Septemba, 2012 kuwa Manispaa ikopeshe *LUWASA*, fedha za kununulia mafuta ya Jenereta. Je, ni lini fedha hizo zitarejeshwa Manispaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vyatupato vinavyotegemewa na mashirika ya utoaji huduma ya maji ni vidogo kwa kuwa hutegemea malipo ya ankar za maji, lakini tatizo la maji kwa kuwa ni kubwa hata wateja wameacha muda mrefu kuunganisha huduma hizo. Hivyo, Serikali inatafuta njia gani mbadala kuwezesha mashirika hayo kumudu gharama za uendeshaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya maji na maji taka ni ya Kikoloni, hivyo Serikali inaisaidiaje *LUWASA* kuona mfumo wa maji taka katika Manispaa ya Lindi unafufuliwa na au kujengwa upya ili kupunguza adha ya wakazi na kupanuka kwa Mji huo wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaje maeneo yaliyoingizwa katika program ya maji ya vijiji kumi kutoka kwa iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi na Kata zake kuingizwa katika Manispaa ambazo ni Chikonji, Mingoyo, Msingahili (Mnali), Mbanja na Tandangoro na Ng'apa ili wananchi hao wanufaike na mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lindi Mjini ambalo hupata lita za ujazo 1,540 kwa siku sawa na asilimia 31 tu ya mahitaji. Pia kukiwa hakuna huduma ya uondoaji wa maji taka na hali ya usafi wa mazingira katikati ya Mji hairidhishi kwa kuwa meza ya maji iko juu. Serikali ina mpango gani wa kulipatia ufumbuzi tatizo hilo? Ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa gari la kunyonya maji machafu na hivyo kupunguza adha ya wananchi kutumia njia chafu ya kutapisha vyoo wakati wa mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje kuhusu kutokuwepo kwa uhakika kwa matumizi ya maji safi na salama ikizingatiwa kuwa dawa inayotiwa kutibu maji *calcium Hypochlorite* inakuwa na uwezekano wa kuchafuliwa maji hayo wakati wa kusambazwa. Na ni lini Tanzania itatumia dawa za kutibu maji kwa kiwango cha Kimataifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje kuhusiana na fedha Sh. 328,000,000/= zilizotolewa na ahadi ya Rais. Lini fedha hizo zitaanza kutumika na zipo mikononi mwa nani hivi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo ya kuridhisha juu ya hoja hizo.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii angalu kutoa mawazo yangu katika Wizara hii ya Maji, Wizara ambayo inatamalaki na uhai wa viumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni sehemu ya uhai wa mwanadamu, lakini maji ni sehemu ya uhai wa viumbe vyote, mwanadamu bila maji hawezi kuishi, wanyama bila ya maji hawawezi kuishi, miti bila maji haiwezi kuishi, ustawi wa viumbe unategemea maji, kwa hiyo, maji ni sehemu ya maisha kwa viumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ustawi wa viumbe unategemea kuwepo kwa maji kama vile mito na maziwa ili visiathiriwe kwa namna yoyote ile. Mionganoni mwa mambo ambayo yanaathiri vyanzo vyaa maji ni kilimo ambacho hakizingatii uhifadhi wa maji, lakini vile vile ukataji wa miti ovyo ni mionganoni mwa mambo ambayo yanakimbiza mvua na hivyo kupoteza sehemu kubwa ya maji mambo ambayo ni kiungo baina yake na viumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya nchi yanategemea maji kwa kiasi kikubwa, kwani hata uzalishaji wa umeme unazingatia uwepo kwa kina kikubwa cha maji ili tuweze kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nilisema kwamba, maji ni sehemu ya uhai wa mwanadamu na viumbe, bila maji hakuna maisha, bila maji hakuna usafi, bila maji hakuna ustawi wa maisha na ndiyo maeneo mengi ya Tanzania na hata Bunge lako Tukufu hulalamikiwa sana na Wabunge kuhusiana na tatizo la ukosekanaji wa maji katika maeneo mengi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu kwa usafi wa miji na usafi wa mazingira, lakini maji yanaweza

kusababisha matatizo na milipuko ya maradhi mbalimbali yasipotumiwa vizuri, hivyo ni lazima utumiaji na uhifadhi wa maji ni lazima uzingatie misingi bora ya utunzaji wa mazingira mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Ziwa Victoria ambalo limeunganisha Tanzania, Kenya na Uganda, Ziwa hili ni tegemeo kubwa kwa ustawi wa maisha ya Watanzania na nchi jirani tulizopakana nazo. Vile vile tuna Ziwa Nyasa, Mto Nile ambalo limekwenda mpaka Misri. Kwa misingi hii kama Serikali yetu iko makini, basi tatizo hili la maji lingekwishaondoka kwa muda mrefu, lakini kusema ni jambo moja na kutenda ni jambo lingine, hivyo maneno na maandishi yetu ni lazima yaandamane na matendo. Maneno matupu bila ya matendo hatufiki popote, ni lazima sasa basi utafiti utakaofanyika uwe wa kweli, wa wazi na wenze tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ichukue hatua za makusudi ili ihakikishe kwamba tatizo la maji kwa Watanzania mijini na vijijini limemalizika kwani si haki hata kidogo kuona baadhi ya Watanzania wanapoteza maisha yao kwa kushambuliwa na wanyama kwa sababu ya kufuata maji.

MHE. MESHACK J. OPULKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maendelezo ya kuridhisha katika bwawa la Meatu lilitoko Mwanjolo, Serikali pia itenye fedha kujenga mabwawa mengine kwenye Kata za Bukundi, Mwabuzo na Mwangudo ili kusaidia mifugo kwenye maeneo haya muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. Naomba nichangie Wizara hii kwa kutoa ushauri mbalimbali ili kuboresha utendaji na pia kuondoa urasimu katika Serikali yetu ili tupate huduma bora ya maji na kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nashauri mabonde yote yapatiwe vifaa zaidi ili waweze kufikia wananchi wengi zaidi kupima maji chini ya ardhi, ubora wa maji na pia mabonde yaweze kuwekwa katika mtandao (*website*) kwa hali halisi ya upatikanaji wa maji na taarifa ya ubora wa maji ambako utafiti umeshafanywa. Mabonde karibu yote yana hali mbaya katika bajeti na zana au vifaa vyia kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hivyo kwa sababu Babati Vijijini, Tarafa ya Mbogwe kwa mfano, eneo la Kata ya Nkaiti na Mwada maji ya chini ya chumvi (*saline*) na *fluorine* kwa kiwango cha juu sana ambapo haifai kunywa kwa binadamu wala mifugo, lakini pamoja na kuwa na taarifa hiyo iliyofanywa miaka ya nyuma bado fedha ya kuchimba maji ya chini hupangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) na ushuru wa forodha (*customs duty*) na kodi yoyote katika madawa ya kutibu maji yaondolewe, kuna baadhi ya Halmashauri

zimesamehewa na nyingi hutozwa na kusababisha kuongeza gharama ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri kwa baadhi ya maeneo ambako hakuna maji ya chini na hakuna chanzo kingine jirani, maeneo hayo yangechimbwa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua. Elimu juu ya technolojia ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua katika majengo yetu pia iendelezwe kwa kasi na pawe na sheria ya kuweka katika michoro ya ujenzi ya nyumba pawe na mfumo wa kuvuna maji na hasa katika majengo ya umma (shule, hospitali, maghala na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia Serikali iangalie kuondoa kodi zote katika mitambo ya kuchimba malambo na mabwawa na mitaro ya maji iondolewe mfano, (*Buldozer, excavator, loader*) mitambo mbalimbali ambayo itasaidia kuchimba mabwawa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kupungua maji ambayo ni uhai wa maisha, kupungua mwaka hadi mwaka ni uharibifu wa mazingira, Serikali imeweza kuona pale lhefu, baada ya kuondoa mifugo na kuboresha mazingira, lhefu maji yameongezeka. Wizara hii haina mamlaka na mazingira, Serikali ingeweka mkakati wa kuunganisha Wizara zote husika ili tuboreshe mazingira ili tutunze vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni wataalam kuamua bila kushirikisha wadau wengine kubuni miradi ya maji na kuongeza kero na ugomvi badala ya

kushirikisha wadau wote na watumia maji wote katika eneo husika kama sheria inavyotaka, mfano mzuri ni Babati Vijijini, mradi wa maji kutoka Darakuta kwenda Minjingu. Chanzo cha Darakuta kina watumia maji wengi na hakuna elimu wala ushirikishwaji uliofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wamesikia mradi upo na wameanza kulalamika kwa sababu wao bila huu mradi wanatumia maji kwa zamu na Mji Mdogo wa Magugu na Vijiji vya Matuta, Mawemiro, Sarawe vyote havina maji safi na salama na wanategemea chanzo hicho hicho. Kuna chanzo kingine cha Mto Magara ambacho hakina watumia maji wengi, ni Kijiji kimoja tu na ni karibu zaidi na yakichukuliwa hapo Magara vijiji vingi zaidi ambavyo havina maji pamoja na shule ya Sekondari ya Ubugwe watapata maji na kupunguza mgogoro katika chanzo cha Darakuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kuanzisha Mamlaka za Maji, elimu ya kutosha haitolewi na kuanzisha mgogoro kama kule Kata ya Galapo (Gawasa), Kata ya Ufana (Lwamanda) na Nar. Tumeanzisha Mamlaka za Maji lakini elimu ya kutosha haikutolewa na kumekuwa na migogoro. Tuangalie upya mfumo mzima wa uendeshaji na upatikanaji wa maji ili kero ndogo ndogo zitatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina bahati ya kuwa na maziwa na mito mikubwa mingi pamoja na vyanzo vidogo vidogo, lakini asilimia kubwa ya Watanzania hawana maji safi na salama. Tunaomba Serikali ikubali kushirikiana na sekta binafsi (*PPP*) kupata mawazo na kuboresha mazingira, kuanzisha viwanda

vya kuzalisha pampu za kuchota maji chini ya ardhi. Tunaamini Wizara inaweza kusaidia kupata ufumbuzi wa tatizo la maji, lakini kuna baadhi ya watu ndani ya Serikali yetu bado wanatakiwa kubadilisha mfumo wao wa kufikiri (*mind set change*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri na Naibu Waziri, ni watu wenyewe sifa na wachapa kazi pia ngazi ya Wizara wanaonesha ushirikiano mkubwa, ni Wizara tofauti yaani ya fedha ndiyo huwa chanzo cha matatizo katika sekta nyingi hasa maji, kilimo, mifugo, viwanda na biashara. Hawako tayari kufikiria na kupata mawazo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ikubali kukaa na wadau mbalimbali nchini hasa Babati Vijijini wapate mawazo yao ya namna ya kutatua matatizo ya maji safi na salama. Naamini mtakubali ushauri wetu ili tuweze kuboresha na kupata ufumbuzi wa maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa hotuba ya Waziri wa Maji, bila kuwasahau Naibu Waziri pamoja na watumishi wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2012/2013, Wizara imetengewa fedha kiasi cha sh. 485,898,613,000 ni bajeti kwa ajili ya maendeleo, ambapo kati ya hizo sh. 140,015,967,000, ni fedha za ndani. Kwa usoefu wa miradi mingi inayoendelea

mara nyingi miradi inayotekelizwa kwa fedha kutoka nje mara nyingi haitekelezeki. Sasa basi kwa fedha kidogo zilizotengwa za ndani kwa maoni yangu ndizo fedha ambazo tunategemea zaidi kuliko zile fedha tunazotegemea kutoka nje. Ndiyo maana miradi mingi inayofadhiliwa kutoka nje inasuasua sana, mfano miradi ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia utekelezaji wake unasuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Geita Vijiji Kumi vinavyofadhiliwa na Benki ya Dunia ni kero kubwa sana kwa wananchi hasa wanaosubiri maji kutokana na mradi huu. Niombe Wizara iangalie namna ya kuharakisha ukamilishaji wa mradi huu. Mradi huu ni wa muda mrefu sasa, mara kwa mara wananchi wanaulizia kuhusu mradi huu. Naomba katika majumuisho nipate maelezo ya kutosha namna ya ukamilishaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nipendekeze kwamba, katika bajeti zijazo bajeti kwa ajili ya maendeleo zitengewe fedha kutoka vyanzo vya ndani, kuliko hivi sasa bajeti ya maendeleo inavyotegemea vyanzo kutoka nje, matokeo yake miradi inasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali iweke kipaumbele katika upatikanaji wa maji vijijini. Vijiji vingi vya Tanzania vina matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji. Mara nyingi nguvu kubwa zimeelekezwa mijini zaidi kuliko vijijini. Vijijini ndiko kwenye Watanzania walio wengi. Naomba Serikali kupita Wizara hii ianze kuelekeza nguvu kubwa vijijini katika Jimbo la Busanda, Geita kuna vijiji ambavyo vina

keru kubwa sana ya maji. Kwa kuvitaja tu ni Vijiji vya Kata ya Nyamalimbe, Bujura, Busanda, Nyakamwaga, Nyarugusu na Nyamigota. Hizi Kata hazimo kwenye mpango wa Mradi wa Benki ya Dunia. Wananchi hawa wanahangaika sana kwa vile Wilaya ya Geita tumezungukwa na Ziwa Victoria, tunaomba mradi kabambe wa maji ya kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu naamini inawezekana kwa sababu maji kutoka Ziwa Victoria yamepelekwa Mkoa wa Shinyanga umbali wa zaidi ya kilomita 200. Geita ambapo umbali ni mfupi zaidi kilomita 20 tu, naamini Serikali ikiamua kuwekeza nina uhakika suala la maji Geita litakuwa historia. Kwa maelezo haya naomba Serikali iwekeze mradi kabambe wa maji ya Ziwa Victoria ili wananchi wa Geita wanufaike na rasilimali maji ambayo Mwenyezi Mungu ametuwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nikiamini kwamba mapendekezo yangu na hoja zangu zitafanyiwa kazi na Serikali ili kuondokana na tatizo la maji Geita.

MHE. BENEDICT N. OLE NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam, kwa kuandaa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada na msaada katika

kushughulikia tatizo kubwa la maji linaloukabili Mji wa Kibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Mji wa Kibaya iwezeshwe kuimarishwa kwa kupatiwa wataalam, fedha na nyenzo ili waweze kumudu tatizo kubwa na sugu la maji Kibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Visima vya Maji vilivyochimbwa na Wamisri na kupata maji mengi, vijengewe miundombinu ili wananchi waweze kutumia na kunufaika na huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maji ya *World Bank* iliyojengewa miundombinu ya mabomba kutandazwa na matenki kujengwa lakini maji yalikosekana baada ya kujaribu kuchimba. Vyanzo vingine vitafutwe au vichimbwe ili miundombinu hiyo itumike na watu na mifugo kunufaika na huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa Miradi ya Maji itakayofadhiliwa na Wamisri, pamoja na kuchimba visima, kufunga *engine* na *pump* kama walivyofanya hapo nyuma, wajenge pia matenki.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi leo hii. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu, bila ya maji hakuna maisha. Ni vyema kuzingatia kwa makini mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo visima mbalimbali vimechimbwa kwa matumizi ya wanadamu, ni vyema Wizara iwe angalifu sana kwa kuweka dawa maji ya matumizi ya binadamu ili kulinda afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kwamba, vipo baadhi ya vijji hadi sasa wanatumia maji ya mito na visima vidogo na hivyo kupata maji machafu. Hali hii ndiyo inayosababisha madhara kwa afya za wananchi; kwa hiyo, ni vyema kuhakikisha kwanza Wizara inaangalia maeneo sugu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vyta maji ni muhimu sana, lazima Wizara ivilinde vyanzo hivyo ili kunusuru hali ya upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ye yeyote anayeweza kuishi bila ya maji, wakati umefika sasa kwa Serikali kupitia Wizara ya Maji, itoe kaulimbiu kuondoa tatizo la maji kwa wananchi wote. Lazima Serikali ione swala hili linapewa kipaumbele kuliko vyote na ni vyema likapangiwa Bajeti kubwa ili kuondokana na tatizo hili kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. SEIF SELEMAN RASHID: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza uwasilishaji wa Hoja ya Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara

ya Maji. Pamoja na kutambua uwekezaji wa Serikali na Wadau katika kutatua changamoto ya maji katika maeneo yote nchini. Ninaomba nichangie katika Hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iondokane na utekelezaji wa Miradi midogo midogo mingi katika vijiji vingi na hivyo kupunguza uwezekano wa kuondoa tatizo la maji kwa kushindwa kupatikana au kutunza vyanzo vya maji, kushindwa kufanya kazi kwa mashine ambazo ni nyingi, mzigo mkubwa wa uendeshaji wa vyanzo vingi na mahitaji ya nguvu kazi au rasilimali watu kuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kuwa iwepo Miradi mikubwa yenye uwezo wa kuwafikia watu wengi waishio katika vijiji vingi kama ilivyo Mradi wa *Handeni Main Trunk*, Mradi wa Chalinze na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ianze kutekeleza hilo katika Wilaya ya Rufiji kwa kuongeza nguvu ya ujenzi wa tenki kubwa pale Mkongo, Kata ya Mkongo, ambapo kuna kisima kizuri, chenye uwezo mkubwa wa kutoa maji ili Mradi huu uunganishwe na Mradi wa Ikwiriri ili maji hayo yaweze kuwafikia wakazi wengi kuanzia Ikwiriri kuelekea Mkonga hadi Mloka. Mradi huu kwa gharama ya usambazaji tu utafikisha maji katika vijiji 20 na watu wanaozidi 60,000 na hivyo kupunguza gharama za kuendelea kusimamia visima vingi vinavyokufa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watu wanaopata tabu ya maji, basi ni watu wa Nyaukonje, Namkono na Kongowe, Kata ya Utete na Ngarambe, Jimbo la Rufiji. Pamoja na juhudzi za kuwapatia maji vijiji hivi, bado changamoto ya kwanza ni gharama kubwa za *survey* za mamlaka ya uchimbaji wa visima na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka hii ni lazima ipewe ruzuku ili iweze kutoa huduma zao katika Halmashauri kwa bei ya chini kuliko ilivyo sasa. Pamoja na mchango wa Mfuko wa Jimbo kuwekeza kwenye vijiji hivyo, bado vijij hivyo havijapata maji kwa sababu ya kuchelewa utekelezaji, uzembe wa baadhi ya watendaji na kuweka gharama zilizo juu kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni mfano ambao ni matumaini yangu kuwa, Serikali itaangalia upya ili vijiji nilivyovitaja viunganishwe na Mradi mkubwa wa Maji uliokamilika wa Mji wa Utete kwa kuongeza gharama za usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba Serikali iendelee kuiangalia Rufiji kwa kukamilisha Miradi, ikiwa ni pamoja na Mradi wa Ikwiriri na kuona uwezekano wa kuufanya uwe mkubwa zaidi kwa kufikisha maji kwa vijiji 20 katika umbali wa chini ya kilomita 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri, anawasilisha

Makadirio ya Bajeti ya Wizara yake, nitaomba aongelee kuhusu Mradi wa Maji Kimbiji na suala la fidia ya eneo hilo. Vile vile ninakumbushia majibu ya barua niliyomwandikia juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mradi wa Benki ya Dunia, kiwango cha kuchangia mia kwa mia kinachotakiwa kutolewa na *beneficiaries* kinaonekana kuwa mzigo wa kukwamisha Miradi katika baadhi ya maeneo. Pendelezo na ushauri, Wizara ishirikiane na Halmashauri za Wilaya husika ili kuwakopesha (vijiji), wahusika na hatimaye kutumia mfumo wa makato kutoekana na ushuru wa mazao na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi mingi imeonekana kuharibika miundombinu na hatimaye kufa kabisa kwa kukosekana usimamizi, matumizi sahihi na matunzo. Ninaishauri Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri husika, ishirikishe vijiji na kupata vijana watakaopewa mafunzo katika ngazi ya ufundu sanifu au stadi ili mafundi hao wa vijiji wapewe na kubeba dhamana ya uendelevu (*sustainability*) ya mitambo na miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji ya Mji wa Tunduru, haifanyi kazi inavyopaswa. Imerithishwa mfumo (*network*) ya maji na miundombinu yake ya mwaka 1953 na ilivyo chakavu kiasi cha kuwa imeoza kabisa na haipo, haipewi fedha za kujiendesha na

haikupewa mtaji wakati inaanzishwa ili iweze kusimama na kujitegemea; je, itawezeshwa lini?

Serikali ina mipango gani ya kuiwezesha Mamlaka hiyo ili iweze kumudu changamoto na majukumu yake? Mamlaka ina mfanyakazi mmoja pekee atafanyaje kazi? Mamlaka imekuwa sehemu tu ya Idara ya Maji ya Halmashauri, haina vitendea kazi, fedha, wafanyakazi, itawezaje kutekeleza majukumu ya kuundwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha Mradi wa *World Bank* ambao kila mmoja anafahamu kwamba unatekelezwa taratibu na kwa muda mrefu sana; Vijiji vya Wilaya ya Tunduru hususan Jimbo la Tunduru Kaskazini, havina maji wala hakuna Miradi yoyote yenye matumaini katika siku za usoni za hivi karibuni.

Je ni lini Serikali (Wizara) itaingiza Vijiji vya Tunduru Kaskazini angalau Makao Makuu ya Tarafa na Kata ili vipate maji *at least* visima vya uhakika?

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Idara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma umejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji, ikiwa ni pamoja na Ziwa Tanganyika, Mto Malagarasi, Mto

Rwiche na Mito mingine midogo midogo lakini maji Kigoma ni ya shida. Naiomba Serikali itusaidie tumalize tatizo hili la maji Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Kasulu maji hayatoshelezi; Vijiji vya Kasulu havina maji. Mji wa Kibondo upo Mlimani, hivyo maji ni ya shida, tunaomba Serikali iweke miundombinu kuweza kumaliza tatizo hili la maji kusudi wanawake waweze kupata unafuu wa kutafuta maji kutwa nzima, huku shughuli za uzalishaji mali zikiwa zimesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yaliyopo katika Ziwa Tanganyika na kwenye Mito, yanaweza kutumika katika kilimo cha umwagiliaji. Tunaomba Serikali iweke miundombinu ili maji hayo yaweze kuchochea uchumi ndani ya Mkoa wa Kigoma na Mikoa jirani ya Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuchangia kama ifuatavyo:-

Lipo tatizo kubwa sana la ukosefu wa maji kwa matumizi ya binadamu katika makazi yao. Hatua zinazochukuliwa na Serikali za kutegemea Banki ya Dunia, haziwezi kuleta utatuzi wa kumaliza tatizo hilo. Serikali inatakiwa itenye fedha za kutosha ili kukabiliana na tatizo hili; kwa mfano, Jimbo langu la Kwela lina matatizo makubwa sana ya kukosekana kwa maji. Nataka kujua nini kinachoendelea katika

maeneo yafuatayo: Mji Mdogo wa Laela, ni Mji Mdogo unaokuwa kwa kasi kubwa. Hata hivyo ni Mji ambao umependekezwa kuwa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya Sumbawanga Vijijini. Mji huu una shida kubwa sana ya maji, naomba Serikali inieleze ni lini itatatua tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Laela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vingine ambavyo vilikuwa katika Mpango wa Benki ya Duniani vyta Nankanga, Kilyamatundu na maeneo mengine; ni lini Serikali itatatua tatizo la maji katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ahadi za Viongozi hazitekelezwi kwa mfano, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kumaliza tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Laela katika Uchaguzi wa 2010; ni lini ahadi hii itatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo ahadi iliyotolewa na aliyekuwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya ya kuwapelekea Wananchi wa Kijiji cha Sakalilo maji ya mtiririko toka mwaka 2008; je, ahadi hii itatekelezwa lini? Naomba maelezo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri nitaunga mkono hoja.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni tatizo kubwa katika nchi yetu na kipaumbele cha kwanza kwa watu wa nchi hii, lakini fedha ambazo zinatengwa kwenye bajeti hazizingatii hilo; inasikitisha sana. Tatizo la maji lipo kila eneo katika nchi hii na

kupishana tu kwa kiwango cha tatizo, kadhalika maji yanaendelea kupungua katika sura ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujua uwepo wa tatizo hili, lakini kama nchi hakuna juhudzi za makusudi zinazoonekana za kukabiliana na tatizo hili la kuhifadhi na kulinda maji yaliyopo. Maelfu ya lita kama siyo mamilioni yanapotea kwa sababu tumeshindwa kuwa na mipango ya kuvuna maji ya mvua. Hivyo basi, sasa Serikali ijielekeze katika kutoa elimu na utaalamu ili wananchi waanze kuvuna maji ya mvua kwa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, kama Taifa hivi sasa tunahitaji kujua akiba ya maji tuliyonayo chini ya ardhi na wapi maji hayo yapo na kiasi gani badala ya njia inayotumika sasa ya kuchimba visima mahali ambapo maji hakuna na kupoteza fedha nyingi. Hivyo basi, utafiti wa kutosha ufanywe na kujua hali ikoje ya akiba ya maji chini ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpanda tuna matatizo pia kuhusu maji safi na salama na miundombinu ya usafirishaji maji katika Mji wa Mpanda. Mradi wa Ikorongo unasuasua na ni chanzo pekee ambacho kitamaliza kabisa tatizo la maji Mpanda Mjini. Liwepo chujio katika vyanzo vya maji Milala, Manga na pia watakapojenga kwenye chanzo cha Ikolongo. Ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji Shamwe kutoka katika chanzo cha Milala ukamilishwe. Naomba pia Wizara isaidie juhudzi za Mamlaka ya Maji Mpanda, iweze kukamilisha Miradi yake na hasa katika kusambaza maji kwenye maeneo ya makazi katika Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mpanda Mjini lina Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Kata ya Kakese ina Vijiji vitano na Vitongoji zaidi ya 25 na eneo hilo lina tatizo kubwa la maji, hakuna visima vya kutosha. Idadi ya wakazi ni kubwa sana hata katika Mpango wa Visima Vijijini. Kata hii haikuwemo katika Mpango wa Halmashauri ya Wilaya Mpanda na kwa sasa Kata hiyo ipo katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda. Naomba katika Programu ya Visima inayoendelea hivi sasa, Kata hii ifikiriwe kupata visima vya maji, ukizingatia mchango wa Kata hii katika uzalishaji wa chakula (mpunga).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kukamilisha Mradi mkubwa wa kuupatia Mji Mdogo wa Mpwapwa maji safi. Mradi huu umetekelizwa na kukamilika kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Ufaransa. Hata hivyo, Mradi huu bado haujazinduliwa au kufunguliwa rasmi na Serikali. Ahadi iliyopo ni kwamba, Mheshimiwa Rais amekubali kuuzindua Mradi huu. Je, ni lini uzinduzi huu utafanyika?

Je, ni lini Bodi ya Mamlaka hii ya Maji itaundwa ili kuwa na Chombo cha Usimamizi na Uongozi wa Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Mpwapwa?

Je, Wizara ina mpango gani wa kufufua Bwawa la Maji la Kimagai ambalo kwa muda mrefu limefunkwa na tope na udongo kiasi cha kupotea kabisa. Miaka ya nyuma Bwawa hili lilikuwa linatumika kuwapatia

wananchi maji kwa matumizi yao na maendeleo kwa ujumla.

Uchimbaji wa Visima virefu vyatia maji katika vijiji kadhaa vilivyopendekezwa bado unasuasua; sehemu kubwa ya vijiji vilivyopendekezwa havijapata maji kwa utaratibu na msaada wa *World Bank Programme*. Je, Wizara imejipanga vipi kwa Mwaka huu wa Fedha wa 2012/2013 kuvipatia maji Vijiji vya Jimbo la Mpwapwa vilivyopendekezwa chini ya Mradi wa *World Bank*?

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na *Team* yote ya Watendaji, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya bajeti finyu. Maji ni uhai. Ipo changamoto kubwa sana ya kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, fedha ndogo ambayo Wizara inapewa, igawanywe kwa usawa katika Wilaya zote za nchi hii kwa kuwa maji ni uhai kwa wananchi wote. Hii ni pamoja na fedha zinazotolewa na wafadhili. Ushauri wangu wa pili ni kuhusu Wataalam wa Maji katika Halmashauri mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara; Wizara ya Maji haina budi kufuatilia kwa karibu sana utendaji kazi wa wataalam hawa, yaani uwajibikaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji wa Wataalam wa Maji katika Halmashauri ya Ngara ni wa mashaka sana. Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya

anashindwa kuwasimamia kikamilifu kwa sababu hana utaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara ni yenye milima na mabonde, ina vijiji 73 na karibu vyote havina maji safi na salama.

Kwa muda mrefu Wananchi wa Ngara wamekuwa wakisikia kwamba, Benki ya Dunia itatoa fedha kwa ajili ya miundombinu ya maji katika vijiji 13 ukiwemo Mji Mdogo wa Rulenge. Hivi karibuni Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Naibu Waziri wa Maji, alinieleza kwamba ni vijiji viwili tu ambavyo vipo kwenye Orodha ya Benki ya Dunia kama Rulenge na Ngundusi. Vijiji hivyo pia havijafikia hatua ya kutangaza zabuni. Nimesikitika kuona katika Mkoa wa Kagera ni Wilaya za Biharamulo na Bukoba, Karagwe na Manispaa ya Bukoba tu ndiyo ambazo zimepiga hatua ya kupatiwa maji katika vijiji kumi. Ngara haimo katika orodha hiyo. Mgawanyo wa namna hii ndiyo unaonifanya nisononeke kwa kufikiria kwamba, kuna upendeleo katika matumizi ya fedha za Benki ya Dunia. Nakuomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, muingilie kati ili Ngara ipewe maji ya Benki ya Dunia katika vijiji kumi viliwyokwisha pangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba pia Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, wahakikishe Mji Mdogo wa Rulenge, wenyewe wakazi wengi na unaokua haraka sana, unapata maji haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kunieleza kwamba, Kijiji cha Rulenge kimetengewa shilingi zaidi ya milioni mia sita. Wasiwasi wangu ni kwa *Engineer* wa Maji wa Halmashauri, Ndugu Rwegasira, kuniletea taarifa kwamba, fedha zilizopo kwenye *account* kwa ajili ya maji ya Rulenge ni shilingi milioni mia tatu na siyo milioni mia sita. Hili ni jambo la ajabu. Naiomba Wizara ichunguze suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi, kutokana na jiografia ya Ngara ya milima na mabonde, akina mama wanateseka kwa kubeba maji kichwani kwa zaidi ya kilomita tatu kwa kuteremka na kupanda milima.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia njema tu naomba kujua kwenye *Development Budget, Item 3216, Sub-Vote 4001 - Rural Water Supply - Expansion and Rehabilitation of Water Supply*; Mradi wa Makonde umetengewa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na kumtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na *Team* yake yote, kwa kuandaa Hotuba nzuri, yenye takwimu na taarifa ya kina ya utekelezaji na maoteo ya mwaka 2012/2013. Naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Miradi ya Mabwawa: Serikali imeendelea kujenga mabwawa kama vyanzo vya maji kwa matumizi mbalimbali na zaidi kwa matumizi ya binadamu na mifugo. Katika michango yangu kwa Wizara, nimesisitiza mara nyingi upotevu wa fedha kujenga bwawa bila kujenga miundombinu ya kusafisha na kusambaza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ya utaratibu huu ipo katika Wilaya yangu ya Bariadi. Bwawa la Bariadi lilijengwa miaka zaidi ya miaka 20 na sasa limekauka bila kutoa huduma iliyokusudiwa kwani miundombinu ya kusambaza maji haikujengwa na chujio limekamilika baada ya bwawa kukauka. Mfano mwingine ni Bwawa la Nkoma lililofunguliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipoanza awamu yake mpaka leo hakuna miundombinu ya kusafisha na kusambaza maji. Aidha, nimeomba Shirika la Umeme Vijiji lilete umeme mpaka kwenye Bwawa hili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifungua Kituo cha Afya Nkoma ambacho kitatumika kama Hospitali ya Wilaya mpya Itilima na kuahidi bwawa hili litaanza kutumika kama ilivyokusudiwa mwaka huu. Aidha, huenda yale yale yatatokea kwa Bwawa la Hubiya. Naomba Sera ya Kujenga Bwawa halafu kuachia Halmashauri irejewe kwani haya ni maamuzi yasiyo na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi juu ya kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa miji. Moja ya changamoto ni kero ya kukata maji kwa watumiaji. Kwa kuwa kuna teknolojia ya Luku, basi Luku zipatikiane katika mamlaka zote ili kero hii iweze

kutoweka kwa kiwango kikubwa. Aidha kuna mtindo umezuka kwa Taasisi za Serikali, Majeshi, kukataa kulipia maji na kwa kutumia vitisho vya Uongozi wa Mikoa pale maji yanapokatwa. Mheshimiwa atamke wazi kwamba kila taasisi inawajibika kulipa la sivyo maji yatakawta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kazi za Wizara hii, lakini fedha zaidi za ndani zilengwe na kutolewa kwa muda mara mwaka wa bajeti unapoanza na siyo kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Bwawa la Nkoma, naomba Mheshimiwa Waziri, awaeleze watu wa Itilima ni mpango gani uliopo ili maji haya yatumike kama ilivyopangwa. Aidha, Sera hii ya kujenga mabwawa bila miundombimu ya kuchuja na kusambaza itarejewa ili Mradi kamili uweze kujengwa na miundombinu ya kusafishwa na kusambaza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoelekeza katika Kamati ya *PAC*, Wizara hii ni muhimu sana kwa maisha ya watu wetu. Kutegemea fedha za nje ambazo hazina uhakika, miaka mingi ya ukaguzi wa Wizara hii fedha inayoahidiwa kutoka nje haipatikani. Hali hii lazima igeuke kama dhamira ya Serikali ya kutoa maji safi kwa wengi itatekelezeka. Njia ni kwa Serikali kutoa fedha za ndani na za nje tu zenye uhakika.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Timu yake yote ya

Wizara ya Maji, kwa hotuba yake nzuri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa Wilaya zilizoanzishwa na Mheshimiwa Rais Kikwete kwa mwaka huu, imo Wilaya ya Kaliua inayozingatia mipaka ya Jimbo la Urambo Magharibi. Eneo hili lina ukame sana kuhusu maji chini ya ardhi japo tuna mvua za kutosha. Eneo halina mito ya kudumu wala maziwa kutokana na hali hiyo, tunalo tatizo kubwa sana la maji ya kunywa. Mara nyingi tumepata wafadhili wa kutusaidia kutuchimbia visima lakini hawapati maji. Cha kusikitisha zaidi ni pale tulipopata Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia kwa vijiji kadhaa vya Wilaya ya Kaliua. Tulikadiriwa kupewa visima 15 lakini kwa masharti kwamba kila kijiji kichangie shilingi milioni tano.

Vijiji vya Kaliua Mashariki, Kaliua Magharibi na Ushokola ambavyo kwa ujumla wao ndiyo vinaunda Makao Makuu ya Wilaya, vilikuwa mionganoni mwa vijiji hivyo. Wananchi tulichangisha na tukatimiza hizo milioni tano kwa kila kijiji jumla shilingi milioni 15 ili tupate shilingi milioni 600 toka Benki ya Dunia. Tulipata *surveyor* wa maji toka Mkoani Tabora akaja kupima na kuelekeza mahali ambapo maji yatapatikana. Kampuni ya kuchimba visima ikaja kuchimba, kwa bahati mbaya visima tisa kati ya 12 vilivyocheinwa vilikuwa havina maji katika vijiji hivi. Kwa Vijiji vya Kaliua Mashariki, Kaliua Magharibi na Ushokola ni kisima kimoja tu ndiyo kilipatikana na maji. Kwa hiyo, vijiji hivi havina maji mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wanaauliza maswali yafuatayo:-

- (a) Katika hali kama hii mwenye kosa ni nani? Wao si Wataalam wa Maji, wameambiwa wachange wamechanga tena kwa shida sana. Leo wanaambulia mashimo tu.
- (b) Hasara hii aibebe nani?
- (c) Lini watapata maji?
- (d) Je, fedha yao watarudishiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Wizara, kwa Mkoa wa Tabora na hususan kwa Wilaya ya Kaliua, iletu Wataalam wa Maji waliobobe idara yao ya Upimaji Maji waje wafanye uchunguzi wa kina waoneshe miamba ya maji inapita wapi ili wachimba visima wa baadaye wasirudie makosa kama haya. Pia naishauri na nazidi kuiomba Serikali, iwafidie wananchi wa Kaliua Mashariki, Kaliua Magharibi na Ushokola, shilingi milioni 600 na Serikali izirejeshe hizi kujenga bwawa kubwa la maji ya kunywa pale Kaliua. Kutokana na mvua tunazopata, nina hakika bwawa hili litajaa kwa mvua za miaka miwili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitatu iliyopita, Serikali iliahidi Wananchi wa Kijiji cha Uliwanoni na King'wangoko mabwawa, kila kijiji bwawa moja. Cha kushangaza, mpaka leo Bwawa la Ulindwanoni halijapewa fedha kabisa ambazo zimekuwa zikitengwa

kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji. Ni shilingi milioni 500 mpaka leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha King'wangoko kilikadiriwa shilingi milioni 700, zikapelekwa shilingi milioni 350 ambazo zimehifadhiwa mpaka leo. Uchimbaji wa Bwawa la King'wangoko umesitishwa mpaka hapo mgogoro wa Hifadhi ya Misitu utakapomalizika. Huu ni uonevu; kwa nini fedha hizi zisiruhusiwe kuanza uchimbaji wa Bwawa hili la King'wangoko uendelee hata kama huko mbele ya safari itaonekana kuwa kijiji kihame kwa sababu kipo ndani ya Hifadhi ya Msitu; si maji yatabaki na wanyama watatumia? Tusingahau kuwa bwawa kubwa pia huwa lina taathira chanya kwenye tabia nchi hususan mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali izingatie ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba nzuri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ni kubwa kuliko tunavyofikiria na hasa vijijini, vijiji vingi havina huduma ya maji ya uhakika na hii inatokana na sababu nyingi. Vipo vijiji Miradi ya Maji ilijengwa zaidi ya miaka 30 iliyopita, lakini kwa kuwa haukuwepo mfumo endelevu wa kuikarabati, sehemu kubwa ni

chakavu na hivyo maji mengi kupotea. Naishauri ifanyike *inventory* upya kwa kila kijiji ili kujua ni watu wangapi wamepata huduma ya maji. Vipo vijiji vingi sidhani kama vitafikiwa na Mradi huu wa Benki ya Dunia ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii ilete Mpango Maalum wa kuvipatia maji vijiji vyote, huduma ya maji safi hata ikiwezekana na hasa vijiji vile ambavyo havina maji kabisa wachimbiwe angalau visima hata vya mkono au vipewe bwawa au mradi wa mtiririko pale unapowezekana ili ahadi ya llani ya uchaguzi ya kufikia asilimia 75 iweze kufikiwa. Hatutaweza kufikia lengo hili bila kuongeza bajeti ya ndani kwa kazi hiyo. Wafadhili wetu ni kweli wanatusaidia lakini wao hawana hiyo *target* ya asilimia 75 na ukichukulia m dororo wa uchumi ni dhahiri malengo yetu yanahitaji "Mpango Maalum 2015."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Waging'ombe, Vijiji vyote vya Kata ya Saja na Kijombe havina maji kabisa, navyo ni Saja, Isimile, Itengelo, Ukulinyambo, Uhenga na Igombe. Kata ya Kijombe isiyo na maji kabisa ni Lyadebwe, Lyamluki, Ukwavila, Kijimbe. Kata ya Waging'ombe ni Mayale, Kitange B. Kata ya Induga ni Iyayi na Mji Mdogo wa Illembula, imejengwa Hospitali ya Rufaa na imekua kwa kasi kabisa na kusababisha huduma ya maji kudorora sana. Naomba Mheshimiwa Waziri, asaidie sana Mradi wa Waging'ombe ufanyiwe mkakati mkubwa kabla ya 2015 na pia Mji Mdogo wa Igwachanya ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Waging'ombe, utahitaji kupanua huduma hii muhimu ya maji.

Kuhusu kutunza vyanzo vya maji, nashauri Kanuni za Sheria Namba 11 ya 2009 kuhusu rasilimali za maji itolewe haraka ili Sheria hii iweze kulinda uharibifu wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtindo wa kuendelea kuruhusu wananchi kuhama ndani ya mita 60 kutoka vyanzo vya maji, nchi yetu itakauka.

Ujenzi wa mabwawa na teknolojia ya uvunaji maji ya mvua, tutilie mkazo na kila mwaka iwepo Bajeti Maalum ya eneo hili kila kila Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapo jumuisha bajeti yake, anieleze namna atakavyonisa idia kutatua tatizo la maji katika vijiji nilivyovielezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie mchango wangu kwa kumshukuru sana Waziri wa Maji, kwa kunipongeza kwa utendaji wangu mzuri nilipokuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji. Namtakia kila la kheri na ari ili Sekta hii muhimu ituongezee kura za CCM tutakapofika 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mradi wa KKKT Njombe kupeleka maji Kidugala wamepungukiwa shilingi milioni 100 ili wasaidie vijiji vitatu ambapo bomba hilo litapita. Naomba sana Mheshimiwa Waziri asaidie tupate fedha hizo ili Mradi huo pamoja na kupelekea maji Kidugala Mission, vijiji ambavyo balaa hili limepitia, waweze kupatiwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii ipite ili pamoja na mengine, maombi yangu yaweze kutekelezwa.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Hotuba nzuri na ya kina iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maji. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wakurugenzi wote wa Wizara na Viongozi wote Wakuu wa Wizara na Maafisa Wakuu wa Mashirika chini ya Wizara ya Maji.

Napenda kuwapongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Maji Bungeni na Kambi ya Upinzani. Ninapenda kuchangia suala la uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imebahatika kuwa na mvua fupi na ndefu katika maeneo mengi ya nchi katika vipindi mbalimbali. Vilevile katika majira ya mvua, mvua hunyesha nyingi ya kutosha, lakini maji mengi huishia ardhini ama kwenye mito ambayo mwisho wake huishia baharini ama katika Maziwa. Napenda kutoa rai kwa Wizara kuongeza nguvu kwa kuwa na Miradi mingi zaidi ya kuvuna maji ya mvua hasa katika maeneo yenye vipindi vifupi vyta mvua na yanayokabiliwa na ukame wa muda mrefu hasa maeneo ya Mikoa ya Kati ya nchi Kaskazini, Mashariki na kwingineko, maeneo haya hususan ya vijiji ni wawekewe Kampuni Maalum ya Miradi ya Uvunaji Maji ili kuwawezesha wananchi hususan wanawake kupunguziwa adha ya kutafuta maji, kuwzesha

maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa mifugo ya wanyama wadogo wadogo kama sungura, mbuzi, kuku na nguruwe ambao wangechangia sana katika biashara na lishe kwa jamii nyingi vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji maji ni teknolojia inayofundisha wananchi na kuwafanya washiriki nguvu kazi yao kujenga. Vile vile uvunaji maji utaboresha afya ya wananchi kuepuka magonjwa yanayotokana na uchafu. Uvunaji maji utasaidia kuondoa umaskini na utachangia kwa kiasi kikubwa katika utunzaji mazingira hasa yanapotumika kupanda miti ya matunda na ya vivuli na mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji mabwawa ya kufugia samaki na majosho ya kuoshea mifugo na kunyweshea mifugo ingesaidia sana kujenga ajira kwa vijana, huzuia wafugaji kuhamahama na vile vile kupunguza migogoro. Ninatoa rai kwa Wizara ya Maji, kushirikiana na TAMISEMI, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji ili kwa pamoja waone ni jinsi gani watashirikiana kusimamia uvunaji maji na kuboresha miundombinu mingine mbadala ya maji yanayotokana na maji ya mvua kama nilivyoainisha hapo juu. Wakitumia fursa ya mvua nyingi inayonyesha kila mara nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bwawa la Matwiga na Chunya ni mkubwa sana. Bwawa linachimbwa na kujengwa katika Kata ya Matwiga lakini likikamilika litaleta maji

katika Kata za Matwiga, Mtnila, Lupa na Mamba. Litasaidia sana kuondoa kero ya maji kwa wananchi wengi sana wanaoishi katika Kata hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuanzisha Mradi huu. Toka umeanza mwaka 2007 mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Alikuja mkandarasi mmoja na watu wake mwaka huo wa 2007, akachimba chimba tu na kuondoka. Mwaka 2008 akaletwa kandarasi mwingine na watu wake, naye akachimba chimba tu na kuondoka. Hivi kuna nini? Huu Mradi utaisha lini? Naiomba sana Serikali itimize ahadi yake na imalize Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Visima Vijiji Kumi kila Halmashauri ni mzuri sana na utapunguza kwa kiasi kikubwa adha ya wananchi kukosa maji. Mradi huu unasuasua muda mrefu sana tatizo ni nini? Wataalam tunao wa kutosha na fedha zipo toka Benki ya Dunia, naiomba Serikali itumie nguvu zake zote kukamilisha Mradi huu ili kabla ya mwaka 2015, Serikali ianzishe Mradi mwingine ili kupunguza matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake nzuri, kama itatekelezeka kwani bajeti yenye ni ndogo na mahitaji ya maji kwa Tanzania ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kila Mtanzania ana haki ya kupata maisha bora. Hii imekuwa ni Kaulimbiu ya Chama cha Mapinduzi katika harakati zake za kutafuta nafasi ya kukamata Dola, ila mara baada ya kufanikiwa kukamata Dola naona kauli imebaki kwenye fulana, kofia na mabango. Maji kama tujuavyo ni muhimu kwa maisha na shughuli mbalimbali za binadamu, ila kwa Tanzania maji yamekuwa hayapewi kipaumbele kama inavyotakiwa. Ukilinganisha bajeti hii ya Wizara utaona nini ninachomaanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana tukiwa tumesherehekea Miaka 50 ya Uhuru wa Taifa letu, Watanzania wengi sana hawana uhakika wa kupata maji safi na salama kwa ajili ya kunywa na matumizi mengine. Suala hili ni changamoto nzito kwa Taifa linalokua kwa kasi ya juu na kuwa na ongezeko la watu kutoka makadirio ya watu milioni nane mpaka milioni 45 kwa makadirio ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha kuna matatizo ya maji Tanzania toka Uhuru (1961) hadi hii leo ndiyo kilio kikubwa kwa Watanzania na wanawake ndiyo tunaokumbwa na adha ya maji kwa kiasi kikubwa na hasa vijijini na hata mijini hutumia muda mwingi kutafuta maji kuliko kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya 2025 ya Serikali ya Tanzania inalenga kufikisha kiwango cha upatikanaji wa maji kufikia asilimia 90, maeneo ya vijijini na asilimia mia kwa mia maeneo ya mijini ya idadi ya watu watakaopata maji salama ifiakapo mwaka 2025. Pia tuna mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na

Kupunguza Umaskini Awamu ya Pili (MKUKUTA II), unazingatia kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa maji kama moja au kipaumbele muhimu katika ajenda yake. Hofu yangu kubwa fungu la bajeti linalotengwa haliendani na Mpango Mkakati wa Wizara, hivyo kufikia malengo hayo tunahitaji nguvu za ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mkakati wake wa kujenga miundombinu na kusambaza maji katika vijiji vikiwemo vyta Wilaya ya Mkinga, Pangani na Kilindi. Kama kweli Serikali itatekeleza haya na siyo hadithi, italeta matumaini mapya kwa Watanzania waliokata tamaa katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Pangani karibu vijiji vyote wana matatizo makubwa sana ya maji, wanateseka sana hasa akina mama; tafadhalii sana, tunaomba Serikali itekeleze waliyoyatamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua unafahamu kuwa upatikanaji wa maji salama ni muhimu sana katika kupigana na umaskini na matatizo ya afya. Hivyo, ninaomba chonde chonde hivyo vijiji mlivyovipitisha katika Halmashauri zetu matatizo hayo ya maji yaondoke ili tusonge mbele kwenye vijiji vingine zaidi.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika

kuwahudumia Watanzania. Pamoja na pongezi hizo, ninayo maoni na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Kanda ya Kati ni kame, ina mvua kidogo na haina Mito wala Maziwa. Kwa hali hii Serikali inapaswa kutumia rasilimali nyingi kusaidia kutatua tatizo moja ambalo ndilo kubwa kuliko yote. Juhudi za Serikali zielekezwe katika kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa makubwa na madogo lakini hadi sasa jitihada za Serikali kutatua tatizo la maji haziridhishi. Kwa mfano, mgao wa fedha za Mfuko wa Pamoja na Programu ya Sekta ya Maji kwenye Halmashauri, Mkoa wa Singida wenyewe ukomo mkubwa umepangiwa shilingi 755,151,000, lakini ni kiwango cha chini kabisa kuliko mikoa yote. Hali hii siyo sahihi na inakatisha tamaa. Iweje mkoa wenyewe shida kubwa ya miji kuliko yote unatengewa fedha chache kuliko mikoa yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kintiku kipo katika Mradi wa Mkopo wa *World Bank*. Walipochimba maji hayakupatikana lakini katika eneo la mwinuko wa Mbwasa (*Saranda Escopment*), kuna visima vyenye maji zaidi ya vitatu havitumiki.

Tunaishauri Serikali ikubali kutumia visima hivyo ili maji hayo yawekewe miundombinu yapelekwe hadi Kintiku (km 20) na kwa kufanya hivyo, vijiji vya njiani; Mawezi, Mvumi na Chilejeho navyo vitapata maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Mpapa, Londoni na Chicheko vimo katika Mradi huu lakini fedha za

utekelezaji hazikutengwa. Je, vijiji ambavyo vimo katika Mpango huu lakini fedha hazikutengwa hatima yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Bwawa la Mbwasa (Manyoni) lina bonde kubwa ambapo mto unapita na iwapo mto utazibwa, litapatikana bwawa kubwa sana litakalotoa maji kwa ajili ya kunywa binadamu, mifugo na kilimo. Wataalam wa Bonde la Kati wamekagua na wameridhika, tunachoomba ni fedha za utekelezaji. *Tanzania-Japan Food Aid Counterpart Fund* wamechangia shilingi 200 milioni, lakini hawataki zitumike kwa *survey* na bila upembuzi ujenzi hautaanza. Ninaomba Wizara iliweke bwawa hili katika mipango yake ili fedha zipatikane zitatue tatizo la upembuzi ili kuwezesha fedha za Japani zitumike maana tayari zipo katika Akaunti za Halmashauri ya Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nasikitika kuna tatizo kubwa sana la maji Manispaa ya Kigoma. Tunalo Ziwa Tanganyika lakini maji hutoka kwenye mabomba mara moja kwa wiki na mara moja hiyo ni mzunguko wa ratiba ya mgao wa maji katika maeneo mbalimbali. Majibu ya Serikali toka Bunge la Tisa ilikuwa tatizo la umeme ambalo lilisababisha ishindikane kuwashaa *pump* ya kusukuma maji kutokea kwenye tanki kuu lakini sasa umeme siyo tatizo na maji bado ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia majibu ya Serikali yaliendelea kuwa mabomba ni chakavu, hivyo Serikali inarekebisha miundombinu ya mabomba ya maji, lakini mpaka leo bado maji ni tatizo. Pamoja na hayo, bei ya maji imepanda bila mpangilio kutoka shilingi 5,200 hadi shilingi 17,500, lakini sasa shilingi 19500 na sasa kupandisha ankara hadi shilingi 23,000 kwa mwezi. Maji yanatoka mara moja kwa wiki halafu bei inaongezwa, huduma hakuna bei juu!

Mheshimiwa Waziri, atuambie katika majibu yake kwa nini wameshindwa kulitumia Ziwa Tanganyika, Mto Mlalagarasi na vyanzo vingi vya maji vilivyopo ili kutatua matatizo yaliyopo Kigoma na nchi nzima kwani tuna vyanzo vingi sana vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itupe majibu mabomba ya Mchina kwa nini mpaka leo hayatoi maji Jijini Dar es Salaam wakati kazi hii ilitumia *USD* milioni 164.6? Chini ya Mradi huo wa *Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Project (DWSSP)*, nakubaliana na maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa, Mkaguzi Mkuu afanye *Special Audit* kwenye Mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nifahamu kwa nini kama chanzo cha maji Ruvu hakitoshelezi Mji wa Dar es salaam msitumie chanzo kingine cha maji ya Mto Rufiji na ni maji mazuri tu? Naomba sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inategemea wahisani kwa kiasi kikubwa sana. Hali hii inafanya Miradi mingi ikwame kwa sababu ya utegemezi. Mfano mzuri ni visima vya maji vya vijiji kumi, navyo

vimegeuka kero kwa wananchi; kwa nini vijiji vingi vimetimiza masharti na vigezo vingi ikiwemo wananchi kuchangia pesa zinazohitajika lakini miradi haianzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo kwa miaka mitatu mfululizo utaona jinsi tunavyotegemea wahisani; mfano, *Sub-Vote 4001 - Rural Water Supply*; 2010/2011 Local ni shilingi 34,505,438,802 za Nje shilingi 96,646,104,930; 2011/2012 Local shilingi 41,565,045,000 na za Nje 387,073,918,000; na 2012/2013 Local ni shilingi 140,015,967,000 za Nje shilingi 325,740,371,000. Je, tutapata maji katika vijiji vyetu kwa kutegemea wahisani? Picha inaonesha hatutatatua tatizo la maji kwani miaka yote tunategemea wahisani lakini Miradi mingi imeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atupe majibu atatekelezaje Miradi ya Maji Vijiji kwa ukamilifu?

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake ya Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuunga mkono noja, ninapenda Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya uhakika juu ya umaliziaji wa ukarabati wa miundombinu ya maji ya Chanzo cha Chiwambo kilichopo katika Jimbo la Lulindi Wilayani Masasi. Wizara ilishakitembelea na kutathmini gharama za Mradi

miaka kumi iliyopita na kutoa tathmini ya gharama ya shilingi 585,000,000 zitakazotumika kukamilisha Mradi wa Chiwambo. Mradi huu unahudumia Kata tisa, nazo ni Lulindi, Namalenga, Mbuyuni, Sindano, Mchauru, Chingutwa, Nanjota na Lipumburu. Katika Bajeti ya mwaka 2011/2013, Serikali imeweza kuleta shilingi milioni hamsini tu; hivyo, kufanya Mradi huu wenyewe gharama ya shilingi 585 milioni. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, Mradi huu ambao pia Mheshimiwa Rais aliahidi kuzitoa hizi fedha, atoe maelezo ni kiasi gani kimetengwa katika bajeti ya Wizara ya 2012/2013 ili kukamilisha Mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ajue kuwa hali ya upatikanaji wa maji katika Jimbo la Lulindi ni mbaya. Hivyo, wananchi wanainungu'nikia Serikali kwa kutotekeleza vyema Mradi huu muhimu. Ni vyema Wizara ikamilishe Miradi ambayo tayari ilikwishaanza kutenga fedha kabla ya kuanzisha Miradi mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu Mheshimiwa Waziri atatoa maelezo ya kina juu ya uhamishaji wa Mradi huu wa Chiwambo na baada ya maelezo hayo, nitaunga mkono Hotuba ya Waziri wa Maji.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Heru Juu, Karungwa na Muhunga vilikuwa na maji siku za nyuma, miundombinu yake imechakaa kwa sasa na mingine imekufa kabisa; kinachotakiwa kufanyika ni kufufua miundombinu hiyo na hivyo kuwezesha wakazi zaidi ya elfu thelathini kupata maji. Kwa mujibu wa Mhandisi wa Maji Wilaya ni kwamba,

kiasi cha shilingi milioni 200 kinahitajika ili kufufua Mradi na miundombinu yake iliyowekwa tangu miaka ya 1970. Hivyo ni vijiji vya kihistoria, utamaduni na asili ya kabilia la Waha ni katika Vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kumwandikia Mheshimiwa Waziri barua ya kuomba kiasi hicho cha fedha. Kwa niaba ya Wananchi wa Kasulu Mjini nitafurahi kusikia kuwa katika mwaka 2012/2013 tunapatiwa fedha hizo.

Vijiji vingine kama Kanazi, Nyansha, Nyantare, Murutiti, Kabanga, Msambara, Mwanga, Kidyama na Malumba, vinahitaji kuongeza mtandao wa mabomba na ukubwa wa matenki kuongezwa ili maji yaweze kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Benki ya Dunia; Kijiji cha Nyumbigwa kimo katika mpango, ni muda mrefu umepita tangu wananchi wachangie ile asilimia inayotakiwa. Majibu ya sasa ya kwamba mnasubiri *no objection* ya Benki ya Dunia yamekuwa ni ya muda mrefu. Naomba kujua utekelezaji wa Mradi huo utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji Kasulu Mjini hayatoshi, naomba kujua iwapo Serikali inaweza kusaidia shilingi milioni 500ili tupunguze kero ya uhaba wa maji Kasulu Mjini 2012/2013?

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa masikitiko yangu kwa Wizara kutotilia umuhimu wa kutatua matatizo ya maji

Jimbo la Manyovu na Kigoma kwa ujumla. Hakuna Miradi ya Maji iliyoainishwa kwenye Hotuba hii ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji katika Kijiji cha Mnanila haufanyi kazi ambapo maji hayo yalikuwa yanasantazwa katika Vijiji vya Mnamila, Mkatanga, Kitambuka, Kibwigwa na Mwayanza, yenyewe wakazi zaidi ya watu 100,000. Tunaomba Wizara itilie umuhimu sana na nitaomba kupata maelezo Wizara itafanya nini na lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Maji iangalie Wilaya mpya hizi ili na vijiji vya jirani vifaidike na maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji sita vya Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi viro ndani ya Jimbo la Manyovu; hivyo, ninaomba vijiji hivyo vipatiwe maji. Vijiji hivyo ni Kirungu, Muzeze, Kigogwe, Nyamugali, Bulimangi na Mmbaga, kijiji hiki ujenzi karibu utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma sasa maji ni siasa. Mimi Albert Obama, niliahidi kufuatilia tatizo la maji Mradi wa Mnanila na Vijiji Kumi. Ninaomba Waziri unisaidie nami niweze kupeperusha Bendera ya CCM tena Jimbo la Manyovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri atembelee Jimbo la Manyovu, tunamhitaji.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo au Wilaya ya Siha, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Waziri wa Maji, kwa Hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina, ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Wote tumefurahishwa na mipango aliyoiweka mbele yetu na tunasema hongera sana. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Siha kazi nzuri imefanyika chini ya *Hai District Water Supply Project*. Chini ya ushauri wa CES na uhisani wa KfW, kazi nzuri imefanyika kwa msaada wa Serikali na watu wengi wanapata maji safi na salama. Hata hivyo, ninaomba nikujulishe tatizo la maji katika Tarafa ya West Kilimanjaro ambayo haikuweza kupelekewa maji kwani taratibu zilikuwa haziruhusu. Sasa mambo ya uskwata yamekwisha. Ombi letu ni Wizara itusaidie kupata fedha kwa ajili ya kumaliza Mradi huo. Tulifanya *fund-raising* lakini bado mambo yakawa hayakukamilika, tulipata shilingi 500,000,000, hii ikiwa ni pamoja na nguvu za wananchi. Tunahitaji msaada wa Serikali usiopungua shilingi 500,000,000 tuweze kukamilisha *Project* hiyo. Ombi hilli tulilifikisha ofisini kwako kuanzia mwaka jana ambapo tulikaa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Lwenge. Katika jopo hilo, Naibu Waziri alikuwa na Katibu Mkuu na Watendaji wengine muhimu wa Wizara. Aidha, tuliomba tupatiwe *no objection* kwa Mradi ule kwani kulikuwa na urasimu mwingi ili kazi hiyo iweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa namna ya kipekee, Wananchi wa Ujerumani chini ya Benki ya Watu wa Ujerumani, kwa msaada mkubwa ambao chini ya *Hai District Water Supply*, kazi kubwa ilifanyika. Kanisa la Kilutheri Dayosisi ya Kaskazini wamefanya kazi nzuri na kutoa ushirikiano wa hali ya juu katika kuwahudumia Wananchi wa Wilaya ya Hai na wale wa Wilaya ya Siha. *Project Manager*, Bwana Michael Braasch, amefanya kazi nzuri yeye na wenzake na tunapenda kumwambia ahsante sana kwa utumishi wa kutukuka. Ahadi yangu kama mlezi wa Mradi, tutaulinda Mradi huu kwa nguvu zetu zote. Nawaomba wananchi wote tushirikiane Mradi huu usije kuhujumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Dkt. Birilith Mahenge, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara na hivyo kuwa msaada mkubwa kwa Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe. Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba, katika mwaka 2011/2012, Wilaya ya Uvinza umetekeleza Mradi mmoja tu Kijiji cha Uvinza. Hii ni hatari, Kata takriban sita zilizo mita mia moja toka usawa wa Ziwa hawana maji wakati Mikoa kama Kilimanjaro, maji yanapatikana mpaka kwenye Mashamba ya Kahawa Kigoma waliopo mita mia moja tu kutoka usawa wa Ziwa, hakuna huduma ya maji. Naishauri Serikali iangalie uwiano sawa na Ukanda huu

wa Ziwa upatiwe huduma ya maji Kata za Kalya, Buhingu, Sigunga, Ilagala, Igulula na Simbo. Kata hizi zinaweza kupata maji ya bomba, kuna vijihi takriban 21 hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Uvinza mwekezaji ametoa mashine ya kusukuma maji lakini Serikali imeshindwa kuendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Malagarasi haujatumika kuondoa tatizo la maji Kata za Uvinza, Mganza na Itebula. Hizi ni Kata zenye jumla ya vijihi 11 ambapo kama Mradi wa Maji ungeandaliwa tungetatua tatizo hili kwa Kata na Vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya visima bado ni tatizo hasa Kata za Kazuramimba, Kanduga, ambapo jumla ya vijihi kumi vinakabiliwa na tatizo la maji. Naomba tatizo hili litafutiwe majibu kwa kuwa hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya Wilaya ya Uvinza kuna miundombinu ya maji, iliyojengwa kwenye Kambi ya Wakimbizi Lugufu kabla haijafungwa. Naishauri Serikali ifufue miundombinu hii kwa kuwa inaweza kurahisisha huduma ya maji kwa haraka katika eneo hili ambalo ni Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mganza palikuwa na Mradi wa Maji lakini mpaka sasa tangu mwaka 2008 Mradi umekufa, hakuna juhudhi za kufufua na baadhi ya vifaa vimeanza kuibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya hatima ya suala hili.

MHE. ANNA MARYSTELLA MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii ya Maji. Kama sote tunavyofahamu kuwa, maji ni uhai, bila maji ya uhakika hatuwezi kuwa na kilimo cha uhakika, bila maji ya uhakika hatuwezi kuwa na uzalishaji wa viwanda; hivyo maji ni uhai pia ni kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kujitahidi kusambaza maji safi na salama nchini, ni Watanzania asilimia 55 - 60 pekee wanapata maji salama hapa nchini na wengi wao wakiwa mjini tu. Wananchi wa Vijiji ni wahangaikaji wakubwa wa maji. Kwanza, Serikali ilipaswa kutambua kuwa badala ya kusema KILIMO KWANZA ilipaswa kusema MAJI KWANZA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa Bunge la Bajeti la mwaka jana (2011), nilichangia na kumweleza Mheshimiwa Waziri wa Maji jinsi wananchi wa vijiji wanavyohangaika kwa kukosa maji safi na salama na nikavitaja vijiji kadhaa ambavyo tangu tumepata Uhuru havijawahi kuchimbiwa visima. Vipo vijiji ambavyo wananchi wanakunywa maji wakichangia na mifugo kama ng'ombe na mbuzi na mpaka hivi leo Serikali haijachukua hatua yoyote ya kuwaokoa wananchi hao ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa mazao kupitia kilimo. Je, haya ndiyo Maisha Bora kwa Kila Mtanzania? Tumeweza na tunazidi kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo Serikali imejaribu kuchimba visima lakini havifanyi kazi kwa maana havitoi maji na vingine vimeharibika kwa kubomokea ndani, lakini kazi ya Serikali ni kumhudumia mwananchi wake. Kwa nini sasa Serikali isichukue hatua hii kukagua visima hivi na kuvifanyia marekebisho? Naiomba Serikali kupitia Wizara hii, ijipange sasa kurekebisha visima vibovu ili wananchi waondokane na adha hii na kujiona wanyonge nchini mwao hasa akina mama wanaohangaika kutembea mwendo mrefu kusaka maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe elimu kwa Wananchi wa Tanzania kuhusu kutunza miundombinu ya mabomba. Itoe onyo kali kwa atakayeonekana anakata bomba, aidha kwa kuza vyuma chakavu au wengine hukata bomba kwa ajili ya kutengeneza bunduki za kienyeji zinazojulikana kama (gobole), ikiwezekana Serikali ifute kabisa biashara ya vyuma chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chanzo cha maji ambacho kinapatikana Mkoa wa Katavi, Kata ya Majimoto. Chanzo hicho ni chemchemi ambayo hutoa maji ya moto kabisa yanayofuka moshi. Wananchi wa Kijiji hicho cha Majimoto wanatumia kwa kunywa na kupikia, kwa kuwa hawana sehemu nyingine ya kupata maji ya baridi yanayoweza kukata kiu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakazi hao wa Kijiji cha Majimoto siyo kwamba wanapenda kunywa maji hayo, bali wanalazimika kwa kuwa hawana jinsi ya

kufanya kwani maji hayo ni ya chumvi na ni ya moto sana mpaka wananchi wapoze ndipo wanywe. Naiomba Serikali iyafanyie utafiti maji hayo ya moto na ni ya chumvi kama hayana madhara kwa wananchi watumiaji. Kutokana na maji hayo kuwashinda wakazi wa Majimoto na kulazimika kununua maji yanayotoka Kijiji jirani cha (Mamba), ambacho maji yake ni baridi, hayana chumvi, yanaporomoka kutoka mlimani na kuingia katika Mto uitwao Mkuruba katika Kijiji hicho cha Mamba na kuwauzia Wananchi wa Kata ya Majimoto kilomita tisa kwa kila lita 20 shilingi 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kama Wananchi wa Kijiji cha Majimoto wanaumia? Kwa nini sasa Serikali isichukue jukumu hili kwa kuweka tanki la maji katika Mto Mkuruba uliopo jirani na Kijiji cha Majimoto na kusambaza bomba zitakazopeleka maji mazuri katika Kijiji cha Majimoto na Vijiji vingine jirani ili vinufaika na kuepukana na maji hayo ya moto yenye chumvi? Pia Serikali itanufaika kwani ikipeleka bomba za maji wananchi watanunua maji hayo kwa bei nzuri. Sina zaidi, naona niishie hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. CLARA DIANA MWATUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kwanza, napenda kuipongeza Wizara hii hasa kupitia Waziri na jopo lake zima, kwa kazi nzuri iliyofanyika yenye kuleta matumaini mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyojulikana ya kuwa maji ni uhai na kitu muhimu katika maisha ya

viumbi vyote vyenye uhai. Suala la maji katika Mikoa ya Kusini, karibu asilimia tisini na nane maji ni tatizo. Nikianza na Wilaya ya Newala, vyanzo vya maji ni vichache. Kwa vijiji vingi wanategemea maji ya mvua ya kuvuna kwenye visima vya kujenga kwa sementi tupu bila mawe kutokana na ukosefu wa mawe ya kuvifanya visima hivyo ili viwe imara. Visima vya kuaminika vinavyotumia mashine, mafuta huwa shida na kusababisha ukosefu na usumbufu kama vile Mitema ambako ndiyo tegemeo la eneo kubwa Wilayani. Naomba Serikali ihakikishe mafuta yanakuwepo muda wote ili kuondoa adha. Wilaya ya Masasi vyanzo ni vingi ila usimamizi siyo mzuri. Visima vilivyochimbwa na Serikali ni vingi lakini hakuna maji, baadhi ya visima hivyo maji ni mengi ila *pump* ni mbovu na hazitengenezwi. Visima vinavyotumia umeme utakuta *motor* zimekufa na hazishughulikiwi. Matokeo yake akina mama hulala visimani wakisubiri zamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndanda kuna maji ya chemchemi isiyokwisha miaka yote kuna maji Mwena ya bomba. Mabomba haya yapo sehemu chache tu, yanatoka Ndanda hadi Masasi. Maji haya vijiji vingine vya njiani yamepita tu bila kuwekewa koki. Matokeo yake nao hutoboa ili wapate, hali ambayo inaleta hasara na kufanya yasifike mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ilifanyie kazi suala hili maana hata hili bomba la Mradi wa Mbwinji kama yatapitishwa bila vituo humo njiani kwenda Masasi Mjini na Nachingwea yatatobolewa pia. Mpaka sasa Masasi Mjini maji yanapatikana kupitia

vijana wa mikokoteni kwa bei ya shilingi 500 kwa dumu la lita 20. Wakubwa pia wana maboz a ambayo pia huuza maji, maji haya hupatikana maili sita ambapo kama yakiwekwa *pump* yatapatikana hata mjini. Maji haya ni mazuri na ni baridi hayana chumvi kama yapatikanayo katika visima vilivyopo eneo la mjini ni ya chumvi, hivyo tafadhali litiliwe maanani suala hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nanyumbu pia maji ni shida nako kufanyiwe juhud ya haraka kuokoa hali hii.

MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, kwa kazi nzuri mnayofanya kuhakikisha Watanzania wanapata maji ya kutosha na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba tushirikiane, yaani Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais, katika kuhifadhi vyanzo vya maji. Vyanzo hivyo vikiachwa bila kuhifadhiwa, Mipango yote ya Taifa haitatekelezeka. Kwa mfano, Mpango Mkakati wa *SAGCOT* wa kilimo, hautawezekana kabisa. Ni vyema tukaweka Mkakati wa Kitaifa kwa kuhusisha wadau kama vile Halmashauri, Shule za Kata, zikiwemo Sekondari na *Primary Schools* na kwa kushirikisha wananchi kupitia Serikali zao za Vijiji na Kata. Mimi ninaamini kabisa tukishirikiane kusimamia vizuri

utekelezaji wa kupanda miti ya asili, rafiki wa maji kwenye vyanzo, tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongwa na Vijiji vyake kuna matatizo makubwa sana ya maji, tunaomba ufadhili kadiri iwezekanavyo kwa Vijiji vya Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo makubwa yapo Chilanjilizi, Mtunguchole, Manyusi, Msingisa, Laikala, Ihanda, Moleti, Ngomai, Chigwingwili, Lengaji, Mkutani na kadhaliha na kadhaliha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nawapongeza wasomi wawili kwa maana ya Waziri na Naibu Waziri wa Maji, kwa kuteuliwa kwao kuiongoza Wizara hii nyeti, yenye changamoto kubwa na yenye kugusa maisha ya kila kiumbe nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango huu mfupi nitaaelekeza moja kwa moja *with reference* kutoka Jimboni kwangu Arumeru Mashariki. Jimbo langu lina vyanzo vingi vya maji, lakini linaongoza kwa ukosefu wa maji. Tuna milima kadhaa yenye maji, chemchemi nyingi, mito mingi, maji mengi ardhini (chini ya ardhi) na Ziwa Duluti (*Lake Duluti*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majumuisho, namwomba Mheshimiwa Waziri, atuambie ni kwa nini Wizara haijafikiria kuvuna maji Ziwa Duluti ili yatumike kwa Wananchi wa Wilaya ya Arumeru na hata Mkoa wa Arusha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Wawekezaji wa Mashamba ya Maua (*Hort Culture*), Hoteli za Kitalii na Viwanja vya Gofu (*Golf*) na Michezo ya Farasi (*Polo Clubs*) ndani ya Meru vina maji lakini wananchi hawana maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maswali ambayo ningependa kupatiwa majibu stahiki. Ahsante.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi nichangie katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji. Tatizo la maji ni tatizo sugu, ambalo linawaathiri sana wakazi wa vijijini. Tatizo hili kwa kiasi kikubwa katika Jiji la Dar es Salaam halipo, kwa sababu watu wengi huwa wanapata maji katika Kampuni ya *Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Company (DAWASCO)*. Maeneo ambayo hayana mtandao huo wa DAWASCO hupata maji kutoka katika visima ya watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni vyema ikaangalia sana hivi visima vya watu binafsi, kwa sababu mara nyingi watu wanajichimbia visima kiholela bila ya kutafuta wataalam wenye uzoefu. Kuna baadhi ya sehemu kuna vyoo vya matundu na

makaro ambayo yanakuwa yako karibu sana na visima hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya maradhi yanatokana na maji ambayo siyo salama. Katika vijiji vingi wanatumia maji ya mito ambayo siyo salama kwa sababu wanatumia wananchi kwa kunywa na matumizi mengine ya nyumbani na wakati huo huo na wafugaji wananyweshea wanyama humo humo, yanachafuka kwa vinyesi na mikojo ya wanyama. Naishauri Serikali iongeze fedha katika Sekta hii ili tatizo hili liondoke.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua fursa hii, kuchangia Hotuba ya Wizara ya Maji kuhusu Mapitio ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za maji Mjini na Vijijini; suala hili limekuwa ni tatizo kwa wananchi wa vijijini. Upatikanaji wa maji safi vijijini ni asilimia 57; asilimia hii ni ndogo sana kwa wakazi wa vijijini. Wananchi wengi wanatumia maji ambayo siyo salama na vyanzo vya maji siyo salama, wanyama watumie maji hayo kwa kunywa na kadhalika. Wananchi pia wanatumia maji hayo na kupelekea kupata maradhi kama kichocho na kadhalika, kwa sababu maji wanayotumia siyo mazuri kwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Waziri ni kwa nini kaya maskini vijijini zinasahaulika

kusambaziwa maji na kuongezeka kwa kiwango cha umaskini mkubwa zaidi vijiji ni kuliko mjini?

Tatizo la maji limeathiri wanawake wengi na kusababisha kuvunjika kwa ndoa na baadhi yao wamekuwa wanabakwa wanapokwenda kutafuta maji; kwani wanaenda kutafuta maji masafa marefu na wananchi hawa wamekuwa wakipoteza muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli nyingine za maendeleo na kuathiri uchumi wa nchi. Je, Waziri husika haoni ni wakati mwafaka wa kutekeleza hizo ahadi kwa vitendo na si kwa maneno? Kwa kuwa visima vyote vyta kizamani vimekuwa vikileta maafa kwa wananchi wa vijiji kwa sababu uchimbaji wake ni vipana na virefu kiasi kwamba wananchi wanatumbukia na kupoteza maisha hasa walemavu. Je, Waziri ana tamko gani juu ya visima hivyo vyenye kusababisha maafa kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana katika Jiji la Dar es Salaam kuhusiana na ulipaji wa ankara za maji kwa wateja wanaopata maji kila siku na wale wanaopata kwa wiki mara moja na wengine wasiopata kabisa lakini wamekuwa wakipata ankara sawa sawa. Je, Waziri ana mikakati gani ya kuhakikisha tofauti ya ankara hizo inakwisha na mtu kulipa kwa kadiri anavyotumia? Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam linakua kwa haraka sana na matumizi ya maji yanaongezeka kila kukicha; je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha maeneo ya majenzi ya makazi mapya kama vile Kimara, Mbezi Msakuzi, Tabata, Kigamboni, Kinyerezi na kadhalika wanapata maji ya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu yake; je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha upotevu huo wa maji unapungua au unakoma kabisa?

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji wa vyanzo vipyta vya maji ni wazo zuri la Serikali la kutaka kuelewa maji yatapatikana wapi. Hata hivyo, Programu hii inachelewa sana hasa kutokana na umuhimu wa maji ikiwa ni uhai wa binadamu. Hivyo, Serikali ifanye haraka sana kazi hiyo ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu wote wanahitaji matumizi bora ya maji, vinginevyo bila ya maji safi na salama, binadamu wenzetu wanapata maradhi na hata kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye mpango wa haraka wa kuona kuhakikisha Wananchi wa Tanzania wanapata na wanatumia maji safi na salama.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia Hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma - Manispaa kumekuwa na tatizo la upandishaji wa ankara za maji bila kuwashirikisha wananchi na hii inatokana na sababu kuwa katika Bodi ya Maji hakuna mwakilishi wa wananchi ambaye ni Mheshimiwa Diwani na Waziri ameandikiwa barua ili Diwani huyu aingie kwenye Bodi lakini haijajibwa. Tunataka majibu ya kina ni kwa nini maji yamepanda kutoka shilingi 5,200 hadi 19,500 kwa mwezi?

Je, ni lini mita zitafungwa?

Je, Waziri sasa yupo tayari kushusha ankara za maji mpaka kima ambacho Bodi itakubaliana na wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 Vitabu vya Halmashauri mbalimbali vilikuwa vinaonesha kuwa kiasi cha shilingi 32,240,623,989.47 zilikuwa kama bakaa ambayo ni sawa na asilimia 58 ya fedha za Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa nini fedha hizi zinashindwa kutumika na wakati shida ya maji ni kubwa? Waziri ana mkakati gani kuhakikisha kiasi hiki hakibakii tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Profesa Maghembe (Mb), Waziri wa Maji, kwa Hotuba nzuri ya Bajeti na kwa uwasilishaji mzuri na fasaha. Pia

nawapongeza Viongozi wa Wizara na Watumishi wote wa Wizara, kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Maji, kwa kazi nzuri ya kuboresha huduma za maji kwa Wananchi wote Tanzania, mijini na vijiji. Wizara iendelee kukaza uzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Bagamoyo tumepata mafaniko mengi kuitia juhudi za Wizara kuboresha huduma za maji. Pamoja na mafanikio, bado kuna changamoto kadhaa katika maeneo mbalimbali ya Jimbo kuhusiana na huduma ya maji safi na salama. Mjini Bagamoyo, huduma haitoshelezi mahitaji, kila siku kuna maeneo ya mjini hayapati maji kwa aina ya mgao wa maji. Pia kuna maeneo hasa Magomeni hakuna mtandao ya maji unaoridhisha. Tunaomba *DAWASA/DAWASCO* waboreshe mtandao wa mabomba ya maji katika Mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Chalinze Awamu II ni ukombozi wa huduma ya maji kwa vijiji vinne katika Jimbo la Bagamoyo na vijiji 42 kwa Wilaya nzima ya Bagamoyo. Katika Jimbo la Bagamoyo, Vijiji vya Vigwaza, Visezi, Buyuni na Makurunge vitafaidika. Changamoto tuliyokuwa nayo ni kuwa miezi ya karibuni Wakandarasi walisitisha kazi kwa sababu ya kutolipwa. Tunaiomba sana Wizara ilinde fedha za Mradi huu kwa kusimamia malipo ya mkandarasi kwa wakati. Wananchi wamesubiri miaka mingi huduma hii,

itapendeza kama Serikali kupitia Wizara itasimamia na kufanikisha Mradi huu bila mkingamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji vingi kandokando ya bomba kuu la maji la Ruvu Chini kwenda Dar es Salaam havipati huduma ya maji. Mtando wa mabomba ya maji ni finyu sana, wanaopata maji ni wale tu walio kando ya bomba kuu. Tunaomba mtando uboreshwe ili wananchi walio karibu na bomba kuu; kwa kipenyo/*radius* ya kilomita moja mpaka mbili wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji unaofadhiwa na Benki ya Dunia haujaonesha mafanikio ya kuridhisha katika Jimbo la Bagamoyo. Wizara iongeze juhudu ya utekelezaji wa Mradi. Pia Kamati za WATSAN zihamasishwe kufanya kazi ya kuwaelimisha wananchi kuunda Kamati zao za Maji za Vijiji na kuunda Mifuko ya Maji ya Vijiji. Wananchi wengi hawafahamu wajibu wao wa kuunda Kamati zao za Maji na kushiriki kuasi Miradi yao ya Maji. Vijiji katika Jimbo la Bagamoyo havina kamati za Maji. WATSAN ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja.

MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni maisha ya binadamu, binadamu bila maji hawezi kuishi kwa kuwa matumizi ya binadamu yoyote ni maji, tena safi. Maradhi hupatikana kwa wingi ikiwa maji hakuna. Wizara ilazimike kuwapatia wananchi maji na kuacha hadithi

ambazo mwisho wa siku hazileti tija ila kuwaweka wananchi katika hali mbaya ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya wanadamu wanahitaji maji katika maisha yao ya kila siku ambayo ni asilimia 80. Mwanadamu anahitaji kunywa maji safi na salama kila siku glasi nane, ili kusafisha damu iliyopo kwenye mwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujikita katika suala la maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kuna maeneo hayapati maji mfano Magomeni. Hivi sasa ni miezi mingi tu, tone la maji hawalioni, ukilinganisha na siku zilizopita. Suala hili linawatesa sana wananchi, mabomba yapo majumbani lakini yanaweka kutu kwa kutotoa maji. Wananchi wanavipara kwa kubeba maji au madumu ya maji. Wanaume mabega yamekwenda upande kwa kusukuma gari na baskeli za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa ni maskini, wana watoto, hawana kazi za ofisini, kazi zao wengine ni za hapa na pale, leo hii wawe kila siku wanunua maji na dumu moja shilingi 2,500; ni kweli watayaweza maisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa vijijini na watoto wao hubakwa kwa kutafuta maji. Watoto hawaendi shule kwa kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kungekuwa na Mpango Maalum hasa kwa watu wanaoishi Jijini kufanyiwa zamu za kuchota maji na siyo sehemu

nyingine hawakosi, wengine wanakosa. Hii angalau wananchi watakuwa na imani na Serikali yao kwamba, inawathamini na pia ukali wa maisha wa kununua maji utawapungukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaohujumu huduma za maji wakamatwe. Mamlaka ya Majisafi na Majitaka iweze kutambua hujuma zinazofanywa na wateja mbalimbali kwa kushirikiana na watumishi wa mamlaka wasio waaninifu. Baadhi ya wateja huunganishiwa maji kinyume na utaratibu, hivyo husababisha upotevu mkubwa wa mapato na kati yao hao huwa Vigogo wa Halmashauri ya Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubovu wa mabomba ni kichocheo cha wahujumu wa maji. Baadhi hupata sababu ya kufanya biashara za maji kwa kutia mpira na kutojali kwamba wananchi wanahitaji maji. Hivyo ni kazi ambayo huwa wameshajajiri. Wizara iwe makini na matatizo hayo kwa kuyasawazisha kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina vyanzo vingi vyaa maji ikiwemo mito, maziwa na chemchemi. Maji haya hutumiwa na binadamu, wanyama, viwandani, majumbani na kumwagilia mashamba. Matumizi ya maji haya ni mabaya, kwani hairidhishi kuona watu wanayaharibu, wanyama, viwanda na wakati huo huo hutumika kwa kazi za nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaokaa vijijini au karibu na vyanzo vyaa maji, hupata maradhi kutokana na matumizi mabaya ya maji katika mito, maziwa, vidimbwi na mabwawa. Wizara inalazimika

kutoa makucha yake kwa kuvidhibiti vyanzo hivi vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia bajeti ya mwaka jana, Waziri alitamka kwamba, maji yatapungua utata mara Wizara itakapopata fedha. Fedha imepatikana kutoka Serikalini na Wafadhili pia wamenyosha mikono yao, lakini bado upungufu upo pale pale; kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe makini katika kutoa mipango yake. Ni vizuri suala la maendeleo ya nchi, fedha yake itoke katika Serikali na siyo kwa Wafadhili, maana wana hiyari yao kutoa na kutokutoa. Nchi hujengwa na Wananchi na Serikali yao. Hivyo, fedha inayopatikana katika makusanyo ndiyo ifanyiwe maendeleo ya nchi ili wananchi waweze kutunza kilicho chao kwa uangalifu zaidi.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MADEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe (Mb), Waziri wa Maji, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge (Mb), Naibu Waziri wa Maji, kwa taarifa iliyowasilishwa kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Aidha, nawapongeza sana wote kwa pamoja kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuiongoza Wizara hii muhimu sana. Nawatakia kila la kheri ili waisimamie Wizara kutekeleza Sera na Sheria za Sekta ya Maji Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza sana Katibu Mkuu, Eng. Nestory Sayi, Naibu Katibu Mkuu,

Eng. Bashir Juma Mrindoko, Wakurugenzi wa Idara za Wizara, Wenyeviti na Watendaji Wakuu wote wa Bodi, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji, kwa jitihada wanazofanya kuondoa kero ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa niaba ya Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, naomba nirudie tena kuwasilisha kilio chao cha muda mrefu ambacho bado hakijapata sikio sikiu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Maagizo ya Rais: tarehe 17 Septemba, 2010, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, ambapo kufuatia taarifa ya kero kubwa ya maji inayowakabili Wananchi wa Wilaya hiyo, iliyowasilishwa kwake, aliagiza kuwa *Master Plan* ya Maji iandaliwe na kuwasilishwa Serikalini ili fedha zitengwe kwa ajili ya kutekeleza Mpango huo ili kumaliza kero ya maji ifikapo 2015. Hata hivyo, pamoja na jitihada nilizochukua kufuatilia ikiwa ni pamoja na kuwasilishwa taarifa juu ya maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa Waziri wa Maji ili atusaidie kutoa maelekezo kwa wahusika, hadi leo hakuna hatua zilizochukuliwa kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais. Tatizo kubwa ni kutokuwepo Mhandisi wa Maji makini na msikivu. Sina sababu ya kuilaumu Wizara, isipokuwa tu ni masikitiko kwamba, pamoja na kuzungumza na Viongozi wa Wizara mara kwa mara, jambo hili halijapewa uzito unaostahili. Naomba sasa Wizara iwaonee huruma Wananchi wa Jimbo langu kwa kuhakikisha kuwa Wilaya inapatiwa Mhandisi mzoefu, msikivu na mwadilifu ili asimamie utekelezaji wa agizo la

Mheshimiwa Rais. Hivi sasa wananchi wameanza kuwa na shaka kuwa ikiwa maagizo ya Mheshimiwa Rais yanapuuzwa ni ya nani yanazingatiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza msongamano katikati ya Jiji la Dar es Salaam, pamoja na kuanzisha vyanzo vipyta vya uchumi na kuboresha makazi; katika mikakati yake ya utekelezaji, Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa, limeanza ujenzi nyumba za gharama nafuu eneo la Kibada ili Wakazi wa Kigamboni watakaopitiwa na ujenzi wa miundombinu na huduma watahamishiwa. Hata hivyo, kikwazo kikubwa cha uendelezaji wa Mradi huo ni ukosefu wa miundombinu ya maji ambapo *NHC* italazimika kujenga, jambo ambalo litaongeza gharama za ujenzi na hivyo kufanya bei ya nyumba hizo kuwa zaidi ya mara mbili ya gharama halisi za ujenzi kama miundombinu muhimu ikiwemo maji ingekuwepo.

Je, Serikali kupitia *DAWASA/DAWASCO* inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa maji ya kutosha yanapatikana Kigamboni na kwa kuanzia Kata za Kibada na Vijibweni ili kuharakisha utekelezaji wa Mradi na kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba za kuishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa njia ya maandishi. Naishauri Serikali, pamoja na dhamira yao ya kutoa visima kumi kwa kila Wilaya, ni vyema katika kugawa rasilimali hizo,

tutathmini kwanza mahitaji ya walengwa. Yapo maeneo mengine ingalikuwa rahisi kutumia fedha kidogo kukinga maji ya mtelemko (*gravity*) na kujenga mtandao wa mabomba. Hapa lengo ni kuyafikisha maji karibu mita 400 toka kila familia. Maeneo mengine ni ujenzi wa malambo sehemu ambapo siyo rahisi kuchimba na kupata maji. Tafakari juu ya mipango ya visima katika Jimbo langu imenionesha kuwa, tija ingepatikana kwa kiasi hicho au pungufu kama mawazo hayo yangezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine ni juu ya usalama na ubora wa maji ya visima hasa hivi ni vyanzo vyta maji ambavyo vinamilikiwa na watu binafsi. Nawapongeza wote waliosaidia Serikali kwa kuchimba visima na kuwahudumia jirani zao japo kwa tozo kidogo. Tatizo hapa ni kuwa wamiliki wa vyanzo hawapimi maji hayo, nashauri mamlaka mbalimbali ziwasimamie watu hawa kwa kuhakikisha maji yanapimwa kila mara na inapobidi maji yatibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maji ya visima vinavyomilikiwa na watu binafsi, kuna tatizo la maji ya malambo. Kama Taifa tuna tatizo la wananchi kunywa, kufua na kunywesha mifugo katika eneo moja. Maji haya usalama wake hata bila kupimwa yako hatarini. Nashauri Serikali iandae mipango ambayo itawezesha maji yote yanayotumiwa na binadamu kupimwa na kutibiwa inapobidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa katika baadhi ya Kata zangu vyanzo vyta maji vinapatikana

karibu, nashauri Serikali ichukue faida hiyo na kusambaza maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa utumishi wake uliojaa unyenyekevu na uadilifu wa hali ya juu. Vile vile nampongeza Naibu Waziri, kwa namna ambavyo amepokea uteuzi wa Mheshimiwa Rais wetu, kwa muda mfupi tumemwona humu Bungeni na nje ya Bunge, anatekeleza majukumu yake. Nawapongeza sana Makamanda hawa wawili wa CCM katika Wizara hii, yaani Mheshimiwa Profesa Maghembe, Waziri wa Maji na Mheshimiwa Dkt. Mahenge, Naibu Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ikifanikiwa kuondoa kadhia hii ya maji kwa Watanzania, Chama chetu cha CCM ambacho katika llani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010 kimepanga kuwafikishia maji Watanzania wanaoishi vijijini asilimia sabini na tano ifikapo 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma hii ya CCM haitaweza kufikiwa iwapo hatuelewi ukubwa halisi wa tatizo hili la maji mjini na vijijini. Naiomba Serikali ituambie mahitaji halisi ya maji kwa Mtanzania kwa kila Mtanzania awe wa mjini au kijijini kwa siku yakoje? Tukilifahamu hili, tutaweza kuwa na mpango ambao utasaidia ufumbuzi wa kero ya maji. Watanzania zaidi ya asilimia sabini wanaishi vijijini na wanategemea kilimo kuendesha maisha yao. Pia ni wafugaji na kwa

maana hiyo wanahitaji maji kuendesha maisha yao. Je, tutawezaje kuwaondoshea kadhia ya maisha magumu wakati msisitizo kubwa wa maji ni kupeleka mjini na siyo vijijini? Naomba Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge lako Tukufu vigezo vyatupendelea wananchi wa mijini walio wachache na kuwaacha wa vijijini walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa kujipanga ili kuunganisha nguvu zake. Wizara ya Maji, Kilimo na ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, zishirikiane kutatua kero ya maji vijijini. Mabwawa na malambo mengi yamejengwa lakini hayana maji na hivyo kuwapa Watanzania matumaini feki. Huu siyo wakati wa kuwadanganya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi hawa Wakuu katika Wizara ya Maji, wana mapenzi ya dhati kwa Watanzania; hivyo, naomba Serikali iwapatie fedha za kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nitoe ushauri hasa kuhusu watumiaji binafsi wa maji. Hawa ni pamoja na wawekezaji katika migodi, viwanda, wakulima wakubwa na wananchi mmoja mmoja wanaomiliki visima. Serikali ichukue takwimu zao na walipishwe kodi ya kutumia rasilimali hii muhimu ya maji. Kodi hizi za maji zitumike kupanua utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kwamba, takwimu ya wanaomiliki visima na mabwawa au

malambo ikifahamika, wasaidiwe kupatiwa madawa kutibu maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesema inavyo vituo 362 vinavyotumika kupima mwenendo wa rasilimali ya maji juu ya ardhi, lakini imesema ni vituo 90 tu kati ya 362 ndiyo vinavyofanya kazi. Naomba ivifufue vyote ili vifanye kazi na hivyo kuiwezesha Serikali yetu iweze kupima kwa uhakika mwenendo wa maji chini ya ardhi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninadhani tungewapa nafasi Waheshimiwa Mawaziri, waanze ku-*respond* kwenye hizi hoja zilizotolewa na Wabunge.

Naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri, yeye atatumia kama dakika 20 na dakika nyingine zitatumiwa na Mheshimiwa Waziri. Kama utaratibu ulivyo, atakapokuwa akisoma majina ya wachangiaji, hayataingizwa kwenye muda wake wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunteua kuwa Naibu Waziri wa Maji ili niweze kutumia nafasi hii kulijenga Taifa langu na kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. Namuahidi kwamba, sitamwangusha, nitafanya kazi zangu kwa uaminifu, uadilifu mkubwa na kujituma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yake,

kwa namna ambavyo wametupa ushirikiano toka tumeanza miezi miwili iliyopita. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Jumanne Maghembe, kwa namna pekee anavyonipa ushirikiano na uzoefu alioupata na mimi pia nimeanza kuupata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wananchi wangu wa Jimbo la Makete, kwa namna ya pekee, wanavyonipa ushirikiano. Nami ninawaahidi kasi ya maendeleo Makete ipo pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao yote mizuri, ya maana na muhimu katika Wizara yetu ya Maji. Tumeipokea michango yao. Ipo michango ambayo ina hisia mpaka za uchungu. Tumepata mifano ya kwamba, yapo maeneo ambapo wananchi wanabadilisha madebe ya mahindi na ndoo za maji, ni la uchungu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyapokea kwa uchungu na tunafahamu kwamba tatizo hili ni kubwa na ndio maana ninawaomba wenzangu mtupe nafasi ili tuweze kuyatekeleza haya ambayo mmeyasema. Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu mimi ni Mbunge mwenzenu, nilikuwa ninakaa pale *bench* nyuma, kwa hiyo, matatizo haya ninayafahamu sana. Tulikuwa tunayasema sote na nimeyaona mpaka kwenye *site*. Tupeni nafasi, mtuamini mimi na Mheshimiwa Waziri wangu tuweze kuyatatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi, tumeshaanza kazi na nyote mmeona. Tuungeni mkono ili tuweze kutatua tatizo hili kubwa la kero ya maji kwa Wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno ya utangulizi, naomba sasa nипитie baadhi ya maeneo ambayo yamejitokeza kwa ufupi. La msingi ni kwamba, maeneo ni mengi na yote ni ya msingi, hakuna ambalo linazidi kuliko lingine. Kila mtu ametoa hoja ambayo ni ya msingi. Kutokana na muda kuwa mfupi, nitapitia baadhi ya maeneo na yatakayobaki atayapitia Mheshimiwa Waziri. Yale mengine tutayatengenezea kitabu ili baadaye Waheshimiwa Wabunge, muweze kuyapata myapitie kwa undani zaidi, lakini la msingi tunayachukua yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa ambalo limejitokeza hapa ni la visima. Suala la visima limeongelewa kwa uchungu sana; visima vimekosa maji na Wakandarasi wamelipwa pesa; ubora wa maji kwenye visima uko chini; na nini hatima ya visima vilivyokosa. Vilevile Wabunge wameongea kwa uchungu sana kuhusu gharama ambazo zimekuwa zikitumika kwenye kazi ya utafiti wa visima na gharama za kuchimba visima vyta awali kwa ajili ya uchunguzi na gharama za ujenzi wa miundombinu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezipokea, lakini niseme tu kwamba, kuhusu suala hili la visima kukosa maji, lipo suala la teknolojia. Kwamba, mpaka sasa hivi tunapoongea, duniani bado haijapatikana teknolojia ambayo inaweza ikatumika kwenye utafiti na

ikatuhakikishia kupata maji kwa asilimia 100. Mpaka sasa njia zote ambazo zimegundulika zinatuhakikishia kupata maji kwa asilimia 50 mpaka 70. Kwa hiyo, lipo tatizo la teknolojia hiyo kwamba, bado hatuna teknolojia sahihi ya kutupatia asilimia 100 kwamba, kuna maji na hii inatokana na kwamba, wakati wa utafiti zile tafiti zinaonesha tu ile miamba ambayo ina tabia ya kutunza maji, lakini haioneshi kwamba ndani kule kuna maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia ndiyo hizo hizo zinazoonesha kwamba, ndani kwenye miamba hiyo kuna mafuta. Kwa hiyo, ndiyo utakuta hata wenzetu wanaofanya utafiti wa mafuta, wanafanya utafiti na baadaye wanakosa wanaondoka. Kwa hiyo, zile tabia zinalingana, unadhani kuna maji, lakini wakati huo huo inaweza kuwa ni mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilidhani hili Waheshimiwa Wabunge, walielewe kwamba, hakuna njia ambayo inaweza ikatupatia asilimia 100; na kwa sababu hiyo, ndiyo maana ni lazima ufanyike utafiti na utafiti wa awamu ya kwanza ni lazima utume fedha ambazo ni lazima zitumike na ni lazima tulipe. Kwa hiyo, haitawezekana kufanya utafiti halafu usilipe. Kwa hiyo, utafiti wa awali ni muhimu watu wajue kwamba ni lazima utalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyojitokeza kwenye hali halisi ni kwamba, utafiti ulifanyika na kilicho jitokeza ni kwamba, kwenye Miradi hii ya Vijiji 10 ilikuwa inasimamiwa na Benki ya Dunia, kwa utaratibu ambao tulikuwa tumejiwekea baada ya kuona Wafadhili

wengi wanachangia na wakakubaliana kwamba, tutumie njia za manunuzi zinazosimamiwa na Benki ya Dunia. Kwa maana hiyo, kazi zote zili kuwa zinapewa taarifa kupitia Benki ya Dunia. Sasa, ikaonekana kwamba, baada ya kutangaza zile *tender* waliopewa kazi ya kusimamia mpaka mwisho ni Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo ambayo tumeyaona, mojawapo ni Mikataba ya waliokuwa wanachimba, haikuwa imekaa vizuri. Kwa maana kwamba, mtu anapewa kazi, akishafanya ule utafiti analipwa fedha, bila kujua kuwa ingetakiwa pengine yule yule aliyefanya utafiti ndiyo afanye kazi ya kuchimba ili itakapoonekana kuwa maji hayakupatikana, basi alipwe *portion* ya utafiti na *portion* ya kuchimba. Alipwe tu gharama ambazo ametumia mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imetokea matatizo; watu wamelipwa fedha wamechimba visima vile vya uchunguzi havina maji, wakaenda hatua mpaka ya kujenga miundombinu wakati wanajua maji hayapo! Niseme kwamba, hili ni tatizo la utekelezaji, ambalo sisi kama Wizara tumelichukua na tunaendelea kulifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize suala la uwepo wa Kampuni tofauti kwamba, aliyefanya utafiti ni kampuni tofauti na aliye kwenda kufanya kile kisima cha uchunguzi ni kampuni tofauti na wa kujenga miundombinu ni kampuni tofauti. Kwa hiyo, ukiona hapa ni kwamba, hakuna uwajibikaji, anayefanya utafiti haimgusi kama atakayekuwa anakuja kufanya

uchunguzi atakosa maji. Tunadhani kwenye mapendekezo yetu hivi sasa kuwe na umuhimu wa yule anayefanya utafiti; huyo huyo ndiyo aende kuchimba kisima cha uchunguzi na kujenga miundombinu. Hii itamlazimisha aifanye vizuri kazi ya utafiti, ili aweze kulipwa hela zake na baadaye alipwe zile za uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Mwenyekit, lingine, tumegundua kwamba, hizi kampuni zote ambazo zilifanya uchimbaji wa visima Vijiji kumi siyo za Serikali, ni za watu binafsi. Huu ulikuwa ni utaratibu wa manunuzi ambao ulizingatiwa na Benki ya Dunia kwamba, Serikali haiwezi kujiingiza kwenye biashara ya kuchimba visima, ingawa sisi tuna wakala wetu wa visima na mabwawa, ambao upo pale Makao Makuu na wana Wataalamu wa kutosha, wana vifaa vya kutosha, lakini hawakuweza kutumika kwenda kusaidia kule kwenye uchimbaji wa visima. Kwa maana hii, wale wachimbaji binafsi, wengi hawakuwa na uwezo wa vifaa na wataalamu.

Sasa hii sababu ilikuwa inasimamiwa na Halmashauri, ambao wao wenyewe Halmashauri, hawana uwezo wa Wataalamu wa Manunuzi na hawana uwezo wa kuwa na Wataalamu wa kusimamia uchimbaji visima, kwa vyovytote vile, ndiyo hii ilijitokeza maeneo kama ya kule Muheza, ambako kisima kimeenda kuchimbwa sehemu ambayo hata utafiti haukufanywa kwa kuwa hawakuzingatia utaalamu, wakidhani popote unaweza ukachimba, maji yakapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yatazingatiwa katika kuboresha eneo lote hili la uchimbaji visima katika awamu ya pili ambayo inakuja mwezi Juni, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hatima ya visima ambavyo vilikosa maji? Hatima ya visima vilivyokosa maji, tumekubaliana kwamba, yale maeneo yatapimwa tena na kama itaonekana lile eneo kwenye kile Kijiji halina dalili za kuwa na maji, tutapima kwenye vijiji jirani vinavyofuata. Kama itaonekana vilevile bado hakuna dalili za kuwa na maji, basi tutatumia mbinu nyingine ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa. Kwa hiyo, ninataka niwahakikishie wananchi kwamba, pale ambapo maji yalikosekana kwenye vile visima kumi, tatarudia zoezi la kwenda kufanya utafiti na zoezi la kuchimba visima vyatuhunguzi. Kama itaonekana hakuna, tutakwenda zaidi ya hapo kutumia mbinu nyingine ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kwenye eneo hili la visima, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wakala wetu wa Visima (*DDC*) sasa hivi wanaendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wachimbaji wa visima (makampuni 126). Mafunzo haya yanagharamiwa kwa ushirikiano wa Tanzania na *JICA*, yatakayowapa uwezo wa kufahamu utaalamu wa ndani zaidi. Vilevile mafunzo haya yatawasaidia kutumia vifaa ambavyo ni vyatuhunguzi, ambavyo tayari viro kwenye Wakala wetu wa uchimbaji wa visima pale Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe rai moja kwenye hili eneo kwamba, tumepokea maombi ya Waheshimiwa Wabunge na njia pekee ya kuanza kuifanyia kazi vizuri ni kwenda kutembelea visima hivi tuone hali yake ili tufanye tathmini ya namna ya kuendelea mbele. Kwa hiyo, tutaenda kuhakiki kazi iliyofanyika ya visima hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni la maji Ziwa Victoria. Naomba nitoe taarifa kama ifuatavyo:-

Wabunge wengi wamechangia. Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza, Shinyanga na Tabora, kilio chao kikubwa tumekisia na tunafahamu kwamba hali ni ngumu. La msingi ambalo ningetaka Wabunge wenzangu watuelewe ni kwamba, dhamira ya Serikali tayari imeshaanza kuonekana. Dhamira hii ilianza kuonekana pale tulipotekeleza mradi wa kutoka ziwa Victoria kupeleka vijiji 54 kwa kutumia fedha zetu za ndani, hii nadhani ni dhamira kubwa Waheshimiwa Wabunge ambayo lazima tuikubali kwamba ni mwanzo mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango ule tulipeleka awamu ya kwanza vijiji 39 toka Kahama, Shinyanga na tulipanga kupeleka vijiji 54, lakini vile viliviyobaki tukavipeleka awamu pili ambayo ilitokana na vijijini 96. Sasa tupeni nafasi ili tutekeleze na awamu ya pili hiyo ya vijiji 96, kwa sababu tayari awamu ya kwanza imeonesha mafanikio na imetoa hamu kwa walio wengi kwamba na sisi tunataka maji Ziwa

Victoria. Kwa hiyo, mahitaji yameongezeka na kazi kubwa ni kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

Katika awamu hii ya pili tumeshaanza kazi. Cha kwanza ambacho tumekifanya, tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwenye vijiji hivyo 96. Vilevile ukiunganisha na dhamira ya Serikali ya kuleta maji mpaka Mkoa wa Tabora kwenye Wilaya za Nzega, Igunga na maeneo mengine. (*Makofi*)

Fedha hizo zikishafanya upembuzi yakinifu, hatua inayofuata ni kutenga fedha za ujenzi. Sasa huwezi kuruka *step* moja kwenda nyingine. Kwa hiyo, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge watupe nafasi, hatua hii ikamilike. Kama hatua ya kwanza ilikamilika ambayo tulitumia zaidi ya shilingi bilioni 270 kwa nini hizi zisikamilike? Kwa hiyo, nadhani mtuamini tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tayari tarehe 4 Julai, 2012 tulitangaza *tender* kwa ajili ya upembuzi yakinifu kuchukua maji Ziwa Victoria kwenda Meatu na Bariadi. Tumetangaza *tender* ya kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Magu na Ngudu. Ninadhani hii ni mipango mizuri. (*Makofi*)

Tulipeleka maji kwenye Vijiji vya Mhalo ambavyo vilikuwa umbali wa kilomita 23, tofauti na ilivyokuwa mwanzoni, lakini kwa kutambua umuhimu wa wale wananchi kupata maji tukapeleka kwenye tanki ambalo lilikuwa limejengwa na wananchi; sasa hivi wanapata maji vijiji vitano na mpango wetu ni

kuhakikisha kwamba vijiji vingine vilivyobaki kwenye ile Tarafa ya Mwamshanga vyote vinapata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, mpango huu unaendelea, tuipe nafasi Serikali iendelee na vijiji vingine vilivyopo kando ya Ziwa Victoria kwa maana kuwa inaweza kutekelezwa. Awamu hii inazingatia zaidi vijiji vilivyo umbali wa kilomita 12 toka katikati ya bomba pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nипитie baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo zinaweza kuwa zinahitaji *attention* tofauti. Kulikuwa na hoja ambayo imeongeleta na Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, aliyelezea kwamba, kuna maziwa makubwa na bahari kubwa nchini, tunashindwa kutumia maji hayo kutatua tatizo la maji nchini. Maelezo ya Serikali ni kwamba, katika utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini, wananchi wana jukumu la kuchagua aina ya teknolojia ya mradi kulingana na uwezo wa kumudu kuchangia gharama za ujenzi, uendeshaji na matengenezo. Hii itahakikisha kuwa, Miradi iliyojengwa inakuwa endelevu. Jamii inahamasishwa kuchangia gharama zinazohitajika. Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya mwekezaji katika Miradi ya Maji nchini kupitia juhudi mbalimbali ikiwemo Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Tulikuwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi; ye ye alielezea kuhusu Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Mjini Tabora kwamba ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, kufikisha maji Mjini Tabora kabla ya

mwaka 2015. Hili nimelielezea kwamba, ndiyo mkakati huo ambao tunafanya upembuzi yakinifu na maeneo yote haya yatafikiwa.

Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema, ameuliza ni wakati gani Mhandisi Mshauri na Mhandisi wataajiriwa ili kutekeleza Mradi wa *Lake Victoria Watsan Two* na ni lini hasa *short term intervention* itakamilika ili wananchi wapate maji ya uhakika katika Miji ya Sengerema. Jibu ni kwamba, Mhandisi Mshauri atapatikana mwishoni mwa mwezi Agosti, 2012, usanifu utakamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, ametaka Serikali itoe ufanuzi wa Miradi ya Jamii ipo katika vijiji gani katika Wilaya ya Kwimba. Wilaya ya Kwimba ipo katika eneo la Dakiyo, Mto Simiyu, ambalo limepewa kipaumbele katika Mradi wa Hifadhi ya Mradi wa Ziwa Victoria.

Mpaka sasa kuna jumla ya Miradi ya Jamii kumi iliyopitishwa kwa utekelezaji katika Wilaya ya Kwimba ikiwa ni pamoja na ile iliyooneshwa katika Jedwali Namba Nne katika Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Miradi hii ni ya bustani ya miche ya miti, upandaji miji, ufugaji nyuki na ujenzi wa vyoo. Vijiji vinavyohusika ni Bugando, Mwambuchuma, Mwasengele, Nyamshana, Icheja, Walemasonga, Vulututu, Maligisu, Kadasi na mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja za Morogoro; Mheshimiwa Amosi Gabriel Makala ameulizia kuhusu Mradi wa Maji Turiani na Mvomero. Miradi hii kasi ya utekelezaji inasuasua, naomba Serikali ithibitishe Mwaka huu wa Fedha wa 2012/2013 kuwa imetenga fedha kwa Miradi hii ya Mvomero na Turiani.

Jibu ni kwamba, katika bajeti ya mwaka 2012/2013, shilingi bilioni 1.6 zimetengwa kwa ajili ya Miradi hii. Mheshimiwa Mchungaji Getrude Lwakatare, tatizo la maji Kilombero hasa Mjini Ifakara, usanifu umepangwa kufanywa na awamu ya pili ya Programu hii ya *WSDP*.

Mheshimiwa Shabiby, Mbunge wa Gairo amesema, hatua za utekelezaji katika Mji wa Ikwiriri imetajwa lakini katika miji mingine sita; Gairo, Kibiti, Kibaigwa, Kilosa, Mvomero na Turiani haikutajwa; kwa nini? Jibu ni kwamba, hatua ya utekelezaji katika miji saba ni kama ifuatavyo: Gairo asilimia 84.34, Kilosa asilimia 60, Mvomero asilimia 74.2, Turiani asilimia 62, Kibaigwa asilimia 80, Ikwiriri asilimia 75 na Kibiti Mradi wake umekamilika asilimia 100.

Mheshimiwa Deogratias Ntukumazina, Mbunge wa Ngara, hoja yake mojawapo ni kwamba, fedha za Benki ya Dunia zigawiwe sawa kwa Halmashauri zote. Tunasema kwamba, Serikali hugawa fedha za maendeleo ya Miradi ya Maji katika Halmashauri kwa Kanuni ilioandaliwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Kanuni inazingatia vigezo vya idadi ya watu katika Halmashauri, idadi ya watu wasiopata

maji na aina ya teknolojia inayotumika kushughulikia hayo maji.

Tunalipokea wazo la Mheshimiwa Mwigulu, Mbunge wa Iramba na Mheshimiwa Capt. John Chiligati, kuhusu suala la uchimbaji mabwawa katika eneo hilo, kwa sababu ya uhaba wa maji kupatikana kwa njia za visima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, ameelezea kuhusu Mradi wa Benki ya Dunia, kiwango cha kuchangia asilimia kumi ya wananchi kinakwamisha Mradi baadhi ya maeneo. Ushauri; Wizara ishirikiane na Halmashauri ili kuwakopesha vijiji husika na hatimaye kutumia mfumo wa makato kutokana na ushuru wa mazao. Majibu ni kwamba, moja ya misingi ya Sera ya Maji ya Mwaka 2002 ni kuwashirikisha wananchi. Wananchi wakishirikishwa kuanzia hatua ya mpango, wanashiriki utekelezaji, wanashiriki mpaka kwenye mapato. Kwa hiyo, itakuwa siyo vizuri ukaanza kutoa huo mchango ambao anapendekeza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Cythia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, ameelezea kusucasua kwa Mradi wa *Masoko Group* ambao kwa bahati nzuri nimeutembelea mwenyewe kule Rungwe. Kweli Mradi huu unasuasua lakini tumekubaliana kwamba, kwa sababu kazi zilizofanyika pale zipo chini ya kiwango na vilevile mkandarasi anatakiwa amalize ile kazi ndani ya miezi kumi na nane, leo amefanya kazi miezi 24, kazi aliyofanya ni asilimia 30. Kwa maana hiyo ni kwamba, ili amalize kazi angehitaji miezi 56, kwa hiyo,

tumekubaliana kwamba, wenzetu Rungwe wafuatilie kuandaa tathmini na Mheshimiwa Waziri ameagiza wataalam wetu waende wakafanye tathmini na waangalie hali halisi ya Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa kunisikiliza, naomba kuunga hoja mkono. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mahenge, Naibu Waziri wa Maji, kwa majibu yako ya utangulizi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite mtoa hoja, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Jumanne Mghembe. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru sana kwa kutupa nafasi ya kutoa maelezo kwa hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Ningependa kusema kwamba, katika siku hizi mbili, kama kuna shule ambayo tumeingia mimi na mwenzangu hapa ni michango mizuri sana ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Wabunge 43 wamechangia kwa kusema na hoja walizotoa ni nzito sana. Ninapenda nichukue fursa hii, tangu awali kabisa niwashukuru sana kwa hoja hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 150 wameleta michango ya maandishi na tulikuwa na jeshi kubwa la wataalam, walisoma na

kutafsiri hoja ambazo zimeletwa na Waheshimiwa na hoja ambazo zimeletwa ni za msingi sana. Sisi kwa upande wa Serikali, tumepata hisia ambazo ni sahihi kabisa za hali halisi ambayo ipo katika Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji katika nchi yetu kama ilivyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge ni kubwa sana, sidhani kama katika historia yangu ya kufanya kazi kama Mwanasayansi kwenye Vyuo Vikuu kama Mfanyakazi wa Serikali na kama Mbunge na kama Waziri, kwa miaka saba, kama nimepata kupokea tatizo kubwa namna hii. Hili ni tatizo kubwa na sisi kwa upande wa Serikali, tumelipokea kwa mambo matatu makubwa sana ambayo yamesemwa hapa na Waheshimiwa Wabunge.

Jambo la kwanza ni kwamba, watu wengi sana hapa nchini kwetu hawana maji hasa katika maeneo ya vijijini na katika maeneo ya miji midogo. Pili, fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuwapelekea maji wananchi. Katika maeneo yote hapa nchini hazitoshi na hazitoshi kabisa katika kukabiliana na tatizo lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu ni kwamba, mfumo uliopo hauwezi kutufikisha mahali ambapo tunataka kwenda kwa wananchi wetu kupata maji vijijini asilimia 75 na wale walioko mjini kupata maji asilimia 90 kama utekelezaji wake unakwenda kwa mfumo ambao Wizara inatekeleza Miradi ile ya Mijini na Miradi Mikubwa ya Taifa na Halmashauri zinatekeleza Miradi yote iliyoko vijijini.

Tunakubaliana kabisa na hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba, wakati umefika tuwe na chombo ambacho kinafananafana hivi na *TANROADS* kwamba, tuwe na kitu kinachoitwa *TANWATER*, ambacho kitakuwa na utekelezaji katika ngazi ya Taifa, kitakuwa na usimamizi na utekelezaji katika ngazi ya mikoa na kutakuwa na mfumo ambao kunakuwa na Kamati ya Maji kama ile ya Barabara ya Mkoa, ambapo kabla hatujaja hapa Bungeni tumepitia kule kwenye Mikoa yetu, kuona Miradi gani muhimu ya maji inatekelezwa na imetekelizwa kiasi gani. Fedha zipo namna gani na mwaka unapokwisha tunapata utekelezaji katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na katika ngazi ya Kata na Vijiji.

Jambo hili tumelipokea, nimezungumza na wenzangu totalitengenezea utaratibu na kupeleka kwenye Serikali ili liweze kupitishwa haraka iwezekanavyo na mfumo huu tuutumie kwa kutekeleza Miradi ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine ambalo limetajwa na Waheshimiwa Wabunge hapa kwa hisia kubwa, hisia ya kilio na hisia ya hatma baada ya miaka mwaka 2015 na huu ni Mradi wa Vijiji Kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ulianza kutekelezwa, nakumbuka wewe na mimi tulilingia Bungeni mwaka 2000, Mradi huu uliletwa kwenye Bunge mwaka 2003 kama Mradi ambao utatekelezwa haraka utaanza na kuajiri mshauri katika kila Wilaya, Mshauri atazungumza na wananchi kuwahamasisha juu ya Mradi. Wananchi watataja wanataka maji yao

yaletwe kwa njia gani kama ni mtiririko, visima, mabwawa, pampu za mkono au za umeme au za mafuta na baada ya hapo mshauri yule atafanya survey ajue huu Mradi utakuwa wapi halafu mkandarasi ndiyo ateuliwe na mkandarasi akiteuliwa achimbe kama ni hivyo visima au aangalie namna ya kuleta maji kwa mtiririko au kuwekwa bwawa na kadhalika. Katika hatua zote hizi, lazima kuwe na vibali vinavyotoka Benki ya Dunia; ni Mradi ambao ulipangwa na *bureaucracy*. Umepangwa hivi kwa sababu kulikuwa hakuna chombo kama kile cha *TANROADS* ambacho kingeweza kutekeleza Miradi hii kwa mfumo ambao ni *transparent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye mwaka 2007 fedha zilizokuwa zimepangwa mwaka 2003 zikawa kwa bei za mwaka 2007/2008, zimekuwa kidogo na kwa hiyo hazitoshi tena kutekeleza vijiji kumi zikawa *scaled down* kwamba, sasa itekelezwe vijiji vitatu. Sasa Wizara imekuwa kwenye hatua za kujaribu kufanya hivyo vijiji vitatu basi vitekelezwe haraka iwezekanavyo. Kufikia mwisho wa mwezi uliopita, Halmashauri 62 zimeruhusiwa sasa zitekeleze hiyo Miradi na fedha zipo kwenye Wilaya na mwaka huu tumetenga shilingi 51.9 billioni kwa ajili ya kutekeleza Mradi huo wa vijiji vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya au Halmashauri nyingine zipo kwenye hatua mbalimbali, lakini tumekutana na wenzetu wa *World Bank* na kuwaambia kwamba, utaratibu wa *business as usual* haukulaliki. Tumekubaliana kwamba, katika mwaka huu wa fedha kwa utaratibu huo wa vijiji vitatu,

Halmashauri 115 zikamilishe utaratibu wote na kutengeneza miundombinu ya vijiji hivyo vitatu.

Bahati nzuri wakati tukisukuma jambo hilo la vijiji vitatu kwamba ni lazima vitekelezwe na hadithi ya kila mwaka ya kulieleza Bunge iishe mwaka huu, tukapata na fedha nyingine shilingi bilioni 30 kutoka *DFID* na kutoka *African Development Bank*, tukafanya uamuzi kwamba fedha hizi zilizoongezeka zitumike kutengeneza Miradi miwili ya ziada katika kila Halmashauri Tanzania nzima. Kwa maana hiyo, kila Wilaya mwaka huu itakuwa na vijiji vitano ambavyo vitatekelezwa kati ya vile vijiji kumi ambavyo vilikuwa vimepangwa tangu awali na kwa sababu fedha hizi zimetoka *DFID* na zinatoka *ADB*, hazitakuwa na kazi ya ule mlolongo wa kupeleka kupata *no objection*. Kwa hiyo, ninatoa rai kwamba, kila Mheshimiwa Mbunge, ashauriane na Halmashauri yake ituletee vijiji katika vile kumi vilivyokuwa vimepewa kipaumbele kwa utekelezaji, vijiji vingine viwili ili katika mwaka huu wa fedha basi tuweze kutekeleza vijiji vitano katika kila Halmashauri Tanzania nzima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili limekuwa kero sana na kwa kuwa sisi katika Bunge hili tulikubaliana kwamba katika kila mwezi wa pili tutakaa tuangalie mpango wa mwaka unaokuja na bajeti, ninawausia wenzangu kwamba, katika kipindi kinachokuja, pamoja na kuhakikisha kwamba tunaipa Sekta ya Maji kipaumbele cha kwanza klichoooneshwa hapa na hotuba zilizotolewa ndani ya Bunge, basi moja ya maeneo ambayo ni lazima tuyakamilishe katika bajeti ijayo ni vijiji vitano ambavyo vimebaki ili

tukimaliza mwaka 2013/2014 tuwe tumemaliza vijiji vyote kumi ambavyo tumevitaja katika mipango yetu ya maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo nilikuwa nataka nianze nayo ili tuwe katika eneo moja.

Jambo la pili, ninapenda tushirikiane sana katika suala la Miradi ya Maji. Tutajitahidi kwa nguvu zetu zote mimi na mwenzangu na tuna Makatibu Wakuu wawili; tuna Katibu Mkuu Christopher Sayi, ambaye ni mzoefu sana na tuna Naibu Katibu Mkuu. Kwa hiyo, tutajitahidi katika hii timu ya watu wanne, tutembelee katika kila Halmashauri tuweze kujua hasa matatizo na utekelezaji wa Miradi hii umefika wapi. Nawaomba sana ndugu zangu, pamoja na juhudhi hizo ambazo tutafanya, tushirikiane na kupeana habari katika utekelezaji wa Miradi na pale ambapo mtakuwa mnaona kwamba utekelezaji unasuasua, ninaomba sana tupate habari ili tuweze kushughulikia mambo haya haraka iwezekanavyo, kwa sababu kama ambavyo imesemwa hapa maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuweka msingi huo, nimeona sasa niwataje Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wameshiriki na kutoa michango katika hoja yangu.

Wabunge ambao walichangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Neema H. Mgaya, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Maji na Mifugo, Mheshimiwa Sabreena Sungura, ambaye ametoa Taarifa ya Waziri Kivuli Kambi Rasmi ya Upinzani,

Mheshimiwa Kaika Saningo Telele, Mheshimiwa Selemani J. Zedi, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda , Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Joshua S. Nassari, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany na Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde , Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkyo, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi Suleiman, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Desderius John Mipata na Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuandika ni Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Nyambari C. Nyangwine, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Wiliam V. Lukuvi, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Geofrey W. Zambi, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashidi, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gregory G. Teu, Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mheshimiwa Janeth Z. Mbene, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati,

Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Anna MaryStella John Mallac, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Joshua S. Nassari, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Charles J. Mwijage, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel J. Nchimbi, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Aliko N. Kibona, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa, Mheshimiwa Dkt. David M. Malole, Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Zabein M.

Mhita, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *there is a lot of mixing here, naomba mnisamehe.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Neema H. Mgaya, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Chirstopher K. Chiza, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Augustino M. Maselle, Mheshimiwa Joshua S. Nassari, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Mheshimiwa Ally Khamis Seif, Mheshimiwa Dkt. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Esther A. Bulaya, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Dickson Kilufi, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, Mheshimiwa Angella J. Kairuki, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa

Charles M. Kitwanga na Mheshimiwa Dkt. David M. David. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia Mheshimiwa John J. Mnyika na Mheshimiwa Josephat S. Kandege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema jana na leo, tumepata hoja nzuri sana na tumepata faida kubwa katika kuweka vipaumbele na katika kuweka mikakati na kuangalia upya mpango mzima wa maendeleo ya maji nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hizi kama nilivyosema nyingine zilikuwa kali sana na za kilio na ningependa nianze na hoja moja ambayo ilitoka jioni kabisa kutoka kwa Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, ambaye alitoa kilio kikubwa na kabla sijaingia Bungeni mchana aliniambia kwamba, alikuwa amepanga kuleta akina mama 60 kwenye basi mojam ambao hawajaoga kwa muda wa wiki mbili ili waweze kuonesha hali mbaya sana iliyopo katika Mji wa Namanyere. Nilimsihi sana Mheshimiwa Keissy kwamba, tatizo hili tulilonalo tunaweza kulitatua kwa mazungumzo hapa Bungeni na kwa kushauriana na wakubwa wetu, badala ya kuwaleta akina Mama ambao hawajaoga kwa wiki mbili waje hapa Bungeni; akasema kwamba kitu muhimu kabisa apate jibu. Jana usiku nilishauriana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama mnavyokumbuka wakati anafanya majumuisho ya bajeti yake alisema kwamba, angeangalia maeneo ambayo yana shida kubwa sana ili aweze kuanza hata kwa mchango mdogo wa Serikali kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu jana akanihakikishia na nimweleze Mheshimiwa Keissy kwamba, kwanza, wiki hii ijayo mimi na yeze twende Namanyere tukazungumze na akina mama na tuwatangazie kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekubali Serikali itatafuta shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Namanyere. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Keissy uunge mkono hoja, kwa sababu hakutakuwa tena na sababu ya kuwaleta wale akina mama ambao wana matatizo makubwa sana ya maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia alitoa ahadi katika Hotuba yake wakati anafanya majumuisho hapa wiki iliyopita kwamba, atautembelea yeze mwenyewe Mradi wa Ntomoko ambao Mheshimiwa Juma Nkamia aliusolezea kwa hisia kubwa sana. Mradi ule ultengenezwa katika miaka ya 70 na unahudumia vijiji vingi sana katika Wilaya ya Kondoa, lakini toka mwaka 1975 mpaka sasa miundombinu yake imechakaa na katika maeneo mengine miundombinu ile imehujumiwa na watu ambao wanachunga au wanafunga. Kuna baadhi ya watu wakiwa wanachunga ng'ombe wanatoboa kwenye bomba ili kupata maji kwa ajili ya mifugo yao na kwa sababu hiyo Mradi ule umezeeka sana na unahitaji ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia Ofisi yake kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, amekubali kuuangalia Mradi huo na atautembelea yeze.

Mheshimiwa Mbunge katika mchango wa maandishi amesema, Mheshimiwa Waziri autembelee Mradi huo. Nami nitakuwepo wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anatembelea ili tuangalie ni kitu gani kinaweza kufanywa ili kuufufua Mradi huo na kuhakikisha unawapatia watu wengi sana ambao wamekosa maji waweze kupata tena maji kutoka kwenye Mradi huo wa Ntomoko. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Nkamia, kwa jambo hili ambalo umelisimamia kwa nguvu sana na kama ulivyosikia kwenye Hotuba yetu, maeneo yale yamekuwa na ongezeko kubwa la watu pamoja na ukuaji mkubwa wa Makao Makuu hapa Dodoma. Kuanzia mwaka ujao wa fedha, tutaanza kazi ya kusanifu Bwawa la Farkwa ili tuweze kutoa maji katika maeneo hayo yaliyobaki ya Kondoa, Bahi na Chamwino na Mji Mkuu Dodoma. Kazi hiyo itaendelea kwa mwaka ujao na tunategemea ujenzi unaweza kuanza katika mwaka 2013/2014, fedha zikipatikana. Tukiungana kama mlivyosema hapa, tuongeze bajeti ya maji, basi sina shaka kwamba, jambo hilo litatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Peter Serukamba, naye alitoa kilio kikubwa sana akisema kwa miaka minane ameambiwa kwamba, Mji wa Kigoma maji yatatengenezwa na amengojea kwa miaka minane hadithi ni hiyo hiyo, Mradi haujatengenezwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Serukamba na Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma, Sumbawanga na Lindi kwamba, tumetangaza ujenzi wa miundombinu ya kupanua huduma ya maji na majitaka katika Miji hii. Miaka hiyo minane iliyopita, fedha ziliikuwa zinatafutwa na wafadhili, wale

Wajerumani walikuwa wameonesha nia kwamba, watatoa fedha lakini hawakutoa fedha mpaka sasa.

Kwa sababu fedha zimetoka, tulitangaza tarehe 26 Juni, 2012 kama mtaangalia Gazeti la *The Guardian*, *construction of water and sanitation infrastructure in Kigoma, Sumbawanga, Lindi and ground water drilling in Sumbawanga and Lindi*. Baadaye tukimaliza hapa nawaomba sana mkishaunga mkono hoja hii basi niwakabidhi jambo hili muweze kuona Serikali ipo *serious* katika kutekeleza Mradi wa Kigoma, Lindi na Sumbawanga na kwamba, *tender zinapokelewa* sasa na mpaka mwisho wa mwezi Agosti Mkandarasi atakuwa amepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, kwa utaratibu huo huo tumetangaza ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika Miji ya Bukoba na Musoma na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii amekuwa anafuatilia jambo hili. Waheshimiwa Wabunge wa Bukoba Vijijini na Muleba, ningependa niwahakikishie kwamba, jambo hili sasa limeshatangazwa na muda usio mrefu tutapata Wakandarasi na Miradi ya kupanua upatikanaji wa maji ili kufikia asilimia 90 ya mahitaji ya miji hiyo itaanza kujengwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hii inafadhiliwa moja kwa moja na Washirika wetu wa Maendeleo ambao ni Shirika la Maendeleo la Ufaransa kwa ajili ya Bukoba na Musoma na Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Ulaya, likishirikiana na Benki ya Maendeleo ya

Ujerumani, kwa ajili ya Kigoma, Lindi na Sumbawanga. Kwa hiyo, sasa ndugu zangu mliotoa hoja hizi, nawaomba na kuwasihi tuunge mkono hoja hizi, pamoja na kwamba, fedha hazitoshi kwa Miradi yote lakini angalau tuanzie hapa wakati tunarudi kujipanga vizuri ili sasa mwaka kesho tukija hapa tuwe na bajeti ambayo inaitikia hotuba ambazo zimetolewa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, tumetangaza kazi ya kusanifu Mradi wa Maji unaouunganisha Shinyanga - Nzega - Isaka - Kagundwa na Tinde. Ule Mradi wa Shinyanga kwenda mpaka Tabora kupitia Igunga na Nzega utoe maji Isaka, Kagundwa na Tinde na jambo hili Serikali inalichukulia kwa uzito mkubwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, amewaeleza kuhusu vijiji vile 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumetangaza *tender* kwa ajili ya ujenzi wa maji katika Miji ya Magu, Bariadi, Meatu mpaka kule Ngudu. Ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, watuelewe kwamba, kazi hii tunaichukulia kwa uzito mkubwa na tutaitekeleza kwa nguvu zetu zote. Nimewasikia Waheshimiwa Wabunge mlivyokuwa mnasema hapa, mmesema kwa hisia kali na mimi nimeyapokea kwa hisia kali kweli kweli. Nimeona ni kazi kubwa na ngumu, lakini sote tulivyoongea hapa tukawa na msimamo na mwelekeo mmoja; kazi hii tunaiweza kwa sababu nia tunayo na uwezo tutautafuta sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nitawataja Waheshimiwa Wabunge ambao kwa bahati mbaya tumewasahau.

Tulipata pia hotuba zingine ambazo zina hisia kali hata kama ziliandikwa kwenye karatasi unaona kabisa kwamba, hizi hisia zilizoandikwa hapa ni kali kweli kweli. Tumepata mchango wa maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Juma Njwayo, ambao ulikuwa tofauti kabisa na ule wa maneno pale. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Njwayo, maana wewe wajina wangu na mimi naitwa Juma Abdallah, tutauangalia kwa makini Mradi wa Makonde ambao ni wa Taifa. Mwaka huu umetengewa karibu shilingi milioni 400 kwa ajili ya shughuli mbalimbali, lakini Bodi yake tutaikamilisha na kazi katika Mradi ule itaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata pia hisia kali kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, ambaye alitufundisha kwamba, Bonde lile la Wembere lilikuwa chini ya Victoria. Mimi sikujuu jiolojia hiyo na ninadhani wengi wetu hatukuijua. Akasema kwamba, ingekuwa msaada mkubwa kama lingejengwa Bwawa hata moja katika miaka mitatu. Nimeshauriana na wenzangu tumekuballana kwamba, katika Bajeti inayokuja tutaweka uwezekano wa kujenga Bwawa hilo kwa sababu kwa hali aliyoitaja ya ukame, hakuna njia ambayo wananchi wanaweza kupata msaada. Jambo hili linahusu pia eneo la Bukene ambalo Mheshimiwa Jumanne Zedi amelizungumzia kwa hisia kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata pia hisia kali kutoka kwa Mbunge wa Muleba, Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Seleman Jafo, kuhusu kama Serikali itapeleka maji Kisarawe kutokana na Miradi ya Kimbiji na Mpera. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, *design* ya Mradi ule imechukua katika mikoba yake kutoa maji katika vijiji na miji ambayo inazungukwa na Mradi ule, ikiwa ni pamoja na Mji wa Kisarawe. Hii ni sawasawa pia na Mradi ule wa Bomba linalotoka Ruvu Juu kuja Dar es Salaam ambalo litatoa maji katika maeneo ya Mlandizi, Kibaha na Vijiji ambavyo viko katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo ningependa sana nimhakikishie dada yangu Mheshimiwa Eugene Mwaiposa kwamba, kwanza, kuna visima ambavyo vimechimbwa kwa ushirikiano katika Serikali ya Tanzania na Ubelgiji katika Jimbo la Ukonga. Tulizotaja pale ni zile Halmashauri tatu za Jiji la Dar es Salaam tukiwa na uhakika kwamba, Majimbo yenu yote yako ndani ya Jiji hilo na maji yatakayoletwa Dar es Salaam yataletwa kwa ajili ya kukidhi kiu iliyopo katika Halmashauri zote hizo na viunga vyaa miji hiyo.

Tulipata pia hotuba kali kidogo hapa ya Mheshimiwa Kasulumbayi kuhusu umeme katika Mji wa Maswa. Ni kweli mwanzoni mwa mwezi Mei, nilipata simu kutoka kwa Mheshimiwa Diwani wa eneo lile, Kata ya Sanzi, ambapo Bwawa lile lipo akieleza kwamba, umeme umekatwa na kwa hiyo mji hauna maji na wakati ule mapema mwezi Mei umeme ulirudishwa. Kwa hiyo, tulifuatilia na mpaka jana Mheshimiwa

Diwani amehakikisha kwamba, Mji wa Maswa na vijiji vyote ambavyo vinapata maji kutoka kwenye Bwawa lile vinapata maji. Vijiji hivyo ni Malita, Sanzui, Maswa, Induki, Buyubi, Dodoma, Nihadiyogolo na Sola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Kasulumbayi alisema, basi kama umeme haurudi sisi tunakuwa Jamhuri ya Maswa. Waheshimiwa, wakati mwingine mnposema maneno haya tunakuwa na wasiwasi na viapo vyenu vya utii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawashauri sana, ninajua Vyama Vingi hivi vina majukumu mengi, lakini ni vizuri kurudi kwenye Jimbo kujua ni kitu gani kinaendelea; maana maji haya yamerudi tangu mwezi Mei na mpaka leo watu kule wanasema maji yapo na Mradi huu ulianzishwa na Chama cha Mapinduzi na Mbunge maarufu sana anaitwa Mheshimiwa Pius Ng'wandu. Tupo na wewe Mheshimiwa Kasulumbayi, kama kuna tatizo tueleze lakini hali tulioambiwa kule ni nzuri na wananchi wanaendelea kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ambazo zimetolewa nyingi zilitolewa na Kamati yetu ya Kilimo, Maji na Mifugo, zikisema mambo muhimu yafuatayo:-

La kwanza, Serikali iongeze bajeti na fedha za maendeleo zitolewe kwa wakati. Haya ni mambo ambayo na sisi tunakubaliana nayo na kama nilivyosema, tutafanya juhudini kubwa kuhakikisha kwamba, kuanzia Bajeti inayokuja ya mwaka 2013/2014, hisia zilizotokea hapa ndani zinaingia katika bajeti yetu, ikiwa ni pamoja na kuongeza bajeti na kuangalia ni jinsi gani bajeti hiyo inasimamiwa na

chombo ambacho kitafikisha huduma na kusimamia Miradi ili tuwe na uhakika wa utekelezaji katika Programu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo Kamati imeomba tulifuutilie ni kodi za dawa za maji na wakaomba zifutiwe VAT. Tumepeleka maombi yetu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili dawa za maji zijumuishwe na dawa za binadamu na ziweze kufutiwa VAT na tupunguze ada za maji katika miji.

Mheshimiwa mwenyekiti, ninapozungumzia juu ya ada za maji nimekumbuka hoja alioitoa Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba, maji ya Kigoma yanalipiwa *flat rate* hata kama unapata mara moja, mbili au nne kwa wiki. Nimeiagiza Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Kigoma waanze kuweka dira za maji kwa wateja wote 8,000 katika kipindi cha miezi minne kuanzia tarehe 1 Agosti, 2012. Ikifika tarehe 31 Desemba, 2012 wateja wote wawe wamepata dira na kila mwananchi alipe kodi ya maji kulingana na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetushauri tutunze vyanzo vya maji; hili tunakubaliana nalo. Tuangalie upya utaratibu wa vijiji kumi; hili tunakubaliana nalo na tutalitolea maelezo. Hoja nyine ni kwamba, Serikali idhibiti biashara ya chuma chakavu kwa sababu inaharibu sana miundombinu ya maji. Hili tunakubaliana nalo na Serikali itakuja na Sheria ya kudhibiti matumizi ya chuma chakavu hapa nchini ili kuzuia na kudhibiti matumizi ya chuma

chakavu yanayoharibu miundombinu ya Taifa.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitajaribu kuzipitia hoja za Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, lakini ningependa kusema kwamba, karibu Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na waliochangia kwa kuzungumza wamechangia hoja ya vijiji kumi. Nitasoma wanavyosema; Mheshimiwa Prof. Peter Msolla alisema, Mpango wa Maji wa Vijiji Kumi katika kila Halmashauri umekuwa hautekelezeki na hasa ukizingatia kuwa wananchi walichangia gharama katika Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri 67 nimeambiwa tayari zimepata vibali tangu leo vya kuanza kujenga miundombinu. Fedha za ujenzi wa miundombinu hiyo zile zilizokuwa zimepelekwa mwaka jana ziko tayari kwenye Wilaya, kwa hiyo, utekelezaji wa vijiji vitatu utaanza mara moja na kama nilivyosema vijiji vile ambavyo havitapata fedha kwa sasa tutatoa fedha zingine tena kwa ajili ya vijiji vingine viwili kwa kukamilisha vijiji vitano katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mbunge wa Mchingga alielezea juu ya vijiji vyake. Ombi la kutembelea vijiji vya Namkongo, Lihimilo, Maloo, Kilolambwani na Mnang'ole limepokelewa. Mimi ama Naibu Waziri kutegemea tutakavyojipanga tutakwenda tumtembelee Mheshimiwa Saidi Mtanda na tutamweleza tukiwa huko ili aweze kuja kushirikiana na sisi tuangalie ni kitu gani cha kufanya zaidi ya yale ambayo yamepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la Mhandisi wa Wizara kwenda Lindi tumelipokea na nimeshaagiza Mhandisi huyu aende kule Mchinga, akahudumie jambo hili. Halmashauri ya Lindi inashauriwa kuweka katika mipango yake ujenzi wa matanki ya kuvuna maji. Aliomba kwamba Serikali itasaidia namna gani uvunaji wa maji na Shule ya Sekondari ya Mipingo, Rutamba, Namilola, zijengewe matanki ya maji. Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inashauriwa kuweka katika mipango yake ujenzi wa matanki ya kuvuna maji ya mvua kwenye Sekondari za Mipingo, Rutamba, Namilola na tutakapotembelea maeneo hayo tutajua kwa yakini zaidi ni kitu gani hasa kinatakiwa na pale ambapo tunaweza kusaidia, hatutasita kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, Serikali inawasaidiaje wananchi wa vijiji katika Kata ya Ukata hasa kijiji cha Litaho ambacho kilikuwa na mradi wa Benki ya Dunia lakini hakuna kinachotendeka. Utekelezaji katika Halmashauri wa Vijiji 10, Kijiji cha Kingerikiti, Uhuli, Lumecha, Litindosili, Mbambabay, Ndesule, Lundu, Litambakuhamba, Kigonsera, Mhato, Kihongo, Litoho na Kilosa. Katika awamu ya kwanza Wilaya ya Mbinga imeweka kipaumbele kwa Vijiji vya Kigonsera, Lundu na Ukuli. Tunaishauri Halmashauri kwamba, inapoleta vijiji vya awamu ya pili, hivyo viwili, basi Kijiji cha Lutoho kiwe kimojawapo ili kiweze nacho kujengewa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Eugen Mwaiposa nimelijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Gregory Teu sehemu kubwa ya vijiji vilivyopendekezwa havijapata maji kwa utaratibu wa msaada wa *World Bank*, je, Wizara imejipanga vipi kwa mwaka huu kuvipatia maji Vijiji vya Jimbo la Mpwapwa vilivyopendekezwa chini ya miradi wa *World Bank*. Katika mwaka huu wa fedha Halmashauri ya Mpwapwa imetengewa kiasi cha shilingi 481,059,000/= kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji. Ni jukumu la Halmashauri kuchagua vijiji vya kipaumbele ambavyo vinaweza kutekelezwa chini ya programu hiyo na kwa sababu ya ongezeko lile la fedha tunakushauri Mheshimiwa Teu ushauriane na Wilaya yako ili tujue ni vijiji vingapi vya ziada ambavyo vitapewa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina alisema, Serikali ifuatilie utendaji kazi wa mtaalam wa maji wa Halmashauri ya Ngara, fedha za Benki ya Dunia zigawanywe sawa kwa kila Halmashauri. Nadhani hili limejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Seif Rashid alisema kwamba, Serikali iwe na miradi mikubwa ili iwe na uwezo wa kuwafikia watu wengi. Mheshimiwa Rashid jambo hilo limejibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale alizungumza kwamba, utekelezaji wa miradi ya maji kwa utegemezi wa ufadhili wa *World Bank* unachelewesha upatikanaji wa maji vijijini, Serikali

iangalie vyanzo vingine vya fedha vya ndani kwa ajili ya kuwapatia maji wananchi. Hii ni kweli, lakini nadhani jambo kubwa hapa tumejifunga sana kwenye ule utaratibu wa *ki-bureaucracy* na tutazungumza upya na washirika wetu wa maendeleo tuone ni jinsi gani tunaweza kupunguza *bureaucracy* baada ya kuanzisha chombo ambacho kitasimamia miradi ya maji kwa uwazi na uwajibikaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour alisema maji safi na salama ni muhimu katika kulinda afya. Vijijini wanatumia maji yasiyo salama. Serikali ilipatie ufumbuzi jambo hili. Jambo hili tumelipokea na tunaimarisha maabara zetu za kuangalia usafi na ubora wa maji katika kanda zote na tunatafutia ithibati ya Kimataifa maabara yetu kuu ya maji Dar es Salaam ili tuweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuangalia sampuli za maji. Kwa hiyo jambo hili tumelipokea na tutalifanyia kazi kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine suala lake limejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mariam Kasembe katika mchango wake alisema kwamba, Jimbo la Masasi lina Kata 16, lakini ni vijiji vitatu ambavyo vilipata maji. Pili, fidia ya wananchi ambao walipisha ujenzi wa mradi wa Mbwinji. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mariam Kasembe kwamba, suala hili la fidia ni kweli kwamba kuna wananchi ambao hawajapata fidia na tutalifuatilia kwa haraka tuhakikishe kwamba wananchi hao wanalipwa. Aidha, tumesikia tatizo la mabwawa ya Lukuledi na yale

mabwawa mengine mawili na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kasembe kwamba, mimi mwenyewe nitakuja kutembelea Wilaya ya Masasi, Nanyumbu na Tandahimba kuangalia maji katika mradi wa Mbwinji pamoja na Makonde na miji ya Mtwara na Lindi na kuangalia upatikanaji wa maji katika Wilaya zile. Kwa hiyo, tutaona itakavyokuwa ili tuone jinsi gani tunashughulikia matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba nimekusikia ulivyosema kwa hisia kali. Kwanza tukiwa hapa Dodoma tutatafuta siku moja ya mwisho wa wiki twende tukatembelee vijiji vyako hivi ambavyo umevitaja hapa na mabwawa ambayo umeyataja. Napenda kukupongeza sana kwa kazi kubwa ambayo unafanya katika Jimbo lako pamoja na kazi ambazo tumekupa kwenye Chama cha Mapinduzi. Tunafarijika sana kwamba pamoja na kazi kubwa tuliyokupa unashughulikia kazi za wananchi kwa nguvu kubwa na sisi tutatoa msaada wowote tunaoweza kufanya ili kuhakikisha kwamba kazi yako inakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nimhakikishie Mheshimiwa Selemani Nchambi kwamba, tutakuja kuangalia yale mabwawa ya maji aliyokuwa anayasema ili tuangalie ni jinsi gani ambavyo tunaweza kuvuna maji katika Jimbo lake lile la Uchaguzi. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyokupa, lakini tutakuja tuangalie yale maji, tunajua jinsi ambavyo unachapa kazi na tunawaeleza watendaji wako kule wakae chonjo kwa

sababu unafuatilia mambo haya kwa karibu sana. Nakupongeza sana na Mungu akulinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Tupitishe bajeti hii, tukishapitisha bajeti hii twende tukafuatilie maeneo yale ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alipita akayaangalia, tuangalie kwenye Kijiji cha Mtemi, Mazengo na kwenye maeneo mengine yote ya Jimbo lako tuone ni jinsi gani tunaweza kuharakisha upatikanaji wa maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Silvestry Koka limejibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu ameuliza mradi wa *World Bank* umekuwa tatizo, wananchi wamechangia asilimia kumi, Serikali ibebe jukumu la kuchangia kwenye maeneo duni. Kwanza niseme tu kwamba, kiasi cha uchangiaji ambacho kimewekwa nchi nzima ni asilimia 2.5. Kwa hiyo, pale inapowezekana basi vile viwango ambavyo vimechangiwa juu ya kiwango hiki mngeviweka vikae katika Mfuko wa Maji wa Vijiji ili viwasaidie wananchi kuendesha miradi ile badala ya kuzihesabu kama ni mchango wa ujenzi wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaongeza jitihada katika kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa katika kila Halmashauri na kwenye kitabu cha hotuba kundi la nne katika utekelezaji Wilaya ya Kilwa ina miradi kadhaa ambayo inasubiri usanifu. Miradi yote inayotekelizwa kwenye mradi wa Vijiji Kumi haifanyiwi

usanifu kwa sababu usanifu ulikwishafanywa. Halmashauri ya Kilwa imepata vibali vyote vya ujenzi kuanzia tarehe 17 Mei, kwa ajili ya Vijiji vya Kandawale na Mtandi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Leticia Nyerere ametoa rai kwamba Wilaya ya Kwimba ina takribani vijiji 150, je, ni jinsi gani visima tisa vinaweza kukidhi mahitaji ya vijiji hivyo kama Mheshimiwa Leticia Nyerere amesoma vitabu vile vya bajeti ,ataona kwamba kuna miradi ambayo ni *Lake Victoria Environmental Programme* pamoja na vijiji vitakavyopatiwa maji kupitia miradi ya vijiji 96 kwenye bomba litokalo Lihelele kwenda Shinyanga kwenda Tabora. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Nyerere kwa ufuatiliaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine hapa la Mheshimiwa Arfi, Kata ya Kaseke ina vijiji vitano na vitongoji zaidi ya 25 na eneo hili lina tatizo kubwa la maji. Napenda pia niunganishe suala hili na la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, kwamba tumejipanga kwenda kutembelea Mkoa wa Katavi ili kujifunza na kujua matatizo yaliyoko kule na sisi tuna uhakika kabisa kutokana na ruhusa hii ya utekelezaji wa Vijiji Vitano mwaka huu na vitano mwaka kesho kwamba sehemu kubwa ya matatizo haya tutakabiliana nayo, lakini tunaendelea kutengeneza *proposal* za miradi mipyä ya maji vijijini na katika miji midogo tunategemea kabisa kwamba vijiji hivyo tutavishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata pia mchango kutoka kwa Mheshimiwa Agripina Buyogera na alisema hapa kwa hisia kali na sisi tutafanya juhudini kuviangalia vijiji alivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramo Makani amezungumzia Mradi wa Benki ya Dunia, kiwango cha kuchangia asilimia 10, ushauri Wizara ishirikiane na Halmashauri ili utaratibu unaofuatwa urekebishwe. Mheshimiwa Makani kama nilivyo sema swali hili limeshajibiwa, Tunduru itaanza utekelezaji mwezi huu kwa hiyo tutafuatilia utekelezaji wake ili kujua unaendelea namna gani.

Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya alizungumza kwamba, visima tisa kati ya 12 vilivyo chimbwa katika vijiji 10 katika Halmashauri ya Urambo havina maji. Suala hili la visima limejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai alisema kwamba, matatizo makubwa yako katika Vijiji vya Mto Chole, Manyusi, Talawi, Musingisa, Laikala, Ihanda, Maleli, Chingwilingwili, Lengaji na kadhalika. Serikali imepeleka sh. 627,843,000 katika Halmashauri ya Kongwa ili vijiji Vitatu vya Mlanje, Chingwilingwili na Muhumba vianze kutekelezwa kwa mwaka huu na vijiji vya ziada vikiletwa na vyenyewe vitatekelezwa kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu sasa kwa sababu muda hautoshi niweze kuwataja watu

ambao tuliwasahau kuwataja katika orodha ya waliochangia nao ni:-

Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeletewa karatasi hapa inasema, Mheshimiwa Waziri usisahau Tarime. Nami nasema, sitasahau Tarime na Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa jibu zuri. Baada ya kikao hiki tumekubaliana na Waheshimiwa Wabunge...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, muda wako umekwisha.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Lakini nilikuwa niseme tu ni kwamba, tutakwenda kutembelea Mkoa wa Mara kabla hatujamaliza Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, hatua inayofuata. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 49 – WIZARA YA MAJI

Kif. 1001 - *Admin and HR Manag.*Shs
2,602,634,000/=

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nataka Mheshimiwa Waziri afafanue hizi Mamlaka za Maji Mijini na Halmashauri za Wilaya na miji nazo pia kuna mkanganyiko hapa katika maslahi. Mfano, *L UWASA* Lindi, pamoja na Halmashauri ya Lindi kuitia mji mdogo wa Mingoyo ambapo kuna mradi wa maji ambao ulikuwa unaongozwa na vijiji wakati ule. Sasa kuna kinyanga'anyiro nani amiliki mradi ule. Sasa ni vyema Mheshimiwa Waziri akatoa ufanuzi hali kama hii inapotokea kisheria nchi nzima mamlaka zinakuaje katika kumiliki miradi kati ya mamlaka na hizi Halmashauri zetu?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Barwany kwa suala hili.

Kwenye maeneo ambayo kuna mamlaka za maji kama Mamlaka ya Majisafi na Majitaka pale Lindi, basi ile Mamlaka kisheria ndiyo inayomiliki chanzo cha maji pamoja na kusambaza maji katika mji na kisheria wanajitegemea wao wenyewe.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimebahatika kutembea sana katika nchi hii na katika maeneo mengi, utakuta mabwawa au malambo ambayo yamejengwa kwa kodi za wananchi au kwa kushirikiana wananchi na Serikali hasa ilijoengwa katika miaka ya 1960 na 1970. Katika maeneo mengi sana ya Tanzania utakuta yamevamiwa na magugu maji na nimekuwa nauliza kwa maandishi, hivi Serikali kupitia Wizara ya Maji ina mpango gani katika kuyanusuru baadhi ya haya mabwawa na malambo ambayo yamevamiwa na haya magugu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mfano Ziwa Victoria, lilipovamiwa na magugu maji Serikali ilikuja kwa nguvu sana na mpaka leo tunaona hali hiyo imedhibitiwa vizuri sana. Napenda kujua, maana ndiyo sehemu kubwa ya vyanzo vya maji kwa wananchi wengi katika nchi yetu. Tuna mpango gani kama hakuna tuambiwe yaache yakauke yafe kwamba hiyo ndiyo sera ya Wizara. Ahsante sana.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika maeneo mengi mabwawa haya hayakutunzwa vizuri. Lakini kutokana na upungufu wa rasilimali za maji hasa maji safi na salama ni muhimu sana mabwawa haya yakaangaliwa na

yakakarabatiwa kila yanapoharibika. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mtemi Chenge kwamba Wizara yangu itaanzisha programu maalum ya kuyashughulikia mabwawa haya.

MHE. LOLESTIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi pia nahitaji ufanuzi, nilivyokuwa nikisoma hiki kitabu cha Bajeti hasa katika programu za maendeleo ya sekta ya maji katika Mikoa na katika Wizara. Nimeona Mikoa mipyä hajawekewa bajeti yoyote ile. Mikoa hiyo ni kama Simiyu pamoja na Njombe. Nahitaji ufanuzi kwa sababu Mkoa wa Geita ambao ndiyo Mkoa wangu haujapangiwa bajeti yoyote. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Swali hilo tutalikuta kwenye *development budget*.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka maelezo kutoka kwa Waziri kwamba katika Sera ya Taifa ya Maji tunasisitiza kwamba kila Mtanzania apate maji safi na salama. Lakini kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali mpaka kufikia tarehe 30 Juni, inaonesha kuna bakaa ya bilioni 32.2 ambayo ilibaki katika miradi ya maji na hii ni sawa na asilimia 58 ya miradi yote ya maji nchini. Je, Waziri anaweza kutuambia ni kwa nini fedha hizo hazikutumika na wakati tatizo la maji kwa Watanzania ni tatizo moja kubwa sana na Wabunge wamelipigia kelele sana?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha anazozisema ni zile ambazo zilipelekwa kwenye Halmashauri wakati zikisubiri upembuzi yakinifu na hatua mbalimbali za kupitia Benki ya Dunia. Kwa hiyo, zilionekana ziko kule na wale wenzetu wa Halmashauri waliambiwa wasizitumie mpaka wapate kibali na walipopata kibali zile Wilaya 62 wameanza kuzitumia.

MHE. ABUU H. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nataka kujua Sera ya Serikali kupeleka miradi ya maji kwa wananchi. Ni sababu zipi zinazosababisha kuchelewa kama kwenye Kata yetu?

MWENYEKITI: Hilo sio suala la kisera hilo ni swali linagusa Jimbo moja kwa moja. Tunaendelea Mheshimiwa Makilagi!

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nikichangia nilieleza kwa hisia kali sana kwamba sera ya maji inatutaka kila palipo na chanzo cha maji wananchi wanaozunguka chanzo kile waweze kupata maji na nikawa nimeeleza kabisa kwamba Mradi wa Kyabakari, Butiama na Mgango wananchi wanaoishi katika chanzo cha maji cha Mgango hawapati maji. Sasa napenda kujua kwamba Serikali inatuambia nini katika mwaka wa fedha au kipindi hiki maana nimeona kumbe ukiongea kwa hisia kali fedha zinapatikana. Serikali inasema nini sasa kupeleka maji katika chanzo cha maji kinachohudumia wananchi wa Mgango, Kyabakari na

Butiama ambako kwa kweli ndipo lilipo kaburi la Baba wa Taifa wa nchi hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina swalii hilo sio la kisera, labda usubiri kwenye *development budget*. Tunaendelea na Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu kuna maeneo yenye madini kama ya *uranium* ambapo visima vya maji haviwezi kuchimbwa, kwa mfano, Wilaya ya Bahi. Je, Serikali inawasaidiaje wananchi wa maeneo hayo kupata maji safi na salama?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama kuna madini ya urani katika eneo ni vizuri kuangalia vyanzo vya maji vya kule kama vimeathiriwa na madini hayo ya urani. Tunachukua sampuli za maji katika maeneo hayo kuyapima na kama hayafikii viwango hivyo tunatafuta viwango mbadala kwa ajili ya wananchi. Lakini kama viwango vilivyopo ni salama basi wananchi wanashauriwa ipasavyo.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la fidia kwa miradi mikubwa ya maji. Je, utaratibu gani ambao unatumika kwa sababu kuna mradi mkubwa wa maji ambao ortalisha Mkoa mzima wa Dar es Salaam lakini ardhi ile bado haijalipiwa fidia. Je, katika hizo fedha ambazo zimetengwa kwa miradi hii katika vitabu hivi sehemu yake itakwenda katika kulipa fidia hiyo?

MWENYEKITI: Hilo ni suala la *development budget*. Sio suala la kisera. Mheshimiwa Mkosamali!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utaratibu kwenye baadhi ya maeneo ya nchi hii kutoza fedha bila kuzingatia utumiaji wa maji na hili limejitokeza kwenye Halmashauri nyingi nchini na kwenye baadhi ya maeneo ya miji. Sasa Serikali inatoa tamko gani kwa mamlaka za maji ambazo zinatoza maji *flat rate* au kwa kukadiria, kwa mamlaka zote nchini na Halmashauri ambazo zinafanya mambo haya?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge. Jambo hili tunaendelea kuondokana nalo. Kwamba tunazishauri na kuzijengea uwezo mamlaka za maji ziweze kuweka dira za maji au mita za maji kwa kila mtumiaji ili watu wasilipe maji ambayo ni ya kufikirika tu. Lakini katika maeneo machache jinsi tunavyokwenda huko bado hatujafikia lengo na bei za maji zinawekwa na *EWURA* ili kuhakikisha haziwi nje kabisa ya bei zenyewe au ile mamlaka haishindwi kutoa huduma kwa sababu haikusanyi mapato.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza masikitiko yangu juu ya upungufu wa maji kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji na Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha sikumsikia akieleza lolote juu ya jambo hili. Naomba Serikali itueleze ina mkakati gani wa ziada kuhakikisha

kwamba wanadhibiti vyanzo vya maji naomba ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa swali zuri kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge. Hili suala ni suala mtambuka, kwa hiyo, Wizara yetu itashirikiana na *NEMC* ili kuona vyanzo vya maji vinalindwa na hiyo mikakati ipo, kinachotakiwa ni kusimamia tu utekelezaji.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba ametoa au alipotujibu maswali yetu hayakutukidhi kwa sababu sisi tulipenda kujua kwamba tangu mwaka 2007/2012 fedha zilitolewa bilioni mia moja themanini na nane bilioni mia tatu na saba milioni mia tisa hamsini na nne mia saba kumi na tisa kwa ajili ya kutekeleza Vijiji Kumi katika kila Halmashauri. Utekelezaji ule ulikwenda kwa awamu tofauti ambapo wengine waliweza kufanya kwa awamu mbili na wengine awamu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo fedha za mwaka huu kwenye bajeti hii wanaanza kutoa kwa vijiji vitatu na majibu yake ya leo amesema ni vijiji vitano ataviongezea hela. Kwa nini tusiende na utaratibu huo huo wa utekelezaji katika kila Halmashauri ikafanya utaratibu wake wa kutekeleza visima vyote kumi au saba vilivyo tayari. Nataka majibu hayo.

MWENYEKITI: Hilo ni suala la sera lina *cut across* Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi katika kila Halmashauri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza hapa kwamba katika kila Halmashauri na Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu vizuri kulikuwa na fedha ambazo Halmashauri zilikuwa nazo ambazo zilipelekwa kwenye Halmashauri katika mwaka wa fedha uliopita. Katika mwaka huu wa fedha Ofisi ya Rais TAMISEMI inazo fedha shilingi bilioni 51.9 ambazo zimetengwa kwa utekelezaji wa vijiji hivyo vitatu, lakini kwa bahati nzuri tumepata fedha za ziada baada ya *ceiling* za Serikali *Africa Development Bank* (ADB) na *DFID* wametupatia jumla ya shilingi bilioni 30 tunadhani kwamba hizi fedha za ziada tuzipeleke kwenye utekelezaji wa Vijiji Kumi na kila Halmashauri itekeleze vijiji viwili zaidi, kwa jumla ya vijiji vitano mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe ndugu zangu, hebu twendeni tufanye hilo na mwaka kesho tulenge kutekeleza vile vijiji vingine vitano vilivyobaki ili Mradi wa Vijiji Kumi uwe umekamilika katika mwaka wa fedha na mwaka ujao wa fedha.

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya maji ni kuhakikisha kwamba maji yanawafikia wananchi na wanapata maji safi na salama, lakini pia utaratibu baada ya pesa za Serikali kutolewa huwa zinahitajika zifike kwenye maeneo husika. Lakini nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri ni sababu gani zinazofanya pesa ambazo tunaziidhinisha na Bunge kwenda Majimboni kwa maana katika Halmashauri zetu zinakuwa hazifiki mfano, mwaka 2011/2012 Mafia hazikufika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naamini kuwa siyo Mafia peke yake, lakini alilolisema Mheshimiwa Amina Makilagi wewe kama vile hukulitilia maanani sana, wale watu wanaosema kwa ukali na kutokuunga ndiyo watu ambao Serikali inawaona na kuwapa miradi hiyo. Sasa ni vipi Mheshimiwa Waziri anatuambia sisi ambao tumeandika na hatuna hulka na kutoa ukali na kutishia Serikali kutounga mkono na lini miradi tulioandikia itakubalika au itapitishwa mwaka huu? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shah, suala la ukali siyo suala la kisera, suala la utekelezaji wa miradi ya maji litatolewa tamko hapa baada ya kumaliza shughuli nzima. Lakini ukianza sasa suala la ukali ndani ya Bunge je, ni suala la kisera? Hilo silo suala la kisera, suala la msingi hapa ni kwa nini Sera yetu inasema wananchi wapatiwe maji na fedha zinapelekwa vijijini lakini hazifiki kwa wakati katika maeneo yote, hiyo ndiyo hoja ya msingi. Mheshimiwa Waziri ni kwa nini fedha hazifiki na Sera inataka fedha zikitengwa za maji zifike?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kweli tu kwamba, muda wa kujibu hoja kama ambavyo zinatolewa kwa siku mbili kwenye Wizara kama ya Maji ni muda mfupi sana wa saa moja. Nawaomba radhi sana Waheshimiwa Wabunge ambao hoja zao hatukupata nafasi ya kuweza kuzijibu, lakini tuna majibu kwenye hoja hizo zote pamoja na vijiji vile vilivyoko kwenye Kisiwa na Kisiwa Kikuu cha Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la *transfer* ya fedha linafanywa na Wizara ya Fedha na najua

kwamba kwa sehemu kubwa ya fedha ambazo zinapelekwa zinafika. Sasa pale ambapo fedha zinapelekwa hazifiki ningewaomba Waheshimiwa tushirikiane ili tufuatilie Wizara ya Fedha kuona ni kitu gani ambacho kimetokea.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliuliza Serikali kwa vile ni Sera ya Maji na Mazingira inayosema kwamba vyanzo vya maji popote pale katika nchi hii vinahitaji vilindwe pamoja na kutunzwa. Katika milima ya Uluguru na milima mingine mingi nchini Tanzania wananchi wanajitolea kuhakikisha kwamba wanalinda hivyo vyanzo vya maji nikauliza, je, Serikali inafanya nini kuhakikisha hawa watu nao wanapata maji safi kama motisha ili waweze kuendelea kutunza hivi vyanzo ili mito mikubwa kama Ruvu na Wami isije ikakauka?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango mkakati wa kulinda vyanzo vyote vya maji nchini vikiwemo vyanzo ambavyo viko katika milima ya Uluguru. Tunaamini kabisa katika mwaka huu wa fedha tukishirikiana na Wizara ya Maji, tutunze hivi vyanzo na kuzihimiza Halmashauri zote pamoja na wananchi wote walio katika maeneo hayo tushirikiane kutunza hivyo vyanzo ili mpango huu uwe endelevu na maji yawe ya kutosha katika vyanzo na maeneo yote ya nchi.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri kwa hoja zangu mbili nilizozitoa, lakini ile ambayo ametoa miezi minne, ni mingi sana angepunguza

angalau iwe miwili. Ukiangalia tatizo la maji ni kubwa sana nchini, nataka nimuulize Waziri kama kuna mpango mkakati au wazo kama ambavyo tuliamua kuchukua maji *Lake Victoria* ambayo tumeyapa maeneo mengi sana isinge kuwa wakati sasa kufikiria kuchukua maji toka *Lake Tanganyika* ambalo lina moja ya kumi na sita ya maji yote yaliyoko Duniani ili maji yale yaweze kusaidia Mikoa hii mikubwa kama Mikoa ya Kigoma, Tabora maana kupanga ni kuchagua. Naamini tukiamua tunaweza, ili kuchukua maji ya *Lake Tanganyika* kwa ajili ya Mkoa mzima wa Kigoma kuja mpaka Tabora na Singida, tutakuwa tumesaidia sana nchi yetu. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kuchukua maji kutoka *Lake Tanganyika*, ni kweli kwamba, kuna maji ya kutosha mle, lakini suala la kuyatoa pale kuyapeleka ni suala la kitaalam ambalo linahitaji lifanyiwe *study* sawasawa. Nataka nimshukuru kwa kutupa wazo hili tutawaambia wataalam waangalie na tuone kama uwezekano wake ukilinganisha na *Ziwa Victoria* uko namna gani.

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu ambazo katika nchi yetu wafanyakazi, walimu mashulenii, madaktari hospitalini na zahanati wamekuwa wakikimbia ni kutokana na tatizo la maji. Lakini hapa tumekuwa tukizungumzia usambazaji wa maji kwenye vijiji na tumeviita Vijiji Kumi na lakini utakuta maji haya mara nyingi yanawekwa kwenye vijiji kwa wananchi pale. Sasa nataka kujua shule za mijini, utakuta karibu zote zina maji, Wizara hii ina mpango gani wa kimkakati wa kuhakikisha

kwamba hizi shule hususani za Kata ambazo zinakimbiwa na walimu zinapatiwa maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Kangi ni swali zuri na linawagusa watoto wetu wanaosoma sekondari moja kwa moja. Sasa kwa kuwa tunapeleka fedha kwenye Halmashauri tutashirikiana na Halmashauri waweke vipaumbele pia vya kupeleka maji katika shule za sekondari ambako kuna watoto wetu.

MHE. HALIMA J. MDEEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali mbali ya kutoa huduma za maji kwa wananchi, lakini vilevile wananchi wanatakiwa kupata maji kwa gharama nafuu. Lakini wakati natoa mchango wangu leo nilizungumzia tatizo kubwa ambalo limeikumba nchi yetu la watu binafsi ambao wanatumia miundombinu ya DAWASA kufanya biashara ya maji. Matokeo yake ni kwamba, wananchi wa kawaida wanauziwa maji kwa gharama kubwa sana kuliko ile gharama ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba wananchi wanakuwa hawapati huduma ya maji kwa sababu wale wafanyabiashara wanakuwa wametengeneza matanki makubwa na vile vile wanatumia pampu. Kwa hiyo, wananyonya maji na yale maji ambayo yanatakiwa kwenda katika maeneo mengine yanakuwa hayafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate kauli ya Serikali kwa sababu kwa taarifa ambazo nimezipata ni

kwamba imefikia hatua sasa wanakata mabomba ili kuweza kuongeza wateja. Nataka nipate kauli ya Serikali kuhusiana na biashara ya maji ya watu binafsi wanaofanya kwa kutumia miundombinu ya Serikali. Je, Serikali iko tayari kufanya *operation* maalum katika maeneo yote ya nchi hii na hususani katika Jiji la Dar es Salaam kuweza kuwakamata watu wote wanaofanya hiyo kazi na kuzuia kabisa uuzaaji wa maji ili kuweza kupunguza kero ya maji na wananchi kuweza kupata maji kwa gharama nafuu. Kwa hiyo, nataka tamko la Serikali katika hayo masuala moja na nusu lakini yanayofanana.

MWENYEKITI: Ni suala moja tu nusu hairuhusiwi. Nusu unabaki nayo mwenyewe, unarudi nayo Jimboni, Mheshimiwa Waziri ni swali moja, nusu haturuhusu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali alilouliza Mheshimiwa Mdee ni swali zuri kwa sababu katika Jiji kama Dar es Salaam kuna upotevu mkubwa wa maji. Tumeanza kazi hiyo kwanza tumewapa *questionnaire* wafanyakazi wote wa DAWASA na DAWASCO watueleze wanachojua kuhusu jambo hili na tumepata *data* nzuri sana na tumemteua mtaalam wa kutufanyia *analysis*. Baada ya kupata matokeo haya tutaanza kazi kubwa sana pale Dar es Salaam, kufuatilia jambo hili mpaka tufike mwisho wake.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni namba 104, Kanuni ndogo ya kwanza kwa Mamlaka niliyopewa naomba kuongeza nusu saa zaidi ili kazi hii iweze kuendelea mbele. Waheshimiwa Wabunge wengine wengi ambao wameomba kupata

nafasi wapate nafasi ya kuendelea kuuliza sera mbalimbali zinazohusiana na maji katika maeneo ambayo wanawakilisha ama nchi nzima ya Tanzania. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza vigezo vinavyotumika katika kutenga pesa kwa ajili ya vyanzo vya maji. Kwa sababu vyanzo vingi vya maji vimepoteza mwelekeo, vyanzo vingi vya maji vimejaa michanga kutokana na tabia nchi na ongezeko la watu.

WAZIRI WA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu awali kwamba tuna mpango mkakati wa kutunza vyanzo vya maji. Ni kweli kabisa kuwa vyanzo vingi vimeharibiwa na hasa vya mito mikubwa kama Kilombero, Rufiji na Pangani na mwezi wa nane kama tulivyoahidi mwaka jana tutaanza kwenda kuwatoa wale wafugaji na wakulima wanaolima Kilombero. Zoezi hili litakuwa endelevu ili kuhakikisha kuwa vyanzo vyote vya maji vinaachwa huru na tuweke mkakati wa Halmashauri. Kwenye swali moja pia nilijibu kwamba tutashirikisha hata na shule zetu za Kata ili kuhakikisha vyanzo vyote vya maji vinalindwa.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakuwa na azma nzuri sana ya kuanzisha miradi mbalimbali katika nchi yetu na sehemu mbalimbali. Lakini ukitembea katika nchi utakuta magofu pengine shule za sekondari hazijakwisha, sehemu zingine miundombinu ya umeme haijakwisha na sababu tuko katika Wizara ya Maji.

Hapa napo kilio cha Wabunge wengi utakuta sehemu nyingi miradi ya maji imeanza lakini hajakwisha na wakati huo huo tunaanza miradi mingine. Labda kuweka mfano, ni pale Mbinga Mjini kulikuwa na mradi wa maji na yale maji yalifika kwenye *point* fulani kuyaleta mjini pia hayajaletwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isiwe na mpango madhubuti wa kuangalia ile miradi ambayo ipo ikaisha kabla ya kwenda katika miradi mingine.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii programu ya maji ilianza mwaka 2007 na inakwenda mpaka 2025, huo ni mkakati lakini utekezaji wake unakwenda kwa miaka mitano, mitano. Kwa hiyo, hatuwezi kwenda awamu ya pili bila kukamilisha awamu ya kwanza, kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba hilo linafanyiwa kazi. Programu hii ya kwanza ya miradi ya maji inakwisha Juni, 2014, hapa tutaanza programu nyingine ambayo itachukua miradi hiyo.

MHE. ALBERT O.NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu tunayo miradi ambayo kuanzia miaka ya sabini mtandao wa maji ulikuwa ni mzuri na vijiji vilikuwa vimeunganishwa vinavyofika sita, saba mpaka nane, lakini miradi hiyo imetelekezwa na Serikali. Baadaye tukaja na Sera ya Vijiji Kumi na vile vijiji vingine ile mitandao ikawa imeachwa. Nataka kujua ni vigezo gani au hatua gani za Serikali sasa zitaendelea kuchukuliwa ili kuinua na kuendeleza ile miradi iliyokuwa imeachwa.

MWENYEKITI: Nadhani swali hili limejibiwa, miradi ambayo ilikuwa haijakamilika. Una majibu ya ziada Mheshimiwa Waziri tusiwe tunajirudia rudia. Mheshimiwa limeshajibiwa katika swali lile liloulizwa mwanzo vijiji ambavyo vilikuwa havijakamilika. Mheshimiwa Mlata!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 78 na 79, amesifu sana wahisani na mashirika mbalimbali ambayo yamekuwa yakifadhili, amesema wamesaidia kufanikisha. Japokuwa amewasahau wananchi ambao na wao wamekuwa wakichangia. Nilimwomba kwamba ni mashirika yapi hasa haya aliyojasifu ambayo yalichangia na yalichangia nini na kwa kiasi gani? Kwa sababu kuna mashirika au wafadhili ambao wamekuwa wakiahidi kutoa pesa lakini hawatoi, matokeo yake Serikali inabaki kwenye matatizo na wananchi wanabaki kuhangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamwomba alete orodha ya Mashirika ambayo yamekuwa yakiahidi lakini hawaleti, ili tuyafute, tuyaondoe humu ili tujue hiso fedha hazipo, Waziri hakufanya hivyo. Kwa hiyo, naomba atusaidie ni akina nani wamekuwa wakiahidi na wameahidi sasa lakini huwa hawatoi hiso fedha ili tuwaondoe, tujue moja kwamba hatuna hiso fedha? Ahsante.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ambao tunashirikiana nao katika maendeleo, nadhani mtu anayewajua vizuri zaidi ni Waziri wa Fedha, lakini wanaweza kuwa wameahidi watatoa shilingi mia moja

wakatoa hamsini, wakati mwagine lakini ni mara chache sana wakaahidi mia moja wakaleta mia mbili. Naliomba Bunge lako Tukufu, watu hawa ni marafiki zetu na marafiki kama amepata tatizo siku hiyo hawakuja wakakuletea walichosema wataleta, basi unaweza kwenda ukamwuuliza pole pole badala ya kumtangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu likubali kwamba marafiki tushirikiane nao vizuri kwa kuheshimiana na kujenga urafiki vizuri zaidi.

MHE. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sera ya Serikali ya kuwa na visima kumi katika kila Wilaya, haijafika kule Vunjo, kule Mwika hakuna maji, Mwika Kaskazini na Mwika Kusini. Kwa bahati nzuri mhisani wetu alikuwa Rais Jakaya Kikwete 2010, alituahidi pale kwenye Mji wa Himo atatupa milioni 150, bahati nzuri amekwishatupatia milioni 50. Juzi alipofika Himo nikamwuuliza ile alibaki iliyobaki vipi, akaniambia utapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kujua sasa namwuuliza Waziri hapa, naiuliza Wizara au naenda kudai wapi? Je, huo mradi wa kukamilisha mradi wa Himo ziko Wizarani au Waziri unazo hapa? Nitashukuru sana kama ukiniahidi kwamba hiyo kazi itafanyika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mrema, nitaomba swalii lako hilo ulilete kwa utaratibu maalum siyo la kisera. Kupeleka maji Vunjo kwa mazungumzo unayoyasema siyo swalii la kisera. Nitaomba umletee Waziri kama

swali maalum la kutaka kujua ahadi inatekelezwa namna gani. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua sababu ambazo zinapelekea Serikali kupitia Wizara ya Maji kutokuruhusu mita ambazo wanafungiwa wananchi kuhakikiwa na wakala wa vipimo na hili limeleta malalamiko makubwa sana kwa wananchi kwamba wanazidishiwa au Mara nyingine wanachajiwa mita bila ya maji kuwa yamepatikana. Ni lini Serikali itapitisha sheria hii au italeta hili jambo Bungeni ili tuweze kuhakikisha kwamba zile mita zinahakikiwa ili kumlinda mtumiaji wa maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mangungu kwa swalii lake zuri, lakini naomba tulichukue ili tuweze kulifanyia kazi kwani ni jambo nyeti na ni jambo muhimu sana.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Nilimwuliza Mheshimiwa Waziri katika maandishi kwamba, ni lini Serikali itaweka wazi kwa watalaan wake namna ya ushirikishwaji wa wananchi katika kubuni miradi mbalimbali ya maji nchini? Mara nyingi watalaan wanakwenda na kufanya mipango ya miradi mahali ya kupeleka maji, lakini kwenye vyanzo vya maji wananchi wale huwa hawashirikishwi, na unakuta tayari utafiti ulishafanywa katika maeneo husika kuwa yale maji hayafai kutumika. Serikali inawekeza fedha na baadaye inajikuta yale maji hayafai kwa kutumia.

Je, ni lini sasa watakuwa wanaweka miradi au tafiti mbalimbali na miradi yote iwe kwenye mtandao ili wengine wapya wanaokuja ambao hawajui historia ya hiyo sehemu, waweze kuipitia vizuri na baadaye tusiingie katika migogoro ya mgongano wa maslahi katika miradi mbalimbali?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti namshukuru sana Mheshimiwa Jitu Soni kwa jambo hili muhimu. Tunachosema kwenye Sera ya Maji ya mwaka 2002 ni suala zima la kushirikisha wananchi kuanzia kwenye kutambua vyanzo vya maji. Hii inasitiza kwamba wanapokuwa wamechagua chanzo cha maji wanazingatia uwezo wao wenyewe baadaye kuweza kusimamia shughuli za uendeshaji. Kwa hiyo, hili likizingatiwa maana yake wanaweza wakawa na umiliki mpaka kwenye utekelezaji na hata kwenye kugawana mapato.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kwamba, Mji wa Shirati ulikuwa na Mamlaka ya maji ambayo ilikuwa chini ya Kanisa la *Menonite*, mwaka 2004 ulikabidhiwa rasmi Serikalini, mwaka huo huo pampu ya maji iliharibika. Lakini cha kusikitisha watumishi wale wameendelea kulipwa mshahara mpaka leo hii. Nataka kujua, je, Serikali imefanya *cross benefit analysis* ya kuwalipa wale mshahara wakati hawafanyi kazi yejote pale na ni hasara kiasi gani Serikali ime-*incur* mpaka sasa hivi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko hilo ni swali *very specific*, wala siyo la kisera, lilete kwa utaratibu unaotakiwa.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nataka kupata majibu kutoka kwa Waziri, kwa kuwa mfumo wa utoaji wa huduma ya maji wakati wa Serikali ya Kikoloni ulikuwa wa kibaguzi kwa kupendelea maeneo ya mijini zaidi kuliko vijijini. Mwaka 1961 ni asilimia sita tu kulikuwa na maji vijijini katika mashamba makubwa ya Wakoloni. Baada ya uhuru tumeona kwamba Sera ya Maji imelenga kutoa huduma ya maji kwa wananchi katika misingi ya usawa. Je, Serikali haioni kwamba imeshindwa kutekeleza sera yake ya kutoa huduma ya maji kwa wananchi kwa misingi ya usawa, kwa vile kwa kiasi kikubwa imeendelea kutegemea wafadhili?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba tumetegemea wafadhili ndiyo maana hatukutoa kwa usawa, hiyo si sahihi. Kama tulivyotoa takwimu hapa fedha ambazo zipo kwa ajili ya maji vijijini zinafikia karibu shilingi bilioni 178. Kikubwa hapa ni kwamba, tatizo ni kubwa na kama ambavyo tumeahidi hapa, tutafanya juhudu ili Serikali iongeze bajeti ya maji na hasa msisitizo wa kupeleka nguvu zaidi katika vijiji na miji midogo.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naiamini sana Serikali, suala ambalo nilitaka kuuliza limeshaulizwa na limeshajibiwa. Nakushukuru.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilitoa mfano wa nchi ya Israel jinsi ilivyoweza kuendelea na baadhi ya nchi nyingine za Falme za Kiarabu kwa kutumia maji ya chumvi. Maji ambayo wanayabadilisha na kuyatumia katika hali za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tuliyonayo ni kwamba, wataalam kutoka Israel waliwahi kufika katika nchi yetu na kuangalia namna ya uwekezano wa kuyabadilisha maji ya chumvi kama vile ya bahari, kuweza kutumika katika maji ya kawaida. Nataka kujua Je, kwa kutumia sayansi uliyonayo, ni lini Wizara yako itakubali au itaanza mradi huu wa kutumia maji ya bahari kuyabadilisha na kuweza kuyatumia katika matumizi ya kawaida hasa katika umwagiliaji na majumbani?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa swali zuri sana. Wiki iliyopita tulikutana na Kampuni ya Kiisrael ambayo ndiyo yenyeye mitambo mikubwa kuliko kampuni zingine zozote duniani, inayochuja maji ya bahari yawe salama na kuyaunganisha na maji ambayo yanatumika kwa wananchi. Tumezungumza nao kuhusu uwekezaji wa kiwanda kitakachozalisha maji yanayofikia *cubic meter* za ujazo laki moja kwa siku. Tunaendelea kuongea nao tutaona ni jinsi gani wanaweza kuzalisha na bei ya maji itakuwaje kabla hatujakubaliana nao.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nimezungumza juu ya uletaji wa maji ya kutoka kwenye Bwawa la Ulyanyama kuja Sikonge Mjini, lakini kwa sababu sijaongea kwa hisia naona sijapata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yangu yanajikita kwenye utaratibu. Hii ndiyo Kamati ya Matumizi na hapa tunapitisha Fungu la Wizara na vifungu vyake vingine vidogo. Nimepata wasiwasi kidogo, nataka unipe mwongozo wako. Wakati Waziri anajibu hapa ametoa maelezo kwamba Waziri Mkuu amempa maelezo kwamba, kuna fedha karibu bilioni mbili zitatolewa kupelekwa Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate maelezo, fungu tunalolipitisha hapa ndilo fungu ambalo lipo kwenye bajeti ya Serikali na vitabu vyote hivi, hiyo bilioni mbili haipo. Nataka kujua bajeti zipo ngapi, tuna bajeti moja halafu tuna bajeti nyingine iko pembedi? Kama ndivyo, bajeti nyingine ipo pembedi na sisi hapa ndiyo tunaopitisha bajeti yote ya Serikali, nafikiri kwamba utaratibu umekosewa, hizo fedha alizoziahidi Waziri Mkuu ziletwe hapa na ziingizwe ili zigawanywe kwa wananchi wote wa Tanzania, ili wananchi wote waweze kufaidika badala ya fedha hizo kutolewa na kupelekwa sehemu moja bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, lakini hasa kwa niaba ya

Waziri Mkuu, mtakumbuka kwamba siku anahitimisha bajeti yake alioneshaa nia ya kuweza kusaidia kama Serikali. Yeye ni Waziri Mkuu na ni Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, anao uwezo wa kusema, anao uwezo wa kuahidi na kutekeleza. Kwa hiyo kama Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni aliahidi kutembelea Kondoa, Namanyere, na watu wengine amewaandikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amesema ataangalia na kuwezesha kuhakikisha kwamba atakwenda na ndiyo maana amemwagiza Waziri wa Maji aende akaangalie Namanyere na wiki ijayo atakwenda Mbeya kufungua miradi mingine ya maji, akaangalie mahitaji yanayotakiwa katika eneo la Namanyere na maeneo mengine. Atalifikisha Serikalini na kiasi kilichotajwa cha shilingi bilioni 2.5 ndiyo mahitaji ya Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zikitolewa zitakuja kuidhinishwa na Bunge hili. Lakini leo tunapitisha bajeti ya Wizara ya Maji, Waziri Mkuu akiridhika na mahitaji hayo na Waziri akimletea mrejesho wa mahitaji halisi ya fedha zinazotakiwa Namanyere na huko Kondoa na sehemu zingine, Waziri Mkuu ataleta kupitia utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Kanuni ya 107 inaruhusu utaratibu wa kuleta bajeti nyingine na utaratibu mwingine wa kuomba fedha utafuata kwa mujibu wa Katiba na Kanuni zetu zinazoruhusu. Waziri Mkuu hajatoa pesa, hana pesa, pesa zitatolewa humu kutookana na hoja atakayoileta wakati ukifika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, unajua mnapoyaweka haya majibu kwa utaratibu huo, labda ningechukua nafasi hii sasa kama Kiongozi ninayesimamia shughuli hii kwa sasa nitoe maagizo.

Tunachokifahamu ni kwamba sisi Wabunge wote tulikubaliana twende na mwenendo mzima wa bajeti za kisekta katika Wizara moja baada ya nyingine, tuone hali halisi ya mahitaji na matatizo tunayokabiliana nayo, lakini mwishoni ndipo tuje kupitisha *Finance Bill*. Tunaamini ninyi Serikalini kwa maagizo tuliyowapa mtusaidie kufanya kila linalowezekana kutafuta fedha nyingine za ziada kutoka vyanzo mbalimbali, fedha hizo zikishapatikana, nafikiri kimsingi mnaona hapa *Development Budget* inavyolemewa na mambo mengi ambayo ni ya kimsingi zaidi.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi ungesimama hapa na kuwaambia Wabunge hawa kwamba zile fedha ambazo nafahamu na najua Waziri Mkuu kupitia timu yake na timu ya Spika, inafanya kazi ya kupunguza ya kuangalia hapa na pale, mtakapokuja humu ndani, *priority* tuipeleke kwenye miradi kwanza ya maji. Nadhani hapo sasa ndiyo tunaweza tukaelewana kuliko hii hoja ya kusimama na kuona *priority* ni Namanyere peke yake na Ntomoko peke yake, wakati bado nadhani tuna miradi mingine mingi sana. Waziri wa Maji ametuambia hapa, akipata fedha za ziada ana uwezo wa kupeleka ajenda ya maji ikasogea mbele zaidi.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, hicho mnachokifanya ni jambo jema sana, lakini tutakapofika huko mwisho fedha hiyo basi *priority* tuiingize kwenye miradi ya maendeleo ya maji na zinazobaki ziende kwingine na mwakani tuendelee kupanga fedha nyingine tena. Nadhani tukienda hivyo tunaweza tukafika vizuri na tatizo hili la maji tukalipunguza kwa kiasi cha kutosha. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, hayo ni maelekezo ya Kiti, nadhani Waziri wa Nchi atakuwa amenielewa vizuri.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ni mionganini mwa matatizo makubwa sana katika Taifa letu. Ni bahati mbaya sana kwamba, Serikali haijaanza kuahidi leo kuhusu namna gani ya kutatua tatizo la maji. Mwaka 1987 Bunge hili lilipitisha mpango wa miaka kumi na tano ambao ndani yake palikuwa na ahadi ya kuhakikisha kwamba asilimia tisini ya Watanzania wanapata huduma ya maji. Mpango ule ungekwisha mwaka 2002. Leo tunazungumza hapa ni miaka 25, robo karne bado mpango huo umeshindikana, naomba Waziri alieleze Bunge hili Tukufu ni kwa nini wananchi wasipoteze imani na Serikali kama imeahidi takribani robo karne na imeshindwa kutekeleza.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea swali la Mheshimiwa Kafulila, ni swali zuri. Lakini natumaini kwamba, Mheshimiwa Kafulila anaelewa kutoka mwaka anaousema 1987 mpaka mwaka 2000 nchi yetu ilipitia katika mitihani gani ya

kiuchumi. Kila Taifa linapita kwenye nyakati ambazo zinakuwa na hali ngumu na kama ikipita hivyo basi malengo mengine yanaweza yasifikasiwe.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Kimsingi, miradi mingi imekuwa ikisuasua hasa Miradi ya Vijiji Kumi kupitia *World Bank*, ukifuatilia unakuta sababu zingine zinasababishwa na Serikali. Kuna tatizo kubwa sana la Wahandisi na hivyo hata kupata *no objection* inakuwa ni tatizo kubwa. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba sehemu zote ambazo Wahandisi hawapo wanapatikana ili waweze kutusaidia katika kutatua tatizo la maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Kandege. Taarifa tulizonazo sisi ni kwamba, kila Halmashauri walijiri Wahandisi wa Maji. Kwa hiyo, kama wapo, tunaomba basi tuwasiliane tupate hiso Halmashauri ili tuone namna ya kufanya hilo zoezi ili waweze kuajiri na wafanye kazi.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nataka kujua, katika nchi yetu miundombinu ya maji mingi ni chakavu na nilitaka kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba maji hayaibiwi wala hayapotei njiani kutokana na miundombinu chakavu kwa sababu sioni bajeti kwa ajili ya *replacement* ya mabomba haya ambayo ni chakavu katika nchi yetu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miji mikubwa hasa ile ya Mikoa mingi utaona miradi ambayo inaendelea ni pamoja na kukarabati na kupanua. Kwa sababu miji mingi imekua haraka hivi karibuni watu wameongezeka na miundombinu ilikuwa bado ni ile ile ya zamani, kwa hiyo, moja ya kazi inayofanywa ni kukarabati na kupanua. Katika maeneo ya vijiji tumeulizwa hivi sasa pia vile ambavyo vimepata maji zamani kuna kazi hiyo ya kukarabati na kupanua.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni sera ipi Mheshimiwa Waziri umeitumia kutamka leo Bungeni bilioni mbili kuwapa watu wa Namanyere kwa kuwa ahadi hiyo iko nje ya bajeti na kwa kuwa iko nje ya bajeti *Hansard* imepokea jambo hilo. Nataka nimwombe afute hilo tamko na asipofuta naondoa shilingi kwenye mshahara wake ukizingatia kwamba kwenye maandishi yangu nilimwomba kama kuna fedha zilizopo wananchi wakopeshwe, maji yasambazwe, walipe pole pole, kumbe fedha ziko pembedni zinapelekwa kwenye Jimbo moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Assumpter Mshama nimeshalitolea maelezo suala hilo kwa sababu lilishaulizwa na Mheshimiwa Said na nimeiomba Serikali ione na kuangalia ushauri ambao nimeutoa hapa kwenye Kiti ili kuondoa huo mkanganyiko na wananchi wote wenyewe matatizo ya maji waweze kupangiwa utaratibu.

MHE. ASSUMPTER N. MSHANA: Hajafuta kauli na mimi nimeondoa shilingi.

MWENYEKITI: Sijakuruhusu kusema Mheshimiwa Assumpter Mshama endelea Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mamlaka zetu za Maji mbali na changamoto za kuwa na fedha ndogo za bajeti wanazozipata, lakini mamlaka hizi zimekuwa zikishindwa kujiyendesha kutokana na taasisi za Serikali kushindwa kulipa madeni. Mbali na jitihada zote ambazo wanazifanya za kukusanya madeni kutoka kwenye taasisi za Serikali wamekuwa wakikwama na hata kufikia hatua ya kuomba msaada kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma. Sasa ningependa kumuuliza Waziri, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha inawasiliana na Wizara zingine katika maeneo husika ili kuhakikisha taasisi zile za Kiserikali zinalipa Mamlaka za Maji ili ziweze kutimiza wajibu wake ipasavyo?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake zuri. Kwanza tumekusanya madeni ya taasisi zote za Serikali ambazo wanadaiwa na Mamlaka za Maji na nitumie kiti chako na Serikali iko hapa na Mawaziri wa Sekta mbalimbali wako hapa, tumewapelekea *bill* zao hizo na tunawahimiza wazilipe mapema iwezekanavyo. (*Makof!*)

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa na upungufu wa kina cha maji katika Ziwa Victoria kiasi cha

kusababisha Wizara ya Ujenzi pamoja na Uchukuzi kupanua mageti yake ili kuwezesha meli zake kuweza kutua kwa usalama. Katika kitabu cha Waziri ameonesha kwamba, wataendelea kuchukua maji katika Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Kahama, Shinyanga na sasa ametamka tena Kwimba na Magu. Je, Serikali inachukua tahadhari gani dhidi ya yale maji yatakayopungua katika Ziwa ili yasileté athari kwa sisi tunaotegemea hasa watu wa Ukerewe wanaotegemea maji ya Ziwa Victoria katika shughuli zao?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha maji kilichoko kwenye Ziwa Victoria pamoja na matumizi ya maji kwenye nchi hizi ambazo zinaitwa *Riparian* inasimamiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye ule mradi wao na kiasi cha maji ambacho tunachukua ukilinganisha na maji hasa ya Ziwa Victoria ni kidogo sana. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kwamba watu wa Ukerewe watakosa maji.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni namba 104(2) muda wetu sasa umeshafika mwisho. Kwa hiyo, tutapitisha sasa bajeti hii kwa fungu la ujumla.

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Shs. 1,022,314,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Shs. 3,527,957,000/=
Kif. 1004 - <i>Government Communication Unit</i> ...	Shs. 133,312,000/=	

Kif. 1005 – *Legal Service Unit* Shs.
220,136,000/=

Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*
Shs.519,524,000/=

Kif. 1007 – *Management Information System* ... Shs.
195,698,000/=

Kif. 1008 – *Internal Audit Unit* Shs.
250,463,000/=

Kif. 2001 – *Water Resource Assess. & Explor....* Shs.
5,945,441,290/=

Kif. 2002 – *Central Stores* Shs.
175,865,710/=

Kif. 2003 – *Water Laboratory* Shs.
1,730,665,000/=

Kif. 2004 – *Directorate of Irrigation and Techn. Serv ...*
... Shs 0/=

Kif. 3001 - *Urban Water Supply and Sew.* Shs.
2,759,348,000/=

Kif. 4001 – *Rural Water Supply* Shs.
923,656,000/=

Kif. 5001 - *Water Develop. and Manag. Instit....* Shs.
135,261,000/=

Kif. 6001 – *Drilling and Dam Construction Agency*
... Shs. 0/=

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 49 - WIZARA YA MAJI

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management*Shs.
23,673,142,250/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Shs.
7,038,882,774/=

Kif. 2001 – *Water Resource Assess. & Explor.* ...Shs
24,727,805,360/=
Kif- 2003 – *Water Laboratory* Shs.
1,483,000,000/=
Kif. 2004 – *Directorate of Irrigation and Techn. Serv.* ...
... Shs. 0/=
Kif. 3001 – *Urban Water Supply and Sew.* ... Shs.
372,056,226,536/=
Kif. 4001 – *Rural Water Supply* Shs.
36,777,281,080/=

(Bunge lilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na Kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2012/2013 kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa

Mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naona ni jambo la ajabu sana hoja hapa imetolewa lakini wa kwanza kuunga mkono ni Mheshimiwa Ally Keissy. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitisha Bajeti hii nadhani kwanza niwashukuru kwa kazi kubwa tulioifanya. Lakini Waheshimiwa Wabunge, naamini kabisa *concern* ya kila Mbunge kwa kweli ni hitaji la maji. Hata mimi kuwekwa hapa mezani leo kwa kweli kidogo imenisikitisha, ningependa na mimi huko nioneshe matatizo ya maji katika Jimbo la Peramiho. Ingawa nimechangia kwa maandishi, lakini Mheshimiwa Waziri hajataja hata Jimbo langu, lakini sasa tunafanyaje hivyo hivyo. Ndio maana nikasema kwamba narudia kusema Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kabisa suala hapa la maji si tu kwa waliosema kwa hisia kali ama kwa wale waliochangia kwa kelele sana ama kwa namna nyingine yoyote ile. Msingi wa hoja ya tatizo la maji kubaki kama tatizo la maji kwenye Serikali yetu na Serikali itambue hilo.

Niendelee kusitiza yale maagizo ambayo nimeiomba Serikali kuyafanyia kazi kwa kweli naomba sana mtusaidie, tutakapokuwa tunahitimisha chochote kitakachopatikana basi tuwe na kazi ya kuona tunafanya nacho nini, lakini *priority* iwe ni kwenye miradi ya maji. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuvute subira, tusubiri huko tunafikia mwisho kwenye *Finance Bill*, halafu tuone nini tunachoweza

kukipata kwa pamoja ndiyo tufanye maamuzi ya wapi tupeleke, kwa muda gani na kwa utaratibu upi.

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.12 usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya
Jumatano
Tarehe 11 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*